# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

### Kikao cha Sitini – Tarehe 28 Juni, 2018

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Mwenyekiti (Mhe. Andrew J. Chenge) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Tunaanza Kikao chetu cha Sitini. Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:**

Hati ya Uhamishaji Fedha Na. 1 ya Mwaka 2017/2018 *(Statement of Reallocation Warrant No. 1 of 2017/2018)*.

Hati ya Uhamishaji Fedha Na. 2 ya Mwaka 2017/2018 *(Statement of Reallocation Warrant No. 2 of 2017/2018).*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**MWENYEKITI:** Maswali. Swali letu la kwanza kwa leo linaulizwa na Mheshimiwa Zacharia Paul Issaay, Mbunge wa Mbulu Mjini.

Na. 505

**Mgao wa Fedha za Barabara**

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY** aliuliza:-

Hali ya barabara zinazosimamiwa na halmashauri ni mbaya sana kutokana na fedha zinazotolewa na Mfuko wa Barabara kukaa kwa muda mrefu na hali ya kuongezeka kwa magari binafsi na yale ya biashara ambapo kila tarafa ina zaidi ya magari 20 na hivyo, kufanya barabara hizo kuharibika na kuwa vigumu kupitika nyakati za masika:-

(a) Je, Serikali haioni haja ya kuleta mapendekezo mapya ya mgao wa fedha za barabara?

(b) Barabara nyingi za Halmashauri ya Mji wa Mbulu zimejifunga katika Tarafa za Nambis na Daudi. Je, kwa nini wataalam kutoka Wizarani wasifike kuzikagua na kutoa ushauri stahili?

(c) Je, kwa nini *BQ* za tenda za barabara ngazi ya mkoa zisiwekwe kwenye kitabu cha *RRB,* ili Waheshimiwa Wabunge na wananchi wafahamu shughuli zitakazofanywa na makandarasi waliopewa kazi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais,TAMISEMI, naomba kujibu swali la

Mheshimiwa Zacharia Paul Issaay, Mbunge wa Mbulu Mjini, lenye Sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kufanya tathmini ya mtandao wa barabara nchi nzima ili hatimaye utumike kuangalia kwa kina utaratibu mzuri zaidi wa mgawo wa fedha za barabara kati ya *TANROADS* inayoshughulikia barabara kuu na barabara za mikoa na *TARURA* inayoshughulikia barabara za Mamlaka za Serikali za Mitaa.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 Barabara za Mji wa Mbulu zilitengewa shilingi milioni 814.56. Kati ya hizo shilingi milioni 262.12 zilitengwa kwa ajili ya barabara kwa ajili ya matengenezo ya muda maalum *(Periodic Maintenance)* Barabara za Ayamaame – Kainam – Hhasama – Mbulu – Endagikot – Tlawi, Tango *FDC,* Waama – Masieda, Ayayumba – Hhayloto zenye urefu wa kilometa 35.7 katika Tarafa za Daudi na Nambisi na kuweka changarawe katika Barabara za Ayamaami – Kainam – Hhasama, Mbulu – Kuta na Ayayumba - Hhayloto zenye urefu wa kilometa 8.13

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kuchonga barabara ya Uhama – Masieda – Hayayumba – Hailoto zenye urefu wa kilometa 31.5 na ujenzi wa kalavati za njia mbili zenye kipenyo cha milimita 900 katika Tarafa ya Daudi. Barabara zilizokuwa zimejifunga kwa kuharibika na mvua sasa zinapitika ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia 95 na kazi inaendelea. Katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 Barabara za tarafa za Nambis na Daudi zimetengewa shilingi milioni 438.8 kwa ajili ya matengenezo.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, ni haki ya wajumbe wa Bodi ya Barabara ya Mkoa na wananchi kupata taarifa za jumla za barabara zilizopangwa kujengwa katika mkoa, ikiwemo gharama za kazi ambazo wajumbe wanaweza kuzipata katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi ya Barabara ya Mkoa.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Issaay.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi kuuliza maswali madogo ya nyongeza. Kwanza niishukuru Serikali kwa sababu swali hili lilikuwa la mwezi wa Pili mwaka huu. Hivi sasa ni kweli, barabara hizo nilizozitaja zimefanyiwa matengenezo, lakini kwa kuwa, sasa fedha zinazotengwa kwa wenzetu wa *TARURA* kutengeneza hizi barabara za vijijini ni kidogo sana je, Serikali haioni umuhimu mkubwa wa kutafuta vyanzo vingine na kuhakikisha kuwa, barabara zote zinazohudumiwa na Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini, anaweza kupatiwa fedha za kutosha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, sisi wote Wabunge humu ndani ni mashahidi, maeneo mengi yanayopata makorongo makubwa katika halmashauri zetu na majimbo yetu yanahitaji mdaraja makubwa. Fedha zinazotolewa kwa wenzetu wa *TARURA* ni kidogo sana kiasi kwamba, hata kama wangepewa fedha makorongo hayo hayapo katika jiografia au mtandao wa barabara wanazohudumia wenzetu wa *TARURA.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa je, Serikali haioni ni wakati wa kuja na mpango mkakati wa kuhakikisha kuwa maeneo yote yanayohitaji madaraja makubwa ambayo ni kikwazo kwa huduma za kijamii zikiwemo kliniki za akinamama, huduma za afya na elimu zinapatiwa mpango mkakati wa kujengewa madaraja hata ya chuma? Kwa kuwa, eneo hilo ni tete na...

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Hapana, Mheshimiwa Naibu Waziri Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Kwandikwa.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ni kweli, fedha ambazo tunazipata kwa ajili ya matengenezo ya barabara nchi nzima,

ikiwemo pesa za *TANROADS* na *TARURA* ni kidogo. Sasa hivi uwezo wa fedha tunazopata ni asilimia 57 ya mahitaji. Hata hivyo niseme tu kwamba, kati ya fedha tunazozipata asilimia 90 zinakwenda kufanya matengenezo ya barabara, kwa hiyo, utaona kwamba ni asilimia 10 tu ndiyo inayokwenda kujenga barabara mpya. Kwa hiyo iko haja ya kuongeza fedha kwenye matengenezo ya barabara zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba, lile zoezi la kutambua *network* ya barabara kwa upande wa wenzetu wa *TARURA,* limefanyika, lakini kulikuwa na changamoto ya *data* ambazo zilipatikana; ikalazimika *TARURA* waende maeneo husika ili tuweze kuzitambua barabara zote ili sasa mgawo wa fedha na mahitaji ya fedha tuweze kuyaona kwa uhakika zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vigezo ambavyo vinatumika ni pamoja na urefu wa mtandao wa barabara, tunatumia vigezo pia vya aina ya barabara, kama ni barabara ya lami, barabara ya changarawe, barabara ya udongo na hali ya barabara ilivyo na idadi ya magari yanayopita katika maeneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tumejipanga na *TARURA* wanafanya kazi nzuri na ni kesho tu tunategemea taarifa itawasilishwa TAMISEMI, itawasilishwa kwenye Mfuko wa Barabara na upande wa kwetu kwenye Wizara, ili tuangalie mahitaji yetu halisi na tuweze kuomba fedha zaidi kukamilisha maeneo ambayo ni korofi. Kwa hiyo, kazi inaendelea ya kuhakikisha barabara zetu tunaziboresha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Flatei.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa, Mheshimiwa Waziri amesema fedha za *TARURA* ni kidogo na yeye amepita barabara za Mbulu, hasa Tumati kwenda Martado ni mbaya sana. Je,

atatusaidiaje kwenye kipindi hiki ili barabara zile ziweze kutengenezwa na wananchi wakaondoa ile adha ya kupita kwenye barabara ambayo haipitiki kwa sasa?

**MWENYEKITI:** Majibu kwa swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Kakunda.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tulivyoeleza katika jibu la msingi na kama ambavyo amejibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa muuliza swali la msingi, Mheshimiwa Kwandikwa Naibu Waziri wa Ujenzi; taarifa ya tathmini ile ya kina ambayo tutaipata kuanzia kesho, hiyo ndiyo itakayotupatia taarifa sahihi ya barabara zote ikiwemo barabara ile ya kwenda Tumati ambayo tulipita na Mheshimiwa Mbunge kuanzia Yaeda Chini mpaka Tumati kule barabara si nzuri sana. Kwa hiyo, tutaiwekea utaratibu mzuri sana wa kipaumbele baada ya kuwa tumekubaliana vizuri zaidi na wenzetu wa Wizara ya Ujenzi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Haonga.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Tatizo la barabara katika Halmashauri ya Mji wa Mbulu linafanana kabisa na tatizo la barabara katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mlowo katika Jimbo la Mbozi. Naomba kuuliza, ni lini sasa Serikali itatengeneza barabara ambazo zipo katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mlowo, Jimbo la Mbozi, ambazo wakati wa mvua mara nyingi zimekuwa hazipitiki?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Jibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Kakunda.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli. Tatizo alilolisema Mheshimiwa Mbunge katika eneo lake ni tatizo ambalo limekuwa likiikabili nchi

nzima wakati wa masika wakati mvua kubwa zikinyesha, hasa barabara zetu ambazo huwa zinaathirika sana ni barabara za udongo na barabara za changarawe, ukiacha barabara za lami ambazo maeneo machache, hasa ya madaraja ndio huwa yanaathirika zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nimpe ndugu yangu *comfort* kwamba, suala hilo linatambulika Serikalini. Katika tathmini ambayo tunaifanya tumezingatia hilo ili tuwe na *backup* ya kutosha wakati wa mvua kuweza kukabiliana na changamoto ambazo huwa zinajitokeza wakati wa masika.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Kiula.

**MHE. ALLAN J. KIULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa, wananchi wa Yulansoni, Lelembo hadi Kitumbili ni wazalishaji wakubwa na barabara hiyo haimo kabisa kwenye mtandao na *TARURA* haiwezi kutengeneza na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI alishatembelea huko na kutoa ahadi ya kutafuta pesa ili barabara hiyo itengenezwe. Je, ni lini barabara hiyo itatengenezwa?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Kakunda.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kiula, Mbunge wa Iramba Mashariki ambako tunaita maarufu Mkalama, lakini wenyewe tu hawajaleta ombi la kubadilisha jina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kwamba, kuna changamoto kubwa sana katika eneo hilo lote la Mkalama. Wiki mbili zijazo nitatembelea Mkalama, tutapita mpaka hiyo barabara anayoitaja. Hata hivyo,

kwa hali halisi nitoe tu *comfort* kwa Bunge lako Tukufu na Wabunge wote, kwamba wenzetu Wahandisi, taaluma yao ni ya kuaminika kwa sababu wanajenga vitu vya kuonekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa si kwamba tunadharau taaluma nyingine, ila ni kwa sababu wanajenga vitu ambavyo vinaonekana. Kwa hiyo ili kusudi wafanye kazi zao vizuri, mazingira ambayo tunayaandaa kupitia tathmini ambayo tumeifanya ni kuhakikisha kwamba, tunaweka mazingira mazuri ili kazi zao watakazozifanya ziweze kuonekana vizuri zaidi kwa wananchi.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Lubeleje.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Chombo cha *TARURA* ni kipya na kilipoandaliwa kilipewa fedha ndogo; na kwa kuwa fedha iliyotengwa na Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa Jafo, anazifahamu sana barabara za Mpwapwa, barabara za mjini na barabara za Mima; je, *TARURA* iko tayari kuongezwa fedha ili zile barabara za Mpwapwa Mjini na Mima ziweze kutengenezwa?

**MWENYEKITI:** *TARURA* iko tayari kuongezwa fedha? Haya, Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli, kwanza katika sehemu ya kwanza ya swali lake, maana kauliza kama maswali mawili; ni kwamba *TARURA* iko tayari kuongezwa fedha, hiyo, niseme wazi. Pia jambo la msingi la pili ni kwamba tunajua mazingira yote katika Tarafa ya Mpwapwa na Tarafa ya Mima kwa sababu, aliuliza swali la msingi hapa na katika swali la

msingi tukamuahidi kwamba, tutatuma wataalam. Wataalam wamekwenda kule wakiwemo Wahandisi walioko kwenye jimbo lake, wamefanya tathmini na wametuletea ofisini, hivyo, tutaifanyia kazi katika mwaka ujao wa fedha.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali linalofuata kwa Ofisi hiyo hiyo ya Rais, TAMISEMI, ambalo linaulizwa na Mheshimiwa Joel Mwaka Makanyaga, Mbunge wa Chilonwa.

Na. 506

**Barabara Inayounganisha Kata ya Haneti na Kata ya Segala**

**MHE. JOEL M. MAKANYAGA** aliuliza:-

Barabara inayounganisha Kata ya Haneti na Kata ya Segala kupitia Kata ya Zajilwa ni muhimu sana kwa kufungua mawasiliano katika kata hizo tatu:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kuwa barabara hiyo, inatengenezwa kwa kiwango cha kupitika muda wote kwa mwaka?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joel Mwaka Makanyaga, Mbunge wa Chilonwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha, 2017/2018 Serikali ilitenga na ilitoa fedha zote shilingi milioni 132.1 ambazo zimetumika kufanya matengenezo, si tu kwenye barabara aliyoitaja Mheshimiwa Mbunge bali barabara ndefu zaidi ya kutoka Segala – Zajilwa –

Haneti – hadi Umoja yenye urefu wa kilometa 80. Barabara hiyo, imekamilika na sasa inapitika muda wote wa mwaka.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Makanyaga.

**MHE. JOEL M. MAKANYAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nichukue nafasi hii kushukuru kwa jibu zuri, fupi, linaloeleweka la Mheshimiwa Naibu Waziri. Hata hivyo, kwa maana ya uelewa wa pamoja nimwombe Mheshimiwa Naibu Waziri tuondoke pamoja twende tukatembelee hii barabara kutoka Zajilwa – Gongolo – Umoja hadi Izava, lakini pia na barabara kutoka Zajilwa hadi Itiso tuone, tushauriane tuone jinsi barabara ilivyo. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ni ushauri tu, una-*confirm?* Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba, ombi alilotoa Mheshimiwa Joel Mwaka Makanyaga tutalitekeleza.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Ritta Kabati.

**MHE. RITA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi, ili niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa katika Manispaa yetu ya Iringa kuna Daraja la Igumbiro, daraja ambalo limekuwa likileta maafa kila mwaka na ambalo limechukua muda mrefu sana kumalizika. Je, ni lini sasa Serikali itatoa pesa ili Daraja lile la Tagamenda liweze kukamilika?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maeneo ambayo tunafanya uwekezaji mkubwa wa

miundombinu ni pamoja na Manispaa ya Iringa. Serikali ya Chama cha Mapinduzi imeamua kuboresha miundombinu katika Manispaa hiyo ya Iringa na hivi sasa tumekamilisha barabara kadhaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Ritta Kabati kwamba wataalam wangu wataenda kufanya tathmini katika eneo hilo ambalo limebakia linaonekana lina changamoto. Lengo letu kubwa ni ili tuhakikishe kama hiyo kazi ina upungufu wa aina yoyote tuweze kuurekebisha ili wananchi wa Iringa wawe katika mazingira mazuri ya kuweza kusafiri.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Jerome Bwanausi.

**MHE. JEROME D. BWANAUSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Suala la kupitika barabara ni suala muhimu sana kwa ajili ya uchumi na maendeleo ya wananchi; na kwa kuwa, Madaraja ya Mipande, Mtengula, Chawara hadi kule Buyuni, lakini pia Daraja la Mwitika Maparawe ni madaraja ambayo yamezolewa na mafuriko kutokana na mvua kubwa. Je, nini kauli ya Wizara ya TAMISEMI katika kuhakikisha madaraja haya yanarudishwa ili kuwe na mawasiliano ya usafiri?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Bwanausi, kwanza kwa kufuatilia madaraja hayo, kwa sababu nikiri wazi kwamba alifika ofisini kwangu na nilimwelekeza aende akakutane na Mkurugenzi wetu wa Barabara Vijijini, Ndugu Digaga na amefanya hivyo. Ofisi yangu sasa hivi wanakwenda kufanya tathmini ya kina ya nini kifanyike kwa sababu wananchi wa eneo hilo wamekwama sana katika suala la usafiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kama alivyofika kwangu

na kama nilivyomwelekeza kufika *TARURA,* ofisi yetu italifanyia kazi kwa nguvu zote eno hilo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Martha Umbulla.

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona. Ni azma ya Serikali kuunganisha Makao Makuu ya Mikoa na Wilaya mbalimbali. Mkoa wetu wa Manyara ambao una Makao Makuu Babati hakuna barabara ya lami inayounganisha Wilaya za Kiteto na Simanjiro na nyakati zingine hazipitiki kutokana na hali mbaya ya barabara hizo kuwa za vumbi na kwa kuwa iko kwenye Ilani kwa muda mrefu. Je, ni lini Serikali sasa itaunganisha barabara kutoka Simanjiro na Kibaya kuja Babati kwa kiwango cha lami?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Kakunda.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nilihakikishie Bunge Tukufu kwamba utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi unaendelea ambayo imeelekeza ujenzi wa barabara hizo kwa kiwango cha lami; na hasa hasa nikitaja barabara ambayo inatoka Kilindi inapita Kiteto inakuja mpaka Dodoma huku Kondoa ambayo ni barabara kumbwa sana itaanza kutengenezwa hivi karibuni chini ya usimamizi wa Wizara ya Ujenzi. Hii barabara ya kutoka Babati kwenda mpaka Simanjiro na ile aliyoitaja nyingine tunaziangalia kwa karibu sana na ndiyo maana matengenezo yake huwa ni ya uangalizi wa juu kabisa chini ya usimamizi ya Mkuu wa Mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usimamizi wake umepelekea barabara hizo kuimarika na kwa sasa zinapitika muda wote wa mwaka isipokuwa matengenezo madogo madogo kama kuna mvua kubwa sana. Kwa hiyo nimhakikishie kwamba utekelezaji utafanyika, naomba tu wananchi wawe na subira.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Willy Qambalo.

**MHE. QAMBALO W. QULWI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kata za Rhotia na Mbulumbulu Wilayani Karatu ni maarufu sana kwa uzalishaji wa mazao ya chakula. Hata hivyo barabara za kuelekea kwenye kata hizo zinazounganisha Makao Makuu ya Wilaya ya Karatu zina hali mbaya sana kwa kukosa matangenezo ya mara kwa mara lakini pia kutokana na mvua zilizonyesha mwaka huu; je, ni nini kauli za Serikali kwa Meneja wa *TARURA* Mkoa ili barabara hizo ziweze kutengenezwa ili wananchi waweze kufika kwenye masoko?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, jibu kwa swali hilo kwa kifupi tu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nimpongeze kaka yangu Mbunge wa Karatu. Kubwa zaidi ni kwamba maelekezo yetu si kwa Meneja wa *TARURA* wa Mkoa wa Arusha peke yake, isipokuwa ni maelekezo yetu kwa Mameneja wa *TARURA* wote katika mikoa yote 26, kwamba wafanye *needs assessment* ya barabara zetu zote zilizoharibika. Lengo letu kubwa ni kwamba kile kichache tutakachokuwa nacho kwa ajili ya ukarabati tuweze kurekebisha maeneo hayo. Kwa hiyo ni maelekezo yangu kwa meneja wa *TARURA* wa Mkoa wa Arusha na hali kadhalika Mkoa wa Babati, Wilaya ya Karatu wafanye hivyo haraka iwezekanavyo watupe taarifa.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kuniona. Barabara zote zilizozunguka Mlima Hanang kutokana na mvua kutoka Gendabi, Hatgabadau, Katesh, Gitting, Gerodom na Gendabi zote zimeharibika. Naamini kwamba zitakuwa zimeoneshwa kwenye *needs assessment.* Je, Mheshimiwa Waziri anasemaje kwa sababu kuna makorongo makubwa yanayozuia akinamama kwenda hospitali na watoto kwenda shuleni?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Kakunda, kwa kifupi tu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):**Mheshimiwa Mwenyekiti, mazingira ya Mikoa hii ya Manyara na Arusha yanafahamika, hasa maji yanapoporomoka kutoka kwenye milima yana tabia ya kuharibu barabara kwa haraka sana. Kwa hali hiyo, kama ambavyo Mheshimiwa Waziri wangu amewaagiza Mameneja wa *TARURA* wote kufanya tathmini ya kina ili maeneo yale yaweze kupata uhakikisho maalum wa matengenezo ambayo yatahakikisha kwamba hayo maji hayaharibu kwa haraka barabara zetu katika maeneo hayo kama ambavyo imekuwa ikitokea. Napenda kumwahidi Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu kwamba tutalifuatilia utekelezaji wa agizo hilo kikamilifu ili maeneo hayo ili tuweze kuyapa kipaumbele kinachotakiwa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Gekul, hapana Mheshimiwa Lyimo.

**MHE. SUSAN A. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Barabara ya Kimara - Bahama Mama - Msewe kwenda Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ilijengwa ili kuondoa msongamano katika Barabara ya Morogoro. Sasa magari haya yanapita Chuo Kikuu na Chuo Kikuu barabara imeharibika sana. Je, ni lini Serikali itajenga barabara ile ya Chuo Kikuu kutoka Msewe kuelekea jengo la Utawala ili kufanya mandhari ya Chuo Kikuu iwe nzuri kwa sababu kwa kweli barabara hiyo imeharibu sana barabara za Chuo Kikuu?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Kakunda.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli barabara aliyoitaja ni muhimu sana

katika kupunguza msongamano wa magari katika Barabara ya Morogoro hasa kwa watu wanaokwenda maeneo ya *City Centre*. Hata hivyo, barabara ile ina changamoto ya ufinyu wake. Kama inatakiwa kutengenezwa vizuri basi inatakiwa fidia kubwa sana ilipwe kwa wananchi ambao wamejenga mpaka karibu na barabara, hasa kuanzia Kimara kuja kupita maeneo ya milima ya Golani, kuja kuteremsha chini kwenye daraja hapo kuna uvamizi mkubwa sana ambao ulifanywa na wananchi, barabara ile ni finyu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo matengenezo yake yanahitaji tathimini ya kina ambayo itaishauri Serikali namna ya kuiendeleza hiyo barabara. Naomba sana kwa sasa hivi matengenezo madogo madogo ambayo yanafanyika wananchi watuvumilie yaendelee hiyo hivyo mpaka ambapo tathmini ya kina itakapokamilika.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea. Swali linalofuata linaulizwa na Mhe. Dkt. Dalaly Peter Kafumu Mbunge wa Igunga na linaulizwa kwa Mheshimiwa Waziri wa Madini.

Na. 507

**Kupungua kwa Wawekezaji kwenye Madini**

**MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU** aliuliza:-

Wawekezaji wanaotaka kuja kuwekeza kwenye Sekta ya Nishati na Madini wamepungua sana katika kipindi cha miaka mitano iliyopita:-

(a) Je, ni nini kimesababisha hali hiyo?

(b) Je, Serikali inachukua hatua gani kuhakikisha kuwa Wawekezaji wanaendelea kuja ili kukuza uwekezaji kutoka nje *(Foreign Direct Investment] (FDI)?*

**NAIBU WAZIRI WA MADINI (MHE. STANSLAUS H. NYONGO)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Dalaly Peter Kafumu, Mbunge wa Igunga, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, vichocheo vikuu vitatu vya uwekezaji katika Sekta ya Madini katika nchi yoyote, cha kwanza ni jiolojia inayoashiria uwezekano wa uwepo wa madini (*prospective geology*). Pili ni mwenendo wa bei ya madini husika kwenye Soko la Dunia na tatu Sera za Uchumi Mkuu (*Macroeconomics*) za nchi husika. Ilani ya CCM tunayoitekeleza hivi sasa ilizingatia vigezo hivi kwa kuhimiza kujenga uwezo wa *Geological Survey of Tanzania* ili waweze kugundua mashapo ya madini, kupunguza gharama za uzalishaji kwa kuboresha miundombinu na kuongeza thamani ya madini ili yawe na bei nzuri kwenye soko la dunia na kubadili Sheria ya Madini ili kuongeza uwazi na manufaa kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipindi cha miaka mitano nchi yetu imeendelea kupokea wawekezaji kwenye sekta ya madini. Jumla ya leseni 102 za uchimbaji mkubwa (*Special Mining Lenience)* na wa kati *(Mining License*) zimetoelewa kati ya mwaka 2012/2013 hadi 2016/2017, ikiwa ni wastani wa leseni 20 kwa mwaka. Aidha, mwaka wa fedha 2012/2013 hadi 2016/2017 leseni 3,136 za utafutaji wa Madini *(Prospecting License*) zilitolewa, hii ikiwa ni wastani wa leseni 627 kwa mwaka. Mwaka 2017/2018, tumepokea maombi 26 ya *Special Mining License* na *Mining License*, yaani uchimbaji wa kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tumepokea maombi 818 ya leseni za utafiti wa madini (*Prospecting License*). Tume ya Madini iliyoundwa hivi karibuni inaendelea kupitia maombi hayo na iwapo yatabainika kukidhi vigezo vya kisheria leseni hizi zitatolewa na hivyo kuendelea kuchangia kuongezeka kwa *Foreign Direct Investment* (*FDI).* Kwa takwimu hizi, bado

wawekezaji wanaonesha nia ya dhati kuwekeza nchini kwani nchi yetu inakidhi sifa tatu nilizoainisha hapo awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kuchukua hatua za makusudi kuandaa mazingira rafiki ya kuvutia wawekezaji na kutangaza fursa zilizopo nchini. Hatua zinazochukuliwa ni pamoja na kuimarisha miundombinu wezeshi kama vile ujenzi wa barabara, reli, kupanua bandari, kujenga miundombinu, maji, umeme, gesi na mawasiliano kuelekea maeneo yanayotazamiwa kuanzishwa migodi. Aidha, Serikali imeendelea kuimarisha uwezo wa Wakala wa Jiolojia Tanzania *(GST)* kwa kuwapatia wataalam vitendea kazi ili kuwawezesha kuongeza kasi ya kufanya tafiti za kina za maeneo yenye madini nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Dkt. Kafumu.

**MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pia namshukuru sana Naibu Waziri kwa majibu yake. Hata hivyo, niseme tu kwamba swali langu la msingi ni nini kimesababisha kupungua kwa shughuli za utafutaji wa madini, mafuta na gesi kwenye nchi yetu halijajibiwa na hilo ndilo swali langu la kwanza la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili la nyongeza ni kwamba, mwaka jana tulitunga sheria nzuri za kulinda rasilimali za uziduaji, yaani madini, gesi na mafuta ambazo ni "*The Natural Wealth and Resources (Permanent Sovereignty) Act, 2017"; The Natural Wealth and Resources Contracts (Review and Re-Negotiation of Unconscionable Terms) Act, 2017;* na ile Sheria ya Madini ilirekebishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu; sheria hizi ni nzuri sana, lakini zimesababisha changamoto kadhaa ambazo zimefanya kupungua kwa shughuli za uwekezaji, ikiwa ni pamoja na kuwekwa kwa asilimia 25 ya *retention* kwa wachimbaji wadogo wanapotaka kuuza madini. Kodi hiyo

inawafanya wachimbaji wadogo washindwe kufanya biashara ya wazi. Je, ni lini Serikali itachukua hatua kurekebisha changamoto hizi ili kuhamasisha uwekezaji katika Sekta ya Madini na Mafuta? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI (MHE. STANSLAUS H. NYONGO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika majibu yangu ya msingi nimejaribu kuelezea ni jinsi gani wawekezaji wanavyozidi kuongezeka kuomba leseni za kufanya tafiti pamoja na leseni za uchimbaji mkubwa na uchimbaji wa kati, vile vile wakiwepo wachimbaji wadogo. Ongezeko hili limezidi na hii inaonesha dhahiri kwamba bado wawekezaji wanazidi kuja kutaka kuwekeza kwenye nchi yetu. Hii ikiwa ni pamoja na mabadiliko ya sheria ambayo tuliyopitisha katika Bunge lako Tukufu mwaka jana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile mabadiliko yale ya sheria yalikuwa ni kwa ajili ya kulinda rasilimali za nchi yetu. Hata hivyo, tunaendelea kuboresha na kuna kanuni ambazo tumezitoa mwaka huu wa 2018 ambazo kwa kweli wawekezaji wengi walisubiri kuangalia zile kanuni zinakwendaje. Baada ya kuzitoa zile kanuni wengi wamezipitia, wameziona na wengi wameona kwamba wana uwezo wa ku-*comply,* yaani wana uwezo wa kuendana na zile kanuni na sheria kadri tulivyoweza kuibadilisha. Kwa hiyo wawekezaji wanaendelea kuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile tunaendelea kuwawezesha *GST* waweze kufanya tafiti za kina, waweze kufanya tafiti hadi kufanya zile *resource estimation,* kwa maana ya kuangalia *resources* tulizonazo ili baadaye tuwe na uwezo wa kuifanya *GST* iweze kuuza leseni kwa njia ya mnada. Ili wawekezaji wanapokuja wawe wanakuja kwa nia ya kuchimba tu, ili tuwaondoe katika ile nia ya kutaka kuja kukwekeza kwa maana ya utafutaji wa madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ule utafutaji wengine unawafanya wasite kuja. Hata ukiangalia dunia nzima siyo Tanzania tu uwekezaji katika kutafuta madini umepungua kidogo. Kwa hiyo sisi kama Serikali inabidi tujiongeze kuangalia namna ya kufanya *resource estimation*, kuangalia kwa kina ili mwekezaji anapokuja aje kuwekeza kwa maana ya kuchimba tu si kutafuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cecil David Mwambe.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza ambalo linaelekezwa kwenye Wizara ya Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti na Mheshimiwa Naibu Waziri mtakumbuka kwamba miaka ya karibuni pamefanyika ugunduzi wa madini ya aina ya *graphite* kwenye Wilaya ya Masasi, Kijiji cha Chiwata, Kata ya Chiwata, vile vile Wilaya ya Ruangwa na vijiji vyake; ikiwemo baadhi ya maeneo ya Jimbo la Mtama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa swali langu, Kampuni ya *Nachi Resources* ndiyo ambao ilionesha nia ya kutaka kuwekeza, lakini mawasiliano ya mwisho tuliyoyafanya na wao yalionyesha kwamba hawawezi kuwekeza kwenye hayo maeneo kwa sababu pamekuwa na ucheleweshaji wa upatikanaji wa ripoti ya *environmental assessment.* Sasa Mheshimiwa Waziri, haoni haja ya kuwasaidia Nachi ili kuweza kukamilisha huu utaratibu ili waweze kuchimba hayo madini?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa swali hilo. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini, kwa kifupi tu.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI (MHE. STANSLAUS H. NYONGO)** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli *Nachi Resources* ni kwamba wanasubiri kupata ripoti kutoka Ofisi ya Makamu

wa Rais (Mazingira) ambayo iko chini ya Mheshimiwa Makamu wa Rais. Sisi hatuna shida kwa upande wa Wizara ya Madini, ni kwamba wale tunaendelea kuwasaidia ili waweze kuwekeza, kwa sababu tunafahamu uchimbaji wa *graphite* sasa hivi duniani ndiyo unahitajika kwa sababu madini ya *graphite* sasa hivi ndiyo yanayohitajika zaidi duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo sisi kama Wizara ya Madini tunashirikiana nao kuhakikisha kwamba baada ya muda waweze kuanza kuwekeza na kuanza kuchimba. Kwa hiyo, nimweleze Mheshimiwa Mbunge kwamba tunashirikiana nao na tunaendelea kuwasiliana na Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) ili iwawezeshe kupata *environment impact assessment report* ili kusudi waweze kuwekeza na waweze kuendeleza shughuli zao za uchimbaji kama kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI**: Ahsante Mheshimiwa**.** Shally Josepha Raymond

**MHE.SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona. Mkoani Kilimanjaro, Wilaya ya Same, Kata ya Makanya yanapatikana madini ya *gypsum*, madini hayo Tanzania nzima yanapatikana Manyoni, Pindilo na Makanya kwenyewe. Hata hivyo, miundombinu ya hapa ni mibaya sana na wachimbaji hao ni wachimbaji wakiwemo akinamama na akinababa. Je, Serikali ina mpango gani kuwasaidia wachimbaji hao wakati tunapoelekea kwenye Sera ya Viwanda na Biashara?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa swali hilo, kwa kifupi Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI (MHE. STANSLAUS H. NYONGO)** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi kama Serikali

tunazidi kuhakikisha kwamba wachimbaji wadogo tunawawezesha kimiundombinu, kimitaji na kuwasaidia kiteknolojia ili waweze kuchimba na waweze kujipatia kipato chao. Ni kweli kabisa hayo madini ya *gypsum* ni madini ambayo ni muhimu na yahahitajika katika soko la dunia na baadhi ya nchi za jirani wanahitaji madini hayo na kwa ajili ya ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Serikali pamoja na kupitisha sheria ile ya mwaka jana ya Marekebisho ya Sheria ya Madini tumetaka kwamba madini yote ya *gypsum* tuweze kuwasaidia wachimbaji waweze kuchimba na kuya-*process* ili kusudi wapeleke kwenye soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo sisi pamoja na Wizara nyingine tunasaidiana kupeleka miundombinu kwa maana ya maji, umeme, barabara kwa wachimbaji wadogo dogo ili waweze kuchimba vizuri na kwa gharama ndogo ili waweze kupata faida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Fatma Toufiq.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa maeneo ya uchimbaji madini *(mining sites)* katika Mkoa wa Dodoma yako zaidi ya 700 na kuna baadhi ya maeneo hayajaanza kuchimbwa kabisa madini. Je, Serikali ina mkakati gani wa kutangaza kwa wawekezaji ili kusudi waweze kuja kuchimba katika Mkoa wa Dodoma?

**MWENYEKITI:** Ahsante. *Promotion* ya Mkoa wa Dodoma, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI (MHE. STANSLAUS H. NYONGO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyojibu katika

jibu langu la msingi, tuna maombi mengi sana ambayo wachimbaji wadogo na wakubwa wameomba katika Wizara yetu kupitia Tume ya Madini. Hapa Dodoma kuna wachimbaji wadogo wadogo wengi wameomba leseni hizo, kwa maana ya kwamba wanataka au wameonesha nia ya kuchimba. Sisi kama Serikali hivi karibuni ile Tume imeshaanza kufanya kazi na zile leseni tutazitoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema toka mwanzo kwamba tunataka tuwawezeshe wachimbaji wadogo. Mradi katika Wizara yetu ambao ni mradi unaopata fedha kutoka *Word Bank*, yaani Mradi wa *SMRP;* mradi huu tunaangalia namna bora sasa ya kuwawezesha wachimbaji wadogo, kwa maana ya kuwasaidia kuwapa teknolojia, elimu na mitaji ili waweze kuchimba. Pia wachimbaji wa Mkoa wa Dodoma na wao wamo kwa sababu sisi tunafanya kazi nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kwa wachimbaji wadogo ambao wako katika Mkoa wa Dodoma, nipende tu kusema, walioonesha nia au walioomba maombi ya leseni, leseni zitatoka na wachimbaji ambao wanataka kuomba leseni sasa hivi Tume imeanza kufanya kazi walete maombi hayo katika Wizara yetu, tuweze kuwapa leseni, na tuangalie namna ya kuwasaidia ili waweze kuchimba na Wizara iko tayari na tunaendelea na kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sophia Mwakagenda.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa kuwa mgodi wa Kiwira, umesimama kwa muda mrefu, je Serikali ina mpango gani ya kutafuta Wawekezaji ambao wanaweza kufufua mgodi ule ambao miundombinu yake inakufa?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa kifupi kwa swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI (MHE. STANSLAUS H. NYONGO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli, Mgodi wa Kiwira sisi kama Serikali tumejipanga kuangalia ni namna gani ya kuwezesha mgodi huo uweze kufanya kazi. Niseme tu kwamba tunashirikiana na Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kuangalia namna sasa ya kuzuia au kuangalia namna ya kuweza kuondoa zile changamoto zilizopo katika mradi wa Kiwira, ili uchimbaji ule wa Makaa uweze kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wawekezaji wengi wameonesha nia ya kutaka kushiriki katika kuchimba Mgodi huo wa Kiwira. Sisi kama Wizara, kwa kweli hatuna shida yoyote, tunahakikisha kwamba ikiwezekana mwaka huu, mgodi huo upate fedha na watu waweze kuchimba na vile vile tutafute wawekezaji wengine ambao wanaonesha nia ya kuwekeza pale, tushirikiane nao kuhakikisha kwamba Mgodi wa Kiwira unaanza kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Laizer Kalanga.

**MHE. JULIUS K. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Madini ya rubi yanayopatikana katika Wilaya ya Longido kule Mundarara, biashara yake imedorora kwa sababu mpaka sasa Serikali haikutoa utaratibu wa kuendesha biashara ya madini hayo. Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi yake ya kuleta mchakato mzima wa kusimamia na kuendesha biashara ya madini yale?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Jibu kwa swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini, Mheshimiwa Nyongo.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI (MHE. STANSLAUS H. NYONGO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli madini ya rubi yanapatikana kule Mundarara, Mkoani Arusha. Madini yale

ni pamoja na madini mengine. Baada ya mabadiliko ya Sheria 2010, tulizuia kutoa madini ghafi nchini. Tunataka madini yote yapitie kwenye uongezwaji wa thamani ili yaongezwe thamani kwa ajili ya kutengeneza ajira kwa wananchi lakini na vile vile kuisaidia nchi kupata kipato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa hivi ni kwamba madini yale, baada ya zuio hilo, imeonekana kwamba imeshindikana kwa wale waliokuwa wanatoa madini ghafi. Sasa hivi sisi kama Serikali tunaangalia utaratibu wa kuhakikisha kwamba tunawakaribisha wawekezaji, na wako wawekezaji ambao wameonesha nia, ya kuja kuyaongezea thamani madini ya rubi ili kusudi sasa yawe yanauzwa katika hali ambayo yameshaongezwa thamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii itawasaidia watu wa Mundarara na wachimbaji wote wengine kwa maana kwamba watakuwa sasa wanapata soko la uhakika kuuza ndani lakini vile vile madini hayo tutayatoa nje, yakiwa tayari yameshaongezewa thamani. Hii itasaidia kwa wawekezaji wa ndani wenyewe, lakini vile vile kama Serikali, itazidi kupata kipato kwa maana kwamba tutapata kodi na mrabaha katika madini ambayo yameongezewa thamani.

Kwa hiyo Mheshimiwa Mbunge kuwa tayari tu kwamba tunaendelea ...

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Yusuff.

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kuna malalamiko makubwa kutoka kwa utatu wa uwekezaji katika maeneo yote ya uwekezaji, kwa maana ya jamii, Serikali, pamoja na mwekezaji mwenyewe, kila mmoja akilalamikia kwamba hapati stahiki zake. Je, ni lini Serikali itakaa pamoja sasa kuuweka utatu huu, kwa maana ya Serikali, jamii na mwekezaji na kuweka mazingira sawia ambayo kila mmoja atampa haki yake kuwe hakuna malalamiko katika uwekezaji kabla ya mwekezaji hajapewa kibali cha kuwekeza?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Kwa kifupi tu Mheshimiwa Naibu Waziri Wizara ya Madini, Mheshimiwa Nyongo.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI (MHE. STANSLAUS H. NYONGO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais mwaka jana alivyoanzisha Wizara Maalum kwa ajili ya Madini, kwa sababu zamani ilikuwa ni Wizara ya Nishati na Madini, lakini mwaka jana mwezi wa Kumi Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli alianzisha Wizara Maalum inayoshughulikia Madini baada ya kuona umuhimu wa kuanzishwa Wizara hii. Kwa kweli tangu Wizara imeanzishwa, sisi tumeanza pale, tumeanza kukaa na wawekezaji, wawekezaji wa kati, wawekezaji wadogo na wawekezaji wakubwa, kuangalia changamoto walizonazo, kuangalia namna bora ya kuweka mazingira ya uwekezaji ili kila mwekezaji aondoke katika kulalamika kutokana na vikwazo anavyovipata katika kuwekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo sisi kama Wizara tuna mikakati mizuri katika kuhakikisha kwamba wawekezaji wanaokuja wanawekeza vizuri na wanawekeza bila vikwazo. Sasa hivi kuna wengine wamelalamikia kuhusu kodi, nao tumewaambia walete malalamiko yao tuyaangalie. Kwa mfano wawekezaji wa chumvi, kulikuwa kuna kodi 16, katika Bajeti hii zimeondolewa kodi 10.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni moja au kiashiria kimoja cha kuona kwamba Wizara inafanya kazi ya kuwasikiliza wawekezaji na wachimbaji kwa nchi nzima na kuangalia namna bora ya kuwaondolea vikwazo ili waweze kuwekeza na waweze kuchimba kwa faida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali linalofuta ambalo linaulizwa na Mheshimiwa Rehema Juma Migilla, Mbunge wa Viti Maalum, linaulizwa kwa Mheshimiwa Waziri wa Kilimo.

Na. 508

**Kuboresha Kilimo cha Tumbaku**

**MHE. REHEMA J. MIGILLA** aliuliza:-

Tumbaku inayolimwa Mkoani Tabora inachangia pato kubwa la Taifa:-

Je, Serikali ipo tayari kuboresha mazingira ya kilimo hicho ili kisiathiri mazingira?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Rehema Juma Migilla, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, zao la tumbaku hulimwa katika Mikoa 11 ambayo ni Tabora, Kigoma, Katavi, Singida, Shinyanga, Mbeya, Ruvuma, Iringa, Mara, Songwe na Morogoro. Uzalishaji wa zao hili husimamiwa na Serikali kupitia Bodi ya Tumbaku Tanzania na kwa kufuata taratibu na kanuni za kilimo kinachojali hifadhi ya mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Tabora unazalisha tumbaku nyingi zaidi kuliko mikoa mingine inayozalisha tumbaku hapa nchini, na hivyo kuchangia sehemu kubwa ya Pato la Taifa. Aidha, katika msimu wa 2015/2016 Mkoa wa Tabora pekee ulizalisha asilimia 47 ya tumbaku yote iliyozalishwa nchini na asilimia 48 kwa ule msimu wa mwaka 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Bodi ya Tumbaku Tanzania inasimamia taratibu na kanuni zote ambazo zinahamasisha kilimo bora cha tumbaku na kinachozingatia hifadhi ya mazingira. Pamoja na mambo mengine, Kanuni zinaelekeza kila mkulima wa tumbaku asajiliwe na awe na eneo la kupanda miti isiyopungua 250 au zaidi kwa kila hekta moja ya tumbaku anayolima.

Miti inayopandwa pamoja na kuwa chanzo cha nishati ya kukausha tumbaku pia husaidia kuhifadhi mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi ya Tumbaku Tanzania imeendelea kuhamasisha na kusimamia ubadilishaji wa mabani ya kukaushia tumbaku kutoka ya awali yanayotumia magogo ya miti na kutumia mabani ya kisasa ambayo yameongezeka kutoka mabani 101,982 mwaka 2014/2015 na kufikia mabani 172,405 mwaka 2016/2017. Aidha, mabani ya zamani yamepungua kutoka mabani 192,975 mwaka 2014/2015 hadi mabani 135,410 mwaka 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati wa Serikali ni kuhamasisha wakulima wote wa tumbaku nchini kutumia mabani ya kisasa kuanzia msimu wa mwaka 2018/2019 ikiwa ni pamoja na kuendeleza juhudi za kutafuta nishati mbadala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Rehema.

**MHE. REHEMA J. MIGILLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi ya kuongeza swali dogo la nyongeza. Kwanza napenda nimpongeze Naibu Waziri wa majibu yake mazuri, lakini nina maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumbaku kwa Mkoa wa Tabora na mikoa mingine inayolima tumbaku, tumbaku ni maisha, tumbaku ni uchumi, lakini tumbaku ni maisha yetu. Napenda kuuliza swali la nyongeza kama ifuatavyo. Kwa kuwa kasi ya upandaji wa miti haiendani sambamba na upandaji na tunaona kabisa zoezi hili limefeli, nataka niulize Serikali, ina mpango gani kwa sasa kuzihakikishia hizi *AMCOS* ambazo zina jukumu la upandaji wa miti ili ziweze kutimiza Sheria ya Namba 24 ya mwaka 2001, ambayo inaitaka kila *AMCOS* kabla ya kusajiliwa iwe na shamba la miti ambayo itawatosha idadi ya wakulima wake kwa mwaka mzima?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, napenda kufahamu; kwa kuwa Bodi ya Tumbaku ndiyo yenye jukumu la kusimamia na kuratibu shughuli zote za tumbaku ikiwa ni sambamba na uhifadhi wa mazingira inashindwa kutekeleza majukumu yake kutokana na changamoto mbalimbali, je, Serikali ina mpango gani wa kuiwezesha hii Bodi ya Tumbaku kuondokana na changamoto za magari, nyumba na ofisi za wafanyakazi ili iweze kufanya kazi kwa uhakika?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Dkt. Mary Mwanjelwa.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naomba nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Mbunge ambaye ninaamini kabisa na yeye ni mkulima wa zao la tumbaku kule Tabora na amekuwa akilima hiyo tumbaku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika maswali yake mawili ya nyongeza, kuhusu suala *AMCOS* na wakulima ni kwamba sisi kwenye ile *Tobacco Industrial Act. No. 24* ya Mwaka 2001 wakulima wetu wote pamoja na hizo *AMCOS* na mambo mengine ambayo yanaelezea katika Sheria hiyo Namba 24 ya Mwaka 2001, ni kuhakikisha kwamba, wakulima wote pamoja na hizo *AMCOS* wanaposajiliwa kuhakikisha kwamba mashamba yao yanaendana na miti isiyopungua 250. Vile vile kuhakikisha kabisa kwamba wanatumia yale mabani ya kisasa na si yale mabani ya zamani ambayo yalikuwa yanatumia magogo kama ilivyokuwa kule mwanzo. Hii yote ni katika kuhakikisha kwamba, tunatunza na kulinda hifadhi ya mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali lake la pili la nyongeza, kuhusu Bodi yetu ya Tumbaku; ni kweli sisi kama Serikali tunahakikisha kabisa kwamba tunaimarisha na tunaboresha hizi bodi zetu zote. Naomba niziase bodi zetu zote kwamba zifanye kazi kwa umahiri na kwa ubunifu zaidi, na vile vile waweze kushirikiana na wadau mbalimbali kuhakikisha kwamba wanatumia zile fursa mbalimbali za kilimo zilizopo katika kuboresha mazao yao, ahsante.

**MWENYEKITI:** ahsante Mheshimiwa Almas Maige.

**MHE. ALMAS A. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru sana na mimi niulize swali moja dogo la nyongeza kuhusu suala la tumbaku. Tumbaku ndiyo siasa na ndio uchumi wa Mkoa wetu wa Tabora. Tatizo kubwa ni masoko, mwaka jana hapa mpaka tukapewa majina ya wazee wa tumbaku na akinamama wa tumbaku, sisi Wabunge wa Tabora. Swali, je, Serikali imefanya nini ili kutafuta masoko mengine ya tumbaku ili sisi tuuze tumbaku yetu?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Jibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Dkt. Mary Mwanjelwa kwa kifupi tu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii hata yeye Mheshimiwa Mbunge pia kumpongeza; kama alivyosema kwamba ni kweli tumbaku ni maisha kwa wananchi wote wa Mkoa wa Tabora na maeneo yote yanayolima tumbaku. Hata hivyo, kama Serikali tumejipanga. Sasa hivi tuna kampuni nne na tayari tumeshaanza kufanya mazungumzo na tumeongea na nchi ya Vietnam nao pia wamekubali kununua tumbaku yetu. Katika msimu huu wameahidi kabisa kwamba watanunua tani 1000 za tumbaku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nape Nnauye.

**MHE. NAPE M. NNAUYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa kuboresha mazingira ya kilimo ni pamoja na upatikanaji wa mbegu bora au miche bora ya zao husika, na kwa kuwa wazalishaji wa miche ya korosho imechukua muda mrefu sana kulipwa pesa zao na wengi wao walikuwa wamekopa fedha kwenye vyombo vya fedha. Je, Serikali pamoja na kuwalipa malipo yao ya stahiki, wako tayari sasa

kuwalipa fidia ya ziada kutokana na hasara iliyotokana na mikopo waliyochukua kwenye vyombo vya fedha?

**MWENYEKI:** Ahsante. Majibu kwa swali hilo, fidia ya ziada, majibu Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli anachoouliza, tumeshafanya uhakiki wa miche milioni kumi na tatu mpaka sasa hivi. Naomba niliambie Bunge lako Tukufu, pesa ya kuwalipa wananchi hawa ipo tayari, lakini suala la fidia halipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa, Aisharose Matembe na Mheshimiwa Magige.

**MHE. AISHAROSE N. MATEMBE** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa alizeti inayolimwa Mkoani Singida ni alizeti bora Afrika Mashariki na Kati. Je, Serikali ina mpango gani wa kuwawezesha wakulima wa alizeti Mkoani Singida, kulima kilimo chenye tija kwa kuwapa pembejeo, mikopo yenye gharama nafuu pamoja na elimu ili waweze kulima kilimo bora?

**MWENYEKITI:** Ahsante, jibu kwa swali hili Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kilimo cha alizeti kinalimwa sana katika Mkoa wa Singida na sisi kama Serikali, tunahamasisha na tunahimiza kuwa na kilimo cha kibiashara na vile vile kuwa na kilimo kinachozingatia kanuni, kwa maana ya kilimo kilicho bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nihamasishe halmashauri zote nchini na wale Maafisa Ugani wetu wote kuhakikisha kwamba wanatoa na wenyewe elimu kwa

umma, wasikae tu ofisini, kazi yao iko mashambani, kuhakikisha wanakwenda kwa wakulima, wanatoa elimu ili wakulima waweze kuwa na kilimo bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kama Serikali tumejipanga kwamba hili zao la alizeti ambalo nalo ni zao la kibiashara na linasaidia sana katika kuleta mafuta ili kupunguza tatizo la kuagiza mafuta zaidi kutoka nje, tumejipanga katika mwaka huu wa fedha kuhakikisha kwamba litazingatiwa na litakuwa ni Kilimo Bora na cha kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nahangaika na tumbaku tu, Mheshimiwa Margaret Sitta, Mheshimiwa Kakoso na Mheshimiwa Richard Mbogo.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Ulimaji wa tumbaku ni uhai kwa wananchi wa Urambo na Mkoa wa Tabora kwa ujumla; na wamekuwa wakiwa na changamoto kubwa sana ya upatikanaji wa pembejeo kwa wakati na bei isiyoeleweka. Je, Serikali inasemaje kuhusu kufika kwa pembejeo kwa wakati na ununuzi wa tumbaku kwa utaratibu wa *bulk procurement* ili bei ya tumbaku isibadilike badilike hovyo?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Kwa kifupi sana Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa, Naibu Waziri Kilimo.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tumbaku ni maisha, kama nilivyokuwa nimesema, hususani katika Mikoa ile inayolima tumbaku ikiwemo na Tabora. Katika swali lake linalohusu pembejeo, ni kweli tumbaku na ile mbolea ya *NPK* ambayo inatumika sana katika suala zima la zao la tumbaku, sisi tumeviagiza Vyama vyetu vyote vile vya Msingi vya Ushirika kuhakikisha kwamba wanafanya jitihada kwa sababu wao wenyewe ndiyo wakulima ili mbolea na pembejeo hizi zifike kwa wakati kwa

msimu unaotakiwa kwa sababu unaeleweka ili wao wenyewe kwa sababu ndio wanaolima, basi ule usumbufu usiweze tena kutokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Catherine Magige.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa kilimo cha mbogamboga na matunda hukubali kuzalishwa sana katika Ukanda wa Kaskazini na Nyanda za Juu Kusini; je, ni nini mkakati wa Serikali katika kuimarisha kilimo hiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa, Naibu Waziri wa Kilimo, majibu kwa kifupi tu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nichukue fursa hii kuwapongeza wakulima wote nchini ambao wamegundua umuhimu wa kilimo hiki ambacho tunaita tasnia ya *horticulture*. Sisi kama Serikali ni kweli tumeona kuna umuhimu sana wa tasnia ya *horticulture,* ndiyo maana hata pale katika Wizara yetu ya Kilimo sasa hivi tumeamua kuweka mtu ambaye atakuwa anashughulikia tu masuala ya *horticulture,* kwa maana ya *focal person*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile tunasisitiza kwamba tasnia hii ya *horticulture* iendelee kuwa ni kilimo cha kibiashara. Kwa sababu licha ya kwamba ni afya katika mwili vile vile kinaliingizia Taifa pato kubwa sana. Pia niziase tena halmashauri zote nchini kuhakikisha kwamba wanakuwa na kitalu nyumba kwenye kila halmashauri na kuweza kufanyika hayo mavitalu nyumba kama shamba darasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Richard Mbogo.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Changamoto zilizoko kwenye zao la tumbaku ni nyingi sana na kwa Mkoa wa Katavi Wilaya ya Mpanda Kampuni ya *TLTC* iliiandikia barua Bodi ya Tumbaku kwamba ina kusudio la kuacha kununua tumbaku katika Wilaya ya Mpanda. Je, nini kauli ya Serikali kuhusiana na suala hili kwa sababu mpaka sasa wakulima hawana uhakika wa kuuza tumbaku yao kwa msimu ujao? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Dkt. Mary Mwanjelwa, majibu kwa kifupi tu kwa hilo.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika zao la tumbaku mara nyingi wakulima wote wa tumbaku wanalima kilimo cha mkataba. Kampuni hizi ambazo zinaingia mikataba na wakulima wale kawaida ile mikataba huwa wanasaini kabla ya msimu kuanza. Niitake Kampuni ya *TLTC* kuhakikisha kwamba pamoja na wale wananchi wa Jimbo la Mheshimiwa Mbunge ule mkataba wao kama unasema alitakiwa kununua kiwango hiki cha tumbaku, basi mkataba ule lazima uheshimiwe na lazima wanunue kiwango kile kinachotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kakoso.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru kwa kunipa nafasi. Zao la tumbaku linategemea sana kununuliwa kwake kuwa na wateuzi wa zao hilo, kwa maana ya ma-*classifier;* Serikali ina mpango gani wa kuongeza *classifier* ili waweze kuliteua zao hilo?

**MWENYEKITI:** Jibu kwa swali hilo Mheshimiwa Mary Mwanjelwa, Naibu Waziri wa Kilimo.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipokuwa najibu swali la Mheshimiwa Mbunge Almas Maige

nilisema kama Serikali tumejipanga kutafuta *Classifiers* wengine, na nikasema zaidi kwamba mpaka sasa hivi tumeongea na nchi kama ya Vietnum na wameshaji-*commit* kwamba katika msimu huu watanunua tani 1,000 za tumbaku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mtolea.

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Serikali imekuwa ikijichanganya kuhusu suala la kilimo na matumizi ya tumbaku, kwa sababu Serikali kupitia Wizara ya Afya imeridhia Sera ya Umoja wa Mataifa ya kupiga vita matumizi ya tumbaku; lakini Serikali kupitia Wizara ya Kilimo inahamasisha kilimo cha tumbaku. Sasa nataka kujua kauli ya Serikali, ni upi hasa msimamo wetu kuhusu kilimo na matumizi ya tumbaku hapa nchini?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Jibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Dkt. Mary Mwanjelwa.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, alichoongea Mheshimiwa Mbunge ni kweli, kwamba katika Shirika letu lile la *WHO* wanapiga vita tumbaku na hususani katika masuala mazima yale ya afya lakini vile vile na mazingira na suala zima la *child labour.* Naomba nichukue fursa hii kipekee kabisa kusema kwamba *nicotine* yetu sisi kwenye tumbaku ni ndogo. Hata hivyo, niase wakulima wote nchini, kwamba wasitegemee tu zao la tumbaku vile vile kuna mazao mengine mbadala ambayo na yenyewe wanapaswa wawe wanazingatia na kuyalima pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Waheshimiwa tunaendelea. Swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa

Grace Victor Tendega, Mbunge wa Viti Maalum na linaulizwa kwa Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria. Kwa niaba yake!

Na. 509

**Kuanzisha Mahakama za Dawa za Kulevya Nchini**

**MHE. JOSEPH R. SELASINI (K.n.y. MHE. GRACE V. TENDEGA)** aliuliza:-

Kesi za dawa za kulevya na upelelezi vimekuwa vikichukua muda mrefu sana na kusababisha wakati mwingine ushahidi kupotea na watuhumiwa kuachwa huru baada ya upelelezi kukamilika:-

Je, kwa nini Serikali isianzishe Mahakama za Dawa za Kulevya kwenye Viwanja vya Ndege, Bandari na mipakani ili watuhumiwa wafikishwe Mahakamani punde tu ushahidi ukiwa mikononi kama zifanyavyo nchi nyingine ikiwemo India?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA (K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Katiba wa Sheria, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Grace Victor Tendega, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la uanzishwaji wa mahakama katika kushughulikia aina fulani ya makosa, ni suala la kisheria linalohitaji ushirikishwaji mkubwa wa wadau wote husika wa haki jinai *(criminal justice).* Kwa kutambua hilo, Serikali imeshaanza mazungumzo ya awali na wadau hao wa haki jinai, ukiwemo mhimili wa Mahakama ili kuona uwezekano wa kusikiliza mashauri ya watuhumiwa wa dawa za kulevya wanaokamatwa katika maeneo ya viwanja vya ndege, bandarini na maeneo mengine ya mipaka ya nchi, kwa kutumia Mahakama zinazotembea *(mobile courts).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, nawaomba Waheshimiwa Wabunge wawe na subira wakati Serikali ikijadiliana na wadau wa haki jinai kuhusiana na suala hilo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Selasini.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu katika nchi za nyingine Afrika Mashariki wako makini sana katika jambo hili na mashauri mengi yamekuwa yakiamuliwa kwa haraka tofauti na sisi. Kucheleweshwa kwa maamuzi ya mashauri haya kunaweza kukapelekea fikra kwamba rushwa inatumika zaidi katika kuamua haya mashauri. Sasa, je, ni lini Serikali itakamilisha huo mchakato wa kuongea na wadau ili maamuzi haya yaweze kufanyika haraka iwezekanavyo kunusuru maisha ya watoto wetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, sheria inataka mali za watuhumiwa wa madawa ya kulevya zitaifishwe. Uwezekano wa kuzitaifisha ndani ya nchi upo, lakini ni utaratibu gani unaotumika kutaifisha mali hizi kama ziko nje ya nchi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mavunde, kwa kifupi tu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA (K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema katika majibu ya msingi, kinachofanyika hivi sasa ni wadau wa haki jinai ambao ni mhimili wa mahakama na pamoja na sisi upande wa Serikali kutafuta namna bora ya kuanza utekelezaji wa shughuli ya kushughulikia masuala ya kesi za madawa ya kulevya katika maeneo ya viwanja vya ndege na mipaka ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu jambo hilo ni la kisheria tunalifanya kwa umakini mkubwa. Hivi sasa

ninavyozungumza tayari Kamishna Jenerali wa Mamlaka ya Dawa za Kulevya na Jaji Kiongozi Feleshi wameshaanza mazungumzo ya kuja na namna bora ya kuweza kuwa na mahakama hizi ambazo zitakuwa tembezi, ili inapotokea kwamba kuna mhalifu yeyote amekamatwa na madawa ya kulevya basi aweze kuchukuliwa hatua kwa mujibu wa utaratibu ambao unakuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ugumu unakuja kwa sababu ukiangalia kesi hizi nyingi za madawa ya kulevya zina masharti yake pia kwa maana ya kisheria. Kwa sababu ni kesi ambazo zinatakiwa zipitie hatua moja mpaka nyingine; kwa maana zinakwenda Mahakama Kuu na zikienda Mahakama Kuu maana yake ni kesi ambazo utaratibu umewekwa kwa mujibu wa sheria zianzie katika Mahakama za Mwanzo. Kwa hiyo si rahisi sana kufanya maamuzi hayo ya kiharaka, ndiyo maana tukasema kwamba kupitia utaratibu huu utarahisisha sana mashauri haya yaweze kusikilizwa kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia tu nimpe taarifa Mheshimiwa Mbunge, imeanzishwa Mahakama ya Mafisadi kwa mujibu wa marekebisho ya Sheria Na.3 ya Mwaka 2016 ambayo imeonesha tija sana na mpaka hivi sasa ninapozungumza tayari kesi 7,517 zimeshaamuliwa kwa uharaka sana na tunaamini kabisa zoezi hili likikamilika basi tutaweza kuwahudumia Watanzania kwa kuhakikisha kwamba wale wahalifu wote wanakamatwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili, ameuliza kuhusu namna ya utaifishaji wa hizi mali nje ya nchi. Nchi yetu imesaini makubaliano na tulishirikiana na baadhi ya nchi na tumekuwa na ushirikiano mzuri na nchi nyingi ambazo kupitia utaratibu wa makubaliano hayo, ikitokea suala la namna hiyo basi mamlaka zote mbili zinafanya kazi kuhakikisha kwamba mhusika ambaye mali zake ziko nje ya nchi pia utaratibu ufuatwe wa kisheria ili ziweze kutaifishwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Khatib.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kuchelewesha haki ni kunyima haki na si kesi za madawa ya kulevya pekee kuna mashtaka ambayo watuhumiwa wakipelekwa kule ni kama wanasahauliwa. Kuna kesi za ugaidi na kuna kesi ...

**MWENYEKITI:** Uliza swali.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujua ni kwa nini mashtaka ya kesi aina hii zinachukua muda mrefu kupelekwa mahakamani na kuhukumiwa?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mavunde kwa kifupi tu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA (K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utaratibu wa makosa yote ya kijinai na kwa mujibu wa Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sura ya 20 umewekwa utaratibu wa namna gani kesi hizi zishughulikiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kesi hizi zinahitaji umakini mkubwa sana, si rahisi kwa namna yoyote ile kuziharakisha pasipokuwa uchunguzi wake umekamilika. Ndiyo maana nawaomba Waheshimiwa Wabunge waendelee kuvuta subira mamlaka zetu zinafanya kazi sasa hivi kuhakikisha kwamba kesi zinapungua na Mahakama imeweka utaratibu wa kuhakikisha kwamba kesi nyingi zinasikilizwa kwa wakati ili haki ionekane imetendeka.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mwita Getere.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Diwani wa Kata ya Mihingo Mheshimiwa Nyambula Nyamhanga yuko *lockup* miezi sita sasa kwa kosa

la uchochezi. Naomba kupata ufafanuzi wa Serikali, ni njia gani tuitumie huyu Diwani apate dhamana, kwa hiyo kesi ya uchochezi kwa sababu ana miezi sita yuko gerezani bila kupata dhamana? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Mavunde. Naona Waziri mwenyewe amesimama, Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu jambo alilolisemea Mheshimiwa Mbunge ni mahsusi na kwa mujibu wa sheria kuna makosa yenye dhamana na kuna makosa yasiyo na dhamana; nimwombe tu Mheshimiwa Mbunge tuje tuliongee. Pia nimpongeze kwa kufuatilia sana masuala ya wapiga kura wake. Kama ni jambo ambalo lina dhamana maana yake taratibu tu za dhamana zitafuata ili ziweze kukamilika na Mheshimiwa Diwani aweze kupata dhamana. Mara zote yale makosa yasiyo na ... *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Semuguruka

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kuniona ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa miongoni mwa sababu zinazochangia kuchelewa kwa kesi hizi ni vidhibiti kutopelekwa maabara kwa Mkemia Mkuu haraka ili kuthibitisha. Je, Serikali ina mpango gani wa kutatua changamoto hii?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Mavunde, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA (K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa marekebisho ya sheria

yaliyofanyika mwaka 2017, hivi sasa Sheria ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya Kifungu cha 4(n) ambacho kimeongezewa baada ya marekebisho kimeweka utaratibu wa kwamba hivi sasa kwa kuzingatia kwamba kuna mashauri mengi ambayo yanasimama kwa kusubiri vidhibiti kutoka katika Ofisi ya Mkemia Mkuu, sasa kupitia sheria hii imeanzishwa *laboratory* katika Ofisi ya Kamishna Jenerali ili kuhakikisha kwamba mamlaka pia nayo iwe na wajibu huo wa kuchunguza na kutoa taarifa ili kujaribu kusaidia *expedite* kesi hizi zisichukue muda mrefu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nimwondolee hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali ilichukua hatua kwa marekebisho hayo ya sheria na hivi sasa ukiacha Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Jeshi la Polisi lakini... kazi hiyo pia.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Waheshimiwa Wabunge.

Wageni waliopo Bungeni asubuhi hii; wageni waliopo ukumbi wa Spika. Tunao wageni wanane wa Mheshimiwa Spika, ambao ni viongozi kutoka Chama cha Wapenda Amani Duniani *(Universal Peace Foundation)* ambacho Makao Makuu yake kwa upande wa Afrika yapo nchini Senegal. Kwa hiyo, tuna bahati ya leo kuwa na Rais wa chombo hicho Dkt. Thomas Walsh. Karibuni sana.

Ameambatana na timu ya wafuatao:- Ndugu Adama Doumbia ambaye ni Katibu Mkuu wa *UPF* Afrika; Ndugu Stylos Simbamwene-Katibu Mkuu *UPF* Tanzania, Mchungaji Paul Bendera, Sheikh Othman Kambaku, Ndugu Neema Uronu, Ndugu Henkribeth Mgina na Anthony John Bosco. *(Makofi)*

Kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge na sisi kama Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tunataka tujiunge, baadhi yetu, kama wajumbe wa chombo hiki na naamini leo chombo hiki kitazinduliwa. Kwa hiyo nawaomba sana Waheshimiwa Wabunge tujitokeze kwa wingi sana

tuweze kufanya uzinduzi wa chombo hiki. Chombo hiki ni kwa faida ya maendeleo ndani ya amani duniani, ni maendeleo; ndiyo maana tunataka sana tushirikishe Wabunge kwa suala hili.

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge; tunao wageni watatu wa Mheshimiwa *Engineer* Atashasta Nditiye, Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ambao ni wapiga kura kutoka Jimboni kwake. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 35 wa Mheshimiwa Anthony Mavunde, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, (Kazi, Vijana na Ajira) ambao ni viongozi wa dini Kata ya Ntyuka, Walimu wa shule za msingi na sekondari, Balozi wa nyumba kumi, viongozi wa CCM, wazee maarufu wa kata na vijana wa bodaboda wote kutoka Kata ya Ntyuka, Mkoani Dodoma wakiongozwa na Diwani Mheshimiwa Theobalt Maina. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Munira Mustafa Khatib ambao ni ndugu zake kutoka Kusini Pemba. *(Makofi)*

Wageni watano wa Mheshimiwa Mary Chatanda ambao ni wasanii kutoka Korogwe Mkoani Tanga. Karibuni sana wasanii wetu. *(Makofi)*

Wageni 52 wa Mheshimiwa Profesa Anna Tibaijuka ambao ni wanafunzi wa Chuo cha St. John cha Dodoma wanaotokea Mkoani Kagera. Mko wapi, Karibuni sana wanafunzi. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Constatine Kanyasu ambaye ni Mchungaji Zacharia Masinga wa Kanisa la Pentecoste Mkoani Morogoro. Karibu sana Mchungaji. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Suzan Kiwanga, ambaye ni ndugu yake kutoka Ifakara Mkoani Morogoro Ndugu John Joseph Katungu. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Jasson Rweikiza, Mbunge, ambaye ni mwanafunzi wa kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, Ndugu Dominick Deogratias, karibu sana. *(Makofi)*

Wageni 74 wa Mheshimiwa Alex Raphael Ghashaza, Mbunge wa Ngara ambao ni wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma wakiongozwa na Ndugu Elia Ethan. Karibuni sana. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Martin Msuha, Mbunge wa Mbinga Vijijini ambaye ni Diwani wa Kata ya Kambarage Wilaya ya Mbinga Vijijini Mkoani Ruvuma Ndugu Gisbert Nchimbi, karibu sana ndugu yetu. *(Makofi)*

Wageni 59 wa Mheshimiwa Mbarouk Salim Ali ambao ni wanafunzi wa Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini wanaosomea Mipango Mazingira na Usimamizi kutoka Mkoani Dodoma wakiongozwa na Ndugu Salim Salim, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge leo orodha ni ndefu. Wageni nane wa Mheshimiwa Omary Badwel, Mbunge ambao ni vijana kutoka Mkoani Dodoma wakiongozwa na Ndugu Jamal Adam. *(Makofi)*

Wageni wanne wa Mheshimiwa Oliver Semguruka, ambao ni Diwani na wakandarasi kutoka Karagwe, Mkoa wa Kagera. Ahsanteni. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Asha Abdullah Juma, Mbunge, ambaye ni mtoto wake Ndugu Zambe Toziri kutoka Tabora, karibu sana. Mheshimiwa Asha Abdallah Juma mnamfahamu, huyo ndiye binti Zambe Toziri. *(Makofi/ Vigelegele)*

Wageni watano wa Mheshimiwa Ritta Kabati, ambao ni viongozi wa Taasisi isiyo ya Kiserikali ya *(AFL Foundation)* na wataalam wa afya kutoka Mkoa wa Iringa. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 10 wa Mheshimiwa Josephine Genzabuke, ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha St. John cha Jijini Dodoma wanaotokea Mkoa wa Kigoma. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Bonah Kaluwa, Mbunge wa Segerea ambao ni Ndugu Ladislaus Joseph Kamoli, baba yake mzazi na Mheshimiwa Bonah ameambatana na Ndugu Issa Shaibu, kaka yake na Mheshimiwa Bonah. Karibu sana mzee wetu. *(Makofi)*

Wageni wanne wa Mheshimiwa Allan Kiula, Mbunge, wa Mkalama ambao ni viongozi wa CCM kutoka Mkalama Mkoani Singida wakiongozwa na Mheshimiwa Abdallah Mangushi. *(Makofi)*

Wageni wanne wa Mheshimiwa Balozi Adadi Rajab, ambao ni wadogo zake kutoka Muheza Mkoani Tanga. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Rose Tweve, ambao ni marafiki zake kutoka Mkoani Dodoma. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Flatei Massay, ambao ni Walimu kutoka Mbulu Vijijini, Mkoani Manyara. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Abdallah Mtolea, ambao ni majirani zake kutoka Mkoani Dodoma. (*Makofi*)

Wageni watano wa Mheshimiwa Venance Mwamoto, ambao ni Makatibu wa CCM kutoka Mkoa wa Iringa. *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge hili kwa ajili ya mafunzo. Tunao wanafunzi 36 na Walimu wanne kutoka shule ya Sekondari ya Al- Qaem ya Jijini Dodoma, karibuni sana wanafunzi kwa mafunzo. *(Makofi)*

**MHE. MARY P. CHATANDA:** Mwongozo wa Kiti.

**MWENYEKITI:** Ngoja. Waheshimiwa Wabunge, mnafahamu mimi huwa sipendi michezo eeh, *please.*

**MHE. MARY P. CHATANDA:** Mwongozo wa Kiti

**MWENYEKITI:** Naendelea na matangazo; tena nimeshamwona simpi mwongozo.

Tunayo sasa matangazo, nianze na hili la Mheshimiwa Spika, Mwenyekiti wa Tawi la Tanzania la *UPF* Mheshimiwa Mussa Ntimizi, Mbunge anawatangazia Wabunge kwamba leo wanachama wa *UPF* saa saba mchana kwenye Ukumbi wa Msekwa kutafanyika uzinduzi wa chombo hiki Tawi la Tanzania. Mgeni rasmi katika uzinduzi huo atakuwa ni Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akiambatana na Mheshimiwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano. Mnaombwa Wabunge wanachama wote mhudhurie.

Tangazo linalofuata, Katibu wa Bunge anaomba awatangazie Wabunge wote kwamba tunaombwa tuchukue nyaraka zetu zote kwenye *pigeon holes,* maana baadhi yake zimejaa na hakuna nafasi ya kuongeza *documents* za ziada na zipo nyingi za ziada zinakuja. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge leo Katibu anawatangazia Wabunge wote kwamba Ofisi ya Waziri Mkuu Bunge imeandaa semina muhimu kuhusu Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Nchini Awamu ya Pili *(ASDP II)* na mchango wa sekta hiyo katika uchumi wa viwanda. Semina hiyo itafanyika leo tarehe 28 Juni saa tisa kasoro robo mchana katika Ukumbi wa Msekwa chini ya uongozi wa Wizara ya Kilimo, hii itakuwa ni baada ya uzinduzi wa tukio nililolitangaza mapema. (*Makofi*)

Mwenyekiti wa Umoja wa Wabunge Wanawake Tanzania, Mheshimiwa Margaret Sitta anaomba awatangazie Wabunge wanawake wa chama hicho *(TWPG)* kuwa leo

tarehe 28 kutakuwa na kikao cha dharura kwa ajili ya Wabunge wanawake wote. Kikao hicho kitafanyika katika Ukumbi wa Msekwa mara tu baada ya semina ile niliyoitaja kama mtaweza.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge kuwa kutokana na mafanikio makubwa yaliyopatikana kwenye hafla ya uchangishaji fedha kwa ajili ya kuboresha mazingira ya mtoto wa kike shuleni iliyofanyika tarehe 22 Juni mwaka huu katika Viwanja vya Bunge, *TWPG* kwa kushirikiana na Ofisi ya Bunge imepanga kuendelea na zoezi hili tarehe 31 mwezi wa Agosti na tarehe Mosi, Septemba, 2018, Jijini Dar es Salaam.

Burudani zote zilizofanyika hapa Dodoma kama vile singeli, sebene, maonyesho ya mavazi, sarakasi, shairi, taarab, kwaya na vichekesho pamoja na maonesho mapya ya ngoma za asili na mechi za kukata na shoka kati ya Simba na Yanga zinazotarajiwa kuchezwa na Waheshimiwa Wabunge Jijini Dar es Salaam zikiwa zimeboreshwa zaidi. *(Makofi)*

Aidha, Waheshimiwa Wabunge wanaopenda kushiriki kwenye burudani hii ya ngoma za asili za Zanzibar na Tanzania Bara wanaombwa kujiorodhesha katika lango kuu la kuingia ukumbini kabla ya kumalizika kwa Mkutano huu wa Bajeti. Maandalizi ya Wabunge washiriki yatafanyika wakati wa vikao vya Kamati vitakavyofanyika kabla ya Mkutano wa Kumi na Mbili wa Bunge, mwezi Agosti Jijini Dodoma.

*TWPG* kwa kushirikiana na Ofisi ya Bunge inapenda kutoa shukrani zake za dhati kwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa, Samia Suluhu Hassan, Mawaziri na kipekee Mheshimiwa Angela Kairuki, Waheshimiwa Wabunge na wadau wote waliojitolea na kushiriki katika kufanikisha uzinduzi wa uchangishaji fedha kwa ajili ya kuboresha mazingira ya mtoto wa kike mashuleni. *(Makofi)*

Niliwaambia leo matangazo yalikuwa mengi eeh, sasa kwa sababu muda umekwenda mnaonaje kama miongozo nitaikataa...

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mwongozo wa Spika.

**MHE. MARY P. CHATANDA:** Mwongozo wa Kiti.

**MWENYEKITI:** Mnaniona nimefanya nini, si nimesimama?

**MHE. MARY P. CHATANDA:** Mwongozo wa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Ngoja wachukue majina leo mimi sichukui majina.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Anza na Haonga.

**MHE. MARY P. CHATANDA:** Mary Chatanda.

**MBUNGE FULANI:** Wewe alishasema hakupi mama unataka nini tena?

**MWENYEKITI:** Tuongee mmoja mmoja, makatibu wataniambia mimi.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Cecil Mwambe, Mheshimiwa Chacha Ryoba, Mheshimiwa Suzan Kiwanga, Mheshimiwa Pascal Haonga...

**MHE. MARY P. CHATANDA:** Mary Chatanda

**MWENYEKITI:** Niliwaambia Waheshimiwa Wabunge, nimeangalia muda. Sasa Waheshimiwa Wabunge nakabidhi Kiti kwa Mheshimiwa Spika ili aendelee na hatua inayofuata.

*Hapa Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alikalia kiti*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Chenge, Katibu tunaendelea.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

**MISWADA YA SHERIA ZA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2018**
***(The Finance Bill, 2018)***

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kwa sababu ya presha ya muda, kama mtakavyokumbuka shughuli za jana na leo zote zinafanyika leo, kwa hiyo muda hatuna kabisa inabidi twende na ratiba inavyotakiwa. Mheshimiwa mtoa hoja, Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Phillip Mpango tafadhali, karibu.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2018 *(The Finance Act, 2018)* pamoja na marekebisho yake sasa usomwe kwa Mara ya Pili.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kutambua michango iliyotolewa na Kamati ya Bunge ya Bajeti chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia, Mbunge wa Mtwara Vijijini wakati wa kuujadili Muswada huu na kutoa ushauri. Wakati wa kipindi chote cha majadiliano Kamati ilitoa michango na changamoto nyingi kwa Serikali kuhusu vyanzo mbalimbali vya mapato pamoja na namna bora ya kukusanya kodi kwa ajili ya maendeleo ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba Muswada huu umezingatia kwa kiasi kikubwa ushauri na mapendekezo mazuri ya Kamati. Aidha, Serikali itaendelea kufanyia kazi mapendekezo mengine ya Kamati kwa lengo la kuongeza mapato ya Serikali katika mwaka ujao wa fedha.

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wote ambao walichangia katika hotuba ya bajeti ya Serikali niliyowasilisha hapa Bungeni tarehe 14 Juni mwaka huu na baadaye kupitishwa na Waheshimiwa Wabunge. Kipekee namshukuru Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mheshimiwa Dkt. Adeladius Kilangi kwa kuandaa Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, lengo la Muswada huu ni kuwezesha utekelezaji kisheria wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2018/2019, niliyoiwasilisha Bungeni tarehe 14 Juni mwaka huu. Muswada huu unabainisha sheria mbalimbali zinazofanyiwa marekebisho.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu kwa kiwango kikubwa umezingatia ushauri na mapendekezo ya wadau mbalimbali wakiwemo wamiliki wa viwanda, wafanyabiashara, taasisi mbalimbali binafsi, taasisi za Serikali na wananchi kwa ujumla. Wizara ya Fedha na Mipango ilishirikisha wadau hawa katika uchambuzi wa hatua za kodi ambazo zimebainishwa katika Muswada huu katika ngazi mbili:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kupitia kwenye Kikosi Kazi cha Maboresho ya Mfumo wa Kodi *(Task Force on Tax Reforms);* na

Mheshimiwa Spika, pili, ni mapendekezo kutoka kwenye kikosi kazi yaliyojadiliwa kwenye Kamati ya Ushauri kwa Waziri wa Fedha na Mipango kuhusu hatua za mapato *(Advisory Committee on Revenue Measures).*

Mheshimiwa Spika, Muswada huu kama ulivyofanyiwa marekebisho unakusudia kufuta Sheria ya Tume ya Mipango, Sura ya 314 na kuzifanyia marekebisho sheria 16 zinazohusu masuala ya fedha, kodi, ushuru na tozo kwa lengo la kuweka, kurekebisha, kupunguza au kufuta viwango vya kodi, ushuru, ada na tozo mbalimbali na kuboresha ukusanyaji wa kodi.

Mheshimiwa Spika, sheria zinazofanyiwa marekebisho au kufutwa ni zifuatazo:-

(1) Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania, Sura 197;

(2) Sheria ya Leseni za Biashara, Sura 208;

(3) Sheria ya Sekta ya Korosho, Sura 203;

(4) Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura 147;

(5) Sheria ya Michezo ya Kubahatisha, Sura ya 41;

(6) Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura 332;

(7) Sheria ya Ardhi, Sura ya 113;

(8) Sheria ya Fedha za Serikali ya Mitaa, Sura 290;

(9) Sheria ya Madini, Sura 123;

(10) Sheria ya Tume ya Mipango, Sura 314;

(11) Sheria ya Tozo ya Huduma za Bandari, Sura 264;

(12) Sheria ya Fedha za Umma, Sura 348;

(13) Sheria ya Tozo za Barabara na Mafuta, Sura 220;

(14) Sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania, Sura 399;

(15) Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Sura 438; na

(16) Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura 148.

Mheshimiwa Spika, maudhui ya Muswada...

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri subiri kidogo, sekunde tu.

Waheshimiwa Wabunge, jamani huwa nawaomba mara kwa mara, hata nyie wenyewe muwe mnasikiliza muone tu jinsi ambavyo yaani hata kilabu cha pombe cha kule Kongwa kina nafuu, kelele nyingi mno. Hapo kwa akina Mheshimiwa Saada Mkuya kuna nini maeneo yote huko kelele sana, *what is it* hamuwezi kunong'ona? Mheshimiwa Waziri endelea.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, Muswada huu umegawanyika katika sehemu 17 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kwanza inahusu masuala ya utangulizi ikijumuisha jina na tarehe ya kuanza kutumika kwa sheria hii ambapo sheria itaanza kutumika tarehe Mosi Julai, 2018.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Pili pamoja na marekebisho yake inapendekeza kurekebisha vifungu vya 34(1) na 35(1) vya Sheria ya Benki Kuu, Sura 197 ili kujumuisha fedha za Serikali zilizopo kwenye akaunti za amana zilizopo Benki Kuu kwenye ukokotoaji wa bakaa katika Mfuko Mkuu wa Serikali na hivyo kupunguza nakisi kwenye Mfuko huu. Hivi sasa fedha za Serikali zilizopo kwenye akaunti za amana hazitumiki katika ukokotoaji huo.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tatu pamoja na marekebisho yake inapendekeza kurekebisha Sheria ya Leseni ya Biashara, Sura 208 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, ni kurekebisha kifungu cha 2 cha Sheria ya Leseni za Biashara kwa kubainisha tafsiri mpya ya neno *business license* ili ihusishe leseni za kielektroniki.

Mheshimiwa Spika, pili, ni kurekebisha kifungu cha 9 kwa kufuta maneno *Central Government* na kuweka maneno *Business Registration and Licensing Agency* na kufanya marekebisho ya kiuandishi katika jedwali la sheria hii ili kuhamishia rasmi shughuli za utoaji leseni kwa Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni *(BRELA).*

Mheshimiwa Spika, kutokana na mapendekezo haya, Wizara yenye dhamana na masuala ya biashara itabaki na jukumu la kusimamia sera zinazohusu masuala ya leseni za biashara.

Mheshimiwa Spika, lengo la marekebisho haya ni kurahisisha utoaji wa leseni za biashara na kuwezesha utoaji wa leseni kwa njia ya kielektroniki kupitia *BRELA.*

Mheshimiwa Spika, tatu, ni kurekebisha kifungu cha 14 kwa kuongeza kifungu kipya cha 14A(1),(2) na (3) ili kuanzisha rejista maalum ya kutunza kumbukumbu za leseni za biashara, kuweka wajibu kwa mamlaka za utoaji leseni, kuwasilisha kwa Waziri mwenye dhamana na masuala ya

biashara taarifa kuhusu leseni za biashara katika muda utakaopangwa kupitia Kanuni za sheria hii.

Mheshimiwa Spika, aidha, kifungu hiki kipya kinaweka utaratibu kwa mtu yeyote kuwa na uwezo wa kukagua rejista husika mara baada ya kulipa ada. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza uwazi na uwajibikaji.

Mheshimiwa Spika, nne, ni kufanya marekebisho ya kiuandishi katika kifungu cha 22(1) na kufuta aya ya (a) na kuiandika upya ili kuongeza adhabu na faini kwa makosa chini ya sheria hii. Lengo la hatua hii ni kuongeza kiwango cha faini kulingana na mazingira ya sasa.

Mheshimiwa Spika, tano, ni kurekebisha kifungu cha 29 kwa kuongeza aya mpya ya (f) ili kumwezesha Waziri mwenye dhamana na masuala ya biashara kubainisha aina ya fomu zitakazotumika wakati wa kuomba leseni ya biashara.

Mheshimiwa Spika, sita, ni kurekebisha kifungu cha 30 kwa kuongeza adhabu kwa makosa yatakayofanyika chini ya sheria hii.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Nne, inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Sekta ya Korosho, Sura 203 kwa kufuta kifungu cha 17A ili ushuru wote wa *export levy* unaokusanywa kwenye korosho ghafi zinazosafirishwa nje ya nchi uingizwe katika Mfuko Mkuu wa Serikali na kuwa sehemu ya mapato ya Mfuko huo badala ya utaratibu wa sasa ambapo asilimia 65 ya mapato ya ushuru huo ni sehemu ya mapato ya Mfuko wa Kuendeleza Zao la Korosho.

Mheshimiwa Spika, kufuatia pendekezo hili, shughuli za uendelezaji wa zao la korosho pamoja na gharama za uendeshaji wa Bodi ya Korosho zitagharamiwa kupitia Bajeti ya Serikali chini ya usimamizi wa Wizara ya Kilimo kama inavyofanyika hivi sasa kwa mazao mengine ikiwemo pamba, kahawa na pareto.

Mheshimiwa Spika, lengo la hatua hii ya Serikali ni kuhakikisha kwamba mapato yatokanayo na ushuru kwenye mazao mbalimbali yanasimamiwa ipasavyo kutumika kwa ajili ya shughuli zilizokusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tano, kama ilivyorekebishwa inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura 147 kwa kurekebisha viwango maalum vya ushuru wa bidhaa yaani *specific duty rates* zisizo za petroli ili kuviuianisha na mfumuko wa bei na viashiria vingine vya uchumi jumla kwa mujibu wa kifungu cha 124(2) cha Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura 147.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, ili kutekeleza azma ya Serikali ya Awamu ya Tano ya kujenga uchumi wa viwanda, napendekeza kutofanya mabadiliko ya viwango maalum vya ushuru kwa bidhaa zisizo za petroli zinazozalishwa hapa nchini na kuongeza viwango vya ushuru wa bidhaa kwa bidhaa zisizo za petroli zinazoagizwa kutoka nje ya nchi. Viwango vya sasa na vile vinavyopendekezwa ni kama ilivyobainishwa kwenye jedwali lililopo katika Ibara ya 14 ya Muswada.

Mheshimiwa Spika, aidha, inapendekeza kufuta neno konyagi lililopo katika jedwali la tatu chini ya *SH Code* 2208.90.10 ili kuondoa dhana kwamba bidhaa hii huagizwa kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Sita pamoja na marekebisho yake inapendekeza kurekebisha Sheria ya Michezo ya Kubahatisha, Sura ya 41 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ni kurekebisha kifungu cha 31(2) kama ifuatavyo:-

(a) Kuongeza kiwango cha kodi kwa michezo ya kubahatisha ya *casino* kutoka kiwango cha asilimia 15 hadi kiwango cha asilimia 18 ya mapato halisi *(GGR)* ambayo hupatikana baada ya kutoa zawadi. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza mapato ya Serikali kupitia michezo hii kwa

kuzingatia kwamba kiwango cha asilimia 15 kimedumu kwa muda mrefu kuanzia mwaka 2012.

(b) Kuongeza kiwango cha kodi kwa michezo ya *casino* za mtandaoni *(internet casinos)* kutoka asilimia 15 ya mauzo halisi *(GGR)* mpaka asilimia 25 ya mauzo halisi. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza mapato ya Serikali na kufanya michezo inayoshabihiana kutozwa kiwango kimoja cha kodi.

Mheshimiwa Spika, mbili, ni kurekebisha kifungu cha 31A(1) kwa kuongeza kiwango cha kodi ya ushindi kutoka 18% hadi 20 kwa michezo yote ya kubahatisha isipokuwa *casino* za ardhini *(land based casinos)* ambazo zitatozwa asilimia 12 ya ushindi. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza mapato ya Serikali na kuifanya michezo inayoshabihiana kutozwa kiwango kimoja cha kodi.

Mheshimiwa Spika, tatu, ni kurekebisha jedwali la pili la sheria kwa kulifuta na kuliandika upya ili kuweka viwango vipya vya kodi katika michezo ya kubahatisha kama ifuatavyo:-

(a) Kuongeza kiwango cha kodi katika michezo ya kubahatisha ya ubashiri wa matokeo ya michezo *(sports betting)* kutoka kiwango cha asilimia sita ya mauzo ghafi hadi kiwango cha asilimia 25 ya mapato halisi *(GGR).*

(b) Kubadilisha kiwango na wigo wa kodi katika mchezo wa bahati nasibu ya *SMS (SMS lottery)* kutoka kiwango cha asilimia 30 ya mauzo ghafi hadi kiwango cha asilimia 25 ya mapato halisi *(GGR).*

(c) Kuongeza kiwango cha kodi kinachotozwa kwenye mashine za michezo ya kubahatisha *(slot machine operations)* kutoka Sh.32,000 hadi Sh.100,000 kwa kila mashine kwa mwezi.

(d) Kuongeza kiwango cha kodi kinachotozwa katika mchezo wa bahati nasibu ya Taifa kutoka asilimia 10 ya pato ghafi hadi asilimia 20 ya pato halisi *(GGR).*

(e) Kuongeza kiwango cha kodi kinachotozwa kwenye eneo linalohusu idadi ya mashine 40 *(40 machines side)* za michezo ya kubahatisha kutoka asilimia 13 hadi asilimia 25 ya mapato halisi ambayo hupatikana baada ya kutoa zawadi.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Saba, ilivyorekebishwa inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura 332 kama ifuatavyo:-

(a) Kurekebisha kifungu cha 3 ili kufuta rejea ya kifungu cha 131 kilichopo katika tafsiri ya neno *approved retirement fund* na kuweka rejea ya kifungu cha 11 cha Sheria ya Utawala wa Kodi, Sura 438 ili kuleta maana iliyokusudiwa.

(b) Kufuta kifungu cha 10A ili kuondoa katazo kwa Waziri mwenye dhamana na masuala ya fedha la kutoa msamaha wa Kodi ya Mapato kwa miradi ya Serikali inayotekelezwa kwa fedha za mikopo ya kibiashara.

Mheshimiwa Spika, lengo la marekebisho haya ni kumpa mamlaka Waziri ya kutoa msamaha wa kodi kwa miradi hiyo ambayo imekuwa na changamoto katika utekelezaji wakati Serikali inapopata mikopo ya aina hii ambayo inakuwa na masharti ya utoaji wa misamaha ya Kodi ya Mapato.

(c) Kurekebisha kifungu cha 65B(2) kwa kufuta rejea ya aya ya 3(5) na kuweka rejea ya kifungu cha 1(5) na kurekebisha kifungu cha 65K(2) kwa kufuta rejea ya aya ya 3(6) na kuweka rejea kifungu cha 1(6) ili kuleta maana iliyokusudiwa.

(d) Kuongeza kifungu cha 129 ili kumwezesha Waziri mwenye dhamana na masuala ya fedha kuandaa kanuni za utekelezaji wa sheria hii.

(e) Kurekebisha jedwali la kwanza la sheria kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, ni kuongeza kiwango cha Kodi ya Mapato kutoka asilimia 20 hadi 30 kwa mlipa kodi ambaye siyo kampuni ambaye si mkazi *(non-resident individual).* Lengo la marekebisho haya ni kuleta uwiano wa utozaji kodi baina ya walipa kodi ambao ni wakazi na walipa kodi wasio wakazi.

Mheshimiwa Spika, pili, ni kupunguza kiwango cha Kodi ya Mapato ya Makampuni *(Corporate Income Tax)* kutoka asilimia 30 hadi asilimia 20 kwa miaka mitano kuanzia mwaka 2018/2019 hadi mwaka 2022/2023. Kwa wawekezaji wapya wa viwanda vya dawa za binadamu na viwanda vinavyotengeneza bidhaa za ngozi. Aidha, Serikali itaingia mkataba wa makubaliano *(performance agreement)* na kila mwekezaji ambao utaainisha wajibu wa kila upande.

Mheshimiwa Spika, lengo la marekebisho haya ni kuongeza uwekezaji katika Sekta ya Dawa za Binadamu na usindikaji wa ngozi ambao kwa sasa haufanyiki nchini na pia kuongeza ajira na mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, tatu, ni kuongeza kiwango cha Kodi ya Mapato kwa makampuni yanayopata hasara ya kodi kwa miaka mitatu mfululizo kutoka asilimia 0.3 hadi asilimia 0.5. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza mchango wa kodi wa makampuni haya ambayo yanapata huduma mbalimbali kwa gharama ya walipa kodi wengine.

(f) Kurekebisha jedwali la pili la sheria kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, moja, ni kuondoa msamaha wa wajibu wa kukata kodi ya zuio kwenye malipo ya kodi ya pango, riba na gawio linalolipwa na makampuni yaliyosajiliwa chini ya sheria zinazosimamia maeneo maalum ya uwekezaji *(Export Processing Zones Act* au *Special Economic Zones Act).*

Mheshimiwa Spika, lengo la marekebisho haya ni kuwafanya walipa kodi waliotajwa kuweza kukusanya kodi ya zuio kwa malipo ya kodi ya pango, riba na gawio yanayofanywa na kampuni ambazo hazina msamaha wa Kodi ya mapato.

Mheshimiwa Spika, pili, ni kutambua msamaha wa kodi kwenye riba inayolipwa na Serikali kwa mikopo inayotolewa kwa Serikali za kigeni na benki na taasisi za fedha za nje ya nchi ili kuwezesha Serikali kupata mikopo kwa ajili ya utekelezaji wa miradi yake. Hata hivyo, msahama husika utahusu mikataba yenye masharti ya utoaji wa msamaha wa kodi kwenye riba.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Nane ya Muswada inayohusu marekebisho ya Sheria ya Bima Sura 394 imefutwa kupitia jedwali la marekebisho.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tisa kama ilivyorekebishwa inapendekeza marekebisho kwenye Sheria ya Ardhi, Sura 113 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, mapendekezo yaliyobainishwa kupitia Ibara ya 30 ya Muswada yamefutwa kupitia jedwali la marekebisho. Pili, kuongeza kifungu kipya cha 33A ili:-

(a) Kusamehe kodi ya pango la ardhi kwa Serikali na taasisi zake na Taassi Zisizo za Kiserikali kama vile Taasisi za Dini kwa ardhi itakayotumika kutoa huduma za elimu, afya na huduma nyingine za kijamii bila kupata faida;

(b) Kumpa mamlaka Kamishna wa Ardhi ya kutoza kodi ya pango ya ardhi kwa sehemu ya ardhi ya taasisi hizo za Serikali ambayo itabainika kwamba inatumika kibiashara; na

(c) Kumpa mamlaka Kamishna wa Ardhi ya kutoza kodi ya ardhi pale inapobainika kuwa eneo lenye msamaha limebadilisha matumizi ya awali ya kutoa huduma bila faida.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kumi kama ilivyorekebishwa, inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura 290 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, ni kurekebisha vifungu vya 6(m) na 7(1) ili kutambua ada ya mabango ya matangazo ya kibiashara kama chanzo cha mapato kwa Serikali za Mitaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, ni kufuta Ibara ya 35 ya Muswada ili kuondoa pendekezo la utoaji wa *produce cess* kwa kampuni zisizochakata mazao; na Tatu, ni kurekebisha kifungu cha 37 kwa kuongeza kifungu kipya cha 37A(1),(2) na (3) ili:-

(a) Kubainisha mamlaka ya Waziri mwenye dhamana na Serikali za Mitaa kuzitaka Serikali za Mitaa kutenga asilimia kumi (10) ya fedha wanazokusanya kutoka kwenye vyanzo vyao vya mapato kwa ajili ya kuwezesha vikundi vilivyosajiliwa vya vijana, wanawake na walemavu.

(b) Kubainisha mgawanyo wa fedha hizo ambapo asilimia 40 itatolewa kwa vikundi vya vijana, asilimia 40 kwa vikundi vya wanawake na asilimia 20 kwa ajili ya watu wenye ulemavu. *(Makofi)*

(c) Mikopo hiyo itatolewa kwa riba ya asilimia mbili.

(d) Kumpa mamlaka Waziri anayehusika na masuala ya Serikali za Mitaa kuandaa kanuni ambazo zitaweka utaratibu wa kusimamia utoaji wa fedha hizo kwa vikundi vya vijana, wanawake na walemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nne, kurekebisha kifungu cha 42 kwa kufuta kifungu kidogo cha (1) na kukiandika upya ili kuweka sharti kwa halmashauri kushauriana na Mhasibu Mkuu wa Serikali kabla ya kufungua akaunti za benki za halmashauri ili kutekeleza masharti ya Sheria ya Fedha za Umma, Sura ya 348.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kumi na Moja ya Muswada inayohusu Sheria ya Kodi ya Majengo ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, Sura 289 imefutwa kupitia jedwali la marekebisho.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kumi na Mbili, kama ilivyorekebishwa inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 90A cha Sheria ya Madini, Sura 123 kwa kuongeza kifungu kipya cha sita ili kufuta ada ya ukaguzi wa madini *(inspection and clearance fee)* kwenye chumvi. Ada hii hutozwa kwa kiwango cha asilimia moja ya thamani ya madini.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kumi na Tatu kama ilivyorekebishwa inapendekeza kufuta Sheria ya Tume ya Mipango, Sura 341 ili kutekeleza muundo wa Serikali ya Awamu ya Tano ambapo kwa mujibu wa hati ya mgawanyo wa majukumu ya Mawaziri namba 144 ya mwaka 2016 *(The Minister's assignment of Ministerial functions notice 2016),* Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alihamishia majukumu ya iliyokuwa Tume ya Mipango kwa Waziri wa Fedha na Mipango.

Mheshimiwa Spika, kufuatia kufutwa kwa sheria hii, majukumu, mali, madeni, haki, mashauri mbalimbali na mikataba iliyokuwa inahusu Tume ya Mipango itahamishiwa Wizara ya Fedha na Mipango. Waziri wa Fedha na Mipango baada ya mashauriano na Ofisi ya Rais akaweza kuhamishia kwa Wizara au taasisi ya Serikali mali na madeni ya Tume hii ambapo uhamisho huo wa mali na madeni utatangazwa kupitia Gazeti la Serikali.

Mheshimiwa Spika, vilevile watumishi wa iliyokuwa Tume ya Mipango ambao watahitajika katika ofisi mbalimbali za Umma watahamishiwa katika ofisi hizo kwa mujibu wa sheria za utumishi wa umma na wataendelea na maslahi ambayo hayatakuwa chini ya maslahi waliyokuwa wakipata wakiwa Tume ya Mipango.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kumi na Nne kama ilivyorekebishwa inapendekeza kurekebisha Sheria ya Tozo ya Huduma za Bandari, Sura 264 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, moja, Ibara ya 55 ya Muswada imefutwa kupitia jedwali la marekebisho ili kuondoa pendekezo la kuongeza tozo ya bandari; na pili, ni kufuta kifungu cha 5(2) ili kuondoa mamlaka ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha kutoa msamaha wa tozo ya huduma za bandari.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kumi na Tano kama ilivyorekebishwa inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Fedha za Umma, Sura 348 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, moja, ni kubainisha tafsiri ya maneno *Treasury Single Account* na *Sub-treasury Single Account* ndani ya sheria ili kuwezesha utekelezaji wa Akaunti Jumuifu ya Hazina *(Treasury Single Account)*.

Mheshimiwa Spika, pili, ni kuongeza kifungu cha 11A, 11B, 11C na 11D ndani ya sheria hii ili kuanzisha Akaunti Jumuifu ya Hazina *(Treasury Single Account)* itakayofunguliwa Benki Kuu ya Tanzania na kusimamiwa na Mhasibu Mkuu wa Serikali. Akaunti hii itakuwa na jukumu la kupokea fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali na kufanya malipo ya Serikali. Uwepo wa akaunti hii pamoja na mambo mengine utarahisisha usimamizi wa fedha za Serikali kwa kupunguza idadi ya akaunti kwenye Benki za Biashara na Benki Kuu, kupunguza gharama za kibenki zinazolipwa hivi sasa na Serikali kufuatia huduma zinazotolewa kwa Serikali na Benki za Biashara, kupunguza nakisi kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali ambapo fedha zilizopo kwenye *account* za Amana zitajumuishwa kwenye ukokotoaji wa bakaa katika Mfuko Mkuu wa Serikali tofauti na utaratibu wa hivi sasa ambapo akaunti hizi hazijumuishwi katika ukokotoaji huo.

Mheshimiwa Spika, tatu, aidha kupitia marekebisho haya Waziri mwenye dhamana na masuala ya fedha

amepewa dhamana ya kuandaa kanuni za kuwezesha utekelezaji wa Akaunti Jumuifu ya Hazina ambayo itaanza kufanya kazi tarehe 30 Septemba, 2018.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kumi na Sita kama ilivyorekebishwa inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Ushuru wa Mafuta, Sura ya 220 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, moja ni kufanya marekebisho ya kiuandishi na kurekebisha kifungu cha 3 kwa kuweka tafsiri ya maneno *Road Agency* na *TANROADS* ili kutambua ndani ya sheria Taasisi nyingine zilizoanzishwa kwa ajili ya usimamizi na ukarabati au ujenzi wa barabara; Mbili, ni kufanya marekebisho ya kifungu cha 4(3) kinachohusu matumizi ya fedha za mfuko ili kuuwezesha mfuko kutekeleza majukumu yake kwa urahisi; na Tatu, ni kufanya marekebisho ya kiuandishi katika kifungu cha 5(4)(6) na (7) na kuongeza kifungu kidogo kipya cha (5) ili:

Mheshimiwa Spika, kwanza, kubainisha kwamba Maafisa wote Waandamizi wa Mfuko wataajiriwa na Bodi; Pili, kuweka sharti kwa wakusanyaji wa tozo na ushuru chini ya sheria hii kuwasilisha taarifa za kila mwezi kwa Bodi.

Mheshimiwa Spika, tatu, kubainisha kwamba Bodi itawasilisha taarifa ya mwaka ya mfuko kwa Waziri mwenye dhamana na masuala ya barabara na Waziri huyo ndiye atakuwa na mamlaka ya kuiwasilisha Bungeni. Hivi sasa sheria inamtambua Waziri wa Fedha ambapo kiuhalisia Waziri mwenye dhamana na barabara ndiye anayetekeleza jukumu hili.

Mheshimiwa Spika, nne ni kufanya marekebisho ya kiuandishi katika kifungu cha 6(1) ili kuleta maana iliyokusudiwa, na; Tano, kurekebisha kifungu cha 14(1) na kuongeza kifungu cha 14A ili kuongeza makosa yatakayostahiri adhabu chini ya sheria hii, ikiwemo matumizi ya mafuta yaliyopewa msamaha kwa shughuli ambayo haikukusudiwa, kutolipa ushuru wa mafuta pale inapostahili na matumizi mabaya ya fedha za Mfuko wa Barabara.

Mheshimiwa Spika, sita, ni kurekebisha jedwali la nne la sheria kwanza kwa kufanya marekebisho ya kiuandishi ili kuleta maana iliyokusudiwa na pili kuweka utaratibu wa uteuzi wa Makamu Mwenyekiti wa Bodi ambapo inapendekezwa Wajumbe wateue mmoja wao katika nafasi hiyo.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kumi na Saba ya Muswada inayohusu marekebisho ya Sheria ya Katani imefutwa kupitia jedwali la marekebisho.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kumi na Nane kama ilivyorekebishwa inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania, Sura 399 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kurekebisha kifungu cha 20, kwa kufanya marekebisho ya kiuandishi ili kutambua cheo cha Ukurugenzi ambacho kinatumika *TRA*. Hivi sasa sheria inatambua Makamishna pekee wakati zipo Idara ndani ya *TRA*...

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri sasa umalizie, kama dakika tano hivi umalizie, kengele ya pili ilishalia.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Sawa.

Mheshimiwa Spika, sheria inatambua Makamishina pekee wakati zipo Idara ndani ya *TRA* zinazoongozwa na Wakurugenzi.

Mheshimiwa Spika, pili, ni kufuta kifungu cha 33(2) ili kuondoa utaratibu isiotumika unaomwezesha Waziri mwenye dhamana na masuala ya fedha kurekebisha sheria za kodi kwa kutumia hati ya kisheria baada ya Bunge idhini kupitia azimio.

Mheshimiwa Spika, tatu, ni kufuta kifungu cha 35 kinachohusu maombi *TIN* kwa maudhui ya kifungu hiki yamebainishwa katika Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Sura 438 kama ilivyobainishwa kwenye Ibara ya 77 ya Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hotuba hii imegawiwa kwa Waheshimiwa Wabunge. Naomba hotuba yote iingizwe kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya hatua zilizobainishwa katika hotuba ya bajeti zitatekelezwa na Waziri husika kupitia kanuni na matangazo ya Serikali *Government Notices* kwa mujibu wa matakwa ya sheria husika, hatua hizo ni pamoja na kufuta ushuru wa mazao ya chumvi unaotozwa na baadhi ya halmashauri. Hata hivyo, halmashauri ambazo zinategemea ushuru wa mazao haya kama chanzo kikuu cha mapato zitaendelea kutoza ushuru huo.

Mheshimiwa Spika, pili, ni kufuta ada na tozo mbalimbali kwenye bidhaa za chumvi kama ilivyobainishwa katika hotuba ya bajeti na; tatu, kufuta ada mbalimbali zinazotozwa na Mamlaka ya Afya na Usalama.

Mheshimiwa Spika, hitimisho, kama nilivyoeleza hapo awali mengi ya marekebisho ninayopendekeza ni utekelezaji wa kisheria wa mapendekezo ya Serikali kuhusu bajeti ya mwaka wa fedha 2018/2019 ambayo tayari yameridhiwa na Bunge hili wakati wa kuhitimisha hotuba ya bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba sasa Waheshimiwa Wabunge waujadili Muswada huu na hatimaye wakubali kuupitisha ili kuwezesha Serikali kutekeleza mipango ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA AFYA, NA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Ahsante sana. Hoja imetolewa na imeungwa mkono, tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango kwa kuwasilisha hoja yako. *(Makofi)*

**MAELEZO YA MHE. DKT. PHILIP ISDOR MPANGO (MB), WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO, AKIWASILISHA BUNGENI MUSWADA WA SHERIA YA FEDHA WA MWAKA 2018 (THE FINANCE ACT, 2018) KAMA ULIVYOWASILISHWA MEZANI**

1. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja kwamba, Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2018 **(The Finance Act, 2018)** pamoja na marekebisho yake sasa **usomwe kwa mara ya pili.**

2. ***Mheshimiwa Spika***, awali ya yote napenda kutambua michango iliyotolewa na Kamati ya Bunge ya Bajeti chini ya Mwenyekiti wake **Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia, Mbunge wa Mtwara Vijijini** wakati wa kuujadili Muswada huu na kutoa ushauri. Wakati wa kipindi chote cha majadiliano Kamati ilitoa michango na changamoto nyingi kwa Serikali kuhusu vyanzo mbalimbali vya mapato pamoja na namna bora ya kukusanya kodi kwa ajili ya maendeleo ya wananchi.

3. ***Mheshimiwa Spika***, napenda kulihakikishia Bunge lako tukufu kwamba, Muswada huu umezingatia kwa kiasi kikubwa ushauri na mapendekezo mazuri ya Kamati. Aidha, Serikali itaendelea kufanyia kazi mapendekezo mengine ya Kamati kwa lengo la kuongeza mapato ya Serikali, katika mwaka ujao wa fedha.

**O:** By deleting Clause 30.

**P:** In Clause 31, by deleting the proposed subsection (1) of section 33A and substituting for it the following new subsection:

“(1) Notwithstanding any provisions under this Act, the payment of rent for a right of occupancy shall not be paid exclusively for-

(a) central or local government use;
(b) government institution or organisation use;
(c) non profit organizations including religious institutions which provide health, education or other social services which are not profit oriented.

(2) The Minister may, by regulations set criteria for determining activities which are exempted from the payment of rent for right of occupancy under subsection (1)(c).”.

**Q:** By deleting Clause 33 and substituting for it the following-

“Amendment of section 6

**33**. The principal Act is amended in section 6(m) by adding immediately after the word “taxes” the phrase “fees for commercial advertisement on billboards posters or hoarding.”.

**R:** By deleting Clause 34 and substituting for it the following:

“Amendment of section 7

**34**. The principal Act is amended in section 7(1) by deleting paragraph (r) and substituting for it the following:

“(r) fee for commercial advertisement on billboards posters and hoarding;”.

**S:** By deleting Clause 35.

**T:** In Clause 36, by deleting subclauses (2) and (3) appearing in the proposed section 37A and substituting for them the following:

“(2) The funds set aside under subsection (1), shall be appropriated equally as loans to registered groups of women, youths and disabled persons in the following proportion:

(a) forty percent for women and forty percent for youth; and
(b) twenty percent for disabled persons.

(3) Loan issued under this section shall be charged two percent interest.”.

**U:** By deleting Part XI.

**V:** By deleting Clause 55.

**W:** In Clause 59, by-

(a) deleting the words “and local government own source” appearing in the proposed section 11B(1)(c); and
(b) deleting the proposed section 11D and substituting for it the following:

“Operation of TSA

11D. The Treasury Single Account shall come into operation on the 30th day of September, 2018.”.

**X:** By deleting Part XVII.

**Y:** In Clause 81, by-

(a) inserting immediately at the end of subparagraph (ii) the words “; or”; and
(b) adding immediately after subparagraph (ii), the following:

“(iii) a grant agreement duly approved by the Minister in accordance with the provisions of the Government Loans, Grants and Guarantees Act entered between local government authority and a donor.

Cap.134

**Z:** By deleting Clause 82.

**AA:** In Clause 84, by-

(a) deleting paragraph (a) and substituting for it the following:

“(a) in item 3, by adding immediately after sub-item 33 the following new sub-items:

“

| | | |
|---|---|---|
| 34. | Oil-cake of soya beans | 2304.00.00 |
| 35. | Oil cake and other solid residues of cotton seeds | 2306.10.00 |
| 36. | Oil cake and other solid residues of sunflower seeds | 2306.30.00 |
| 37. | Maize Bran | 2302.10.00 |
| 38. | Wheat Bran | 2302.30.00 |
| 39. | Lysine | 2922.41.00 |
| 40. | Methionine | 2930.40.00 |
| 41. | Mycotoxin binders | 3824.10.00 |

”;

(b) deleting HS code “10.12.20” appearing in paragraph (d) and substituting for it HS code 2710.12.20; and

(c) deleting paragraph (e) and substituting for it the following:

“(e) adding immediately after item 22 the following new items:

“

| | |
|---|---|
| 23. | Revenue Stamps of HS Code 4907.00.90 |
| 24. | Electronic cash register Code 8470.50.00 |

”

**BB:** By renumbering-

(a) Part IX to XX as Part VIII to XVII; and

(b) sections 6 to 84 as sections 5 to 69.

Dodoma, **PIM**

…… June, 2018 *MoFP*

**FURTHER SCHEDULE OF AMENDMENT TO BE MOVED BY HON. PHILIP MPANGO, THE MINISTER FOR FINANCE AND PLANNING AT THE SECOND READING OF THE BILL ENTITLED "THE PUBLIC PRIVATE PARTNERSHIP (AMENDMENT) ACT, 2018"**

*(Made under S.O 88(6))*

A Bill entitled "The Public Private Partnership (Amendment) Act, 2018 is further amended as follows:

**A:** In paragraph C: which amends Clause 4 by deleting paragraph (c) and substituting for it the following:

"(c) deleting subsection (6) and substituting for it the following:

"(6) Every contracting authority shall, at the beginning of every budget cycle, submit to the PPP Centre concept note and prefeasibility study of potential public private partnership projects:

Provided that-

(a) the potential public private partnership project complies with the national development priorities; and

(b) the concept note and prefeasibility study of potential public private partnership projects is approved by the respective Minister.""

**B:** In paragraph H: which amends Clause 10 by deleting the proposed subsection (3A) appearing in paragraph (e) and substituting for it the following:

"(3A) The Minister may make regulations prescribing procedure for deposit and refund of commitment deposits under subsection (3)."

Dodoma, **PIM**

…………………, 2018 *MFP*

**FURTHER, FURTHER SCHEDULE OF AMENDMENT TO BE MOVED BY HON. PHILIP I. MPANGO,THE MINISTER FOR FINANCE AND PLANNING AT THE SECOND READING OFA BILL ENTITLED "THE FINANCE ACT, 2018"**

*Made under S.O.86 (10)(b)*

The Bill entitled "The Finance Act, 2018" is further amended as follows:

**A:** By inserting immediately after Clause 3 the following new clause:

"Amendment of the section 2

**4**. The principal Act is amended in section 2, by inserting the words "save for sections 35 and 36," at the beginning of section 2.

Dodoma
………. June, 2018

**PIM**
*M&FP*

**SCHEDULE OF AMENDMENT TO BE MOVED BY BUDGET COMMITTEE AT THE SECOND READING OF THE BILL ENTITLED "THE FINANCE ACT, 2018"**

*[Made under SO 86 (11))]*

The Bill entitled "The Finance Act, 2018" is generally amended as follows-

**A:** In Clause 4 by deleting the phrase "voted and non voted funds" and substituting for it "voted funds and balance carried forward"

**B:** In Clause 8, by deleting the proposed section 14A.-(1) and replacing it with the following:

> "There shall be a register to be kept by every licensing authority at its principal office which shall contain name of the business, particulars of the owner, type of business and such other business licence information as may be prescribed in the regulations."

**C:** By deleting Part IV.

**D:** In Clause 14, as follows-

| Heading | H.S. Code No. | Description | Unit | Old Excise Rate | New Excise Rate |
|---|---|---|---|---|---|
| 20.09 | | Imported fruit juices | | Tshs. 221.00 per litre | Tshs. 271.00 per litre |
| | HS.2204.10.00 | Other | | Tshs. 2,349.00 per litre | Tshs. 2,849.00 per litre |
| | HS.2204.21.00 | Other | | Tshs. 2,349.00 per litre | Tshs. 2,849.00 per litre |

| Heading | H.S. Code No. | Description | Unit | Old Excise Rate | New Excise Rate |
|---|---|---|---|---|---|
| | HS.2204.29.00 | Other | | Tshs. 2,349.00 per litre | Tshs. 2,849.00 per litre |
| | HS.2208.20.00 | -Spirits obtained by distilling domestic grape wine or grape marc content exceeding 75% | | Tshs. 3,481.00 per litre | Tshs. 450 per litre |
| | 2208.90.10 | -Domestic distilled spirits<br><br>-Imported distilled spirits | | Tshs. 3,481.00 per litre<br><br>Tshs. 3,481.00 per litre | Tshs. 2,000 per litre<br><br>Tshs. 3,655.05 per litre |

**E:** In Clause 17, by-

(a) deleting the proposed schedule and replace it with the following:

| Item No. | Type of Game | Gaming Tax |
|---|---|---|
| 1. | Sports betting | Twenty percent of gross gaming revenue |
| 2. | SMS Lotteries | Twenty percent of gross gaming revenue |

| | | |
|---|---|---|
| | | |
| 3. | Slot machines | Tshs. 60,000 per machine per month |
| 4. | National Lotteries | Twenty percent of gross gaming revenue |
| 5. | Forty Machines Sites | Twenty percent of gross gaming revenue |

**F:** In Clause 24, by-

(a) deleting paragraph (a);

(b) deleting paragraph (b) and replace it with the following-

"(c) a newly established entity, or any entity which has been in production for three years at the commencement of this Act, dealing in the manufacture of pharmaceuticals for human or veterinary medicines, sanitary pads, agricultural inputs and implements or leather products or for preserving fishery products and having a performance agreement with the Government of the United Republic of Tanzania shall be taxed at a reduced corporate rate of twenty percent for five consecutive years from year of commencement of production."

**G:** By deleting Part VIII.

**H**: By deleting Clause 30.

**I**: By deleting Clause 31.

**J:** By deleting Clause 34 and substituting for it the following-

"33. The principal Act is amended in section 7(1) by-

a) by inserting the phrase "salt producers whose produce cess shall be zero and" between the word "except" and "for";

b) deleting paragraph (r) and substituting for it the following-

(r) fees for commercial advertisement on stationary billboards, posters or hoarding;"

**K:** By deleting Clause 35.

**L:** In Clause 36, by re-writing the proposed section 37A.-(2) and (3) as follows-

"(2) The funds so set aside under subsection (1) shall be appropriated equally as loans to registered groups of women, youth and disabled by forty per centum for women, forty per centum for youth and twenty per centum for disabled."

"(3) Loans issued under this section shall be subjected to interest at the rate of two per centum."

**M:** In Clause 37, by adding the following phrase at the begging-

"Without prejudice to section 15 of the Public Finance Act,"

**N:** By deleting Part XI.
**O:** By deleting Part XIII.

**P:** In Clause 59, by

a) deleting the proposed section 11B (1) (c) and substitute for it the following-

"to receive balance carried forward from Sub-TSA;"

b) deleting section 11B (2); and

c) re-designating section 11B (1) as section 11B.

**Q:** In Clause 59, by deleting section 11D as proposed and substitute for it the following:

"The Treasury Single Account shall come into operation on the 30th day of September, 2018."

**R:** In Clause 60, by-

"Retaining the proposed section as follows-

The principal Act is amended in section 12 by adding immediately after subsection (1) the following proviso:

Provided that, this subsection shall not apply to amounts allocated to the fund from the Consolidated Fund and any other funds or moneys referred to under Article 135(2) of the Constitution."

**S:** In Part XVI, by adding new Clauses at the end of this part as follows-

(a) "70. The principal Act is amended in section 4A (b) by deleting figure "50" at any place it appear and substituting for it figure "100".

(b) "71. The principal Act is amended by deleting the Second Schedule and substituting for it the following-

**SECOND SCHEDULE**

*(Made under section 7(6))*

**TOLLS FUEL FILLING POINT**

| | *Fuel* | *Rate of Toll* |
|---|---|---|
| 1. | Petrol (MPS and MSR)……………… | Shillings 363/= per litre |
| 2. | Diesel (GO)…………………………….. | Shillings 363/= per litre |

**T:** In Part XVIII, by adding a new Clause as follows-

"76. The First Schedule is amended by deleting item 1 and 5 appearing in Part B."

**U:** In Part XX, by-

a) adding a new Clause as follows-

"80. The principal Act is amended in section 48 by adding a new sub-section (2) as follows-

48.-(2) Notwithstanding the provisions of sub-section (1) of this section, where water, gas, oil, electricity or thermal energy is supplied throu gh pipeline, cable or other continuous distribution network from a place in Mainland Tanzania and delivered to a place in Tanzania Zanzibar shall be treated as a supply made in Zanzibar."

b) Renumbering section 48 as section 48(1).

**V:** In Clause 81, by-

a) adding the phrase "or any local government authority" between the words "Tanzania" and "and";
b) adding the following new paragraph (ii)-
a grant through an agreement between a local authority and a donor for financing community based projects in the area of jurisdiction of the local authority."

**W:** By deleting Clause 83.

**X:** In Clause 84, by-

(a) adding the following in paragraph (a)-

| | | |
|---|---|---|
| 35 | Oil cake and other solid residues of cotton seeds | 23.06.30.00 |
| 36 | Oil cake and other solid residues of sunflower seeds | 2306.30.00 |

(b) deleting item 1 in paragraph (b) and substituting it with the following:

| | | |
|---|---|---|
| 1 | Essential human and veterinary medicine, drugs and equipment which have been approved by the Minister responsible for health or livestock, as the case may be. | |
| | | |

(c) adding new item 3 in paragraph (b) as follows:

| | | |
|---|---|---|
| | Equipment for agricultural and livestock | |
| | | |

(d) deleting paragraph (c) and replace it with the following:
"The Principal Act is amended in the Schedule by adding a new part as follows-

PART III

ZERO-RATED SUPPLIES

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Sanitary Pads | 9619.00.10 |
| | | |

(e) deleting paragraph (e);

(f) in item 1, by adding immediately after sub-item 23 the following new sub-items:

| | | |
|---|---|---|
| 24. | Meter pumps for irrigation | |
| 25. | Solar pumps | |
| 26. | Equipment for drilling | |

(g) in item 3, by adding immediately after sub-item 34 the following new sub-item:

| | | |
|---|---|---|
| 35. | Seed Packaging Materials<br><br>Provided that, the packaging material is specifically designed for packaging seeds and printed for use by local manufacturer whose name appears on the packaging material. | |
| | | |

(h) in item 8, by adding immediately after sub-item 10 the following new sub-item:

| | | |
|---|---|---|
| 11. | Milk Packaging Materials<br><br>Provided that, the packaging material is specifically designed for packaging milk and printed for use by local manufacturer whose name appears on the packaging material. | |
| | | |

(i) adding a new item 24 immediately after item 23 as follows:

"24. Equipment and machines used for gemstones and jewelry lapidary."

**Y:** By-

(a) Renumbering Parts **V, VI, VII, VIII, IX, X, XII, XIV, XV, XVI, VIII, XIX** and **XX** as Parts **IV, V,VI, VII, VIII, IX, X, XI, XII, XIII, XIV, XV**, and **XVI** respectively; and

(b) Clauses **13** up to **84** as Clause **11** to **66** respectively.

Dodoma, (SIGNED)
28th June, 2018 ... Constituency

**FURTHER SCHEDULE OF AMENDMENTS TO BE MOVED BY BUDGET COMMITTEE AT THE SECOND READING OF THE BILL ENTITLED "THE FINANCE ACT, 2018"**

*[Made under SO 86 (11))]*

The Bill entitled "The Finance Act, 2018" is further amended as follows-

**A:** In item C as follows-

a) deleting item C and substitute for it the following-

i. Part IV is amended by inserting a new Clause 12 as follows

"The principal Act is amended in section 5 (2) by inserting a new paragraph (d) as follows-

(d) Supervise, administer and regulate the utilization of the cashew nut industry development levy as shall be remitted to it by the Ministry responsible for finance;

ii. Re-designate paragraph (d) to (g) as paragraphs (e) to (h) respectively.

b) By adding a new Clause 12A after the proposed Clause12 as follows-

"12A.The principal Act is amended in Clause 17A as follows-

"(a) deleting subsection (2) and substituting for it the following:

(2) The total amount of export levy collected under subsection (1) shall be apportioned to the Cashewnut Board of Tanzania and the Consolidated Fund after consultations between the Minister responsible for finance and stakeholders of cashewnut industry.

(3) The money apportioned to the Board shall have due regard to the following requirements-

(a) research necessary for the development of the cashewnut industry;

(b) training and capacity building;

(c) marketing information;

(d)industrial development aimed at cashewnut crops processing; and

(e) any other requirement aimed at developing the cashewnut industry.

c) By adding a new Clause 12B after the proposed Clause 12A as follows-

i. "The principal Act is amended in section 25 by inserting a new paragraph (b) as follows-
(b) sums of money remitted by the Ministry responsible for finance from collections of export levy charged on exportation of raw cashewnut; and

ii. re-designate paragraph (b) to (d) as new paragraphs (c) to (e) respectively.

**B:** In item D, by deleting and substituting for it the following-
"Clause 14 is amended as follows-

**FOURTH SCHEDULE**

*(Made under section 124(2))*

| Heading | H.S. Code No. | Description | Unit | Old Excise Rate | New Excise Rate |
|---|---|---|---|---|---|
| 20.09 | | Imported fruit juices | | Tshs. 221.00 per litre | Tshs. 271.00 per litre |
| | HS.2204.10.00 | Other | | Tshs. 2,349.00 per litre | Tshs. 2,849.00 per litre |
| | HS.2204.21.00 | Other | | Tshs. 2,349.00 per litre | Tshs. 2,849.00 per litre |
| | HS.2204.29.00 | Other | | Tshs. 2,349.00 per litre | Tshs. 2,849.00 per litre |
| | HS.2208.20.00 | -Spirits | | Tshs. 3,481.00 | Tshs. 450 |

| Heading | H.S. Code No. | Description | Unit | Old Excise Rate | New Excise Rate |
|---|---|---|---|---|---|
| | | obtained by distilling domestic grape wine or grape marc content exceeding 75% | | per litre | per litre |
| | 2208.90.10 | -Imported distilled spirits | | Tshs. 3,481.00 per litre | Tshs. 3,655.05 per litre |
| | 2208.30.00 | -whiskies | | Tshs. 3,481.00 per litre | Tshs. 3,981.00 per litre |
| | 2208.40.00 | -rum and other spirits obtained by distilling fermented sugar cane products | | Tshs. 3,481.00 per litre | Tshs. 3,900.00 per litre |
| | 2208.50.00 | Gin and geneva | | Tshs. 3,481.00 per litre | Tshs. 3,900.00 per litre |
| | 2208.60.00 | vodka | | Tshs. 3,481.00 per litre | Tshs. 3,900.00 per litre |
| | 2208.70.00 | Liquors and cordials | | Tshs. 3,481.00 per litre | Tshs. 3,900.00 per litre |
| | 2208.90.90 | other | | Tshs. 3,481.00 per litre | Tshs. 3,900.00 per litre |

**C:** In item E, by-

a) inserting a new paragraph (a) as follows-

"The principal Act is amended in section 31A by-

i. deleting subsection (1) and substituting for it the following-

"(1) The gaming tax of eighteen per centum on winnings is hereby imposed on the amount or value of the winnings in connection with operation of the gaming activities.

ii. Adding a new sub-section (4) as follows-

"(4) For the purposes of this section, winnings means the positive difference between a payout made and stakes in a month by each player, payable to a winner by the licensed sports betting operator under this Act."

b) re-designate paragraph (a) as (b).

**D:** In item X, by-

a) deleting paragraph (b) and replace it with the following

| | | |
|---|---|---|
| 1 | Essential human and veterinary medicine, drugs and equipment which have been approved by the Minister responsible for health or livestock, as the case may be and Packaging materials specifically designed for packaging pharmaceutical product and printed for use by a local manufacturer whose name appear on packaging material. | |
| | | |

b) in item 1, by adding immediately after sub-item 23 the following new sub-items:

| | | |
|---|---|---|
| 24. | Solar water pumps | |
| 25. | Water pumps with meters | |
| 26. | Equipment used for drilling borehole for water | |

c) re-numbering item 25 to 27 as item 26, 27 and 28 respectively;

d) in item 3, by adding immediately after sub-item 34 the following new sub-item:

| | | |
|---|---|---|
| 35. | Seed Packaging Materials<br><br>Provided that, the packaging material is specifically designed for packaging seeds and printed for use by local manufacturer whose name appears on the packaging material. | |
| | | |

e) re-numbering item 35 to 37 as item 36, 37 and 38 respectively;

f) in item 8, by adding immediately after sub-item 10 the following new sub-item:

| | | |
|---|---|---|
| 11. | Milk Packaging Materials<br><br>Provided that, the packaging material is specifically designed for packaging milk and printed for use by local manufacturer whose name appears on the packaging material. | |
| | | |

g) adding a new item 24,25 immediately after item 23 as follows:

“24. Equipment and machines used for gemstones and jewelry lapidary.”
"25. Excavator and bulldozer used for construction of Dams by registered farmers.

h) re-numbering item 10 and 11 as item 11 and 12 respectively.

Dodoma,
28th June, 2018

**HAG**
Chairperson – Budget Committee

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa moja kwa moja nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti na baada ya Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti tutaanza na uchangiaji kwa sababu kama kawaida Upinzani wao hawana mawazo ya upande wa pili na safari hii sijui watasema nini kwamba Spika amekalia hotuba yao.

Waheshimiwa Wabunge, hivyo, baada tu ya Mwenyekiti wa Kamati ya bajeti tunashukuru kupata nusu saa ya Upinzani ya bure. Mheshimiwa Leah Komanya utakuwa mchangiaji wa kwanza jiandae, Mheshimiwa Mwenyekiti wa Bajeti tafadhali, uzingatie muda una nusu saa.

**MHE. HAWA A. GHASIA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 86(5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2016, naomba kutoa maoni na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha ya Mwaka 2018.

Mheshimiwa Spika, tarehe 14 Juni, 2016, Waziri wa Fedha na Mipango aliwasilisha Bungeni Mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fedha kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018, 2018/2019 na kuelezea hatua mbalimbali za kodi, ushuru, ada na tozo zitakazochukuliwa na Serikali zenye lengo la kuongeza mapato ili kugharamia Bajeti ya mwaka wa fedha wa 2018/2019.

Mheshimiwa Spika, baada ya mawasilisho ya Waziri, uliagiza Kamati ya Bunge ya Bajeti kuchambua Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2018 na kushauriana na Serikali kisha kutoa maoni kuhusu Muswada huo.

Mheshimiwa Spika, madhumuni wa Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2018 una lengo la kufanya marekebisho kwenye Sheria mbalimbali kwa kubadili mfumo wa kodi, ushuru na tozo mbalimbali. Marekebisho hayo

yanalenga kurekebisha viwango, kupunguza au kufuta baadhi ya kodi, ushuru au tozo mbalimbali. Kwa msingi huo, Muswada huu unakwenda kufanya marekebisho ya sheria kumi na tisa (19).

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bajeti, kwa nyakati tofauti ilifanya vikao na wadau mbalimbali wanaoguswa na Muswada huu ili kupata maoni yao. Tarehe 20 na 21 Juni, 2018 Kamati ilikutana na Wadau wafuatao:-

Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania *(TPSF);* Wamiliki wa Viwanda Tanzania *(CTI);* Baraza la Kilimo (*Agriculture Council of* Tanzania); Kiwanda cha Nguo *(A to Z Textiles Mills Ltd);* Wadau wa Michezo ya Kubahatisha; Wazalishaji wa Chumvi; Viwanda vya Sigara vya *TCC* na *PMI;* Viwanda vya Vinywaji Baridi *(Pepsi, Cocacola na Azam)*; Viwanda vya Bia (Serengeti na *TBL*); Umoja wa Wamiliki wa Viwanda vya Nguo *(TEGAMAT);* Wazalishaji wa Mafuta ya Alizeti Nchini; Kiwanda cha Karatasi *(Mufindi Paper Mills Limited)*; *Tanzania Chambers of Minerals and Energy (TCME);* Jumuiya ya Utalii; na Jumuiya ya Bima.

Mheshimiwa Spika, Kamati imepitia Muswada huu kifungu kwa kifungu kwa madhumuni ya kujielimisha maudhui ya kila kifungu. Baada ya kujiridhisha na maudhui yake, Kamati ilifanya majadiliano ya kina na Waziri wa Fedha na Mipango pamoja na Watendaji wa Wizara yake kuhusu mapendekezo ya marekebisho ya Sheria Kumi na Tisa zilizopo kwenye Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, maoni na ushauri wa Kamati kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha ya mwaka 2018; sheria ya Marekebisho ya Benki Kuu ya Tanzania, Sura 197. Sehemu ya Pili ya Muswada inapendekeza kurekebisha kifungu cha 3 na cha 4 cha Muswada wa Sheria ili kuweka utaratibu wa kuhuisha baadhi ya akaunti zilizoko nje ya Mfuko Mkuu wa Serikali ili kuleta mtengamano wa Sheria katika kupata bakaa halisi ya kiasi cha fedha za Serikali zilizoko benki.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua umuhimu wa marekebisho haya yanayolenga uanzishwaji wa Akaunti Jumuifu ya Hazina. Hata hivyo, Kamati inaona kuwa marekebisho ya kifungu cha nne cha Muswada hayaleti maana sahihi katika masuala ya kifedha na kibajeti kwa kuwa bado tafsiri ya neno *voted* na *non-voted funds* haijatolewa na Serikali kama mbadala wa neno *budgeted revenue na payments of Governments*.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, marekebisho yanayoletwa yanaendelea kutokuwa na maana pamoja na usare kwa kuwa maneno yanayokusudiwa kubadilishwa yanaendelea kutumika kama yalivyo kwenye kifungu cha 35, 36 na 37 cha Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania, Sura ya 197. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati haipingi dhana ya uanzishwaji wa Akaunti Jumuifu, hata hivyo, inaliomba Bunge lako Tukufu litoe fursa kwa Kamati kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango kujiridhisha kwa nadharia na vitendo uanzishwaji wa akaunti hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia kwa upande mwingine, Sheria hii ni ya Muungano, ni muhimu Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ishauriane na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ili kabla ya kuanza utekelezaji kuwepo na maridhiano ya pande zote mbili za Muungano. Aidha, sehemu hii ya Muswada ianze kutumika baada ya mashauriano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua kuwa utaratibu wa Akaunti Jumuifu ya Hazina (*Treasury Single Account –TSA*) unapendekezwa pia na vyombo vya fedha vya kidunia kama vile *IMF* na *World Bank,* hata hivyo utaratibu huu unategemea muundo wa Serikali husika, mifumo ya kitaasisi, mifumo ya fedha, ubora wa mifumo ya mawasiliano, katiba na sheria za nchi husika, maendeleo ya kiteknolojia na ukuaji wa mfumo wa sekta ya benki.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Leseni ya Biashara, Sura ya 208; Sehemu ya Tatu ya Muswada inapendekeza kurekebisha kifungu cha 5 cha Muswada ili kurahisisha utoaji wa leseni za biashara. Kamati haina pingamizi na marekebisho haya kwa kuwa lengo lake ni jema na mamlaka ya utoaji wa leseni yanahama kutoka Serikali Kuu yaani *Central Government* kwenda *BRELA* (*Business Registration and Licensing Agency*). Hii itasaidia kuondoa usumbufu na kero ya upatikanaji wa leseni za biashara.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapendekeza kuwa leseni za biashara zinazotolewa na Mamlaka za Udhibiti pia zitolewe na *BRELA* ili kupunguza uwingi wa leseni, isipokuwa tu kwa michezo ya kubahatisha ambayo mchakato wake wa upatikanaji wa leseni ni mrefu na unahusisha masuala ya *due diligence* hivyo ni vema zikaendelea kutolewa chini ya Bodi ya Michezo ya Kubahatisha.

Mheshimiwa Spika, pia Kamati inapendekeza kuwa marekebisho ya kifungu cha 8(1)(2) na (3) yahusishe pia kuongeza taarifa zaidi katika rejesta kama vile jina la kampuni na kiasi kinachotakiwa kulipwa kama ada.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Tasnia ya Korosho, Sura ya 203; Serikali inapendekeza kufuta kifungu cha 17A cha Sheria ya Tasnia ya Korosho, Sura 203 lengo hasa la mapendekezo haya ni kuondoa utaratibu uliopo sasa wa mgawanyo wa mapato yatokanayo na mauzo ya korosho nje yaani (*export levy*), ambapo Mfuko Mkuu wa Serikali ulikuwa unapata asilimia 35 na Mfuko wa Kuendeleza Sekta ya Korosho unapata asilimia 65. Hivyo, Kamati inapendekeza kuwa sehemu ya Nne ya Muswada huu ifutwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa majukumu ya kuendeleza zao hilo yamehamishiwa kwenye Bodi ya Korosho, Kamati inapendekeza kuwa fedha kwa ajili ya kuendeleza zao la korosho nchini zipelekwe Bodi ya Korosho kupitia Wizara ya Kilimo kwa mgawanyo utakaokubalika kati ya Serikali na Wadau wa Korosho nchini. Hivyo, Kamati inapendekeza kufanya mabadiliko katika kifungu cha 5(1) cha Tasnia ya

Korosho ili pamoja na mambo mengine kuongeza jukumu kwa bodi ya korosho kusimamia uendelezaji wa zao la korosho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura 147; kifungu cha 14 cha Muswada kinachohusu Jedwali la Nne la marekebisho katika Muswada huu Kamati ina maoni yafuatayo:-

(i) Ushuru wa bidhaa kwenye maji ya matunda (juisi) yanayotengenezwa nje na kuingizwa nchini yenye (HS –*Code* 20.09) uongezeke kutoka kiwango cha Sh.221 kwa lita hadi kiwango cha Sh.271 kwa lita. Hatua hii itasaidia kuendeleza na kulinda viwanda vya matunda nchini na kuhamasisha kilimo cha matunda kwa ajili ya viwanda vyetu; pia itaongeza pato la Serikali.

(ii) Jedwali la nne Ushuru wa bidhaa pia irekebishwe kwa kuongeza aya nyingine itakayohusu ushuru wa bidhaa kwenye vinywaji vikali yaani (*spirits*) vinavyotengezwa hapa nchini kwa mchuzi wa zabibu inayozalishwa hapa nchini kwa kiwango kisichopungua asilimia 75 kitozwe kodi ya kiwango cha Sh.450 kwa lita. Hatua hii, inatarajiwa kuhamasisha kilimo cha zabibu Dodoma na kulinda viwanda vya ndani. *(Makofi)*

(iii) Pia kuondoa Kinywaji cha Konyagi kilichotumika kama mfano kwenye HS *Code* 2208.90.10 kwa kuwa kinywaji hicho kinazalishwa hapa nchini.

(iv) Kamati inapendekeza kuongeza ushuru wa bidhaa kwa shilingi 500 kwa bidhaa zenye HS *Code* 2204.10.00, na HS Code 2204.21.00, na HS. Code 2204.29.00. Ongezeko hilo halitakuwa na athari yoyote kwa viwanda vya ndani kwa kuwa bidhaa hizo zinazalishwa nje ya nchi. Hatua hii inatarajia kuchochea uzalishaji wa bidhaa hizo kwa viwanda vya ndani.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Michezo ya Kubahatisha, Sura 41, Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Serikali

ya kurekebisha jedwali la pili kwenye sheria hii kwa kuongeza kiwango cha asilimia 25 *Gross Gaming Revenue (GGR)* kinachotozwa kwenye kodi ya michezo ya kubahatisha yaani (*gaming tax)* kwa michezo ya kubahatisha. Hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali kupunguza kiwango cha tuzo yaani (*winning tax*) kilichopendekezwa na Serikali kutoka asilimia 20 iliyopendekezwa hadi asilimia 18 ya awali.

Mheshimiwa Spika, aidha, upande wa mchezo wa *slot machines*, Kamati inapendekeza kiwango cha kodi cha michezo ya kubahatisha yaani (*Gaming tax)* kilichopendekezwa kishuke kutoka Sh.100,000 kwa mashine hadi Sh.60,000 kwa mashine kwa mashine kwa mwezi.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kamati inapendekeza kufanyia marekebisho kifungu cha 3 cha sheria ya *Gaming tax*, CAP 41 ili kuongeza maana au *definition* ya neno *winnings.* Hata hivyo, kwa mujibu wa mashauriano na wadau wanapendekeza iwe '*Winnings' means the positive difference between a payout made and stakes in a month, by each player, payable to a winner by a licensed sports betting operator under Act*.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura ya 332; Kamati imepitia na kufanya uchambuzi wa kina kuhusu mabadiliko yanayopendekezwa kwenye Sheria hii ya Kodi ya Mapato na ina mapendekezo yafuatayo:-

(i) Kamati ya Bajeti imekubaliana na hatua iliyochukuliwa na Serikali ya kurekebisha Jedwali la Kwanza ili kuweka kiwango cha punguzo la kodi la asilimia 20 kwa miaka mitano tangu kuanza kwa uzalishaji wa madawa ya binadamu na bidhaa ya ngozi kwa viwanda vipya. Pamoja na hatua hii nzuri, Kamati inapendekeza kuwa punguzo hili lihusishe pia viwanda ambavyo tayari vimeanzishwa nchini ambavyo vipo ndani ya miaka mitano toka sheria hiyo kuanza kutumika.

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa kuwa Serikali kupitia hotuba yake imeipa kipaumbele Sekta ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, hivyo basi Kamati inaishauri Serikali kuongeza wigo wa punguzo hili kwa viwanda vya uchakataji mazao ya kilimo yaani *Agro-processing industry* na viwanda vya madawa ya mifugo yaani *Vertenary medicine*.

(ii) Kamati inakubaliana na marekebisho ya kufuta kipengele cha 10(a) ili kutoa fursa kwa Waziri wa Fedha na Mipango kutoa msamaha wa kodi kwenye miradi ya Serikali inayotekelezwa kwa fedha za mikopo ya kibiashara pamoja na kodi ya zuio inayotozwa kwenye riba za mikopo inayotolewa kwa Serikali. Hatua hii itasaidia kutekeleza miradi iliyokwama kutokana na changamoto hii.

(iii) Baada ya mashauriano Serikali imekubaliana na ushauri wa Kamati wa kushusha kiwango cha kodi cha mapato ghafi ya kampuni ambayo inajiendesha kwa hasara kwa zaidi ya miaka mitano kutoka asilimia moja iliyokuwa inapendekezwa hadi asilimia 0.5. Lengo likiwa ni kuziba mianya ya makampuni yanayotengeneza hasara kwa makusudi ili yasilipe kodi yaani *phantom losses"*

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Bima, Sura ya 394, baada ya mashauriano, Serikali imekubali kufuta Sehemu ya Nane ya Muswada kwa lengo la kutoa fursa kwa Serikali kuandaa Sera ya Bima, kupitia upya Sheria ya Bima na baadaye kutengeneza kanuni zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Ardhi, Sura 113, baada ya mashauriano, Serikali imekubali kufuta Ibara ya 30 ya Muswada huu; pendekezo la Sheria ya Ardhi kuhusu pendekezo la pango kwa maeneo yaliyo na hati miliki na yasiyo na hati miliki ya ardhi vijijini. Aidha, Serikali imekubali kufanya marekebisho katika Ibara ya 31 ya Muswada kwa lengo la kutoa msamaha wa kodi ya pango la ardhi kwa Serikali Kuu na Taasisi zake pamoja na kuongeza Serikali za Mitaa. Vilevile marekebisho hayo yamejumuisha Taasisi zisizo za Kiserikali zisizokuwa za kibiashara.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura ya 290; Kamati inakubaliana na marekebisho ya Sheria hii kwa kuongeza kifungu kipya cha 37A ili kuweka utaratibu wa kuzitaka Mamlaka za Serikali za Mitaa kutenga asilimia 10 ya Mapato ya ndani kwa ajili ya kutoa mikopo kwa wanawake na vijana. Serikali imekubaliana na Kamati kuwa mgawanyo wa mapato uwe asilimia 40 wanawake, asilimia 40 vijana na asilimia 20 ya watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Spika, pia, kamati imekubaliana na Serikali kuweka riba ndogo ya asilimia mbili tu ili kuhamasisha wakopaji kuwajibika na hivyo kurudisha rejesho litakalosaidia kuendeleza Mfuko huu. Kamati inashauri kuwa, halmashauri zenye makusanyo madogo zipate ruzuku kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya kuweza kutekeleza sheria hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati inapendekeza marekebisho kwenye kifungu cha 33 cha Muswada ili kiweze kutoa msamaha kwa magari yanayomilikiwa na makampuni husika kutumia matangazo hayo kwenye magari yao pasipo kulipa ada isipokuwa kwa zile *billboards* ambazo zumesimikwa yaani *billboards affixed on trucks and car registered and owned by the company.*

Mheshimiwa Spika, Serikali itoe ufafanuzi wa kifungu cha 6(1)(u) cha sheria hii kinachotaka halmashauri kukusanya asilimia 0.3 ya ushuru wa huduma ya mauzo ghafi ya kutoka kwa makampuni. Kwa kuwa, kifungu hiki kinatumiwa vibaya na baadhi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kutoza ushuru huo kwa wafanyabiashara wadogo kama vile mama lishe na kwa wauza samaki wa reja reja na wengineo ambao siyo makampuni kama Sheria inavyotaka.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kutoa ufafanuzi kuhusu mkanganyiko wa utozaji wa ushuru wa huduma *(Service Levy)* kwa wafanyabiashara wadogo na Mawakala unaofanywa na Halmashauri. Aidha, Kamati inapendekeza kuwa Serikali isifute ushuru wa huduma yaani

*service levy 0.3* kwa viwanda vya chumvi kwa sababu ushuru huo ni chanzo kikuu cha mapato kwa baadhi ya Halmashauri kama vile Uvinza. Hata hivyo, wenyewe Wadau wa chumvi walikubali kutozwa ushuru huo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri mapendekezo ya Serikali kwenye kifungu cha 34 cha Muswada kipengele cha kukusanya kodi za *billboards* na *posters* ambazo zinahusu biashara siyo matangazo ya shughuli za siasa, dini, au shughuli za kijamii.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kamati inaipongeza Serikali kwa kukubaliana na Kamati kufuta kifungu cha 35 cha Muswada kwa kuwa kitaongeza kero kwa wananchi. Vilevile, kwa upande wa kifungu cha 37 cha Muswada huu Kamati inapendekeza kifanyiwe marekebisho kwa kuzingatia kifungu cha 15 cha Sheria ya Fedha za Umma ya Mwaka 2004.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Kodi ya Majengo ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa, Sura 289, Serikali imekubaliana na mapendekezo ya Kamati ya kufuta Sehemu ya Kumi na Moja ya Muswada huu iliyohusu Sheria ya Kodi ya Majengo ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, Sura 289 ambayo ilikuwa na lengo la kuiwezesha Mamlaka ya Mapato kukusanya kodi ya majengo katika maeneo ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa zilizopo Tanzania Bara.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Madini, Sura 123; Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Serikali ya kurekebisha kifungu cha 90A na kuongeza kifungu kidogo cha (5) kinacholenga kutoa msamaha wa tozo ya ukaguzi wa wazalishaji wa chumvi ili kuwezesha ustawi wa sekta ya uzalishaji wa chumvi nchini.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Tume ya Mipango, Sura 314; Kamati ya Bajeti haikubaliani na mapendekezo ya Serikali ya kufuta Sheria ya Tume ya Mipango, Sura ya 314. Kamati, inaona pendekezo la kufuta Sheria hii siyo sahihi kwa sababu uamuzi wa Serikali wa kuunganisha Tume ya Mipango na

Wizara ya Fedha hauondoi umuhimu wa uwepo kwa Sheria hii. Hivyo, endapo sheria hii itafutwa na ikaonekana Tume hii kuhitajika kuwepo miaka ijayo itailazimu Serikali kuja Bungeni ili kutunga upya Sheria hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Tozo ya Huduma ya Bandari, Sura ya 264; Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Serikali ya kutokuongeza tozo ya huduma ya Bandari kwa wasafiri wakazi na wageni kutoka Sh.500 hadi Sh.1,000.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Fedha za Umma, Sura 48, mapendekezo ya Serikali ni kuanzisha vifungu vipya vya 11A, 11B, 11C na 11D vitakavyokuwa na maudhui ya kuanzisha Akaunti Jumuifu itakayofunguliwa Benki Kuu ya Tanzania. Kamati inaliomba Bunge lako likubali kutoa muda zaidi kwa Serikali na Kamati ya Bajeti kuliangalia suala hili kwa undani na kwa niaba ya Bunge ili kuhakikisha suala hili linafanyiwa kazi kwa ufasaha na ufanisi.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kamati inaishauri Serikali kukamilisha mashauriano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuhusu suala hili. Kamati inapendekeza Serikali kufanya mabadiliko katika kifungu cha 11D ili kuweka sharti la kuwezesha utaratibu huu kuanza kutumika tarehe 30 Septemba, 2018 kama ambavyo Mheshimiwa Waziri wa Fedha ametamka.

Mheshimiwa Spika, Mapendekezo ya kutengeneza kanuni chini ya kifungu cha 11C(2) cha Muswada huu yameandikwa kwa lugha pana bila kuwekewa mipaka na hayaendani na majukumu ya Akaunti Jumuifu yanayopendekezwa kwenye kifungu 11B cha Muswada.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Kodi ya Tozo za Barabara na Mafuta, Sura ya 220, Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Serikali yaliyoletwa kwenye Sura ya 16 ya Muswada huu. Aidha, Kamati inapendekeza pia kufanya mabadiliko kwenye Sheria hii *(The Road and Fuel Tolls Act, CAP 220)* kifungu 4A(b) ikisomwa pamoja na Jedwali la pili ili kuongeza kiasi cha Sh.50 kwenye tozo ya mafuta kutoka Sh.50

hadi Sh.100 kwenye mafuta ya *diesel* na *petrol* yanayoingizwa nchini ili kiasi cha fedha kitakachopatikana kipelekwe katika utekelezaji wa miradi ya maji vijijini.

Mheshimiwa Spika,inakadiriwa pendekezo hili litaiongezea Serikali Jumla ya Shilingi bilioni 125 kwa kuangalia mwenendo wa makusanyo wa mwaka wa fedha 2017/2018. Suala hili limekuwa ni kilio cha muda mrefu cha Bunge ili kukidhi mahitaji ya maji hasa vijijini.

Mheshimiwa Spika, wakati Waziri wa Fedha akihitimisha hoja hapa Bungeni, aliliarifu Bunge lako kwamba mafuta...

Mheshimiwa Spika, naomba nisisome niende kwenye *code* zingine, lakini pia naomba kwa umuhimu wa Sheria hii uniongezee muda kidogo.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Sekta ya Katani, Sura 30, Kamati inaipongeza Serikali kwa kukubali mapendekezo ya Kamati ya kuondoa Sura ya 17 kwenye Muswada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania, Sura ya 399; Kamati inakubaliana na mapendekezo yaliyotolewa na Serikali ya kufuta kifungu cha 33(2) cha kurekebisha Muundo wa Mamlaka ya Mapato Tanzania. Hata hivyo, Kamati inapendekeza kufanya mabadiliko katika Jedwali la Kwanza Sehemu B la Sheria ya Mamlaka ya Mapato, Sura 399 ili kuondoa Sheria ya Kodi ya Majengo kwenye orodha ya Sheria zinazosimamiwa na Mamlaka hiyo. Kamati inapendekeza Kifungu cha 16 cha Sheria Mama kufuta Kifungu cha 2 na kifungu cha 2(a) cha Sheria hiyo ili iendane na mahitaji ya wakati huu.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Sura 438; Kamati inakubaliana na marekebisho yanayoletwa na Serikali kwenye sheria hii ili kuimarisha usimamizi wa kodi katika eneo la usajili wa walipa kodi, kusamehe sehemu ya riba au malimbikizo ya madeni ya nyuma ya

riba na adhabu inayotokana na malimbikizo hayo. Hata hivyo, ili kuleta mwitikio mzuri wa utekelezaji wa pendekezo hili, Serikali izingatie kuwalinda walipa kodi watakaojitokeza kutumia fursa hii isipokuwa kwa makosa yafuatayo:-

(i) Usafirishaji haramu wa binadamu; na

(ii) Madawa ya kulevya na ujangili.

Mheshimiwa Spika, hatua hii itasaidia kuhamasisha ulipaji wa kodi na hivyo kuongeza mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura 148; Kamati inakubaliana na marekebisho yanayotolewa na Serikali kwenye Sheria hii. Hata hivyo, Kamati inapendekeza marekebisho yafutayo:-

(i) Kifungu cha 81 cha Muswada kirekebishwe ili kujumuisha pia mikopo na misaada itakayopatikana kutoka katika Taasisi nyingine ambazo sio za Kiserikali kwa ajili ya miradi yenye manufaa ya jamii;

(ii) Kifungu cha 82 na 83 cha Muswada kifutwe ili kuwezesha Asasi zisizokuwa za kibiashara kunufaika na marejesho ya kodi;

(iii) Kifungu cha 84(a) kiboreshwe kwa kuongeza upatikanaji wa mashudu na pamba;

(iv) Kifungu cha 84 (b) kiboreshwe na hivyo kumjumuisha Waziri mwenye dhamana na mifugo. Mapendekezo mengine ni kama yanavyoonekana kwenye *HS code* zilizotajwa hapo chini.

Mheshimiwa Spika, maoni na mapendekezo ya jumla, baada ya uchambuzi wa kina wa Muswada huu na kutoa maoni kama yanavyoonekana kwenye Taarifa hii, naomba kuwasilisha maoni ya jumla kwenye maeneo yafuatayo:-

(a) Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004; Kamati imepata fursa ya kupitia mabadiliko yaliyofanyika katika Sheria ya Forodha ya Afrika Mashariki na kubaini kwamba hatua zilizochukuliwa na Tanzania zina malengo ya kuendelea kutoa unafuu kwa viwanda vya uzalishaji wa bidhaa na vyakula vinavyotumia ngano; kuongeza ufanisi katika udhibiti wa kodi; kuziba pengo la sukari nchini; na kulinda uhamasishaji wa mbegu za mafuta ya kula.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hatua hizi muhimu Kamati inatoa angalizo katika hatua zifutazo:-

(i) Mheshimiwa Spika, Kamati haina pingamizi ya kutoa ushuru wa forodha wa asilimia 15 badala ya asilimia 25 kwenye karatasi. Hata hivyo, Kamati imegundua kuwa *HS Codes* zinazopendekezwa hapa kwenye sheria hazihusiani na kutengeneza karatasi nyeupe zinazotumika kutengeneza vitabu na madaftari, yaani *HS Codes* zilizoainishwa kwenye ukurasa wa 59 wa Hotuba ya Bajeti ya Serikali zinahusu aina za karatasi ambazo wadau wa viwanda nchini wakiwemo Mufindi *Paper mills* wamekuwa wakitengeneza. Hizo zinazotumika kutengeneza karatasi kwa ajili ya mifuko ya saruji, makasha ya kuhifadhi vitu, bahasha, mifuko na vifungashio vya bidhaa ambavyo huuzwa ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, baada ya tathmini Kamati inapendekeza marekebisho haya ya Serikali yahusishe *HS Codes* zinazohusu karatasi za kutengenezea vitabu na madaftari kama vile *HS Code* ambazo zipo katika hotuba yetu na nyingine ili kupunguza gharama kwa wazalishaji na waagizaji wa bidhaa hiyo nchini.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kamati inapendekeza kuwa ushuru wa forodha wa asilimia 25 uendelee kwenye karatasi zinazotumika zenye *HS Code* ambazo zimeorodheshwa katika hotuba ambazo kimsingi ndizo zinazozalishwa kwa wingi na viwanda vyetu vya ndani na

kuuzwa ndani na nje ya nchi na hivyo kuendelea kulinda viwanda vyetu vya ndani.

(ii) Kutoza ushuru wa forodha wa asilimia 25 badala ya asilimia 100 kwenye Sukari ya matumizi inayoagizwa toka nje kwa vibali maalum. Hatua hii itasaidia kulinda viwanda vya uzalishaji wa sukari nchini.

Mheshimiwa Spika, Malipo ya ushuru wa asilimia 15 wa kuingiza sukari ya viwandani; mabadiliko yaliyofanywa na Serikali ya kulipa zaidi kiwango cha asilimia 15 ya ushuru wa forodha kwa Makampuni ya Sukari yanayoagiza bidhaa toka nje yanaendelea kuwa na athari hasi kwa viwanda vinavyotumia sukari ya viwandani kama malighafi ya kuzalisha bidhaa nyingine kama juisi na soda, ukizingatia kwamba katika Jumuiya ya Afrika Mashariki hakuna kiwanda hata kimoja kinachozalisha sukari hiyo.

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa Serikali inadaiwa kiasi cha shilingi bilioni 35 ambayo ilitakiwa kurejeshwa kwa wenye viwanda. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali kubadilisha utaratibu wa kudhibiti sukari ya viwandani.

Mheshimiwa Spika, naomba taarifa hii iiingie kwenye *Hansard* kama ambavyo tumeileta kwa sababu huko ndani tumeangalia pia viwanda vya magunia, tumeangalia jinsi ya kulinda kiwanda cha kuzalisha vyandarua kilichopo Jijini Arusha. Pia tumeangalia jinsi ya kukuza uzalishaji wa tumbaku nchini.

Mheshimiwa Spika, hitimisho, naomba kutumia fursa hii kukushukuru kwa kunipa fursa hii ili niweze kuwasilisha Taarifa ya maoni ya Kamati kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha ya Mwaka 2018/2019 mbele ya Bunge lako Tukufu. Vilevile napenda kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango, Waziri wa Fedha na Mipango na Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango kwa ushirikiano mkubwa walioutoa mbele ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia Sheria nyingi sana ambazo Wizara ilizileta imezitoa kwa ajili ya kwenda kuzifanyia kazi zaidi. Lakini pia tumekubaliana na Waziri wa Fedha kuhusu uanzishaji wa Akaunti Jumuifu uanze tarehe 30 Septemba, 2018 ili kutupa nafasi zaidi kuweza kurekebisha yale ambayo kwa namna moja au nyingine tulikuwa bado hatujaweza kuyakamilisha.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee napenda nimshukuru Makamu wangu Mheshimiwa Jitu V. Soni, Mbunge wa Babati kwa ushirikiano mkubwa anaonipatia pamoja na Wajumbe wa Kamati. Kwa siku hizi mbili tumekuwa tukitoka katika ukumbi kuanzia saa 8.00 usiku.

Mheshimiwa Spika, napenda pia nikushukuru wewe mwenyewe pamoja na Naibu Spika kwa kuiwezesha Kamati kufanya kazi yake vizuri pamoja na Sekretarieti ya Kamati hii.

Mheshimiwa Spika, napenda pia ili kuweka taarifa sahihi, hatukuwasilisha Muswada jana si kwa sababu Kamati ilikwamisha, ni kwa sababu kazi ambayo ilikuwa mbele yetu na Wizara ya Fedha ilikuwa haijakamilika. Hii imetokana na kwamba, wakati sisi Kamati tunaendelea na majadiliano Waziri wa Fedha alikuwa hawezi kuja kwenye Kamati kwa sababu majadiliano ya Wizara ya Bajeti Kuu ya Serikali yalikuwa yanaendelea. Kwa hiyo, asingeweza kutoka ukumbini akaja kwenye Kamati. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri amekuja kwenye Kamati kwa siku mbili na kama unavyofahamu haya ni masuala ya kifedha, ni masuala ya kihasibu, lakini pia ni masuala ya sheria. Kwa hiyo, mnapofikia kwenye suala ni lazima kila mtu aelewe kwa upande wa uchumi linamaanisha nini, kihasibu linamaanisha nini ili wanasheria waweze kutuwekea vizuri kisheria.

Mheshimiwa Spika kwa hiyo, napenda wananchi wote wapuuze na uchochezi ambao unaendelea kwenye magazeti likiwemo Gazeti la Tanzania Daima.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, Mheshimiwa Hawa Ghasia.

**MAONI YA KAMATI KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA FEDHA WA MWAKA 2018 *(THE FINANCE BILL, 2018)* KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI**

## 1.0. UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 86 (5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2016 naomba kutoa maoni na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2018 (The Finance Bill, 2018).

**Mheshimiwa Spika,** tarehe 14 Juni, 2016, Waziri wa Fedha na Mipango aliwasilisha Bungeni Mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fedha kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018, na kuelezea hatua mbalimbali za kodi, ushuru, ada na tozo zitakazochukuliwa na Serikali zenye lengo la kuongeza mapato ili kugharamia Bajeti yake kwa Mwaka wa fedha 2018/19. Baada ya mawasilisho ya Waziri, uliagiza Kamati ya Bunge ya Bajeti kuuchambua Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2018 na kushauriana na Serikali na kisha kutoa maoni kuhusu muswada huo.

## 2.0. MADHUMUNI YA MUSWADA

**Mheshimiwa Spika,** Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2018 una lengo la kufanya marekebisho kwenye Sheria mbalimbali kwa kubadili mfumo wa kodi, ushuru na tozo mbalimbali. Marekebisho hayo yanalenga kurekebisha viwango, kupunguza au kufuta baadhi ya kodi, ushuru au tozo mbalimbali. Kwa msingi huo, muswada huu unakwenda kufanya marekebisho ya sheria **Kumi na Tisa (19).**

## 3.0. UCHAMBUZI WA MUSWADA

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Bajeti, kwa nyakati tofauti ilifanya vikao na wadau mbalimbali wanaoguswa na Muswada huu ili kupata maoni yao. Tarehe 20 na 21 Juni, 2018 Kamati ilikutana na Wadau wafuatao:- Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania *(Tanzania Private Sector Foundation-TPSF)*, Wamiliki wa Viwanda Tanzania *(Confederation of Tanzania Industries –CTI*), Baraza la Kilimo (Agriculture Council of Tanzania), Kiwanda cha Nguo (AtoZ Textiles Mills Ltd), Wadau wa Michezo ya Kubahatisha, Wazalishaji wa Chumvi (TASPA), Viwanda vya Sigara (TCC na PMI), Viwanda vya vinywaji baridi (Pepsi, Cocacola na Azam), Viwanda vya Bia (Serengeti na TBL), Umoja wa wamiliki wa Viwanda vya Nguo (TEGAMAT), Wazalishaji wa mafuta ya Alizeti nchini, Kiwanda cha Karatasi (Mufindi Paper Mills Ltd), *Tanzania Chamber of Minerals and Energy (TCME)*, Jumuiya ya Utalii, Bima

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imepitia Muswada huu kifungu kwa kifungu kwa madhumuni ya kujielimisha maudhui ya kila kifungu. Baada ya kujiridhisha na maudhui yake, Kamati ilifanya majadiliano ya kina na Waziri wa Fedha na Mipango pamoja na Watendaji wa Wizara yake kuhusu mapendekezo ya marekebisho ya **Sheria Kumi na Tisa (19)** zilizopo kwenye Muswada huu.

## 4.0. MAONI NA USHAURI WA KAMATI KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA FEDHA YA MWAKA 2018

### 4.1 Marekebisho ya Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania Sura 197.

**Mheshimiwa Spika**, sehemu ya Pili ya muswada inapendekeza kurekebisha **kifungu cha 3 na 4,** cha Muswada ili kuweka utaratibu wa kuhuisha baadhi ya akaunti zilizoko nje ya Mfuko Mkuu wa Serikali ili kuleta utengamano wa Sheria katika kupata bakaa halisi ya kiasi cha fedha za Serikali zilizoko benki.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua umuhimu wa marekebisho haya yanayolenga uanzishwaji wa Akaunti Jumuifu ya Hazina (Treasury Single Account –TSA) hata hivyo Kamati inaona kuwa marekebisho ya kifungu cha 4 cha muswada hayaleti maana sahihi katika masuala ya kifedha na kibajeti kwa kuwa bado tafsiri ya neno *Voted* na *Non-Voted funds* haijatolewa na Serikali kama mbadala wa neno *budgeted revenue and payments of the Governments*. Hata hivyo marekebisho yanayoletwa yanaendelea kutokuwa na maana pamoja na usare kwa kuwa maneno yanayokusudiwa kubadilishwa yanaendelea kutumika kama yalivyo kwenye kifungu cha 35, 36 na 37 cha Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania, Sura ya 197.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati haipingi dhana ya uanzishwaji wa Akaunti Jumuifu hata hivyo, inaliomba Bunge lako tukufu litoe fursa kwa Kamati kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango kujiridhisha kwa nadharia na vitendo uanzishwaji wa akaunti hiyo.

**Mheshimiwa spika**, kwa kuwa Sheria hii ni ya Muungano, ni muhimu Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ishauriane na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) ili kabla ya kuanza utekelezaji kuwepo na maridhiano ya pande zote mbili za Muungano. Aidha, sehemu hii ya muswada ianze kutumika baada ya mashauriano.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua kuwa utaratibu wa Akaunti Jumuifu ya Hazina (Treasury Single Account –TSA) unapendekezwa pia na vyombo vya fedha vya kidunia kama vile IMF na World Bank hata hivyo utaratibu huu unategemea muundo wa Serikali husika, mifumo ya kitaasisi (quality of public institutions), mifumo ya fedha (financial management systems), ubora wa mifumo ya mawasiliano (communications infrastructure), katiba na sheria za nchi husika, maendeleo ya kiteknolojia (technological development) na ukuaji wa mfumo wa sekta ya kibenki (degree of maturity of the banking system).

## 4.2 Sheria ya Leseni ya Biashara, Sura ya 208

**Mheshimiwa Spika,** sehemu ya tatu ya Muswada inapendekeza kurekebisha kifungu cha 5 cha muswada ili kurahisisha utoaji wa leseni za biashara. Kamati haina pingamizi na marekebisho haya kwa kuwa lengo lake ni jema na mamlaka ya utoaji wa leseni yanahama kutoka Serikali Kuu (Central Government) na kwenda BRELA (Business Registration and Licensing Agency); hii itasaidia kuondoa usumbufu na kero ya upatikanaji wa leseni za biashara. Hata hivyo, Kamati inapendekeza kuwa leseni za biashara zinazotolewa na *Regulatory Bodies* pia zitolewe na BRELA ili kupunguza uwingi wa leseni, isipokuwa tu kwa Michezo ya Kubahatisha ambayo mchakato wake wa upatikanaji wa leseni ni mrefu na unahusisha masuala ya '*due deligence'* hivyo ni vema zikaendelea kutolewa chini ya Bodi ya Michezo ya Kubahatisha.

**Mheshimiwa Spika**, pia Kamati inapendekeza kuwa marekebisho ya kifungu cha 8(1), (2) na (3) yahusishe pia kuongeza taarifa zaidi katika rejesta (register) kama vile jina la kampuni na kiasi kinachotakiwa kulipwa kama ada (*prescribed form*).

## 4.3 Sheria ya Tasnia ya Korosho, Sura ya 203

**Mheshimiwa Spika,** Serikali inapendekeza kufuta kifungu cha 17A cha Sheria ya Tasnia ya Korosho SURA ya 203 lengo hasa la mapendekezo hayo ni kuondoa utaratibu uliopo sasa wa mgawanyo wa mapato yatokanayo na mauzo ya korosho nje (export levy), ambapo Mfuko mkuu wa Serikali ulikuwa unapata asilimia 35 na Mfuko wa kuendeleza sekta ya korosho unapata asilimia 65. Hivyo, Kamati inapendekeza kuwa sehemu ya Nne ya Muswada huu ifutwe.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kuwa majukumu ya kuendeleza zao hilo yamehamishiwa kwenye Bodi ya Korosho, Kamati inapendekeza kuwa fedha kwa ajili ya kuendeleza zao la korosho nchini zipelekwe Bodi ya Korosho kwa mgawanyo utakaokubalika kati ya Serikali na Wadau wa Korosho nchini.

Hivyo, Kamati inapendekeza kufanya mabadiliko katika kifungu cha 5 (1) cha Sheria ya Tasinia ya Korosho ili pamoja na mambo mengine kuongeza jukumu kwa bodi ya korosho kusimamia uendelezaji wa zao la korosho.

### 4.4 Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura 147

**Mheshimiwa Spika,** kifungu cha 14 cha Muswada kinachohusu Jedwali la Nne la marekebisho katika muswada huu Kamati ina maoni yafuatayo:-

(i) Ushuru wa bidhaa kwenye maji ya matunda (juisi) yanayotengenezwa nje na kuingizwa nchini (HS –Code 20.09) uongezeke kutoka kiwango cha shilingi 221.00 kwa lita hadi kiwango cha shilingi 271.00 kwa lita. Aidha, hatua hii itasaidia kuendeleza na kulinda viwanda vya matunda nchini na kuhamasisha kilimo cha matunda kwa ajili ya viwanda vyetu;

(ii) Jedwali la nne la Ushuru wa bidhaa lirekebishwe kwa kuongeza aya nyingine itakayohusu ushuru wa bidhaa kwenye vinywaji vikali (spirits) vinavyotengezwa hapa nchini kwa mchuzi wa zabibu unaotengenezwa hapa nchini kwa kiwango kisichopungua asilimia 75 kitozwe kodi ya kiwango cha shilingi 450 kwa lita. Hatua hii, inatarajiwa kuhamasisha kilimo cha zabibu Dodoma na kulinda viwanda vya ndani.

(iii) Kuondoa Kinywaji cha Konyagi kilichotumika kama mfano kwenye HS Code 2208.90.10 kwa kuwa kinywaji hicho kinazalishwa hapa nchini.

(iv) Kamati inapendekeza kuongeza ushuru wa bidhaa kwa shilingi 500 kwa bidhaa zenye HS Code HS.2204.10.00, HS.2204.21.00, HS.2204.29.00. Ongezeko hilo halitakuwa na athari yoyote kwa viwanda vya ndani kwa kuwa bidhaa hizo zinazalishwa nje ya nchi. hatua hii inatarajia kuchochea uzalishaji wa bidhaa hizo kwa viwanda vya ndani.

### 4.5 Sheria ya Michezo ya Kubahatisha, Sura 41

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Serikali ya kurekebisha jedwali la pili kwenye sheria hii kwa

kuongeza kiwango cha asilimia 25 *Gross Gaming Revenue (GGR)* kinachotozwa kwenye kodi ya michezo ya kubahatisha (*gaming tax)* kwa michezo ya kubahatisha. Hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali kupunguza kiwango cha tuzo (*winning tax*) kilichopendekezwa na Serikali kutoka asilimia 20 iliyopendekezwa hadi asilimia 18 ya awali. Aidha, kwa upande wa mchezo wa *slot machines*, Kamati inapendekeza kiwango cha kodi ya michezo ya kubahatisha (*Gaming tax)* kilichopendekezwa kishuke kutoka shilingi 100,000 (mashine/ mwezi) hadi shilingi 60,000 (mashine/mwezi).

**Mheshimiwa Spika**, aidha Kamati inapendekeza kufanyia marekebsiho kifungu cha 3 cha sheria ya Gaming Act, CAP 41 ili kuongeza maana (definition) ya neno **'winnings'** hata hivyo kwa mujibu wa mashauriano na wadau wanapendekeza iwe **'Winnings' means *'the positive difference between a payout made and stakes in a month, by each player, payable to a winner by a lincensed sports betting operator under Act'***.

### 4.6 Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura ya 332

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imepitia na kufanya uchambuzi wa kina kuhusu mabadiliko yanayopendekezwa kwenye Sheria ya Kodi ya Mapato na ina mapendekezo yafuatayo:-
i. Kamati ya Bajeti imekubaliana na hatua iliyochukuliwa na Serikali ya kurekebisha Jedwali la Kwanza ili kuweka kiwango cha punguzo la kodi la asilimia 20 kwa miaka mitano tangu kuanza kwa uzalishaji wa madawa ya binadamu na bidhaa ya ngozi kwa viwanda vipya. Pamoja na hatua hii nzuri, Kamati inapendekeza kuwa punguzo hili lihusishe pia viwanda ambavyo tayari vimeanzishwa nchini ambavyo vipo ndani ya miaka mitano toka sheria hii kuanza kutumika. Aidha, kwa kuwa Serikali kupitia hotuba yake imeipa kipaumbele sekta ya Kilimo, mifugo na uvuvi, hivyo basi Kamati inaishauri Serikali kuongeza wigo wa punguzo hili kwa viwanda vya uchakataji wa mazao ya kilimo (agro-processing industries) na viwanda vya madawa ya mifugo (vertenary medicine)

ii. Kamati inakubaliana na marekebisho ya kufuta kipengele cha 10A ili kutoa fursa kwa Waziri wa Fedha na Mipango kutoa msamaha wa kodi kwenye miradi ya Serikali inayotekelezwa kwa fedha za mikopo ya kibiashara (non concessional loans) pamoja na kodi ya zuio inayotozwa kwenye riba za mikopo inayotolewa kwa Serikali. Hatua hii itasaidia kutekeleza miradi iliyokwama kutokana na changamoto hii

iii. Baada ya masahauriano Serikali imekubaliana na ushauri wa Kamati wa kushusha kiwango cha kodi cha mapato ghafi ya Makampuni ambayo yanajiendesha kwa hasara kwa zaidi ya miaka mitano kutoka asilimia 1 iliyokuwa inapendekezwa hadi asilimia 0.5. Lengo ikiwa ni kuziba mianya ya makampuni yanayotengeneza hasara kwa makusudi ili yasilipe kodi *"phantom losses"*

## 4.7 Sheria ya Bima, Sura ya 394

**Mheshimiwa Spika**, baada ya mashauriano, Serikali imekubali kufuta sehemu ya Nane ya Muswada kwa lengo la kutoa fursa kwa Serikali kuandaa Sera ya Bima, kupitia upya sheria ya Bima na baadae kutengeneza kanuni zake.

## 4.8 Sheria ya Ardhi, Sura 113

**Mheshimiwa Spika,** baada ya mashauriano, Serikali imekubali kufuta ibara ya 30 ya Muswada huu, pendekezo la Sheria ya ardhi kuhusu pendekezo la pango kwa maeneo yaliyo na hati miliki na yasiyo na hati miliki ya ardhi vijijini. Aidha, Serikali imekubali kufanya marekebisho katika Ibara ya 31 ya Muswada kwa lengo la kutoa msamaha wa kodi ya pango la ardhi kwa Serikali Kuu na taasisi zake pamoja na kuongeza Serikali za Mitaa. Vilevile marekebisho hayo yamejumuisha taasisi zisizo za kiserikali zisizokuwa za kibiashara (Non –Profit Organisation)

## 4.9 Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura ya 290

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inakubaliana na marekebisho ya sheria hii kwa kuongeza kifungu kipya cha 37A ili kuweka

utaratibu wa kuzitaka Mamlaka za Serikali za Mitaa kutenga asilimia 10 ya Mapato ya ndani kwa ajili ya kutoa mikopo kwa wanawake na vijana. Serikali imekubaliana na Kamati kuwa mgawanyo wa mapato uwe asilimia 40 wanawake, asilimia 40 vijana na asilimia 20 walemavu. Pia, kamati imekubaliana na Serikali kuweka riba ndogo ya asilimia 2 tu ili kuhamasisha wakopaji kuwajibika na hivyo kurudisha rejesho litakalosaidia kuendeleza mfuko (revolving fund).

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inashauri kwa Halmashauri zenye makusanyo madogo zipate ruzuku kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya kutekeleza sheria hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapendekeza marekebisho kwenye kifungu cha 33 cha Muswada ili kiweze kutoa msamaha kwa magari yanayomilikiwa na makampuni husika kutumia matangazo hayo kwenye magari yao pasipo kulipa ada *'except for billboard affixed on trucks and cars registered and owned by the company'*

**Mheshimiwa Spika,** Serikali itoe ufafanuzi wa kifungu cha 6 (1) (u) cha sheria hii kinachotaka Halmashauri kukusanya asilimia 0.3 ya Ushuru wa huduma ya mauzo ghafi ya kutoka kwa Makampuni. Kwa kuwa, kifungu hiki kinatumiwa vibaya na baadhi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kutoza ushuru huo kwa wafanyabiashara wadogo kama vile mama lishe na kwa wauza samaki za reja reja na wengineo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Serikali kutoa ufafanuzi kuhusu mkanganyiko wa utozaji wa ushuru wa huduma (*service levy)* kwa wafanyabiashara wadogo na mawakala unaofanywa na Halmashauri. Aidha, Kamati inapendekeza kuwa Serikali isifute ushuru wa huduma (service levy 0.3) kwa viwanda vya chumvi kwasababu ushuru huo ni chanzo kikuu cha mapato kwa baadhi ya Halmashauri kamavile Uvinza.

**Mheshimiwa Spika**, aidha kamati inashauri mapendekezo ya Serikali kwenye kifungu cha **34** cha muswada kilenge kukusanya kodi za *billboards* na *posters* ambazo zinahusu

biashara sio matangazo ya shughuli za siasa, dini, au shughuli za kijamii. Aidha, Kamati inaipongeza Serikali kwa kukubaliana na Kamati kufuta kifungu cha **35** cha Muswada kwa kuwa kitaongeza kero kwa wananchi. Vilevile, kwa upande wa kifungu cha **37** cha Muswada huu Kamati inapendekeza kifanyiwe marekebisho kwa kuzingatia kifungu cha 15 cha Sheria ya Fedha za Umma ya Mwaka 2004

### 4.10 Sheria ya Kodi ya Majengo ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa, Sura 289

**Mheshimiwa Spika**, Serikali imekubaliana na mapendeezo ya kamati ya kufuta sehemu ya Kumi na Moja ya Muswada huu iliyohusu Sheria ya Kodi ya Majengo ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa, Sura 289 ambayo ilikuwa na lengo la kuiwezesha mamlaka ya mapato kukusanya kodi ya majengo katika maeneo ya mamlaka ya Serikali za Mitaa zilizopo Tanzania Bara.

### 4.11 Sheria ya Madini, Sura 123.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Serikali ya kurekebisha kifungu cha 90 A na kuongeza kifungu kidogo cha (5) kinacholenga kutoa msamaha wa tozo ya ukaguzi kwa wazalishaji wa chumvi ili kuwezesha ustawi wa sekta ya uzalishaji wa chumvi nchini

### 4.12 Sheria ya Tume ya Mipango, Sura 314

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Bajeti haikubaliani na mapendekezo ya Serikali ya kufuta Sheria ya Tume ya Mipango, Sura ya 314. Kamati, inaona pendekezo la kufuta sheria hii si sahihi kwa sababu uamuzi wa Serikali wa kuunganisha Tume ya Mipango na Wizara ya fedha hauondoi umuhimu wa kutokuwepo kwa sheria hii. Hivyo, endapo sheria hii itafutwa na ikaonekana Tume hii kuhitajika kuwepo miaka ijayo itailazimu Serikali kuja Bungeni ili kutunga upya Sheria hii.

### 4.13 Sheria ya Tozo ya Huduma ya Bandari, Sura ya 264

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Serikali ya kutokuongeza tozo ya huduma ya bandari kwa wasafiri wakazi na wageni kutoka shilingi 500 hadi shilingi 1,000.

### 4.14 Sheria ya Fedha za Umma, Sura 48

**Mheshimiwa Spika,** Mapendekezo ya Serikali ni kuanzisha vifungu vipya vya 11A, 11B, 11C na 11D vitakavyokuwa na maudhui ya kuanzisha Akaunti Jumuifu itakayofunguliwa Benki Kuu ya Tanzania. Kamati inaliomba Bunge lako likubali kutoa muda zaidi kwa Serikali na Kamati ya Bajeti kuliangalia suala hili kwa undani kwa niaba ya Bunge ili kuhakikisha suala hili linafanyiwa kazi kwa ufasaha na ufanisi. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kukamilisha mashauriano na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kuhusu suala hili. Kamati inapendekeza Serikali kufanya mabadiliko katika kifungu cha 11D ili kuweka sharti la kuwezesha utaratibu huu kuanza kutumika tarehe 30 Septemba 2018.

**Mheshimiwa Spika,** Mapendekezo ya kutengeneza kanuni chini ya kifungu cha 11C (2) cha muswada huu yameandikwa kwa lugha pana bila kuwekewa mipaka na hayaendani na majukumu ya Akaunti Jumuifu yanayopendekezwa kwenye kifungu 11B ya Muswada.

### 4.15 Kodi ya Tozo za Barabara na Mafuta, Sura ya 220

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inakubaliana na Mapendekezo ya Serikali yaliyoletwa kwenye sura ya Kumi na Sita ya Muswada huu. Aidha, Kamati inapendekeza pia kufanya mabadiliko kwenye Sheria hii ***(The Road and Fuel Tolls Act, CAP 220)*** **kifungu 4A (b)** ikisomwa pamoja na jedwali la pili ili kuongeza kiasi cha **shilingi 50** kwenye tozo za mafuta kutoka **shilingi 50 hadi shilingi 100** kwenye mafuta ya dizeli na petroli yanayoingizwa nchini ili kiasi cha fedha kitakachopatikana kipelekwe katika utekelezaji wa miradi ya maji vijijini.

Inakadiliwa pendekezo hili litaiongezea Serikali Jumla ya Shilingi **bilioni 125** kwa kuangalia mwenendo wa makusanyo wa mwaka wa fedha 2017/18. Suala hili limekuwa ni kilio cha muda mrefu cha Bunge ili kukidhi mahitaji ya maji hasa vijijini.

**Mheshimiwa Spika,** wakati Waziri wa Fedha akihitimisha hoja yake hapa Bungeni aliliarifu Bunge lako kwamba mafuta yana jumla ya tozo 19 ambazo zinatozwa na Mamlaka mbalimbali za Serikali. Pendekezo la Kamati ya Bajeti la kuongeza shilingi 50 litasababisha mfumuko wa bei. Katika mwaka wa fedha 2016/17 Serikali ilifanya uamuzi wa kuhamisha kodi ya magari *"road licence"* kwenda kwenye mafuta wakati Serikali inapendekeza suala hilo sababu za mfumuko wa bei hazikutajwa. Ni wakati muafaka kwa Bunge lako kufanya maamuzi sahihi kama tulivyokubali mapendekezo ya Serikali yetu ya mwaka 2017/18. Ni maoni ya Kamati kuwa endapo madhara yatajitokeza wakati wa mapitio ya Bajeti ya Serikali Nusu Mwaka wakati wa kutekelezwa kwa suala hili, jambo hili linaweza kuletwa Bungeni kupitia Muswada wa mabadiliko ya Sheria mbalimbali na Bunge lako litafanya maamuzi.

**4.16 Sheria ya Sekta ya Katani, Sura 30**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kukubali mapendekezo ya Kamati ya kuondoa Sehemu ya 17 ya Muswada huu.

**4.17 Sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania, Sura ya 399**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inakubaliana na mapendekezo yaliyoletwa na Serikali ya kufuta kifungu cha 33(2) ya kurekebisha Muundo wa Mamlaka ya Mapato Tanzania. Hata hivyo, Kamati inapendekeza kufanya mabadiliko katika Jedwali la Kwanza Sehemu B la Sheria ya Mamlaka ya Mapato Sura 399 ili kuondoa Sheria ya Kodi ya Majengo *(The Urban Authorities (Rating) Act Cap 289*) kwenye orodha ya Sheria zinazosimamiwa na Mamlaka hiyo. Kamati inapendekeza Kifungu cha 16 cha Sheria mama kufuta

Kifungu cha 2 na 2(a) cha Sheria hiyo ili iendane na mahitaji ya wakati huu.

### 4.18 Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Sura 438

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inakubaliana na marekebisho yanayoletwa na Serikali kwenye sheria hii ili kuimarisha usimamizi wa kodi katika eneo la usajili wa walipa kodi, kusamehe sehemu ya riba au malimbikizo ya madeni ya nyuma ya riba na adhabu inayotokana na malimbikizo ya kodi. Hata hivyo, ili kuleta mwitikio mzuri wa utekelezaji wa pendekezo hili Serikali izingatie kuwalinda walipa kodi watakaojitokeza kutumia fursa hii isipokuwa kwa makosa yafuatayo:- usafirishaji haramu wa binadamu, madawa ya kulevya na ujangili. Hatua hii itasaidia kuhamasisha ulipaji wa kodi na hivyo kuongeza mapato ya Serikali.

### 4.19 Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura 148

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inakubaliana na marekebisho yanayoletwa na Serikali kwenye sheria hii, hata hivyo Kamati inapendekeza marekebisho yafutayo:-

i. Kifungu cha 81 cha Muswada kirekebishwe ili kujumuisha pia mikopo na misaada itakayopatikana kutoka katika taasisi nyingine ambazo sio za kiserikali kwa ajili ya miradi yenye manufaa ya jamii;

ii. Kifungu cha **82** na **83** cha Muswada kifutwe ili kuziwezesha Asasi zisizokuwa za kibiashara kunufaika na marejesho ya kodi;

iii. Kifungu cha **84(a)** kiboreshwe kwa kuongeza upatikanaji wa mashudu na pumba;
iv. Kifungu cha **84 (b)** kiboreshwe na hivyo kumjumuisha Waziri mwenye dhamana na mifugo;

v. Kamati inaipongeza Serikali kwa kukubali usahuri wa Kamati wa kufuta Kifungu cha 84 (e) cha Muswada kinachohusu kuhusu huduma za usafiri wa anga kwa kutumia ndege za kukodi.

vi. Kuongeza msamaha wa kodi kwenye vifungashio vya maziwa na mbegu kama ilivyofanya kwenye madawa.

vii. Kutoa msamaha wa kodi kwenye pampu za maji za *solar,* pampu za maji zenye mita na mitambo ya kuchimbia visima vya maji.

viii. kutoa msamaha wa kodi kwenye mashine na vifaa vinavyotumika kuchonga madini ya vito na usonara.

ix. kutoa msamaha wa kodi kwenye mitambo ya kuchimba mabwawa kwa makampuni ya kilimo yaliyosajiwa.

x. Hatua ya Serikali kusamehe kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye taulo za kike (Sanitaty pads) HS Code 9619.00.10 ili kuwezesha kupatikana kwa bidhaa hii kwa bei nafuu haitakuwa na manufaa kama Serikali haitalenga kuongeza viwanda vya bidhaa hii nchini. Serikali ibainishe malighafi zinazotumiwa na wazalishaji wa ndani katika kuzalisha bidhaa hii ili zisamehewe kodi kwa lengo la kuwarejeshea kodi hiyo *(input tax claims)* watakazokuwa wamelipa wakati wa ununuzi wa malighafi hiyo.

## 5.0. MAONI NA MAPENDEKEZO YA JUMLA

**Mheshimiwa Spika**, baada ya uchambuzi wa kina wa Muswada huu na kutoa maoni kama yanavyoonekana kwenye Taarifa hii, naomba kuwasilisha maoni ya jumla kwenye maeneo mbalimbali:-

### (a) Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, ya mwaka 2004.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imepata fursa ya kupitia mabadiliko yaliyofanyika katika Sheria ya Forodha ya Afrika Mashariki na kubaini kwamba hatua zilizochukuliwa na Tanzania zina malengo ya kuendelea kutoa unafuu kwa viwanda vya uzalishaji wa bidhaa na vyakula vinavyotumia

ngano; kuongeza ufanisi katika udhibiti wa kodi (electronic fiscal devices); kuziba pengo la sukari nchini; kulinda uhamasishaji wa mbegu za mafuta ya kula. Pamoja na hatua hizi muhimu kamati inatoa angalizo katika hatua zifutazo za kikodi:-

**(i)** **Mheshimiwa Spika**, Kamati haina pingamizi ya kutoza ushuru wa forodha wa asilimia 15 badala ya asilimia 25 kwenye karatasi. Hata hivyo, Kamati imegundua kuwa HS Codes zinazopendekezwa hapa kwenye sheria hazihusiani na kutengeneza karatasi nyeupe (cultural printing paper) zinazotumika kutengeneza vitabu na madaftari. HS Codes zilizoainishwa kwenye ukurasa wa 59 wa Hotuba ya Bajeti ya Serikali zinahusu aina za karatasi ambazo wadau wa viwanda nchini wakiwemo Mufindi Paper mills Ltd wamekuwa wakitengeneza (sack kraft, bagkraft, kraftliner, testliner na corrugating medium au fluting) zinazotumika kutengeneza karatasi kwa ajili ya mifuko ya saruji, makasha ya kuhifadhi vitu, bahasha, mifuko na vifungashio vya bidhaa ambavyo huuzwa ndani na nje ya nchi.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya tathimini Kamati inapendekeza marekebisho haya ya Serikali yahusishe HS Codes zinazohusu karatasi za kutengenezea vitabu na madaftari kama vile HS Code 4801.00.90, HS Codes 4802.55.00 na nyingine ili kupunguza gharama kwa wazalishaji na waagizaji wa bidhaa hiyo nchini.

**Mheshimiwa Spika**, aidha, Kamati inapendekeza kuwa **ushuru wa forodha wa asilimia 25 uendelee** kwenye karatasi zinazotambulika katika HS Code 4804.11.00; 4804.21.00; 4804.31.00; 4804.41.00; 4804.19.90; 4804.29.00; 4804.39.00; na 4804.59.00; ambazo kimsingi ndizo zinazozalishwa kwa wingi na viwanda vyetu vya ndani na kuuzwa ndani na nje ya nchi na hivyo kuendelea kulinda viwanda vya ndani.

(ii) Kutoza ushuru wa forodha wa asilimia 35 badala ya asilimia 100 kwenye Sukari ya matumizi (gap sugar) inayoagizwa toka nje kwa vibali maalum. Hatua hii itasaidia kulinda viwanda vya uzalishaji sukari nchini.

**(b) Malipo ya ushuru wa asilimia 15 wa kuingiza Sukari ya viwandani**

**Mheshimiwa Spika,** mabadiliko yaliyofanywa na Serikali (*administrative measures*) ya kulipa zaidi kiwango cha asilimia 15 ya ushuru wa forodha kwa makampuni ya Sukari yanayoagiza bidhaa toka nje yanaendelea kuwa na athari hasi kwa viwanda vinavyotumia sukari ya viwandani kama malighafi ya kuzalisha bidhaa nyingine kama juisi na soda, ukizingatia kwamba katika jumuiya ya Afrika Mashariki hakuna kiwanda hata kimoja kinachozalisha sukari hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, mapaka sasa Serikali inadaiwa kiasi cha shilingi **Shilingi 35,000,000,000** ambayo ilitakiwa kurudishwa kwa wenye viwanda vilivyoagiza sukari nje. Kamati inashauri Serikali kutafuta utaratibu mwingine wa kuweza kudhibiti uagizaji wa Sukari ya viwandani pamoja na kutafuta namna ya kurudisha fedha (refund) kwa waagizaji wa sukari ili waweze kujiimarisha katika uzalishaji.

**(c) Kutoza ushuru stahiki kwa nguo kutoka nje ili kulinda viwanda vya nguo nchini.**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipata fursa ya kukutana na wamiliki wa viwanda vya nguo nchini ambao wanatumia pamba kwa jili ya kutengeneza nguo. Changamoto iliyoibainishwa na wamiliki hao ni kuwa nguo zinazoingizwa nchini (takribani ya asilimia 85 ya nguo zote) zinatozwa kodi ndogo na hivyo kuuzwa kwa bei ya chini ikilinganishwa na nguo zinazotengenezwa na viwanda vyetu hapa nchini.

**Mheshimiwa Spika**, sababu ya nguo za ndani kuuzwa bei ya juu ni kutokana na gharama za uzalishaji (uchakataji) kuwa juu na hivyo kusababisha nguo zetu kuonekana ghali na kushindwa kuuzika. Hivyo, Kamati inashauri Serikali kupitia TRA ifanye utafiti na kupata bei halisi (ex-factory price) ya nguo zinazoagizwa toka nje na hivyo kuwa na *base* kwa ajili ya kutoza kodi stahiki na hivyo kulinda viwanda vyetu vya ndani vinavyozalisha nguo kupitia malighafi ya pamba.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya Bajeti inaona kuna umuhimu wa kuhamasisha kilimo cha zao la pamba ili kupata pamba ya kutosha kukidhi mahitaji ya uzalishaji wa nguo nchini. Aidha, inapendekeza kutoza Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwa kiwango cha asilimia sifuri (zero rated) kwa bidhaa zote zinazozalishwa na viwanda vya nguo nchini kutokana na pamba iliyozalishwa nchini.

**(d) Kulinda viwanda vya magunia ya mkonge nchini.**

**Mheshimiwa Spika,** uzalishaji wa magunia nchini umekuwa ukikumbwa na changamoto mbalimbali kwa sasa kuna viwili tu vya uzalishaji wa magunia ya katani ambavyo vinazalisha chini ya uwezo kutokana na ushindani uliopo wa magunia ya jute kutoka India na Bangladesh. Ili kuinua uzalishaji wa viwanda vya magunia nchini kamati inapendekeza kuwa, Serikali iongeze ushuru wa uingizaji bidhaa (*import duty)* kwa magunia kutoka nje ya nchi kutoka asilimia 25 iliopo sasa hadi asilimia 45. Hatua hii itatoa nafasi kwa magunia yetu ya mkonge kupata soko la ndani kwa mazao ya korosho, kahawa, mahindi na maharage.

**Mheshimiwa Spika**, aidha kamati inashauri kufanya marekebisho katika jedwali Namba 5 la Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, ya mwaka 2004 ili kuondoa msamaha kwa ushuru wa forodha kwa magunia na vifungashio vya mazao ya kilimo yanayouzwa na nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ili kutoa fursa kwa magunia ya mkonge kununulika na wanachama wa Jumuia.

**(e) Kulinda kiwanda cha kuzalisha Vyandarua Vyenye Viuatilifu vya kuzuia Mbu wa Malaria (LLINs):**

**Mheshimiwa Spika, kiwanda cha** A to Z Textile Mills Ltd kilichopo Arusha-Tanzania ni kiwanda pekee Afrika kinachotengeneza vyandarua vya kuzuia Mbu wa malaria kwa muda mrefu. Sheria Mpya ya Kodi ya Ongezeko la Thamani Sura 148 ya Mwaka 2014 iliondoa vyandarua vya kuzuia malaria kutoka jedwali la bidhaa zinazotozwa Kodi ya

ongezeko la tahamani kwa asilimia sifuri *(ZERO RATE)* na kuviweka kwenye jedwali la bidhaa zilizosamehewa kodi hiyo *(EXEMPT SUPPLY)*. Utaratibu huu umevifanya vyandarua vinavyozalishwa nchini kuwa na bei ghali kuliko vyandarua vinavyoingizwa nchini kutoka nchi za Asia mfano Thailand, Vietnam, China, India na Pakistan.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mantiki hii kamati inashauri Serikali mambo yafuatayo:-

i. Serikali irejeshe vyandarua katika jedwali la awali la zero rate kama ilivyokuwa kabla ya 2014 ili kiwanda kiweze kumudu ushindani.

ii. Kuweka HS Code nyingine kwa vyandarua vya polyster ambavyo havina viuatilifu ili kuvitofautisha na vyandarua vyenye viuatilifu (HS Code 6304.91.10 ili kuepusha mkanganyiko wa utozaji wa kodi.

iii. Kurejesha malipo ya VAT (VAT Refunds) yanayotoka na malimbikizo ya manunuzi ya malighafi ya kiwanda ambayo yamekuwa ni changamoto kubwa kwenye kuendeleza biashara. Mathalani TRA hawajarejesha malimbikizo ya VAT yanayofikia takribani Shilingi Bilioni 19.7. Kutorejeshwa kwa fedha hiyo inaathiri uendeshaji na uwekezaji wa kiwanda.

**(f) Kukuza uzalishaji wa tumbaku nchini na kukuza viwanda vya tumbaku nchini.**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Bajeti imekuwa ikishauri mara kwa mara Serikali kuangalia uwezekano wa kuweka mazingira wezeshi kwa viwanda ambavyo vinatumia kwa kiwango kikubwa Tumbaku inazalishwa nchini. Pamoja na Serikali kutoongeza ushuru wa bidhaa kwenye bidhaa ya sigara, kamati inaendelea kuishauri Serikali kuviwezesha viwanda vinavyototumia kwa wingi kiwango kikubwa cha tumbaku inayozalishwa hapa nchini kutengeneza sigara. Aidha, Serikali ipunguze ushuru wa bidhaa kwa kampuni hizo zinapoagiza nje ya nchi asilimia 25 ya tumbaku ambazo hazizalishwi nchini ili mradi Kampuni hizo zitatumia zaidi ya

asilimia 75 ya tumbaku ya ndani katika sigara zao kama vile Sigara aina ya Malboro ambayo ina mchanganyiko wa aina tatu za tumbaku *(Virginia, Burley na Oriental).* Kimsingi, tumbaku inaayozalishwa nchini ni aina moja tu iitwayo Virginia. Hatua hii itasadia kuendelea kuhamasisha walimaji wa tumbaku nchini.

**(g) Kutolingana kwa Hotuba ya Bajeti ya Serikali na vifungu vilivyoainishwa kwenye muswada.**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya Bajeti imebaini kuwa katika Hotuba ya Bajeti Waziri wa fedha hakuanisha Sheria zote zinazotarajiwa kufanyiwa mabadiliko na malengo yake. Mfano Sheria ya Bima Sura ya 394, Sheria ya Ardhi Sura ya 113 na Sheria ya Tume ya Mipango Sura ya 314. Kamati inashindwa kuelewa ni kwanini Serikali haikubainisha Sheria hizo na malengo ya mabadiliko yake ili kutoa Taarifa kwa Umma. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha inabainisha nia na malengo ya mabadiliko ya Sheria katika hotuba zake za Bajeti ya Serikali ili kuujulisha Umma.

**(h) Mfumo wa Stempu za Kodi za Elektroniki**

**Mheshimiwa Spika**, Serikali imedhamiria kuanzisha Mfumo wa Stempu za Kodi za Kieletroniki (ETS) ili kudhibiti udanganyifu wa wazalishaji wa bidhaa zinazotozwa ushuru wa bidhaa. Muwekezaji atasimika na kuendesha mitambo ya mfumo huo kwa mfumo wa *self financing* ambao unamtaka mwekezaji kurudisha gharama zake kwa kutoza stampu ya kieletroniki kwa kila bidhaa itakayozalishwa. Kamati inaunga mkono mfumo wa Stempu za Kieletroniki jambo la msingi ambalo Kamati inaendelea kuishauri Serikali ni kuanza na bidhaa ambazo zilikuwa zinatumia stempu ya karatasi kama vile pombe kali na sigara badala ya kuhusisha bidhaa nyingine kama vile maji, soda na juisi ambazo kimsingi zinatumiwa na wananchi wa hali ya chini.

**Mheshimiwa Spika**, aidha Kamati imefanya utafiti na kugundua kuwa Serikali imekamilisha utungaji wa kanuni wa

jambo hili kwa kutoa GN No. 16 iliyotangazwa tarehe 2 Februari, 2018, ambayo kimsingi haijawahi kuwasilishwa bungeni na kuridhiwa na Bunge. Ni vema Bunge lako tukufu likapata maelezo kuhusu ukiukwaji kifungu cha 122(3) cha Sheria ya Ushuru wa Bidhaa Sura 147 kinachotaka kabla ya kanuni kuanza kutumika ziletwe Bungeni kwanza. Kamati inapendekeza kabla ya kanuni hizo kuanza kutumika ni lazima ziletwe Bungeni ili Bunge liweze kuzipitia na kutoa maamuzi.

**Mheshimiwa Spika**, kamati imetaarifiwa kwamba wazalishaji wa bidhaa zinazotozwa ushuru wa bidhaa watatakiwa kutoa Dola za Marekani Milioni 3 kwa ajili ya usimikaji wa mitambo ya uendeshaji wa mfumo wa Stempu za Kielectroniki. Aidha, wazalishaji wa bidhaa hizo watatakiwa kuingia mkataba na SCIPA ili kutoa huduma za mitambo hiyo pindi itakapopata hitilafu. Ni wazi kwamba gharama hizi zote anazolipia mzalishaji zitahamishiwa kwa mtumiaji wa mwisho. Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuangalia upya mkataba na Kampuni ya SCIPA ili Serikali nayo inufaike na mapato yatokanayo na mfumo huo tofauti na ilivyo hivi sasa ambavyo mapato yote yatachukuliwa na muwekezaji kwa kipindi cha miaka 5.

## 6.0. HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, Naomba kutumia fursa hii kukushukuru kwa kunipa fursa hii ili niweze kuwasilisha taarifa ya maoni ya Kamati kuhusu muswada wa sheria ya fedha kwa mwaka 2018/19 mbele ya Bunge lako Tukufu. Vilevile napenda nimshukuru Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango (Mb), Waziri wa Fedha na Mipango, Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji (Mb), Naibu Waziri wa Fedha na Mipango kwa ushirikiano wao walioutoa kwa Kamati. Aidha, napenda kuwashukuru Watendaji wote wa Wizara ya Fedha pamoja na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kwa maoni na ushauri wao ulioiwezesha Kamati kuchambua Muswada hadi hatua hii. Kamati pia inawashukuru wadau wote wa masuala ya kodi waliofika mbele ya Kamati na kutoa maoni yao kuhusu Muswada huu.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kumshukuru Mhe. Jitu Vrajlal Soni, Mbunge wa Babati pamoja na Wajumbe wote wa Kamati hii kwa umahiri wao katika kuchambua vifungu vya Muswada huu na kuweza kufanya maamuzi sahihi. Naomba niwatambue Wajumbe hao kama ifuatavyo.

1. Mhe. Hawa Abdulrahman Ghasia, Mb – Mwenyekiti
2. Mhe. Jitu Vrajlal Soni, Mb - Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. Balozi Adadi Mohamed Rajabu, Mb
4. Mhe. Ali Hassan Omar, Mb
5. Mhe. Abdallah Majura Bulembo, Mb
6. Mhe. Prof. Anna Kajumulo Tibaijuka, Mb
7. Mhe. Albert Obama Ntabaliba, Mb
8. Mhe. Dkt. Dalaly Peter Kafumu, Mb
9. Mhe. David Ernest Silinde, Mb
10. Mhe. Freeman Aikael Mbowe, Mb
11. Mhe. Hasna Sudi Katunda Mwilima, Mb
12. Mhe. Dkt. Immaculate Sware Semesi, Mb
13. Mhe. Ibrahim Hassanali Mohammedali Raza, Mb
14. Mhe. Makame Kassim Makame, Mb
15. Mhe. Maria Ndilla Kangoye, Mb
16. Mhe. Martha Jachi Umbulla, Mb
17. Mhe. Mendrad Lutengano Kigola, Mb
18. Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki, Mb
19. Mhe. Mbaraka Kitwana Dau, Mb
20. Mhe. Oran Manase Njeza, Mb
21. Mhe. Riziki Said Lulida, Mb
22. Mhe. Stephen Julius Masele, Mb
23. Mhe. Andrew John Chenge, Mb
24. Mhe. Hussein M. Bashe, Mb
25. Mhe. Shally Josepha Raymond, Mb
26. Mhe. Suleiman A. Sadiq, Mb

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee naomba nikushukuru wewe binafsi Mhe. Spika, Dkt. Tulia Akson, Mb - Naibu Spika na Ndugu Stephen Kagaigai - Katibu wa Bunge pamoja na watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Aidha, kwa namna ya pekee napenda kuishukuru Sekretarieti ya Kamati ya Bajeti ikiongozwa na Kaimu Mkurugenzi Ndugu

Lina Kitosi, Kaimu Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Michael Kadebe na Makatibu wa Kamati hii Ndg. Godfrey Godwin, Emmanuel Rhobi, Stephano Mbutu, Matamus Fungo, Lilian Masabala na Maombi Kakozi kwa kuratibu shughuli za Kamati pamoja na kutoa ushauri wa kitaalamu na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja hii.

Hawa Abdulrahman Ghasia (Mb)
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI**
Juni, 2018

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea baada ya muda si mrefu, tutaanza na uchangiaji na kama nilivyotaja Mheshimiwa Leah Komanya atakuwa wa kwanza kutufungulia na tutaendelea na wengine.

Waheshimiwa Wabunge, orodha niliyonayo ni kubwa na muda ni mdogo sana. Kwa hiyo, mtu yeyote ambaye yuko kwenye orodha yangu nikimwita akawa hayupo humu ndani ajue hiyo nafasi yake ndio imeshapotea haitarudi tena. Bado tunapima kama jambo hili tulimalize leo au tulimalize kesho asubuhi. Tukimaliza leo tutalimaliza kwa *guillotine*, tutaangalia kadri tunavyoenda.

Sasa tuendelee na uchangiaji, natumaini Mheshimiwa Leah Komanya yupo. Naam, nakuruhusu hebu washa chombo utuambie unasemaje.

**MHE. ZITTO Z.R. KABWE:** Mheshimiwa Spika, hatuna hotuba ya Kamati wala *schedule* of *amendment* ya Kamati mpaka sasa.

**SPIKA:** Una maana hazigawanywa *copy*?

**MHE. ZITTO Z.R. KABWE:** Ndiyo.

**SPIKA:** *Ok* hilo litafanyika, litafanyika muda si mrefu. *Schedule of Amendment* ya Kamati bado kwa sababu inabidi Kamati wayatoe yale mambo yote ambayo Mheshimiwa Waziri alishayarekebisha ili wasiwe na *repetition*. Kwa hiyo, kazi hiyo inafanya hivi sasa, ndio maana mnaona hamjagawiwa *schedule of amendment* ya Kamati.

Mheshimiwa Leah Komanya.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuwa mchangiaji wa kwanza. Napenda niunge mkono hoja ya Mabadiliko ya Sheria mbalimbali, nimwombe tu Waziri baada ya mabadiliko kupita alete waraka haraka mahali husika ili sasa mabadiliko hayo yaanze kutumika mapema.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kuchangia na mchango wangu utajikita katika kutenga asilimia 10 inayotokana na mapato ya halmashauri. Nishukuru Serikali sasa kwa kuliona hili maana limekuwa na muda mrefu, halmashauri zimekuwa hazitekelezi kwa sababu mara ya kwanza kulikuwa na mwongozo. Naishukuru Serikali pia kwa kufanya mabadiliko yale ya 50/50 kwenda kwa asilimia 40/40/20 kwa sababu ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, fedha hizi mwongozo huu ulitolewa kwa ajili ya kusaidia makundi ambayo yalikuwa yameachwa nyuma kimaendeleo. Makundi haya yalikuwa ni Wanawake, Vijana, wakiwemo na Walemavu. Kwa hiyo, tukitoka 50 / 50 kwenda *four, four, two*, maana yake ni nini? Tutachukua na wale wanaume walemavu ambao walikuwa wasihesabike katika kundi la vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaamini pia kundi la walemavu na wenyewe wako nyuma sana katika maendeleo wanatakiwa wasaidiwe ili waweze kusonga mbele. Kama

fedha hizi halmashauri itazitoa na kuzisimamia vizuri zitaweza kusaidia makundi hayo katika kujikwamua kiuchumi, maana yake nini? Halmashauri itaendelea kutenga kila mwaka katika bajeti yake asilimia10, kwa wakati huo huo kutakuwa na marejesho ya vikundi maana yake fedha hiyo itakuwa na mzunguko.

Mheshimiwa Spika, hapo tatizo liko wapi? Fedha hii awali ilikuwa ina akaunti yake ilikuwa kwa wanawake na vijana, lakini Serikali iliamua kupunguza akaunti zake kutoka thelathini na kitu mpaka sita. Kwa hiyo fedha hizi zilijikuta zinaingia kwenye Akaunti ya Amana. Tunavyoelewa akaunti ya amana ina fedha za kila aina, zikiingia mle zinatumika kwa matumizi mengine. Naishauri Serikali kama tumedhamiria kuyasaidia makundi haya naomba basi ifunguliwe akaunti maalum kwa ajili ya Mfuko wa Wanawake, Vijana na Walemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali pia kwa kutenga riba ndogo ya asilimia mbili ambayo itaenda kushawishi wakopaji. Fedha hizi baada ya kurudisha kumekuwa na tatizo, Maafisa Maendeleo ya Jamii wamekuwa wakizitumia kwa matumizi mengine badala ya kufanyika kama fedha ya mzunguko yaani *revolving fund*. Hivyo nashauri katika fasili ya nne Waziri mwenye dhamana anapoweka kanuni aangalie matumizi ya fedha hizi.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa pia na tatizo katika kubadilisha matumizi ya fedha. Halmashauri kila mwaka zimekuwa zikifanya bajeti kabla ya kupitishwa na TAMISEMI lazima watenge asilimia 10 ya wanawake na Vijana na walemavu, lakini sasa utakuta halmashauri imekusanya asilimia 100 mapato yake, imetumia kwa asilimia 100 ndani yake kuna kifungu cha mchango wa asilimia 10, lakini ukiangalia hakuna fedha yoyote iliyotolewa kama mchango wa asilimia 10, maana yake nini? Halmashauri ilifanya matumizi aidha kwa kupokea maagizo mbalimbali ya Serikali ama ilipoona baadhi ya vifungu vilizidiwa ikabadili yale matumizi ya asilimia 10. Nashauri kwenye kanuni fedha zile zisifanyiwe mabadiliko ya matumizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baadhi ya halmashauri zimekuwa hazitambui michango ile kama madeni baada ya mwaka kufunga zinaposhindwa kuyalipa. Niombe sasa taratibu za kihasibu zinaruhusu kuyaingiza kama madeni ili yatambulike mwisho wa mwaka na baadaye zile vikundi viweze kunufaika.

Mheshimiwa Spika, tatizo lililopo lingine sisi Wabunge na Madiwani kwenye vikao vyetu tumekuwa tukijitahidi kuwaomba Wakurungenzi watoe hizi fedha, bajeti ipo lakini wanatoa sababu kuna matumizi mbalimbali. Nishauri katika taratibu Waziri mwenye dhamana akasimu Madaraka kwa Katibu Tawala wa Mkoa ili aweze kuwafuatilia Wakurugenzi ambao hawataweza kutekeleza utoaji wa hizo fedha ili waweze kuchukuliwa hatua. Maana yake kutenga ni kitu kingine na kutoa fedha ni kitu kingine.

Mheshimiwa Spika, huo ndio ulikuwa mchango wangu, nashukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA**: Ahsante sana, Mheshimiwa Leah Komanya. Sasa namwita Mheshimiwa Cecil Mwambe.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwenye hoja iliyoko mbele yetu. Kwanza nataka tu kuweka sawa *record* ya Bunge lako kwa sababu juzi wakati Waheshimiwa Mawaziri wanajumuisha na Mheshimiwa Attorney General alipewa nafasi ya pia naye ya kutoa mchango wake. Naomba ku-*refer* sehemu ambayo alikwenda, nina *document* ambayo ninayo hapa naomba niisome wakati ninajaribu kujenga hoja yangu.

Mheshimiwa Spika, *AG* alipopewa nafasi ya kutoa maoni yake sina uhakika kama ni makusudi kabisa au kuna mtu alimwagiza aamue kulidanganya Bunge lako. Wakati anatoa taarifa yake, naomba kuisoma, alisema kwamba:

*"Pamoja na marekebisho yatakayoletwa na Serikali kuchangia hasa zaidi kwenye hii sheria inayohusiana na masuala ya korosho, kwamba hukumu iliyotolewa na*

*Mahakama Kuu mwaka 2000, Desemba ilisema kwamba, pesa zile ambazo Serikali imekuwa ikikata kwa maana ya export levy, ilikuwa ni mali ya Serikali, mali ya umma"*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, alisoma tu baadhi ya vifungu ambavyo yeye *AG* kwa malengo yake mwenyewe alikuwa anavitaka, lakini hata hivyo kimsingi ukienda kusoma kwenye ile hukumu ukurasa wa 17 ambayo ninayo hapa na naomba niisome ili kuweka *record* sawa, tuone ni kwa namna gani *AG* alikuwa ameamua kulidanga Bunge lako na niliomba hapa mwongozo na bahati mbaya sikupata hiyo nafasi ili kiti chako kiweze kufanya maamuzi juu ya jambo hili. Sehemu ya hukumu inasema hivi:

, *"In view of the above were certified that, the trial Judge rightly held that there was no agency relationship between the parties. We are further more certified that since the cashewnuts export levy was not a tax, and the Government or Tax Authority did not legislate for such tax at all. They was also no agency relationship between the Government and the Appellant whatever the case the cashewnut export levy money was not revenue from the taxation so it was not and is not Government revenue. Ordinarily the money would belong to the cashewnut farmers and the right of the above the appeal is lacking the merit we are accordingly dismissed with cost". (Applause)*

Mheshimiwa Spika, sasa Mheshimiwa *AG* aliposimama, alisema hizo pesa zote ni mali ya Serikali, asilimia 35 na asilimia 65.

**TAARIFA**

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**: Taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Cecil.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**: Mheshimiwa Spika...

**SPIKA**: Ndio Mheshimiwa Olenasha

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**: Mheshimiwa Spika, nataka nimpe Mheshimiwa Cecil taarifa kwa sababu anatoa maelezo kuhusu hukumu ambayo sio yenyewe aliyosemwa. Katika Sheria uamuzi kawaida ukifanyika na mahakama kuna kitu kinaitwa *obiter dictum* na kuna kitu kinaitwa *dictum*. Sasa yeye alichokuwa anasoma ni kitu kinachoitwa *Obiter dictum. Obiter dictum* ni pale Jaji anapoamua kuzungumza *by the way* lakini *dictum* kile ambacho ndio msingi wa maamuzi. *(Makofi)*

Sasa kwenye kesi ambayo anasoma ambayo *actually* ni Mahakama ya Rufaa siyo ya Mahakama Kuu. Msingi au uamuzi wenyewe uko kwenye *paragraph* ya mwisho ambayo amesema ile inayosema *in the right of the above the appeal is the lacking in merits*. *We according dismiss appeal*, maana yake nini? Kilichoenda mahakamani, ilikuwa ni ku-*challenge* uamuzi wa Mahakama Kuu ambayo nataka nimpe taarifa ni taarifa.

(*Waheshimiwa Wabunge walizungumza bila utaratibu)*

**SPIKA:** Naomba tuheshimiane na tusikilizane sana. Kwa sababu hizi vurugu vurugu ambazo hazina maana hazisaidii, sisi ni Bunge hatuwezi kulazimisha vitu ambavyo havipo,tupeane taarifa. Kwa hiyo muacheni Waziri atoe taarifa.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, kilichoenda mahamani ni kwamba, *Cashewnut Board of Tanzania* haikuridhika na maamuzi ya Mahakama Kuu ambao uamuzi ule pamoja na mambo mengine katika *page* ya 11 ile imesema:

*"The whole three percent export levy is the public fund, collected under the statute, therefore its remain to be the property of the Government. The defender as the public board is collecting the levy on behalf of the Government"* pamoja na mambo mengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa ndio Bodi ikaenda mahakamani ku-*challenge*. Sasa uamuzi wa Mahakama ya rufaa ume-*dismiss* ile rufaa maana yake nini? Ime-*uphold* uamuzi wa Mahakama Kuu. Kwa hiyo, alichofanya Jaji taarifa ni kwamba, kwenye mahakama ya rufaa yale aliyokuwa anasoma ni mazungumzo ya *by the way* sio *basis* ya *decision* ni *obiter dictum,dictum* ni kwamba kesi imekuwa *dismiss,* kwa hiyo, uamuzi wa Mahakama Kuu ndio unasimama, uamuzi wa kisheria wa Mahakama ni huo unaosema kwamba, ile asilimia tatu ni *Public Fund* na ni mali ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Zitto unajua kabisa taarifa juu ya taarifa haikubaliki.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, taarifa kwa Mheshimiwa Mwambe.

**SPIKA:** Hapana sio utaratibu Mheshimiwa Zitto. Lazima nimrudishie aliyepewa taarifa ili kama anaipokea au haipokei. Mheshimiwa Mwambe taarifa, umepewa hiyo.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, taarifa hiyo sipokei na nina hiyo kesi hii mbele yako, naiweka hapo kwa maana Serikali ichukue, lakini wakati huo huo fuatilia kwenye *Hansard* maneno ambayo aliongea *AG* na niliyoyasema mimi na mimi nilikuwa nataka kusema kuhusu jambo hili.

**SPIKA:** Wahudumu naomba mchukue hiyo nakala tuone.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba hiyo nakala ikae mezani kwako, ambayo ndio hukumu hiyo tunayoiongelea sisi.

**SPIKA:** Hukumu unayoiongelea ni ya mahakama ipi?

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, hukumu hii hapa, ni...

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, taarifa

**SPIKA:** Ngoja kidogo

**MHE. MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, nataka nimpe taarifa Mheshimiwa Mwambe.

**SPIKA:** Maana hata hajatufafanulia hata anachokiongea ni kipi kwanza kidogo. Mheshimiwa Mwambe hiyo taarifa, hiyo hukumu yako unayosoma ni ya Mahakama Kuu, ni Mahakama ya Rufaa.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, ni Mahakama ya Rufaa, wakati huo naomba uangalie pia muda wangu kwa sababu isije ukatumika vibaya.

**SPIKA:** Suala la muda wala usinikumbushe, ni kazi yetu, mpe tu huyo bwana nakala ailete. Haya Mheshimiwa Zitto.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpa taarifa Mheshimiwa Mwambe kwamba, hukumu aliyoisema na maneno aliyozungumza kuhusiana na maelezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ni maelezo sahihi. Kwa sababu, hukumu ni ya mwaka 2001 na *parties* zilizokuwa zinahusika na kesi ni Mfuko wa Korosho na Bodi ya Korosho. Sio Mfuko wa Korosho na Serikali na kutokana na hukumu hiyo ya Mahakama Rufaa ndio maana Bunge lako Tukufu lilikaa kurekebisha matatizo yale na kutunga kifungu cha 17A, ili kutekeleza amri ya mahakama. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mbona hayo unayoyasema, Mheshimiwa Mwambe hajasema sasa ni taarifa ipi unampa? *(Kicheko)*

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, naomba nimalize.

**SPIKA:** Unamsahihisha Mwambe wapi hiyo taarifa yako?

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie.

**SPIKA:** Haya dakika moja.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, na napenda kumalizia kwa kusema Mwanasheria Mkuu wa Serikali ali-*mislead* Bunge kwa kusoma kesi ambayo haihusiani na mjadala uliopo hapa Bungeni. Naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu liagize Kamati ya Maadili ya Bunge impe *charges* Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa Mujibu wa Sheria ya Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge kwa kulipotosha Bunge makusudi na aadhibiwe kwa makosa hayo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwambe hiyo ni taarifa yako, sio kwangu.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, kwanza nishukuru.

**SPIKA:** Endelea bwana dakika zako tunazitunza

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza nishukuru sana, taarifa ya Mheshimiwa Zitto naipokea na huko ndiko nilikokuwa naelekea na ndio maana nilisema kwamba Mheshimiwa *Attorney General* amelidanganya Bunge lako. Sasa kwa sababu Mheshimiwa Zitto amemaliza hili na ameliweka sawa naomba hiyo taarifa yake pia iwe sehemu ya mchango wangu. *(Makofi/vicheko)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo machache sasa nataka nirudi, panapokuwa na nia mbaya

hata wale walioagizwa kwenye kutekeleza hiyo nia mbaya na wenyewe wana *tendency* ya kufanya *contradictions*. Wakati tunachangia humu ndani na Mheshimiwa *Attorney General* akatoa maelezo yake akasema kwamba hili jambo haliko kisheria hii pesa ilikuwa ya Serikali, lakini hizo hukumu zinaonesha hizi pesa ilikuwa ni mali ya wakulima. Kamati pale Mheshimiwa Mwenyekiti tumesikia naye Mama Ghasia anasema kwamba anaishauri Serikali, anamshauri Waziri waitishe tena kile kikao cha wadau ili waweze kukubaliana namna bora ya kutumia hizi pesa na kuzirudisha kule chini. *(Makofi)*

**TAARIFA**

**SPIKA:** Taarifa Mheshimiwa Mwambe unamuwekea maneno Mheshimiwa Hawa.

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Spika, kwa kweli naomba kumpa taarifa hayo anayoyasema ni ya kwake ushauri wetu wa Kamati unaonekana vizuri kabisa kwenye taarifa yetu, kwa hiyo, naomba nisiwe sehemu ya hiyo taarifa yake. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwambe usiwawekee watu maeneno midomoni bwana.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru, kwa sababu mama naye dhahiri masuala ya korosho anayafahamu, tutajadili wenyewe tutakapokutana nje, lakini natambua tu taarifa ya Kamati na yenyewe inapendekeza kwamba Serikali ikatafakari upya namna hili jambo kwa sababu pia mwisho wa siku kuna haja ya kwenda kukutana na wadau na kufanya majadiliano na kuona namna bora ya kuzitumia pesa hizi. Sasa pale Serikali ilipoamua kutaka kuondoa hili suala mbele ya Bunge lako hapa ukisikiliza taarifa ya *Attorney General* ni taarifa tofauti kabisa na tuliyopata tukiwa ndani ya Kamati taarifa ambayo ilitolewa na *PST*.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa huyu Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha wakati anatoa taarifa yake anasema kwamba Serikali imeamua ku-*control* hizi pesa kwa sababu kuna ubadhirifu mkubwa ambao umekuwa ukifanyika hizi pesa zinapopelekwa kule chini, sasa swali linakuja, kwa nini wakulima wote wa korosho waadhibiwe kwa sababu tu ya ubadhirifu wa watu wachache?

Mheshimiwa Spika, vile vile anasema ameagizwa ameagizwa *Controller and Auditor General* kwenda kufanya ukaguzi wa hesabu za korosho imeonekana kule ndani kuna madudu, amemuagiza zaidi ya mara mbili, zaidi ya mara tatu, sasa Serikali i na mkono mrefu na tulikuwa tukiambiana hapa kila mara, kama kweli Serikali ina mkono mrefu ikachukue hatua.

Mheshimiwa Spika, tumeona mabadiliko ya bodi yamefanyika mara mbili, bodi wamebadilisha mara mbili uongozi, watendaji wa bodi wameondolewa mara mbili lakini Mwenyekiti wa bodi hii anayesimamia masuala haya yote bado yuko pale pale.

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Huyo anayetoa taarifa nani na yuko wapi

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Dkt. Mollel.

**SPIKA:** Ongeza sauti basi.

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, nataka kumpa rafiki yangu taarifa kwamba Serikali haina nia ya kuwaadhibu wakulima wa korosho, lakini Serikali ina nia ya kuhakikisha wale watu wa kati ambao wanafanya wakulima wa korosho wasiweze kufaidi korosho kama ilivyotakiwa waweze kudhibitiwa na sasa zao la korosho liweze

kusaidia wakulima wa korosho pamoja na Watanzania wengine kwa ujumla. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Taarifa kwako Mheshimiwa Mwambe.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, labda ikae kwenye *record* sawasawa na mtakapofanya vikao vyenu vya chama mwambieni Dkt. Mollel apunguze kujipendekeza kwa sababu anachokifanya hakimpi yeye uhalali wa kuonekana...

**SPIKA:** Unachofanya unajua kabisa kwamba unavunja kanuni Mheshimiwa Mwambe, hiyo siyo lugha ya heshima kwa Mbunge mwenzako na kwa kweli sidhani kama yeye katika mchango wake alikutukana, kwa hiyo si vizuri.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka niseme kwamba...

**SPIKA:** *Withdraw* hiyo uliyosema, Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Nimeondoa.

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nataka kusema kwamba nimeondoa taarifa yako nimeondoa taarifa yangu , kwa hiyo nataka niseme kwamba Serikali kaama wana nia ya kuchukua hii pesa basi pafanyike majadiliano, kwa sababu kwenye taarifa ya *CAG* inaonesha wazi kabisa na anadiriki kusema kuna ubadhirifu ulikuwa ukifanyika ndio maana ndio maana Serikali ikaamua kuchukua huu mfuko. Mheshimiwa Katibu Mkuu amekiri hiyo mbele ya Kamati sasa tunajiuliza sisi kwa nini hatua tu zisichukuliwe kutokana na report ya *CAG* badala yake Serikali inaamua kufuta Mfuko mzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeona baadhi ya maeneo kuna kesi hapa 1.5 trilioni imepotea, pesa ya Serikali wanasema kwamba haijulikani namna ilivyotumika, lakini pia tumeona kuna Wizara nyingi zimepata hati chafu mbona hizi Wizara hazifutwi, inakuwaje sasa Mfuko wa Korosho wanasema kuna matumizi mabaya matokeo yake wanafuta Mfuko mzima na wanakwenda kudhoofisha kwa wazalishaji wa korosho.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niombe tu pamoja na Serikali kuamua kufanya ubabe, kung'ang'ania hiyo hoja wanasema wao hawataki kubadilika na ndio inavyoonekana kwa sababu Waziri Mpango mara nyingi hata Mheshimiwa Nape alipotoa hoja yake aliitwa mbele ya Kamati aje kutoa maelezo kwa nini hii pesa haipelekwi, matokeo yake Waziri hakuja pale, hakuna kilichoeleweka na wewe mwenyewe Spika ulitoa hapa maelekezo kwamba watu wakaae na uliongea kwa masikitiko makubwa kabisa kwamba hili jambo linavyofanyika si haki kwa sababu zao limekuwa likikua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na upungufu uliopo sasa tunaomba Serikali ijaribu kufikiria tena upya, hata hivyo hizi sheria sio *retrospective* sheria hii inaanza tarehe moja ya mwezi wa Saba mwaka huu, mpaka sasa hivi wakulima wa korosho kutokana na sheria wanayokuja kufuata sasa kwa makusudi ili kuhalalisha kuchukua hiyo pesa, bado ile pesa nyingine kule haijapelekwa. Sasa inakuwaje hawataki kulipa deni la zamani, halionekani kwenye bajeti iliyopita, leo wanataka kufuta sheria na kuhalalisha ile pesa iweze kwenda kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, pia ukienda kwenye maombi yangu ya kutaka kubadilisha baadhi ya hizi sheria nimeomba pia kuhusu sheria ya masuala ya mfuko mmoja namba 348. Hata hivyo, yenyewe jinsi ilivyokaa ukiangalia ile sheria ni kwenda kuziua halmashauri zetu. Tunaposema mapato ya halmashauri yaende yakasaidie halmashauri, hii kazi ya *D by D* imefanyika kwa muda mrefu sana na Serikali hii miaka

mitano, miaka 10 yote iliyopita hiyo kazi ilikuwa inafanyika, leo hii Serikali hii adhimu tunayosema inawajali wanyonge, inapenda kugatua madaraka kila mtu aweze kufanya katika sehemu yake, inarudi tena na hii sheria wanataka kuondoa hicho kipengele pesa zote zikusanywe ziende kwenye Mfuko Mkuu.

Mheshimiwa Spika, hii haitaweza kusaidia halmashauri watakapoondoa hizi pesa tafsiri yake shughuli za halmashauri zitakwama na sasa hivi majimbo yameonekana yana pesa nyingi kuliko halmashauri zetu, kwa sababu pesa za majimbo zinakwenda moja kwa moja kwa Wabunge kwa ajili ya kufanya kazi, lakini pesa za halmashauri zina mlolongo mrefu wa kuzipata.

Mheshimiwa Spika, ukirudi huko chini kwenye halmashauri zetu, Wakurugenzi wanalalamika, Wakuu wa Idara wanalalamika, hakuna pesa, lakini bado Serikali hata kile kidogo ambacho kilikuwa kinabakia kule na chenyewe wanakihitaji, wanataka sasa kukiweka kwenye Mfuko wa pamoja, *process* ya matumizi kwenye Mfuko huu wa pamoja ni ndefu sana, mambo mengi yatakwama.

Mheshimiwa Spika, uzalendo sio kukusanya kila kitu pamoja, kuna sehemu tulisema sisi unapoamua kuwa mzalendo hakikisha unachokifanya leo kitawasaidia na wazalendo wenzio wanaokuja au watu wengine ambao hawana nia njema. Kwa hiyo, niombe tu kuunga mkono hotuba iliyosomwa hapo mbele na Kamati ya Bajeti na kwamba mambo haya yakafanyiwe kazi ili tuweze kwa hakika kabisa kuliboresha Taifa letu, kuweza kuweka mambo mazuri.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**SPIKA**: Ahsante sana. Niwakumbushe tu Waheshimiwa Wabunge, haisaidii sana kuendelea kujenga hoja kama vile

ndio tuko kule tulikoanzia. Toka tulikoanza mpaka sasa hivi kuna *development* nyingi sana ambazo zime-*take place* ziko hoja za msingi ambazo unapotaka kujenga hoja Serikali ikusilikize, jaribu basi kujibu yale ambayo ni *pending* katika hilo jambo. Kwa mfano kama mazao yote kahawa, pamba, pareto, chai na kadhalika yana hizo *levy* na zinaingia kwenye Mfuko Mkuu na hakuna kelele na nyie ndio Wabunge mnaowakilisha mazao hayo, kwa nini zao hilo peke yake liwe hivyo, mbona hamjibu hilo, yaani kwa nini iwe nyinyi tu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ndio mambo hayo unapotaka kujieleza, tusubiriane mbona unapiga kelele David, *you have to behave yourself, you have too,* kwani hapa kuna kosa gani katika kusema hivyo, ndio namna ya kujenga hoja, siwezi kusema Kongwa wakati kumbe nchi nzima nikisema Kongwa tofauti na nchi nzima lazima nieleze kwa nini Kongwa na tofauti na sehemu nyingine ya nchi. Nawasaidieni, Wale ambao mko kwenye *agenda* hiyo huko mbele tunapokwenda katika kuchangia.

Mheshimiwa Mollel tuendelee, kwa hiyo, mjiandae kwa nini korosho, ndio swali.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, wako Mollel wawili.

**SPIKA:** Mollel, wako wawili Dkt Godwin wa kwanza kwenye orodha ya CCM.

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kusoma kulingana na maandiko Matakatifu sifa za mtu maskini. Sifa za mtu maskini akili yake inaona matatizo tu na haioni fursa, uwezekano wala kufanikiwa, lakini hujaa masononeko na lawama siku zote huzungumza ugumu wa maisha hiyo ni Mithali 23:7 na ile ya kwanza ni Marko 9:23. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuchangia kwa kwenda kwenye ile Sehemu ya Nne, Sura ya 203 kwenye zao ambalo limezungumziwa, lakini nizungumzie kwanza historia, ukiangalia huku nyuma kwenye zao la korosho kabla ya bodi ambayo inapigiwa kelele sasa haijaanzishwa wakati huo zao la korosho asilimia 40 ilikuwa inabanguliwa ndani ya Tanzania, lakini wakati ule kulikuwa na viwanda vinne vya kubangua korosho ndani ya Tanzania. Pamoja na matatizo yake yote ilikuja hiki ambacho nacho kilikuwa na nia nzuri na kikafanyika lakini kwa muda wake ule wote vile viwanda vinne vyote vilikufa lakini vilevile sasa India ndio inatajwa kuwa ndio nchi ya kwanza kwa kuuza korosho duniani.

Mheshimiwa Spika, lakini asilimia 83 ya korosho yote ambayo inauza ni inatoka Tanzania, Marekani inauza tano, nafikiri Uarabuni huko nne, Kenya mbili, maana yake ni nini lakini ukiangalia sasa asilimia 90...

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Itafika mahali ambapo hatutapokea tena taarifa, ndio anaanza kabisa kueleza historia ya jambo amesema nini cha taarifa.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Spika, moja tu amesema uwongo, amedanganya.

**SPIKA:** Haya nakupa nafasi. Nomba mnaotoa taarifa kwa kweli mjiandae taarifa leo sipendi mambo ya kuchelewesha muda nina orodha ndefu ya wachangiaji na kama mnavyojua muda wetu ni mdogo sana.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Spika, nataka nimpe taarifa mzungumzaji kwanza amezungumza kwamba India inaoongoza kwa kuza korosho ni kweli, lakini amesema asilimia 83 ya korosho inayouzwa ndia inatoka Tanzania sio kweli. India wenyewe ni wakulima wakubwa sana wa korosho na wanatushinda hata sisi kwa kuzalisha kwa hiyo, wakisikia

wenyewe wasije tukadhani kwamba korosho yote ya India inatoka Tanzania sio kweli...

**SPIKA:** Kwa hiyo, umesimama kama Balozi wa India

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Spika, hapana, lakini la mwisho...

**SPIKA:** Unatuchelewesha hebu kaa chini, bwana unatuchelewesha kaa chini. .Nasema kaa chini, Ubalozi wa India unatusaidia nini, tupoteze muda hapa kwa ajili ya India, hebu endelea Mheshimiwa, tena nakuomba ujiheshimu usitupotezee muda.

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru umenisaidia na sitamjibu nilikuwa na jibu dogo lakini sitamjibu. kwa maana hiyo sasa...

**SPIKA:** Mheshimiwa toka nje mpaka Bunge lijalo ndio tutakapokutana hapa ndani. Tuheshimiane hili ni Bunge, mtu anachangia mawazo yake, unageuka kuwa Muhindi inakusaidia nini, toka nje unatuchelewesha, hebu sogeeni apite. *(Makofi)*

Endelea Mheshimiwa Mollel

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, lakini hali ilivyo kwa sasa maana yake asilimia 95 ya korosho inaenda nje na maana yake huko nyuma tulikuwa tunabangua wenyewe asilimia 40. Hata hivyo, twende kwanza kwenye bei ya korosho maana yake kwa taarifa tunazozipata tunaambiwa ni Sh.3,800 tuseme ni Sh.4000, lakini ukibangua wanauza kwa kilo dola 35. Maana yake korosho ambazo hazijabanguliwa kilo mbili zinatoa kilo moja maana yake wao wanauza kilo moja iliyobanguliwa kwa Sh.39,000.

Mheshimiwa Spika, maana yake nini fedha zinazotuletea mgogoro hapa na mvutano ni asilimia ndogo ya Sh.4000, maana yake tunapoteza zaidi ya Sh.35,000. Kwa hiyo, ukiangalia Bodi iliyoko sasa, hatukai kabisa kwamba wamefanya kazi nzuri sana ya kuhakikisha mikoa mingine imepata korosho na mashamba mengine makubwa yameanzishwa na idadi ya tani ya korosho zimezalishwa.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, ukiangalia kwa maana ya biashara *per se* na faida tunakoelekea kwenye sera ya viwanda na kama kweli tunataka tufike mahali na sisi tumiliki uchumi wa nchi yetu maana yake ni kwamba sisi tumegeuka ni shamba la watu wengine kufanya biashara ya korosho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndio maana nasema ni lazima tuunge Muswada huu mkono kwa sababu unaenda kuiondoa Tanzania kuwa shamba la korosho na kuwa wazalishaji wa korosho na kuuza na sisi korosho duniani ili tuweze kupata mapato halali. Niwaambie kwamba kuna watu nashindwa kuelewa, hata tukifikiria kwa mfano Daraja la Mkapa limejengwa sio na pesa ya korosho, limejengwa na pesa ya Mlima Kilimanjaro, ya Ngorongoro na pesa ya madini huko Mwanza.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, kwa hiyo watu tunataka utusaidie, tufike mahali tunapoingia kwenye mijadala kwenye Bunge hili, tuhakikishe kitu cha kwanza kinachokuwa kwenye kichwa cha mtu kuunga na kuhakikisha unapomaliza kuzungumza na kukaa chini unaliacha Taifa letu likiwa pamoja na tukifikiri pamoja kwa ajili ya kuijenga nchi. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niseme kwamba Muswada huu tunauunga mkono na tunaunga thabiti kabisa na tunasema mawazo ya kusema tunaiendeleza korosho ni mawazo mazuri, lakini sheria iliyobadilika sasa haiendi kumnyang'anya mkulima wa korosho haki yake ya kupata pato lake. Sheria hii inaenda kuondoa watu wa kati ambao tukitafuta wawekezaji wa kuwekeza viwanda ndani ya Watanzania wanapigwa vita mpaka wanakimbia.

Mheshimiwa Spika, sasa hii sheria itaenda kuwalinda kitakachotokea hapa yatatokea viwanda kwa ajili ya korosho ndani ya Tanzania. Pia tutaanza kupata mapato ya kutosha na hela nyingi zitapatikana zaidi kwa ajili ya kwenda kumsaidia mkulima wa korosho na kusaidia ukuaji wa korosho kwenye maeneo mengine katika Taifa hili lakini vilevile kusaidia mazao mengine ya mkakati kwa ajili ya Taifa letu la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hicho ndicho kikubwa, hata hivyo, nashauri tutafakari zaidi pamoja na tunazungumzia hili zao la korosho, lakini tunazungumzia mazao mengine. Nitoe mfano mmoja wa zao la parachichi au matunda. Ukiangalia utaambiwa mara nyingi sehemu nyingi ambao wanalima matunda hayo tukichukulia mfano Wilaya yangu ya Siha wanalima parachichi unaambiwa wamepewa *EPZ*.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia *EPZ* waliyopewa unauliza kwa sababu wanafanya *process* nauliza *definition* ya *process* ni nini? Naambiwa sasa kwa maparachichi utakuta mtu anachukua parachichi anafanya *sorting,* anachagua kubwa na dogo linalofaa, halafu anafanya *serialization,* halafu anapaki, tayari amepewa *exemption,* anaambiwa aende, afanye *process.*

Mheshimiwa Spika, hapa nilitegemea kwamba, kama ni kufanya *process* ina maana angezalisha kile

ambacho kinatokana na mazao ya parachichi ili kama tunakosa kodi kwingine, basi tuhakikishe tunapata kwa kuwaajiri watu wetu na mambo mengine ambayo yatatokea. lakini bahati mbaya anaenda an afanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tumeangalia korosho tumeangalia na mazao mengine, twendeni tuingie ndani kwa sababu inawezekana *definition* niliyopewa na mtumishi mmoja wa Wizara ya viwanda inawezekana *definition* ya halali. Tuangalie hizi *definition* tunazofundishwa kwenye semina, wakati mwingine zimeficha vita vya kiuchumi ndani yake ili kuendelea kutunyonya ili kuhakikisha kwamba pamoja na kwamba sasa tunataka kuwa Taifa linalojitegemea watu wanakuja kwa kutumia hizi semina, kutumia uwezeshaji, tunapewa *definition* ambayo unajiuza mwenyewe bila kujijua na ukijiita mtalaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile kwa sababu sasa tunaenda kuunda sheria hii, naomba mtu yoyote atakayepewa leseni basi apewe sheria na utaratibu kabisa na kusimamiwa ndani ya miaka mtatu awe amewekeza kiwanda kwa ajili ya kubangua korosho na asipofanya hivyo basi anyang'anywe leseni na apewe mtu mwingine.

Mheshimiwa Spika, tuache wasiwasi wa kufikiri kwamba tutakosa wawekezaji na watu wa kuweza kununua korosho. Watu wengi wanahitaji kununua korosho, kinachotakiwa ni kuzingatia maneno ya Biblia ya kujiamini na kuamini kwamba tunaweza na wote kwa pamoja Bunge hili tuanze kuungana, tuamini kwamba Shida yetu ni Tanzania, shida yetu sio vyama vyetu tunafika tunaendaje Ikulu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapa muda mwingi tunaiua nchi yetu sisi wakati tukigombea madaraka tukifikiria ni namna

gani natoka, ni namna gani chama changu kitakuwa. Hapa tunachokisimamia ni Taifa letu la Tanzania twendeni tutulize akili, hili Bunge sasa ligeuke ni tanuru la tafakuru kwa ajili ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, tulipoletwa kutoka majimbo yetu hatukuletwa kuja kujenga vyama vyetu huku ndani, tumeletwa kuja kumsaidia Rais Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwenye dhamira yake ya kufanya ukombozi wa pili wa Mtanzania kiuchumi kwa sababu tulichokuwa tunakitafuta hatukutafuta uhuru wa bendera, tulihitaji uhuru wa bendera lakini rasilimali za Taifa hili tuanze kuzimiliki sasa sisi wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa vita hiyo imeanza, twendeni tuungane kwa pamoja, kila mtu aende kwenye tafakuri, aondoe hisia zake, uanze kuwa na mdomo mkubwa kuliko ubongo, tufanye kazi sasa ili tuweze kwenda mbele. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA**: Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Mollel. Mchangiaji anayefuata tunahamia *CUF,* Mheshimiwa Katani Katani.

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hoja iliyo mbele yetu. Binafsi napata ukakasi mkubwa wa jambo hili hususan hii fedha ya korosho ambayo tunaizungumza. Shida kubwa ninayoipata kwa sababu hii fedha tumeizungumza sheria ambayo ipo na kwa miaka sita mfululizo hizi fedha zimekuwa zikienda kule na zikiwa zinafanya kazi husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, miaka hii miwili ndiyo kimetokea kizungumkuti hiki ambacho kimekuja kuleta sheria hii ambayo tunatakiwa kufanya mabadiliko. Hii inanipa shida, kama maelezo yanayotolewa na Serikali ndivyo yalivyo, wakati Mwanasheria Mkuu wa Serikali anasema, aliyazungumza mambo mengi zikiwemo kanuni na vitu vingine, lakini ukijiuliza haya mambo nani aliyakosea? Ni wakulima wale tunaotaka kuwapa adhabu leo, au ni sisi watunga sheria au ni wasimamizi wa Serikali ambao ndio walipaswa kutunga hizo kanuni? Sijapata majibu yaliyo sahihi sana, dhamira ya Serikali kwenye jambo hili ni ipi?

Mheshimiwa Spika, nasikitika sana, amezungumza ndugu yangu Mheshimiwa Mwambe, alipokuwepo Katibu wa Fedha, Mheshimiwa Doto aliyazungumzia matumizi mabaya yaliyofanywa na Bodi pamoja na Mfuko. Tumezungumza hapa kwamba ripoti ya *CAG* imesema ubadhirifu unaonekana. Kwa nini kama kuna ubadhirifu, wasichukuliwe hatua wale wanaohusika? Mara kadhaa tumeona Serikali ikichukua hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwanzo, Mheshimiwa Waziri Mkuu amesimama hapa, akavunja Mfuko wa Kuendeleza Zao la Korosho, tukapiga makofi wote. Haikupita muda, akaondolewa Mkurugenzi wa Bodi ya Korosho wa kwanza, Ndugu Mfaume, tukaona Serikali inachukua hatua. Haukupita muda akaondolewa aliye-*act* Ukurugenzi wa pili juzi, Mheshimiwa Jarufu akaondolewa, tukaona Serikali imechukua hatua. Kuna ukakasi gani kama majibu haya ya Serikali yanayokinzana, maana mmoja anasema tatizo ni kanuni, mwingine anasema kuna matumizi mabovu ya fedha. Lipi tulibebe sisi wawakilishi kuwaambia watu wetu kule? Tunapata shida kwenye jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna suala la sheria ambalo tumelizungumza hapa, sheria ambayo imetungwa na Bunge. Kama kuna tatizo kwenye sheria, nani alikosea? Sasa kama ndiyo wameleta *amendment,* ni sawa, lakini je, fedha zile za miaka miwili ziendelee kubaki? Kule Mtwara Bodi ya Korosho

inadaiwa miche. Miche ambayo imepandwa Kongwa na Mpwapwa, wanaoizalisha ni wakulima wadogo, ambao hata leo Spika ukienda au ukiunda Tume iende kule; hata Mheshimiwa Dkt. Mpango analijua hili vizuri, amepeleka watu wake kufanya utafiti. Kama kutakuwa na upungufu ni tofauti ya hiyo miche.

Mheshimiwa Spika, Bodi labda inasema Sh.20,000/=, lakini ukienda utakuta labda ni Sh.19,000/=, lakini utakuta kweli kuna madeni ya msingi ambayo wanapaswa kulipwa wakulima na ndio wazalishaji wa miche ile. Hiyo miche ya korosho tunayozungumza, haizalishwi na mtu gani, ni wakulima. Ukienda Tandahimba, kuna vikundi vya wakulima wanazalisha miti, ukienda Naliendele, kuna vikundi vya wakulima wanazalisha hiyo miche.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2017 zimegaiwa pembejeo na Serikali bure. Waliogawa pembejeo wanadai fedha zile. Tunapozichukua zile fedha, hawa watu wanalipwa fedha kutoka wapi? Kama nia njema ya Serikali ipo hivyo, kwenye *amendment* yangu, nimeleta mapendekezo. Naona kabisa inawezekana Serikali ina nia njema kutafuta vyanzo vya mapato. Nikasema kwenye sheria ile badala ya kufuta, basi wachukue hamsini wao na sisi tubaki na hamsini ili korosho ziweze kuendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi jirani ya Msumbiji kwa miaka 11 sasa wakulima wa zao la korosho wanapewa dawa bure, wanapewa viuatilifu bure. Kwa nini tusiende kujifunza? Sasa kama wakulima wameandaa *MoU* wakakubali wenyewe kwamba tunaweza kukubali kupata fedha kwa namna hii, fedha zinapatikana, hata zile tulizokubaliana, tulizotungia sheria nazo zinakuwa ni matatizo. Shida iko wapi kwenye jambo hili? Nadhani itumike busara sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niseme wazi kabisa hakuna Mbunge wa Kusini anayetetea fedha hizi kwa maslahi ya Kusini. Kuna maneno yanazungumzwa hapa ambayo wakati mwingine hayana ushahidi.

Mheshimiwa Spika, labda hukuwepo, kuna Watu wamesimama wanachangia kwenye Bunge hili, wanasema kuna Wabunge wanahusika na wizi wa fedha hizo. Kama wapo, kwa nini wasichukuliwe hatua? Kama kweli kuna Mbunge anaonekana kwenye *documents* zao anahusika na mambo hayo, Wabunge hao wanatokana na vyama vyetu. Vyama vina taratibu zao na Serikali ina taratibu zake. Kama kweli kuna Mbunge anahusika, ndiyo maana nasema tunapokuja Bungeni tuje kwa nia njema. Tusije kutengeneza hoja ya kushawishi watu kwa sababu kuna jambo watu wanashawishi iaminike kwamba kuna Wabunge wamefanya biashara na hizo Bodi.

Mheshimiwa Spika, Serikali huwa inazungumza maneno haya chini chini. Kama kweli watu hao wapo na ushahidi upo, ndiyo sababu tumeunda Mahakama watu wapelekwe Mahakamani badala ya kuja hapa bila kuwa na hoja na ushahidi. Ukiwauliza waliotoa hoja zile kwamba lete ushahidi; Mheshimiwa Mwambe amezungumza habari ya hiyo kesi, ameleta na *document* kwamba Mahakama iliamua moja, mbili, tatu.

Mheshimiwa Spika, mtu anasimama tu hapa anasema kitu, ukimwuliza ni Mbunge gani? Hataji Mbunge. Kwa hiyo, unakuta kabisa kwamba kuna nia isiyo njema kwa wakulima wa korosho wa Tanzania, sio wa Mtwara. Sisi wa Mtwara tunazungumza maneno haya kwa sababu asilimia karibu 85 ya korosho zinatoka Mtwara na Lindi. Ni lazima tuseme, lakini hatusemi kwa maana kwamba tuna chuki na maeneo mengine, tuna chuki na Serikali. Ndiyo maana tumeshauri. Mfano, nimeshauri hapa kwamba fedha hizo hamsini iende huko kwenye *Consolidated Fund,* nyingine ibaki kwenye tasnia ya korosho.

Mheshimiwa Spika, sasa linapokuja suala watu wakajenga vitu ambavyo havipo, sisi tunazungumza kwa ajili ya kuitetea Serikali hiyo hiyo. Wakulima hawa wa korosho tunaowasema ni wakulima wa kipato cha chini sana. Ungepata fursa ya kwenda maeneo ya korosho, ni shida. Kuna kitu kwa Kimakonde kinaitwa *uhangu*. *Uhangu* ni kitu kimoja

cha hatari sana, ni upupu kwa Kiswahili. Huu ukikuwasha wewe Mheshimiwa Spika ambao hujakutana nao, utajua balaa la korosho lipoje. Wallah hizi fedha ungeomba kabisa kwamba hizi shilingi bilioni 200 ambazo Mheshimiwa Dkt. Mpango amezihifadhi (mimi najua kuna mahali alipozihifadhi) awapelekee basi, ziende zikalipe yale madeni, halafu baadaye ndiyo aje na nia njema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilisema mwanzo kwamba hii *amendment* ingeletwa kwa nia njema zaidi kama tungekaa; ulizungumza mwanzo kwa hekima sana kwenye Kiti chako. Mwanzo ukasema twende kwenye Kamati ya Bajeti. Tumekaa zaidi ya siku tatu sisi. Mwanzo alipata dharura, alifiwa, tukakubali amefiwa, akaitwa kikao kingine ambacho yupo, hakuja. Yaani hiyo yote, nia njema ya pamoja kabisa kwamba hili jambo kabla hatujafika huko kupiga makelele tungekuwa tumemaliza na Mheshimiwa Dkt. Mpango, hakuja. Ukakaa, jambo ambalo mpaka leo sijui majibu yake yako wapi mpaka leo?

Mheshimiwa Spika, siku hiyo hiyo ukazungumza kwamba Waziri Mkuu hayupo, akija Waziri Mkuu mwenye jambo hili mtakaa kulizungumza. Hata lenyewe sikuona hata huo muda wa kupata kukaa kulizungumzia jambo hili.

Mheshimiwa Spika, mwanzo tumeanza na Wizara ya Kilimo kwa nia njema. Mheshimiwa Dkt. Mpango angejua nia njema ya kwetu wala tusingefika hapa kwenye mgawanyiko usiokuwa na sababu. Kwa sababu leo analigawa Taifa kwa misingi ya watu kupandikiza chuki kwamba Wabunge wa Kusini labda kuna maslahi fulani wanayatetea, kumbe sisi tunatetea kitu ambacho kipo kisheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba sana, mnaodhani kwamba kuna watu wana maslahi kwa Wabunge wa Kusini, vyombo vya sheria vipo, kama mna ushahidi, hao watu wachukuliwe hatua. Hata ningekuwa

mimi ninayezungumza nikaonekana nahusika kwenye huo ubadhirifu mnaosema, nichukuliwe hatua kwa mujibu wa sheria za nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakulima wale, watu wale wa Bodi ya Korosho ambao wana madeni, fedha hizi ziende ili kunusuru matatizo yaliyokuwepo kwenye tasnia ya korosho. Nawaomba sana, ukipata fursa kwenda *Ivory Coast,* ninyi wakati mnaondoa hii *Export Levy* ya kwenye korosho, *Ivory Coast* wao wanatoa asilimia 85 wakulima wa Korosho. Sijui sisi tunajifunza wapi haya mambo.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana tumeshauri na nimeendelea kushauri kwamba Mheshimiwa Dkt. Mpango, tunajua kwamba Serikali ina shida ya fedha, basi tuchukue hamsini wapelekeeni watu wa korosho, hamsini chukueni Serikali, tuendelee kuiendeleza nchi yetu kwa nia njema ile ile ambayo tunaikusudia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Katani. Kidogo ninachokifahamu ni kwamba Wabunge wa Kusini mlikutana na Mheshimiwa Waziri Mkuu juzi tu hapa, hata siku tatu hazijakwisha, Mheshimiwa Katani ukiwepo. Sasa leo tena unakanusha hapa kaka! Haya! Pia hujajibu lile swali la hawa Wabunge, kwa nini utaratibu huu wa korosho upo peke yake?

Tunaendelea na michango. Mheshimiwa Zitto, atafuatiwa na Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa na Mheshimiwa Mgumba atafuatia.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Muswada huu wa Fedha na nina mambo matatu tu. Nina suala la *Treasury Single Account* kama jinsi linavyopendekezwa, suala la kodi kwenye maji kama ambavyo Kamati ya Bajeti inavyopendekeza na nina suala la Sheria ya Korosho. Naomba nianze na hili la Sheria ya Korosho.

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba Bunge lako Tukufu lifahamu, kwamba hakuna zao lingine lolote Tanzania lina *Export Levy.* Naomba hili lieleweke vizuri, kwa sababu inaonekana kama kuna *misinformation* ambayo inasambaa ili ionekane kwamba watu wa korosho wanahitaji *special treatment*.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi nimetoka kusoma kwenye tovuti ya *TRA*, inasema *exports are free of duty and taxes except for three items; raw hides and skins, raw cashewnuts and these are wet blue hides and skins* na wameweka *charge* zao pale. Kwa hiyo, naomba hili liwe *very clear.*

Mheshimiwa Spika, Tanzania hii ni zao moja tu lina *Export Levy.* Pamba haina *Export Levy,* kahawa haina *Export Levy,* chai haina *Export Levy* na tumbaku haina *Export Levy.* Soma *Tobacco Industry Act, Cotton Industry Act, Tea Industry Act, Coffee Industry Act. So,* naomba hili liwe *very clear. Why Korosho Export Levy? (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii kodi imeanzishwa na Wadau wa Korosho wenyewe. Hii kodi haikuanzishwa na Serikali. Wadau wa Korosho walikaa wakaamua kwenye Mkutano wao kwamba tunataka tuongeze thamani ya korosho humu ndani. Tufanyeje Serikali haina hela? Wakakubaliana na *exporters.* Ninyi *exporters* lipeni, walianzia *3%,* sasa hivi imefika 15%. Ndiyo ule msingi wa kesi ambayo Mheshimiwa *Attorney General* aliizungumza hapa na kuli-*mislead* Bunge kabisa. Mimi namheshimu sana, nimesoma naye Chuo Kikuu, nilikuwa naye *Human Rights Association* ya Chuo Kikuu. Nimeshangaa sana.

Mheshimiwa Spika, kesi ile ilikuwa inahusu Bodi ya Korosho na hao wadau wa korosho. Wadau wenyewe ndio walioanzisha hii, wakaja kutuomba Bungeni mwaka 2010 tulikaa wewe ukiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Maliaslili na Utalii. Mmoja wa watu tulikaa nao kwenye kikao kikiongozwa na Marehemu Abdallah Kigoda, ni Mheshimiwa Waziri wa

Utawala Bora yuko hapa. Wameomba wenyewe, jamani tutozeni hii kodi ili tuendeleze sekta.

Mheshimiwa Spika, sasa Serikali wanataka nini? Ndiyo maana watu wa pamba hawana, hawakuomba; tumbaku hawana, hawakuomba; na chai hawana, hawakuomba. Hivi hatuoni aibu! Watu wameomba wenyewe watozwe ili waendeleze zao lao, halafu sisi tunasema aah, tunazichukua zote asilimia 100, haiwezekani. Ni ubinadamu tu, tusiwe wakatili jamani. Kwa nini tuwe katili kwa jambo ambalo watu wameomba wenyewe? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia nilifahamishe Bunge lako Tukufu...

**SPIKA:** Kwa maana ya ufafanuzi tu Mheshimiwa Zitto...

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Naam!

**SPIKA:** Kwa maana ya ufafanuzi tu. Endelea tu kusimama, wala huna haja ya kukaa. Waliomba wenyewe watozwe, una maana ya wakulima? Mbona anayetozwa ni *expoter* na sio mkulima? *(Makofi)*

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Nitalieleweshа vizuri tu hili. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Spika, hawa watu wa korosho wana Mkutano kila mwaka, unaitwa Mkutano Mkuu wa Wadau wa Korosho. Kila mwaka wanakutana na Serikali, wanakubaliana wafanye nini? Kuna kipindi uzalishaji wa korosho ulikuwa mdogo sana, ilifika mpaka tani 20,000 tu. Kumbuka, nilikuwa napenda hili nimweleze Ndugu Mollel vizuri, ni vema awe anaelewa historia vizuri.

Mheshimiwa Spika, mwaka 1975 ndiyo mwaka wa mwisho tumezalisha zaidi ya tani 100,000 za korosho na tukaenda kukopa *World Bank* kwa ajili ya viwanda. Kwa hiyo, maelezo aliyoyatoa siyo sahihi. Kwa hiyo, hawa wadau wakasema kwa nini zao haliendelei? Wakasema ninyi

*exporters* lipeni kidogo, tuweze kununua pembejeo ya kufanya uzalishaji uongezeke. *Exporters* wakakubali. Hizi hela ziende wapi? Wakakubaliana ziende Mfuko wa Kuendeleza Zao la Korosho. Mfuko ukaundwa kwa mujibu wa Sheria ya Kabidhi Wasii Mkuu, tofauti kabisa na maelezo ambayo Mheshimiwa *Attorney General* aliyatoa hapa Bungeni. Hata huo uvunjaji wa Mfuko katika hali ya kawaida ilikuwa ni kinyume cha sheria.

Mheshmiwa Spika, ule mfuko una *exporters,* una wakulima, una wanunuzi, ni jambo lao. Wakaiomba Serikali tuchukulieni hii kodi. Mwanzoni ilikuwa inatolewa na Bodi kwa *regulations.* Bodi wakawazunguka wadau, wakaamua waiombe *TRA* ndiyo mantiki ya sheria ya mwaka 2010. *TRA* wakasema, sisi tukikusanya mnatupa nini? Wakasema sawa, sisi tupeni 65% nyie chukueni 35%. Ndiyo *the origin* ya *section 17A.* Sasa mtu aliyekuja kuomba, leo unaona aah, unachukua chote, haiwezekani! Hizi ni fedha zao za kuendeleza zao lao. Sisi tuwaachie waendelee.

Mheshimiwa Spika, kama alivyosema Mheshimiwa Katani na naomba hii Serikali iliangalie. Wakati *proposal* ya 65% na 35% inatoka, uzalishaji ulikuwa mdogo, kwa hiyo, fedha hazikuwa nyingi sana. Sasa hivi uzalishaji umeongezeka sana, fedha zimekuwa nyingi sana. Hoja hapa ni Serikali ingerudi kwenye Mkutano wa Wadau kama walivyofanya kabla, wakakubaliana, jamani hizi hela nyingi sana, basi tugeuze hii 65% ndiyo iende Mfuko Mkuu, hii 35% irudi kwa wakulima. Wala wakulima hawawezi kuwa na shida na jambo hilo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba utu-*guide* vizuri *on that.* Kwa hiyo, nimemaliza katika hilo eneo. Naunga mkono mapendekezo ya Kamati ya Bajeti kama jinsi ambavyo imewasilishwa na Kamati. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Moja dogo sana Mheshimiwa Zitto nalinda muda wako wala usiwe na wasiwasi. Endelea kusimama tu. Waliunda *Trust Fund* hawa watu?

**MHE. KABWE ZUBEIR R. ZITTO:** Ndiyo.

**SPIKA:** Wanapounda *Trust Fund* kwa Kabidhi Wasii Mkuu, hiki ni kitu *Private Trust Fund.* Maana kikishakuwa *Trust Fund* ni kitu kiko huko, cha wenyewe. Iweje *TRA* ya Serikali iwe inakusanya hela halafu inapeleka kwenye Mfuko wa mtu binafsi?

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, swali zuri sana hilo.

**SPIKA:** Yaani ni wapi kwingine ambako *TRA* inaweza kukusanya hela, halafu ikampelekea mtu binafsi?

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, swali zuri sana. Hicho ndicho ambacho *Section 17A* ilikijibu kufuatia hukumu ya Mahakama. Kwa sababu katika mazao yote, Bodi zimepewa *powers* za kuweka *regulations* za makusanyo. Kukawa na mgogoro kati ya Bodi na *Trust Fund. Trust Fund* ikaenda Serikalini ikaomba, *TRA* wakauliza hivyo hivyo. Ndiyo *Trust Fund* ikasema, basi ninyi mtachukua 35%.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana hili ndiyo zao pekee lina *Export Levy.* Kwa nini hamna kwenye pamba, hatuuzi pamba ghafi nje? Kwa nini hamna kwenye kahawa, hatuuzi kahawa ghafi nje? Kwa nini hamna kwenye chai, hatuuzi chai ghafi nje? *The genesis of this matter* ni kwamba wameomba wadau. Wakaiomba *TRA* iwe Wakala wao na wanamlipa *TRA* asilimia 35. Hii ndiyo hali halisi ya jambo hili.

Mheshimiwa Spika, naomba niendelee na hoja zangu za mwisho. Sasa nakuja na suala la *Treasury Single Account.* Wazo la *Treasury Single Account* ni wazo zuri sana. Nimeshiriki kwa ruhusa yako kwenye Kamati ya Bajeti na tumelijadili, ni wazo zuri sana, lakini lina jambo la Kikatiba. *Treasury Single Account* ina jambo la Kikatiba; na tukifanya makosa tukaipitisha leo, Bunge hili litakuwa linakwenda kuvunja Katiba. *Section 136* ya Katiba inaelezea namna ambavyo..

**SPIKA:** Hapo nenda polepole.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Sawa sawa.

**SPIKA:** Muda wako tutaulinda, wala usiwe na wasiwasi. Katibu namwongezea dakika tano. Mia thelathini na...

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, *Section 136(1)(b)*. Inaelezea namna ambavyo matumizi yanaidhinishwa na Bunge. Naombeni ile tuliyopitisha juzi, *Appropriation Act.* Hii *Appropriation Act* ndiyo ambayo inakuwa *referred to* na *Section 136*(b) ya Katiba.

Mheshimiwa Spika, tukishatimiza wajibu wetu, tumepitisha *Appropriation Act.* Pendekezo la Serikali linataka moja, fedha ambazo sisi hatuhusiki nazo, *un-voted* ziingie Mfuko Mkuu wa Serikali, hazitajwi na Katiba. Hatuhusiki nazo, hazimo kwenye *Appropriation Act.*

**MHE. OMARY T. MGUMBA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Naomba nimalize, utatoa taarifa.

**SPIKA:** Vumilia nitakupa nafasi, lakini tumpe nafasi ajenge hoja maana hatujamwelewa vizuri. Endelea Mheshimiwa Zitto.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, naomba niendelee.

**SPIKA:** Endelea Mheshimiwa Zitto.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, nenda *Section 143(2)* kuhusiana na namna ambavyo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anapaswa kuwa, ni kwamba fedha zote zinazotoka Mfuko Mkuu wa Hazina kwenda kwenye mafungu ambayo Bunge limepitisha *Appropriation Act,* Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali anaidhinisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali inataka nini?

**MBUNGE FULANI:** Mh!

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Serikali inataka ichukue fedha ambazo ziko Mfuko Mkuu wa Hazina iziiingize kwenye *Treasury Single Account* halafu ndiyo iende ikazigawe. Huwezi kufanya hivyo bila ku-*ammend Public Audit Act* ili sasa impe mamlaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ku-*approve* fedha zinazotoka Mfuko Mkuu wa Hazina kwa ujumla wake bila *Appropriation Act,* halafu wakati mnazitoa kutoka *Treasury Single Account* kwenda kwenye mafungu aweze kuzi-*approve* kwa kupitia *Appropriation Act. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pendekezo hili la Serikali linamfanya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuwa *redundant.* Ataona *32 trillion* kwa ujumla wake kuingia Mfuko Mkuu ile *TSA…*

**SPIKA:** Sasa subiri, kuna Taarifa huko unapewa. Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. OMARY T. MGUMBA:** Mheshimiwa Spika, nilikuwa nataka kumpa Taarifa mzungumzaji anayeongea. Katika mazungumzo yake anasema *TRA* walikuwa wanakusanya pesa za wakulima wa korosho wa Mtwara…

**SPIKA:** Naomba tusikilizane.

**MHE. OMARY T. MGUMBA:** Kitu ambacho kutokana na Sheria Na. 15 *Cap* 203 ya 2010 hiyo anayo-*refer* ipo hapa, naomba ninukuu:

*An Act to impose and alter certain taxes duties, levies, fees and amended certain written laws relating to the collection and management of public revenue.*

Inakwenda katika *Section* (4), inasema; 17A(1) "*A person who exports raw cashewnut, shall pay an Export Levy*

*to be computed and collected by Tanzania Revenue Authority at the rate of 15% of FOB value or the amount equivalent to United States Dollars 160 per metric tonnes."*

Mheshimiwa Spika, sasa anaposema kwamba *TRA* walikuwa wanakusanya fedha za wakulima kama wao ni Mawakala wao, siyo kweli. Hii ni *public revenue,* ni pesa ya umma ilikuwa inakusanywa na *TRA* kama ulivyosema Mheshimiwa Spika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zitto, Taarifa hiyo.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, kubwa sana na naomba radhi kwa Wabunge wengine wapya. Wabunge wapya wawe wanapata semina sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa Wabunge wazoefu wanajua, unapoleta *Finance Act* unaingiza na sheria nyingine ambazo hazihusiani kabisa na fedha na ndiyo kama *Cashewnut Industry* na mengine yote ambayo tunafanya. Ni rafiki yangu, nitakaa naye pembeni nitamwelewesha kwa sababu pia amesoma maeneo ambayo siyo... *(Makofi/Kicheko)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU):** Taarifa.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie. *TSA* tayari, naomba nimalizie na maji.

**SPIKA:** Naomba umwache amalizie. Malizia! Aah, *Chief Whip, ok!* Samahani, nilikuwa naisikia nyuma huko. *Chief Whip, please.*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Spika, nimekuwa namfuatilia sana Mheshimiwa Zitto na hasa alipofika kwenye Kifungu kinachohusu Akaunti ya Pamoja *(TSA)* na alikuwa anajenga hoja hapa ambayo naielewa, lakini naomba nimpeleke Mheshimiwa Zitto kwenye *amendment* ambayo imeletwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, akiangalia ile *amendment*, tumefanya mabadiliko ambayo yanakwenda sasa kukidhi mazingira halisi ambayo hayataisababisha Serikali kwenye kufunja sheria wala Katiba wala kwenda kinyume na utaratibu wowote. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Zitto.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, ndiyo maana Kamati ya Bajeti imeomba jambo hili lipewe muda zaidi. Hiyo *amendment* ambayo imeletwa na Serikali, yaani haina hata maana, kwa sababu wanasema ni *un-spent funds.* Haina hata maana. Ukisoma Taarifa ya Kamati ya Bajeti ndiyo maana tuliiomba hii Taarifa mapema, watakuonesha, kwenye *Bank of Tanzania Act* kuna *other sections, section 35, 36* ambazo bado zina-*refer unvoted revenue* ambapo ilipaswa zifanyiwe *amendment.*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, huwezi kuwa na *TSA* leo, hujafanya *amendment* ya *Public Audit Act.* Hamna kwenye hii sheria. Huwezi kuwa na *TSA* leo hujafanya *amendment* ya Katiba yetu kwa ajili ya ku-*widen* mamlaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuwatazama. Mnaweza mkaamua, mkaipitisha, mkaweka tarehe na mapendekezo tarehe 30 Septemba ni karibu mno. Toeni miezi sita, mwaka mmoja ili kipindi hiki cha katikati matayarisho hayo yaweze kufanyika. Kwa sababu hili jambo ni zuri, lakini lina mambo ambayo hayajafanyiwa kazi, *Public Audit Act* lazima iwe *amended, Bank of Tanzania Act* inapaswa kuwa *amended in totality* kwa mujibu wa Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nimalize. Hili la maji wengine wataliongea.

Waheshimiwa Wabunge wenzangu, sisi humu kama Bunge, wanaotufanyia kazi ni Kamati za Bunge ambazo Mheshimiwa Spika ameziunda, ndiyo wanaokaa mpaka saa nane usiku kufanya *analysis.* Kamati inapoleta taarifa yake ndani ya Bunge, wewe ukai-*reject* Taarifa ya Kamati, umelikataa Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba hili jambo kwa mara nyingine uwape Semina Waheshimiwa Wabunge. Kamati ndiyo Bunge, zinafanya kazi kwa niaba yetu. Kama Kamati ya Bajeti imeleta mapendekezo, imeyafanyia kazi, imeita watu, imeita watafiti, watu wamekaa mpaka saa nane usiku, ikaingia humu ndani mkai-*disregard,* sijui tutakuwa ni Bunge la namba gani.

Mheshimiwa Spika, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mchengerwa, atafuatiwa na Mheshimiwa Mgumba.

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kukushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia, lakini nianze kama vile ambavyo Vladimir Lenin Mwasisi wa Taifa la Kirusi amekuwa akianza katika hotuba zake kabla ya *Russian Revolution* mwaka 1905 - 1907 kwa kumwomba Mwenyezi Mungu kuendelea kuipa hekima na busara Serikali yangu ya Awamu ya Tano na kumpa afya njema Rais wangu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mjadala huu umesababisha kuibuka kwa hoja nyingi ambazo kwa namna moja au nyingine zinadhihirisha wazi kabisa kwamba kuna matabaka ya kikabila na ya kikanda ambayo yamekuwa yakiibuka kwenye Bunge lako hili Tukufu.

Mheshimiwa Spika, nami naiomba sana Serikali kuzingatia Kanuni *(The Law of Connection),* zile Kanuni ambazo ziliwahi kutolewa na Dkt. Maxwell. Tuwashike mioyo wananchi wetu. Kabla hatujakwenda kuwaomba mikono, basi tuzingatie kuwashika sana mioyo wananchi wetu na tuwahurumie sana wananchi wa Mikoa ya Kusini na Pwani. Tunapozungumzia Pwani tunaanzia Kibiti, Rufiji pamoja na maeneo ya Kusini Lindi na Mtwara kwa kuwa mijadala ya korosho ni siasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipindi hiki cha siku mbili, tatu mjadala huu umeibuka, tumetengeneza *heroes* wengi ndani ya Bunge lako hili Tukufu pengine bila Serikali kutambua jambo hilo.

Mheshimiwa Spika, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ya 63 na Ibara ya 64 ya Katiba hii imeipa mamlaka Bunge kutunga sheria. Ibara ya 13(5) imeipa mamlaka Bunge kutunga sheria. Zipo sheria ambazo zinapaswa kutungwa na Bunge, sheria zile zikawa na *element* za kibaguzi.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kabisa, Bunge linaweza kutunga sheria ambayo inaenda kubagua watu au sehemu fulani. Hayo aliyafanya hata Mwalimu Nyerere miaka ya 1970 pale alipotoa mwamko wa elimu kwa watu wa Kanda ya Kati na kutunga Kanuni za Elimu ambazo ziliwasaidia watu wa Kanda ya Kati ambao kwa kipindi kile walikuwa hawajapata mwamko mkubwa wa elimu.

Mheshimiwa Spika, hili tuliliona kwa sababu wapo maprofesa ambao walisoma nchi hii kwa kuwa Mwalimu Nyerere alitunga Kanuni za kiupendeleo wakati ule, lakini pia hata sheria hizi ambazo leo hii zimezungumzwa sana kwenye Bunge lako Tukufu...

**SPIKA:** Mheshimiwa Mchengerwa, sisi watu wa Kanda ya Kati tulitungiwa sheria ya kupendelewa kitu gani? *(Kicheko)*

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA:** Mheshimiwa Spika, Mwalimu Nyerere alitoa upendeleo kwa baadhi ya maeneo. Naomba nijikite katika Ibara ya 13(5), naomba niisome, inasema hivi:

*"Kwa madhumuni ya ufafanuzi wa masharti ya Ibara hii neno 'kubagua' maana yake ni kutimiza haja, haki au mahitaji mengineyo kwa watu mbalimbali kwa kuzingatia Utaifa wao, kabila, mahali walipotokea, maoneo ya kisiasa, rangi, dini, jinsia au hali yao ya kimaisha.*

Mheshimiwa Spika, inaendelea kusema kwamba, watu wa aina fulani wanafanywa au kuhesabiwa kuwa dhaifu au duni, kuwekewa vikwazo au masharti ya vipingamizi ambapo watu wa aina nyingine wanatendewa tofauti au wanapewa fursa au faida iliyoko nje ya masharti au sifa za lazima. Isipokuwa kwamba neno kubagua halitafafanuliwa kwa mujibu wa Katiba hii, kwa maana hiyo, itazuia Serikali kuchukua hatua za makusudi zenye lengo la kurekebisha matatizo mahsusi katika jamii.

Mheshimiwa Spika, pengine wakati sheria hii ya korosho inatungwa, wakati huo Mwalimu...

**SPIKA:** Nilikuuliza, watu wa Kanda ya Kati, umesema walitungiwa sheria ya kupendelewa na Mwalimu Nyerere. Walipendelewa jambo gani? Si ufute tu kama uliteleza ulimi! *(Kicheko)*

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA:** Mheshimiwa Spika, naomba niseme kwamba ipo mipango ambayo Serikali ilifanya, pengine siyo sheria wala siyo kanuni, naomba niondoe maneno hayo ambayo mipango au taratibu zile ziliweza kuwasaidia baadhi ya watu wakapata elimu ili kuweza kuondoa ile hali ambayo ilikuwepo katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, msingi wa mjadala huu wa siku ya leo ninaomba nijikite katika Sura ya 203, Sura ya147 pamoja na Sura ya 123. Nchi yetu hii, Serikali imepata mamlaka kwa mujibu wa Ibara ya 8 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwamba wananchi ndiyo msingi wa Serikali na Serikali itapata madaraka na mamlaka yake yote kutoka kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, lengo kuu la Serikali wakati wote liwe ni ustawi wa wananchi wake na mimi nianze kwa kusema kwamba ninaunga mkono jitihada za Serikali katika kupambana na kudhibiti matumizi mabaya. Naunga mkono kwa hali zote. Mjadala huu uliweza kumwibua Mwanasheria Mkuu wa Serikali na nimeona hapa Mheshimiwa Mwambe

amezungumzia kesi ambayo Wakili namba moja wa nchi yetu hii, Mwanasheria Mkuu wa Serikali aliizungumza kesi hii.

Mheshimiwa Spika, sitaki kwenda ndani kwenye msingi wa kesi hii, japokuwa tunafahamu kwamba hukumu za Mahakama zinazingatia mambo makuu matatu; zinazingatia maelezo ya kina yaliyopo katika kesi husika, lakini pia zinazingatia *analysis* ya ushahidi pamoja na sheria zilizotumika katika kufanya maamuzi ya kesi husika na mwisho kabisa zinazingatia *reason* ya hukumu iliyotolewa na Mahakama.

Mheshimiwa Spika, msimamo wa Mahakama utaendelea kuwa kwamba fedha hizi ni za wakulima. Hii ni kwa mujibu wa hukumu iliyotolewa na Mahakama. Hapo hapo natambua kwa dhati kabisa jitihada za Serikali ya Awamu ya Tano za kwenda kudhibiti matumizi mabaya. Nami nampongeza sana Rais wangu wa Serikali ya Awamu ya Tano kwa namna ya kipekee kabisa, baada ya kuona kwamba matumizi ya fedha hizi haziendi kuwasaidia wananchi au haziendi kusaidia lengo lililokusudiwa wakati wa kutungwa kwa sheria hii naomba kutoa mapendekezo yafuatayo Serikali iweze kuyapokea:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, kwa kuwa watu wa Pwani na Kusini wanaona kabisa kwamba kwa muda mrefu Serikali imekuwa ikiwaacha pembeni na pengine ndiyo sababu ya msingi ya kutungwa kwa sheria hii. Naiomba Serikali kuzingatia matakwa ya Ibara ya 9 ya Katiba ambayo yanasema kwamba, shughuli za Serikali...

**SPIKA:** Mheshimiwa Mchengerwa, yako maneno ambayo wala hayatujengi kama Taifa. Hii habari ya kusema kwa muda mrefu watu wa Pwani sijui na wapi wanaachwa na Serikali, unayatoa wapi? Yana ushahidi gani? Yaani wapi ambako sisi tuna...; maana Serikali kama ni fedha sisi Wabunge ndio tunapitisha hapa na kadhalika. Sasa huo ubaguzi unaouzungumzia kwamba kuna watu wanabaguliwa, wanaachwa, kivipi? Kwa nini sisi Wabunge ndio tunaanza kuweka hii chumvi mbaya kwa watu wetu?

Ndiyo maana mwanzoni nikakuuliza, umesema watu wa Kanda ya Kati walibaguliwa, nikakuuliza tulibaguliwa nini sisi? Sisi kama hatukusoma, hatukubaguliwa, ni sisi wenyewe tu na mambo yetu. Sisi tulikuwa tunaona kuchunga ng'ombe ndiyo shughuli yenyewe. Wenzetu wa Kaskazini na wapi wakaona kusoma ndiyo shughuli yenyewe na kadhalika. Pwani nako walikuwa nao na vionjo vyao. *(Makofi/Kicheko)*

Kwa hiyo, hivi vitu vya ubaguzi tusivipende sana. Ni ushauri tu wa ujumla. *Yah!*

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA:** Mheshimiwa Spika, kimsingi nilikuwa najikita kwenye maoni yaliyotolewa na Wabunge wengi kwenye Bunge lako Tukufu, hayo yalikuwa ni maoni ya Wabunge wengine wala siyo maoni yangu, naomba nirekebishe jambo hilo.

Mheshimiwa Spika, niseme kabisa kwa dhati mimi binafsi natambua jitihada za Serikali hususan jitihada anazichukua Rais Dkt. John Pombe Magufuli kudhibiti matumizi ya fedha. Ndiyo maana katika moja ya mapendekezo yangu ninaiomba Serikali, kwa kuwa dhamira ya kuendeleza zao la korosho ni pamoja na kuwepo kwa tafiti na maendelo ya watu, niiombe Serikali sasa kwa namna ile ile kuangalia yale madeni yaliyopo kwa sasa na kuona uwezekano wa Serikali kudhibiti fedha zile yenyewe. Hayo ni baadhi ya maoni yangu.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa nukuu ya Baba wa Taifa, Mwalimu Nyerere aliyowahi kuitoa mwaka 1962 na nukuu hii naomba nijielekeze moja kwa moja kwa kijana mwana-CCM Tegemeo Saambili ambaye aliwahi kuandika kuhusu maana halisi ya kiongozi akifanya *reference* ukurasa wa 50 wa hotuba ya Mwalimu Nyerere.

Mheshimiwa Spika, kwa ridhaa yako naomba niisome hotuba hii. Mwalimu Nyerere aliwahi kusema:

"Uhuru tulioutaka haukuwa uhuru wa kuondokana na Wakoloni, tulitaka uhuru uwepo kwa kila mwananchi na

kushirikiana na mwenzake kuijenga nchi yetu mpya, nchi ambayo raia wote ni sawa bila kugawanyika baina ya watawala na watawaliwa, baina ya matajiri na masikini, wajinga na wenye elimu, wenye taabu na wenye raha. Tulitaka kujenga nchi ambayo raia wote wanayo furaha ile ile ya kupata heshima, elimu na riziki na wote wakiwa na nafasi ile ile ya kuitumikia nchi yao kwa kadri ya uwezo wao."

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naridhia mapendekezo ya Serikali. Pia, naiomba Serikali sasa iende kudhibiti matumizi ya fedha hizi ili sasa yale matakwa ambayo yalikusudiwa katika matumizi ya fedha hizi yaende moja kwa moja kama ambavyo Serikali imedhamiria kufanya.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mchengerwa, ukisikia mtu ambaye hakujiandaa kabisa kuchangia Muswada huu, ni wewe. *(Makofi/Kicheko)*

Huu ni Muswada wa Sheria ya Fedha. Unapojadili sheria, ni tofauti kabisa na unapojadili Bajeti ya Wizara nyingine. Unapojadili sheria, hapa tulipo sasa ni mahali pa kipengele, kifungu, kitu gani kina tatizo wapi? Sasa sijui kwenye Sheria hii ya Fedha ubaguzi uko wapi? Au nini kiko wapi? Jamani mnapojiandikisha humu mjiandae kidogo. Mjielekeze kwenye hoja zilizopo mezani muisaidie Serikali. Maana nimemwangalia Waziri wa Fedha mwanzo, mwisho hakushika kalamu yake kabisa. Hata hivyo tunapokea mchango wako.

Sasa jioni tutaanza na Mheshimiwa Mgumba na wengine. Naomba tuwahi ili tuweze kuendelea na mjadala wetu. Mjadala ni mzuri, unataka mtu ufikiri, utulie, uone ni wapi pa kuchangia.

Kwa hiyo, nasitisha shughuli za Bunge hadi saa kumi na moja kamili jioni.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge lilisitishwa mpaka Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, inabidi tutumie muda wetu vizuri kadri inavyowezekana, wachache tutapata nafasi, baada ya hapo itabidi tuingie kwenye vifungu ili twende *straight* kwenye maeneo ambayo Waheshimiwa Wabunge mngependa kujielekeza kwa hayo.

Kwa hiyo, mchangiaji wetu wa kwanza, tuanze na upande wa CHADEMA, Mheshimiwa David Silinde, dakika 10 tafadhali.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia fursa hii nami kuchangia Sheria ya Fedha ya Mwaka, 2018.

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza ambalo napenda kuanza nalo ni hii sheria ambayo Serikali inakwenda kufuta Tume ya Mipango. Katika jambo ambalo kwa mara ya kwanza katika Taifa linashangaza kweli kweli, ni uamuzi wa Serikali kwenda kufuta Tume ya Mipango. Hii kwa mara ya kwanza ni kitu ambacho kinashangaza.

Mheshimiwa Spika, miaka yote hii sheria imekuwepo, tangu mwaka 1994 kumekuwepo na Tume ya Mipango kwa maana ya *The Planning Commission*. Cha ajabu katika mwaka huu wa fedha kwenye Sura hii ya 13, Serikali imekuja na *amendment* ya kufuta Tume ya Mipango. Sasa unajiuliza, hivi lengo la Serikali kufuta Tume ya Mipango ni nini? Wanakwambia unajua hii sheria iliyopo ni kama inamlazimisha Rais kuitekeleza. *There shall be establishment* ya hii *Planning Commission*.

Mheshimiwa Spika, sisi kwenye Kamati jana tulikaa, tukabishana na Serikali tukawaeleza kuna ubaya gani ama

kuna athari gani za kiuchumi za kufuta Sheria ya Tume ya Mipango? Serikali ikasema tunatakiwa tuifute kwa sababu mwenye mamlaka hataki kutumia.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa mkali sana kwenye hili na haya maneno alizungumza Waziri wa Fedha ndani ya Kamati ya Bajeti. Nikamwambia kama mwenye mamlaka hataki tuhoji jambo hili, mmelileta kwenye Kamati ya Bunge kufanya nini? Yaani unaleta kufuta sheria halafu unatuambia tusihoji mamlaka. Tukasema hatuwezi kuishi katika huu mfumo. Kwa hiyo, kumbe haya maamuzi hatutungi sheria kwa ajili ya kusaidia nchi, ni kwa ajili ya kumsaidia mtu. Imenisikitisha sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa unajua kabisa umuhimu wa Tume ya Mipango, nchi zote duniani zina Tume ya Mipango hata kama zinatengenezwa katika majina tofauti. Kuna nchi nyingine wanaita *National Development Plan, National Development Vision,* yaani majina tofauti.

Mheshimiwa Spika, leo Tanzania kwa mara ya kwanza tunakwenda kuifuta sheria ya mwaka 1994 baada ya miaka 24, tunaona haina umuhimu. Ukimuuliza huyo mtu ambaye anakwenda kuifuta, Mheshimiwa Waziri wa Fedha ndio ambaye alikuwa Katibu wa Tume ya Mipango; yaani miaka mitano ya Jakaya Kikwete ndio alikuwa Katibu wa Tume ya Mipango. Leo wanasema majukumu ya Tume ya Mipango yanahamishiwa Wizara ya Fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuambiane ukweli, Wizara ya Fedha na Mipango imejikita zaidi upande wa fedha kuliko mipango, yaani kama kina kitu ambacho Wizara ya Fedha haifanyi ni Mipango. Leo unapokwenda kuifuta hii Sheria ya Mipango, maana yake ni kwamba tunawaachia sasa Serikali yaani Wizara ya Fedha, uamuzi wa wao kuamua kujipangia mambo na kutekeleza wao wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa maoni yangu ni nini? Kwa nini wanakwenda kuifuta hii Tume ya Mipango? Hata hivyo wameshaifuta, kwa nini? Ni kwa sababu wamekuwa na

mipango ya kushtukiza ambayo haipo na wala Bungeni hatukupangia Bajeti. Sasa kutokana na kuona kwamba wamekuwa ni watu ambao hawajui mwelekeo unakwendaje, wameamua kwenda kufuta ili wawe wanapanga mambo wanayotaka wenyewe. Huo ndiyo ukweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa Taifa bila Tume ya Mipango ni sawa na gari ambalo lipo kwenye mwendo kasi halafu limekosa *break,* linakwenda kuanguka. Sasa napendekeza na ndiyo maoni ya Kamati, hakuna tatizo lolote Serikali ikiiacha Tume ya Mipango ikabaki kama ilivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunawaomba sana muiache hiyo Tume, kwa maana ya sheria, kwa sababu hii sheria tangu imekuwepo Mheshimiwa Mkapa hakuitumia, Mzee Mwinyi hakuitumia lakini Mzee Kikwete alipokuja akaitumia, ndiyo hii mipango mnayoona leo.

Mheshimiwa Spika, hii Mipango ya Maendeleo ya miaka 2025, Mipango ya Maendeleo ya 2063, inatengenezwa na *think tank* ya pamoja. Kitendo cha Serikali kwenda kuua Tume ya Mipango, nafikiri moja ya uamuzi wa ovyo kabisa ni huu hapa wa kufuta hii Tume. Kwa sababu wanasema, tukawauliza maswali, ikitokea sasa ninyi mmeondoka, Rais mwingine amekuja madarakani, atafanyaje kama ndiyo anataka kuitumia Tume ya Mipango. Akasema atatengeneza sheria nyingine.

Mheshimiwa Spika, yaani tunakuja tena kulipa kazi Bunge lijalo litengeneze sheria mpya katika hatua zake zote tatu wakati sheria ipo. Ambacho kilitakiwa kifanyike hapa na Wizara ni kuboresha tu hii sheria ama kuianza kwa sababu hata ikikaa *dormant* mtu yeyote anaruhusiwa kuitumia hii sheria pale anapotaka. Sheria iko wazi tu, haijamlazimisha Mheshimiwa Rais kuitumia kama hahitaji kuitumia. Kwa hiyo, nataka na hilo nilizungumzie na Serikali ielewe kwamba uamuzi huu ni moja ya uamuzi wa ovyo kabisa ambao nafikiri wakiendelea kuufanya utaligharimu Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, nataka kuzungumzia Sheria ya Fedha za Umma, Sura 334. Sheria hii inahusu kuanzishwa kwa Akaunti Jumuishi ya Pamoja, hiyo tunaita *TSA*. Alitangulia Mheshimiwa Zitto akazungumza hapa. Kuanzishwa kwa hii Sheria ama kuanzishwa kwa Akaunti moja Jumuishi siyo kosa katika nchi, lakini utaratibu tunaokwenda kuuanzisha Tanzania, nasema hivi, tunaweka Taifa kwenye *risk* ambayo siku moja Taifa linaweza lika-*paralyse*.

Mheshimiwa Spika, kwa nini nalizungumza hili? Nimepitia nchi ambazo zinatumia mfumo wa *TSA.* Mfumo wa hizo nchi ni kwamba nchi inakuwa na fedha, kwa mfano, kuna fedha ziko Momba, ziko kule Ruangwa na Kongwa. Inapofika mwisho wa siku, taarifa za fedha zinaletwa Benki Kuu, zinakwenda kwenye Akaunti ya Pamoja kwamba leo Momba tumebakiwa na kiwango kadhaa cha fedha. Kwa hiyo, wamekuwa wakiendesha mfumo huo kwamba inapofika jioni nchi inajua ina ukwasi kiasi gani?

Mheshimiwa Spika, sheria yetu inavyokwenda kuonesha na ukiipitia tu vizuri kabisa, ni kwamba fedha zote za nchi hii mpaka zile za kwenye Halmashauri zinakwenda Mfuko Mkuu halafu baada ya hapo zinakwenda katika Mfuko wa Akaunti moja. Yaani hela za nchi nzima zinakwenda kwenye Akaunti moja. Ukipitia kwenye sheria utaona sheria inampa mamlaka Waziri wa Fedha kutunga *regulation* juu ya namna ambavyo *Paymaster General* atautekeleza ule mfuko, matumizi yake yatakuwaje na namna atakavyokuwa ana-*limit*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kinachokwenda kutokea ni nini? Hii Akaunti moja inakwenda kusimamiwa na watu watatu tu katika nchi. Hela zote tunapeleka katika chungu kimoja. Sasa mimi nikawaambia, hivi ikitokea siku moja *system* hiyo ya kifedha, hiyo Akaunti moja *system* yake ikafa, maana yake siku hiyo nchi imepotea.

Mheshimiwa Spika, ikitokea akaja Rais mzalendo, mmemwekea fedha zote peke yake, akiamua kutoroka nchi,

akiondoka na hizo hela zote nchi itakuwa katika usalama gani? Sijui kama wamenielewa! Kwa sababu akaunti hii inaenda kuwa *controlled* na watu tatu. Ninachokueleza, hii ndiyo halisi. Najua unacheka, lakini ndiyo hali halisi. Narudia tena, ikitokea wamekuja Marais...

**SPIKA:** Najaribu ku-*imagine* Mheshimiwa David kwamba kuna Kiongozi atakuja sijui na ndege ya ukubwa gani ya kubeba hizo hela zote kwa pamoja. Endelea Mheshimiwa. *(Kicheko)*

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Spika, ni kwamba hizi hela hazihamishwi kwa kubebwa kwenye ndege ni ku-*transfer ni* ku-*transfer* tu. Watu wana-*transfer* fedha kwenda kwenye akaunti ya nchi nyingine. Watu wanafanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, Nigeria wakati wa mfumo wa Jonathan walipoanzisha huu mfumo; leo Serikali ya Buhari wanakwambia mfumo wa *TSA* kwa sababu haukutengenezwa vizuri, ndiyo ulipelekea fedha zote na ufisadi mkubwa ulifanyika, kwa sababu fedha zote zilipelekwa pamoja. Cha ajabu, sasa hivi kinachokwendwa kwenye hii *TSA* kunakwenda kupitishwa fedha ambazo hazipo kabisa, Bunge hatujapitisha. Ukipitia kwenye sheria, utaona hapa kuna kitu kimeandikwa *unspent*. *(Makofi)*

**SPIKA:** Malizia Mheshimiwa.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Spika, ukipitia hapa kwenye *schedule* ya Waziri utaona ameelezea hapa kwamba moja ya fedha zinazokwenda kwenye hii Akaunti ya *TSA* kuna kitu kimeandikwa *unspent balances* na ukienda mwanzoni kwenye yale mawazo yao ya mwanzo kwenye sheria utaona kuna fedha imeandikwa *non voted fund.* Fedha hizo sisi kama Bunge hatupitishi. Sasa matokeo yake, fedha ambazo hazijapitishwa na Bunge, fedha zilizopitishwa na Bunge, zote zinakwenda katika akaunti moja.

Sasa ukichanganya na Serikali ambayo haina Tume ya Mipango, maana yake kesho tutakapokuwa tunawahoji

wanatekeleza mipango, watakwambia hela tulizozitoa ni zile *unspent balances* ambazo ninyi Bunge hamna mamlaka nazo. Sasa imekiuka Katiba, vifungu tumeviuliza katika Bajeti yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunachokitaka, Serikali ipate muda wa kuipitia ili hili jambo liwe kwa faida ya Taifa na siyo kwa ajili ya kunuifasha watu wachache ambao wanafikiri ni wazalendo kwa wakati wa sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa. Mheshimiwa Ally Saleh nasikia hujajiandaa bado. *(Kicheko)*

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Mheshimiwa Spika, nitachukua hivyo hivyo.

**SPIKA:** Ahsante. Karibu kama uko tayari.

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Juzi nilipokuwa nawasilisha, nilizungumzia juu ya suala la kutokuwepo fungamanishi la kiuchumi baina ya chumi zetu hizi mbili. Pia nikasema chumi hizi mbili hazionekani kusomana kiasi ambacho *it is disadvantage of Zanzibar*, Zanzibar inaathika sana. Nikasema kuna maeneo matatu; maeneo ya kisera, maeneo ya kibajeti na maeneo ya muundo wenyewe wa Serikali ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, sasa hapa leo nitazungumzia jambo moja ambalo linaathiri hayo niliyoyasema kwamba kuna tatizo la kutokusomana chumi zetu kiasi ambacho hatufikiriani kwamba tukifanya hii ni *advantage* ya huyu; huyu anapata na huyu anapata tukatengeneza *win win situation*. Nalo ninalotaka kuzungumzia ni suala ya *VAT* katika umeme.

Mheshimiwa Spika, *VAT* katika umeme imesemwa sana na Wabunge wengi kutoka Zanzibar, kwamba Wazanzibar wanalipa *VAT* mara mbili. Wanalipa wakati wa kununua huku kwa sababu wanauziwa kama watu wa

kawaida, *ZECO,* kisha tukifika kule Zanzibar tunalipa tena *VAT* nyingine asilimia 18. Kwa maana Wazanzibari wanalipia *VAT* ya umeme ya kitu kimoja asilimia 36.

Mheshimiwa Spika, ni Kanuni ya uchumi kwamba *VAT* inalipiwa kule inakotumiwa, sasa kwa nini Zanzibar walipe *VAT* huku kisha waende wakalipe kule asilimia 36? Ndiyo yale, chumi hazisomani. Kwa maana nyingine, upande mmoja wa Muungano unachajiwa *VAT* asilimia 18, basi, kwa maana ya mlaji lakini kule tunalipa mara mbili. Hasara yake nini? Hasara yake, kwanza biashara inakuwa mbovu Zanzibar kwa sababu tunalipa umeme ghali zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, tunakuwa hatuna *competition* na kile ambacho wenzetu wanaweza kufanya. Kwa mfano, kama ilikuwa mtu ana Hoteli, anafanya biashara; labda ana biashara Bara, kwa hivyo gharama ya Hoteli Zanzibar itakuwa kubwa zaidi kwa maana ya kwamba tutakimbiza mtalii ambaye angetaka kuja kulala Zanzibar akaamua kulala Dar es Salaam kwa sababu Dar es Salaam is *cheaper* kulala kuliko Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, pia kama kuna uzalishaji ambao Zanzibar wanataka bidhaa ile wailete huku upande wa pili wa Muungano, kuzalisha inakuwa ghali zaidi Zanzibar kwa sababu unalipa asilimia 36 kulinganisha na huku asilimia 18. Kwa hiyo, kama mtu anazalisha tuseme ana kifungashio fulani anafunga ina maana gharama yake itazidi kwa asilimia 18 kwa sababu ya umeme lakini pia asilimia nyingine ya kusafirisha kutoka Zanzibar kuja huku Bara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la tatu ni kwamba tunayafanya maisha ya Wazanzibari yawe ghali zaidi kwa asilimia 18 ya *VAT* ya nyongeza. Kwa hivyo hii siyo haki, siyo sawasawa na hii inapaswa irekebishwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho, tuna *unfair treatment* katika nchi ambayo ina soko moja, ina chumi moja, ina *tax regime* mmoja, lakini bado tumekuwa tukiliachia hili bila kujali kwa miaka yote. Naambiwa kumekuwa na

mazungumzo kwa zaidi ya miaka minne hivi sasa, watu wanakwenda, wanarudi, lakini Serikali ya Muungano haioni uchungu na inakataa kulimaliza hili na hatujui kwa sababu gani.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, labda kwa lugha ya Kizanzibar tunasema mpaka kuna kedi ndani yake inafanyika kwa Serikali ya Muungano, hawataki kulimaliza tatizo hili. Kwa hiyo, nafikiri kuna haja ya hili suala la *VAT* linawezwa kumalizwa humu ndani kwa kauli ya Mheshimiwa Waziri. Halitaki kungojea wala halina ulazima wa kungojea, kwa sababu hatua nyingi zilishapitiwa na inaonekana kwamba kuna makubaliano kwamba Zanzibar katika hili hawatendewi haki. Kwa hiyo, nafikiri kuna haja.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, sasa hivi kwa sababu ya hilo, Zanzibar imekusanya deni kubwa *TANESCO* ambalo halina umuhimu wowote kuwepo. Hili likirekebishwa Zanzibar inaweza ikapata afuweni. Kwa hiyo, hili tunaweza kulimaliza humu ndani kwa kauli ya Mheshimiwa Waziri na tukasonga mbele.

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho ninalotaka kulizungumzia ni suala *Export Levy* ya korosho. Kumetolewa *compromise* leo hapa leo; imetolewa *compromise* ya Mheshimiwa Katani ya 50:50 kwa maana ya 50 katika zile inazoenda Serikalini, 50 iende kwa Bodi; pili, ilitolewa *option* na Mheshimiwa Zitto, kaigeuza kinyume nyume asilimia 35 ibakie kwenye Bodi na asilimia 65 iende Serikalini. *Options* hizi napenda Mheshimiwa Waziri mojawapo tuitumie. Kwa sababu kama ambavyo imeletwa hapa inaweza ikaleta matatizo, tunaweza tukapata watu wakakataa kulima korosho au kukatokea chochote kile katika korosho.

Mheshimiwa Spika, tukilazimisha hii, pengine korosho inaweza kuwa na hasara. Kwa hiyo, nafikiri twende katika *compromise* mojawapo, hata Mheshimiwa Waziri atakuwa na nyingine. Kuendelea tu kukataa, kusema kwamba yote iende huku na zile hoja zote zilizoletwa hapa kwamba hii korosho inakwenda mikoa 17; kwa hiyo, anayesema

kwamba hii korosho ni kwa ajili ya watu wa Kusini au *levy* ni kwa ajili ya watu wa Kusini siyo kweli. Inakwenda kwenye mikoa 17 na pengine itakwenda zaidi, tafiti zitaonesha kwamba Korosho inaweza kulimwa sehemu nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, sisi ni Watanzania ni Bunge la wananchi, tuna uwezo wa kufanya maamuzi na maamuzi haya ni kutafuta *compromise.* Tukishindana, hatuna faida nalo. Tumeona Pemba watu watu walikataliwa mikarafuu, watu waliingia katika magendo ya karafuu. Hatuna haja ya kwenda huko. Kama Taifa napenda uliongoze Bunge hili tutafute *compromise*, tusitafute kitu ambacho hakina ulazima wa kwenda huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Ally Saleh kwa kutumia muda vizuri. Mheshimiwa Omary Mgumba, nilishakutaja tangu mwanzo, atafuatia Mheshimiwa Pauline Gekul.

**MHE. OMARY T. MGUMBA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami nitoe mchango wangu kwenye mjadala uliokuwa mbele yetu. Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema na mwingi wa ukarimu, aliyetuwezesha kufika jioni hii ya leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nami naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Sababu ya kuunga mkono ni kwa sababu Serikali ina lengo kubwa la kutaka kujenga uchumi wa Kitaifa ambapo haikuanza kuleta makusanyo yote ya fedha ya Serikali katika Mfuko Mkuu. Tuliona kwenye *Finance Bill* ya mwaka 2016 Serikali ilihamisha fedha za taasisi zake kama *EWURA* na *TCCRA* ambao walikuwa wanatakiwa kuchangia tu *15%* kwenye Mfuko Mkuu, lakini 85% ilikuwa inabaki kwenye mifuko hii, lakini zote zilienda Mfuko Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, tuliona mwaka 2017 katika *Finance Bill,* pia tulihamisha fedha za bandari, zote asilimia 100 zilikuwa zinatumika huko. Nao walikuwa wanachangia *15%* tu, lakini zote zilihamishwa. Kwa hiyo, wanapokuja mwaka huu kuhamisha fedha hizi kwenda Mfuko Mkuu naamini wana lengo lile lile la kuweka uchumi wa Kitaifa, mapato ya Kitaifa ili yaweze kutumika sehemu zote kutokana na mahitaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nayasema haya kwa sababu mazao ya kimkakati yako matano ambayo ni korosho, tumbaku, kahawa, mkonge na chai. Kwa hiyo, kwa kuweka katika Mfuko Mkuu na hela hizi zikarudi katika mikoa inayozalisha mazao haya kwa mujibu wa bajeti ambayo tutapitisha sisi Bungeni, maana yake zile hela zitawafikia wakulima kutokana na mahitaji yao kwa sababu wawakilishi wao tupo Bungeni, tutakuwa tumelifanya hilo.

Mheshimiwa Spika, pia zile hela tutakuwa na uhakika sisi Wawakilishi wa wananchi ambao ndio wenye jukumu la Kikatiba kuisimamia Serikali. Tunawezesha *CAG* kwenda kukagua chombo ambacho kitakuwa *CBT,* kwa hiyo, sisi tutakuwa na nafasi ya kuisimamia Serikali badala ya sasa hela hizi kutumika au kusimamiwa na chombo binafsi ambacho hakimpi fursa *CAG* kwenda kukagua. Maana yake hata sisi Bunge hatuna uwezo wa kuisimamia Serikali katika upande huo. *(Makofi)*

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**MHE. OMARY T. MGUMBA:** Mheshimiwa Spika, naomba niendelee na kutoa mchango wangu.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa Taarifa.

**MHE. OMARY T. MGUMBA:** Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo na kuunga mkono hoja, nianze na mapendekezo yangu machache niliyokuwa nayo kaama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, la kwanza; mazao ya kimkakati yaliwekwa wakati huo mwaka 1984 ni ili yatuletee fedha za kigeni na kutoa ajira kwa wananchi wetu. Sasa hivi kuna mazao mengine yameonekana yana umuhimu mkubwa sana na masoko yake yako ndani ya nchi na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, napendekeza kwa Serikali, katika hayo mazao matano ya kimkakati ni vizuri tungeongeza mazao mengine matatu. La kwanza, tungeongeza miwa kwa sababu ina mahitaji makubwa ndani ya nchi na nje ya nchi, kwa sababu, tunatumia kiasi kikubwa sana cha pesa za kigeni kuagiza sukari nje ya nchi. Ni vizuri ikaingia miwa ikiwepo miongoni mwa mazao ya kimkakati ili tuweze kuongeza uzalishaji wa miwa na kuzalisha sukari nyingi hapa nchini ili tuweze kutoa ajira pamoja na kuokoa fedha za kigeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zao la pili; tungeongeza ngano kwa sababu, tunatumia kiasi kikubwa sana cha pesa kuagiza ngano na viwanda vyetu vyote vya ngano; aidha, Bakhresa, Monaban, Azania na vingine vingi vinaagiza ngano kutoka nje wakati tuna uwezo wa ardhi kubwa ya kuzalisha mazao yao hapa na kutoa ajira na kutengeneza soko la ndani. Nayasema haya kwa sababu biashara yoyote ukifanya kwanza angalia soko linalokuzunguka.

Mheshimiwa Spika, nayasema haya kwa sababu, kwanza tuna soko la ndani, lakini pia tuna soko la nchi za Afrika Mashariki na Kati, tukiyaingiza hayo badala ya kugombaniana kuzalisha mazao kama mbaazi tunategemea soko la nje ambapo mlaji naye akizalisha, hatuna soko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zao la tatu; tungeongeza katika mkakati mbegu za mafuta kwa maana ya alizeti, ufuta na mazao mengine. Nayasema haya kwa sababu tuna viwanda vikubwa vya kusindika mafuta hapa nchini, kwa mfano, *Mount Meru,* Abood pale *MOPROCO* Morogoro. Kiwanda cha Abood kina uwezo wa kusindika mbegu za mafuta zaidi ya tani 70,000 kwa mwaka, lakini cha kusikitisha mwaka

mzima ndugu yangu Abood anapata tani 5,000 tu. Unaona namna gani tukiweza kuzalisha mbegu za mafuta na kwa kuwa viwanda tunavyo tutaweza kutengeneza ajira, lakini pia tutaweza kuokoa fedha nyingi za kigeni tunazopoteza kuagiza mafuta ya kula kutoka nje ambayo siyo safi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile hata ndugu zangu wa Kigoma maweze yale tukiyawekea mkakati mzuri, yataongezeka na tutazalisha hapa, tutatengeneza ajira nzuri na uchumi mzuri kwa watu wetu. Pia nitolee mfano Kiwanda cha *Mount Meru,* viwanda vyake vyote vina uwezo wa kusindika mbegu za mafuta zaidi ya tani 400,000, lakini kwa mwaka vinapata tani 40,000 tu. Maana yake ni 10% ya mahitaji yake. Unaona ni namna gani tuna fursa kama nchi au Taifa ya kuweza kuongeza uzalishaji zaidi kutengeneza ajira na kuweza kuokoa fedha za kigeni tunazotumia nje.

Mheshimiwa Spika, nayasema haya kwa sababu ya mazingira tuliyokuwanayo ambapo Soko la Kimataifa, Soko la Dunia, lina ushindani mkubwa sana. Sasa ni vizuri *focus* kubwa tukaangalia kwenye mazao ambayo bidhaa zake zina mahitaji makubwa ya ndani na nchi zinazotuzunguka kuliko kuendelea kuhangaika na mazao ambayo tunategemea soko la nje ambayo wauzaji siyo sisi peke yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho, katika mchango wangu wa leo ni kwa ajili ya Serikali ilipovunja Mfuko wa Korosho mwaka 2017. Mfuko ule ulikuwa na *balance* ya shilingi bilioni 51 na hela zile zilihamishwa kwenye *CBT,* Mamlaka ya Korosho. Kwa hiyo, ni vizuri Serikali ikajiridhisha, ikafanya ukaguzi maalum pale *CBT* ili kugundua hela hizi ambazo zilikuwa ni mapato ya Korosho ya *Export Levy* kwamba zilitumikaje kwa maana ya *sulphur* tu na mbegu za mwaka 2017 walizotoa bure kule Kusini kwa ndugu zetu? Siamini kama shilingi bilioni 51 zinaweza kuishia kwa ajili ya magunia tu, *sulphur,* pamoja na miche ya mbegu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho kabisa, Serikali imekuja na sheria, nami naipongeza hii *Finance Bill,* lakini sheria inaanza hapa kwenda mbele. Baada ya kumaliza mchakato wao, kuchakata, kuhakiki madeni yote yanayodaiwa na Mfuko wa Korosho, ni vizuri sana tukaanza kuyalipa madeni yale hela zikarudi kule Kusini, wote wanaodaiwa walipwe ili tuondoke na mkwamo huu tuanze sheria hii kuitekeleza kuanzia leo kwenda mbele badala ya kutumia zile fedha zilizokusanywa nyuma.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja kwa asilimia moja. Ahsante sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Kicheko/Makofi)*

**SPIKA:** Alichosikia Spika ni asilimia mia moja. Mheshimiwa Pauline Gekul, utafuatiwa na Mheshimiwa Adadi Rajab. *(Makofi)*

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nami niweke mawazo yangu katika sheria hii, *Finance Bill* ya mwaka huu ambayo inakwenda kukusanya kodi katika vyanzo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kwanza naipongeza Kamati ya Bajeti kutoka moyoni. Wamefanya kazi kubwa sana ya kizalendo usiku na mchana bila kuchoka. Kwa mara ya kwanza nimeona Kamati hii haikuleta tu taarifa yake, lakini imeleta na *schedules* za *amendments.* Yale waliyokuwa wanayaongea wameyaleta...

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa mara nyingine nawaombeni tusikilizane. Baada ya muda siyo mrefu sana tutaingia kwenye vifungu, wengine mtakuwa hamwelewi hata tunajadili kitu gani na kitu gani kipo wapi. Kwa sababu, kwa kweli, yaani kuna watu wanakuja hapa wala hawako Bungeni, wana yao tu. Tusikilizane. Mheshimiwa Gekul, endelea.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Spika, nilikuwa namalizia kuipongeza tu hii Kamati. Niseme kazi waliyoifanya ilikuwa ni kazi ya kizalendo kwa sababu, pamoja na tofauti zao na Serikali, wakabaki na msimamo kwamba hayo kwa maslahi ya wananchi tunatamani yawe hivi. Nawapongeza kutoka moyoni. Nami nafikiri pia Mungu tu anaweza akawalipa kwa haya waliyoyafanya.

Mheshimiwa Spika, naomba nami nitoe mapendekezo kadhaa katika hii *Finance Bill.* Katika *Amendment of Land Act, Cap 113, Section* 33, hii kuondoa au kusamehe kodi ya pango la ardhi, naomba nitoe mawazo yangu. Serikali imefanya jambo jema kusamehe Taasisi za Serikali, za Dini na nyingine, lakini imesahau *private schools.* Siyo shule zote ambazo zinatoa huduma na zahanati zote ambazo zinatoa huduma zinakuwa chini ya taasisi fulani fulani za kidini au *organisation* fulani fulani.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba kwa sababu muda mrefu wenzetu wenye shule binafsi wamekuwa wakilalamika kuhusu tozo nyingi na wanatusaidia kutoa elimu kwa watoto wetu, wawakumbuke pia hii tozo iondoke, kwa sababu hii tozo mwisho wa siku anayelipa ni yule mzazi ambaye amepeleka mtoto pale.

Mheshimiwa Spika, kama lengo ni jema, wanatoa elimu, wanatoa huduma za afya kwa watu wetu, tuwasamehe na hii kodi ambayo tumekuwa tukitoza taasisi nyingine ili angalau pawepo na *equal ground* ya hawa watu kutoa huduma. Kwa hiyo, vile ambavyo mmefungua huu mlango wa kusaidia taasisi mpaka za dini na taasisi nyingine na hawa watu wenye *private schools,* wenye *private dispensaries,* waweze kusamehewa na hii kodi isaidie. Hilo ni pendekezo Mheshimiwa Waziri natamani wakati wa kujibu atuletee majibu ambayo yanaeleweka.

Mheshimiwa Spika, kwenye *Local Government Finance Act, Cap 290, Section* 37A, kuhusu Mfuko wa Vijana na Akinamama, mimi bado niishauri tu Serikali kwamba tuna

sababu ya kuongeza. Pamoja na nia njema waliyofanya ya kuongeza walemavu, hebu wafikirie kuhusu wazee. Tuongeze kipengele kingine cha wazee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wazee wa nchi hii wameomba muda mrefu sana *pension,* waliahidiwa katika Serikali iliyopita lakini hawakusikilizwa. Hebu wafanye wao sasa, kwamba, kwenye zile asilimia tuweke ya wanawake, vijana, walemavu na wazee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nafikiri wakati Mheshimiwa Waziri anatunga kanuni au wakati Waziri wa TAMISEMI anatunga hizi kanuni sasa tu-*specify* kwamba hawa wazee kuanzia labda miaka 60 mpaka 80 wana uwezo wa kufanya kazi. Hao wazee ninaowazungumzia ni wa jinsia ya kiume sasa, jinsi ya ‘me’, kwa sababu wazee wa jinsi ya ‘ke’ wao wanaingia kwa akina mama na wanapata hii fursa ya mikopo.

Mheshimiwa Spika, wale wazee, baba zetu na babu zetu ambao na wao wanahitaji wapate mtaji huu lakini hawapati. Tuwa-*accommodate* maana ndiyo tunatunga sheria. Isipokuwa wakati wa kutunga kanuni, tuki-*limit age* kwamba mpaka miaka 80, basi tu-*limit* ili tuweke kundi ambalo wanaweza wakafanya kazi, ni vizuri iwekwe kwenye kanuni. Ila kwa sasa tuwa-*include* wazee wa nchi hii, wamelia kwa muda mrefu sana na naamini hili Mheshimiwa Waziri atalifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nilipenda kuchangia ni suala la Tume ya Mipango. Kiukweli nchi hii bado Tume hii tunaihitaji. Kwa sababu, haiwezekani tu kila kitu kikawa chini ya Wizara hii. Leo tunavyoongea kuna Msajili wa haya mashirika yako chini yake, lakini huyu Msajili wa Hazina mpaka leo unaona hata bajeti yake juzi alipewa asilimia 17 tu na tuna mashirika zaidi ya 280. Kwa hiyo, kwa hali ya kawaida kuendelea kuiongezea mzigo inakuwa haifai. Hii Tume iendelee, ijitegemee, ipange mipango. Japo nchi hii hawafuati mipango na hapa wasitake kutudhihirishia kwamba sasa hii nchi wanaiendesha kwa

asubuhi mtu ameamkaje, basi ndiyo hicho wanakuja wanaleta kwenye bajeti. Wawe *honesty,* hii Tume ibaki vile ambavyo Kamati imeshauri na naipongeza Kamati kwa msimamo wao huo.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni kuhusu *Public Finance Accounts,* lakini suala la *TSA.* Mimi niseme hiki kitu bado hakijaiva. Ni vizuri wakakaa chini jinsi ambavyo wametofautiana mara nyingi sana kwamba kutakuwa na *Sub-TSA,* lakini wakati huo kutakuwa na *voted* na *non-voted sources* hizo, lakini wakati huo huo hii *non-voted* wamekuwa wakishindwa kutafsiri kwamba fedha zikishapita muda zirudi huko kwenye *TSA Account* halafu Katibu Mkuu sasa aweze kutoa *go ahead* tena.

Mheshimiwa Spika, kama Waheshimiwa Wabunge tunashauriwa na Kamati, Kamati hii imesema jambo hili lisubiri mpaka Septemba. Nashauri kwamba hatuna sababu ya ku-*rush* kwa sababu hiki kitu hakijafanyiwa kazi vizuri. Kifanyiwe kazi vizuri na tusi-*rush* hilo la Septemba, waende wakakae chini, watafute hizo *sources* ambazo zitakuwa zinaingia huko. Wanaona Kamati ilivyofanya kazi kubwa mpaka tukatoa *own sources* za Halmashauri zetu, walikuwa wameshaweka mpaka *own sources, you can imagine that fight,* mpaka *own sources* zikatolewa, sasa tumeingia kwenye *contradiction* ya *voted* na *non-voted.* wakae chini wa-*settle. Where are we rushing?* Kwa sababu, mwisho wa siku lazima tufanye *thorough analysis* ya maamuzi ambayo tunafanya kama Wabunge. Kwa hiyo, nashauri lisubiri na wala siyo hiyo Septemba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nataka kushauri, katika *Tax Administration Act, Cap* 438, *Section* 79(c), naomba kwa hili pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwamba amesamehe hizi *interest* ambazo wafanyabiashara walikuwa wameshindwa kulipa. Nimshauri, kwenye hiyo *Section (c)* kwamba anapoenda kutunga sasa zile kanuni, *eligibility* na *duration* ya ule msamaha namwomba wale wenye *principle* wasibanwe kutakiwa walipe leo ndiyo wasamehewe *interest.* Wapewe muda angalau wafanye *installment within those*

*six months* ambazo Mheshimiwa Waziri amezisema ili wafanyabiashara wetu wengi waweze ku-*qualify* kusamehewa hizi *interests.*

Mheshimiwa Spika, kwenye kanuni ukienda akaandika anavyotaka wewe, maana yake hawa wafanyabiashara unaweza ukamwambia lipa ndani ya mwezi huu *principle then* usamehewe *interest.* Mimi naomba tu, hii nia njema ambayo Mheshimiwa Waziri ameionesha katika kuwasamehe aende sasa kwenye kanuni ambayo ame-*provide* katika ile *Section 79(c)* kwamba, kanuni itatungwa, lakini itaonesha *eligibility* na *duration,* azingatie suala la *payment* au *installments* za *principles* ili wafanyabiashara wetu walipe wakiwa wame-*relax* badala ya kuwa na *stress. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashauri katika suala zima la *Local Government Finance Act, Section* 33 na 34. Hili najua limebaki kwenye Halmashauri zetu, hizi *sources* mpya ambazo Mheshimiwa Waziri amezi-*introduce* baada ya ule Mfuko wa Pamoja kukwama kwamba *own sources* zetu hazitaingia kule, maana hivi vyanzo tutakusanya. Wamependekeza...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Pauline Gekul. Nilishakutaja Mheshimiwa Adadi Rajabu, atafuatia Mheshimiwa Jitu Soni.

**MHE. BAL. ADADI M. RAJABU:** Mheshimiwa Spika, nami nashukuru sana kwa kupata nafasi hii ya kuchangia hii *Finance Bill* ambayo ni sheria muhimu sana. Kwanza napenda kumpongeza sana Waziri wa Fedha pamoja na wasaidizi wake wote. Waziri wa Fedha amefanya kazi kubwa sana kwa sababu, mapendekezo ambayo yamekuja kwenye Muswada huu na vifungu ambavyo vimekuja kwenye Muswada huu kwenye Kamati ya Bajeti ni vingi, lakini Waziri wa Fedha amekuwa *very flexible.*

Mheshimiwa Spika, hoja nyingi ambazo Kamati imeweka, zimekubalika. Hoja nyingi amekubali kuzirekebisha na ndiyo maana amekuja na hii *schedule of amendment* ambayo iko hapa. Ni hoja chache ambazo Kamati imemshauri kama mlivyoona kwenye ripoti ili Wizara ikae ijaribu kuzirekebisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza nitaanza na *Treasury Single Account, Cap 34(a).* Mwanzoni nilipata bahati ya kuchangia Wizara ya Fedha na nilifikiri kwamba mfumo huu unakusanya fedha zote unapeleka kule Hazina au Benki Kuu ndiyo wanaanza kugawa. Baada ya kukaa kwenye Kamati na kwa muda mrefu sana na ku-*present* hoja mbalimbali, Waziri huyu wa Fedha amekubali kubadilisha mambo chungu nzima. Tulifikiri kwamba hela zote mpaka kwenye Halmashauri zetu zinakwenda na zote zinachukuliwa na huu Mfumo wa *Treasury Single Account* na kweli aliweka kwenye sheria, lakini amebadilisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiangalia Kifungu cha 11*B(1)(c),* Waziri wa Fedha ame-*delete,* ameondoa kile kifungu ambacho kilikuwa kinachukua mapato yote ya Halmashauri, *own source* na kupeleka kwenye Mfuko wa *TSA.* Sasa hilo ningependa kumshukuru sana na mambo mengi ambayo ameyafanya pale. Nilifikiri pia hii Mifuko ya *Special Accounts* inakwenda kwenye *TSA,* lakini mifuko hiyo ni mifuko ambayo iko *ring fenced;* Mifuko ya Maji, Barabara, Reli na mifuko yote ambayo ni *special* ambayo imeelezewa kwenye Katiba *135, Subsection (2),* yote iko vilevile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa hili nashauri Waheshimiwa Wabunge kwamba mfumo huu una matatizo madogo madogo ambayo yameonekana na tulikubaliana kwamba mfumo huu basi uanze tarehe 30 Septemba, 2018 ili kipindi hiki cha miezi mitatu, Mheshimiwa Waziri aweze kurekebisha mambo ambayo yapo. Kwa hiyo, mfumo huu kama ambavyo upo, mwanzoni pia tulifikiri kwamba unavunja Katiba, lakini hakuna kitu kama hicho. Mfumo huu hauvunji Katiba na uko sawasawa kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, ni suala la ku-*repeal Plan Commission.* Suala hili tunaelewa kabisa sababu za *Planning Commission* ni *think tank,* lakini Serikali imeamua kufuta. Wameleta Muswada wa kufuta hii Cap. 314, kuondoa kabisa.

Mheshimiwa Spika, Kamati baada ya majadiliano marefu imeona kwamba kwa kweli kama Serikali inataka kuendelea kufuta kama ambavyo imewasilisha, basi wasifute sheria, ibaki jinsi ilivyo. Kama ni kufuta basi waangalie *administratively* wahamishe watu, wahamishe Ofisi, lakini sheria isifutwe ibaki vile vile, kwa sababu kesho na keshokutwa tutakuja kuiona umuhimu wake hii sheria.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, bado tunasisitiza kwamba sheria hii isifutwe kwa sababu kwanza imeletwa katika *Finance Act,* siyo kwa utaratibu. Hii ilitakiwa ije kwenye *miscellaneous* kwa sababu haihusiani kabisa na mambo ya fedha na *Finance Bill*. Nashauri kwamba sheria hii isiwe *repealed,* naunga mkono mawazo ya Kamati na mambo mengine ya utawala kama Serikali inataka kuendelea, basi iendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu ambalo nataka kushauri ni suala la ukusanyaji wa kodi za majengo. Suala hili pia Kamati imeliangalia sana na imeona ile *Part XI* ambayo iko kwenye sheria ambayo imeletwa, baada ya mawasiliano marefu, Waziri amekubali kuondoa vipengele vyote vya *Part XI* na kuacha suala la ukusanyaji wa kodi ya majengo libaki vile vile kwa Halmashauri. Kwa hiyo, kutuondolea kifungu cha 38 – 47, yote yamekuwa *deleted* na iko kwenye *amendment* yake ambayo amei-*present* hapa. Kwa hiyo, suala hili limekuwa *handled* vizuri.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nataka kushauri ni suala la *Road and Fuel Toll, Cap. 220.* Kamati imependekeza sana kwamba ongezeko la Sh.50/= kwenye mafuta ya petroli ili iweze kuongeza Mfuko wa Maji, suala hili tumelizungumza kipindi kilichopita lakini halikuweza kupita.

Mheshimiwa Spika, safari hii tunasisitiza kabisa ni muhimu suala hili la hizi Sh.50/= kwamba zitoke kwenye mafuta zikatunishe Mfuko wetu wa Maji, tulipitishe kwa sababu ni suala muhimu ambalo tunaliona kwamba linaweza likasaidia tatizo la maji. Serikali ya Awamu ya Tano imefanya mambo mengi sana, lakini kwenye Sekta ya Maji bado kunasuasua. Kwa hiyo, tunaona kwamba labda hizi hela zikiongezeka pale zinaweza kusaidia kwa njia moja au nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la *gaming,* tumekwenda na mahojiano mbalimbali na Mheshimiwa Waziri na hiyo ukiangalia kwenye *Cap. 41* na kwenye *proposal* za *amendments,* Mheshimiwa Waziri amekwenda mpaka kupunguza asilimia 25 kwenye hii Michezo ya Bahati Nasibu, lakini Kamati inazidi kusisitiza baada ya kuongea na wadau tumeona kwamba ni vizuri basi Waziri aka-*consider* tumeleta mapendekezo iwe kwenye asilimia 20 isipokuwa kwenye mambo ya *Casino,* basi iendelee kwenye asilimia 15 badala ya kwenda kwenye asilimia 18.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunashukuru sana kama marekebisho hayo yataweza kuchukuliwa na tunamshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kufanya *consideration* kwa mapato yote kwenda kwenye *GGR.* *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna suala la mgao wa zile fedha kwenye Halmashauri. Baada ya ushauri mkubwa, Mheshimiwa Waziri amekubali mawazo ya Kamati na nimeona *schedule of amendment*s nyingi za Waheshimiwa Wabunge hapa, badala ya kwenda kwenye *fifty fifty* kwa vijana na wanawake, basi ameleta *schedule of amendiment* ambayo itakuwa kwenye 40 vijana, 40 wanawake na 20 kwa walemavu. Kwa hiyo, hayo ni mambo mazuri ambayo ameyafanya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, nashauri kwamba ziko *amendments* chache ambazo

zimeletwa ambazo Kamati imeleta. Kwa hiyo, tumeshukuru sana kama Wizara ingeweza ku-*consider* na ku-*come up* na hiyo *solution*.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Adadi Rajab. Ahsante sana. Mheshimiwa Jitu soni, atafuata Waziri wa Kilimo, dakika kumi.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba nitumie fursa hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu na pia nashukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia siku ya leo.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii kuishukuru Wizara ya Fedha na wataalam wake wote ikiongozwa na Mheshimiwa Dkt. Mpango kwa kazi ambayo wanafanya, lakini muhimu kuliko yote ni namna tunavyoshirikiana kuhakikisha kwamba tunaelewana ili mambo mengi yaende. Siku zote kwenye mambo ambayo ni magumu, lazima pawe na mvutano, lakini kwa mambo mengi tumeweza kukubaliana. Tunamshukuru kwa hilo Mheshimiwa Dkt. Mpango pamoja na timu yake mzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nishauri jambo moja na ikiwezekana tukija kwenye Bunge lijalo tubadilishe *timing* zetu kwa sababu muda huu ambao tunasoma bajeti na Wajumbe wanachangia, halafu mara baada ya hapo inakuja *Finance Bill,* muda unakuwa ni mdogo sana kuweza kukaa na kuleta mabadiliko ya uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mbali na hiyo, napenda pia kushauri kwamba badala ya sisi kusubiri kufanya mabadiliko na kukutana na wadau hiki kipindi cha mwezi mmoja kabla ya kufikia kwenye bajeti, *process* hii tungeanza mara baada ya mwaka mpya wa fedha kuanza, Bunge kwa mfano hili la mwezi wa Nane tungeanzia hapo kukaa na wadau ili yale

mabadiliko ambayo tunataka kuyafanya tuweza kuyaangalia vizuri, kushauri vizuri, tukae na Serikali, tukae na wadau ili tunapofikia huko, maamuzi yote yawe tumeshamaliza. Hiyo ndiyo itakuwa njia pekee, kwa sababu kuna mengi ambayo tumependekeza.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano nikiangalia kwenye hii Sekta ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, kuna mengi nimependekeza leo ni mwaka wa saba, unakuta kila mwaka unaambiwa basi tutaangalia mwaka ujao. Haya yote yasingetokea kama ingekuwa tunakaa mapema na kujadiliana.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nilikuwa naomba tuangalie ni jambo muhimu sana. Wizara ya Fedha na Serikali kwa ujumla iwe na timu maalum, iangalie nini kinafanyika kwenye nchi zinazotuzunguka ili kabla ya kwenda kwenye Kikao cha Afrika Mashariki, yale yote ambayo yanahusiana na *East African Customs Union* ambapo Bunge hili hatuna uwezo, wala kubadilisha chochote, tutaongea hapa yanapelekwa mwakani ili maoni mengi yawe yanachukuliwa mapema na wakifika huko wajue nini kinaendelea kwenye nchi zinazotuzunguka ili nasi tuje na mabadiliko kwa sera yetu ya kodi na tozo mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia wamekuja na *blue print.* Nashukuru kwamba wameiandaa, lakini hii *blue print* imesubiriwa kwa muda mrefu na kwa sasa hivi hakuna mabadiliko yoyote yaliyokuja kwenye huu Muswada wa Sheria. Kwa hiyo, bado kwa mwaka nzima ujao hatutaona mabadiliko yoyote kwenye sekta hii ya viwanda wala kilimo wala nini kwa sababu mengi kuhusu kero ambazo zinafanya sekta zetu zote zisiendelee ikiwemo viwanda yapo kwenye ile *blue print. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mbali na hilo, kuna suala la *double taxation* ambayo pia ilibidi tukae mapema tuangalie nini kifanyike ili kuondoa huu utitiri wa kodi, tozo na ada? Pia mahali ambapo mtu analipa mara mbili au mara tatu;

kwa mfano, mtu anayelipa ushuru wa mazao, yakisindikwa analipa 0.3% *Service Levy,* lakini yale mazao ambayo ni *by product* kwa mfano mashudu yanaendelea kutozwa ushuru wa mazao ambapo mashudu siyo mazao, ni *by product* ya huko viwandani.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo ni muhimu, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kuleta katika Muswada huu mabadiliko ya sheria ambayo itamruhusu Waziri kusamehe kodi ya mapato na kodi ya ongezeko la thamani (*VAT)* kwenye masuala mbalimbali ya Kiserikali.

Mheshimiwa Spika, Kamati imekuja na pendekezo, tunashauri kwamba pia Serikali iangalie katika eneo la *VAT* kwamba maeneo ambayo yana miradi ya kijamii hasa katika Halmashauri zetu na miradi mbalimbali ambapo tunapata ufadhili, Serikali iweze kusamehe hizo kodi ili tuweze kutekeleza miradi. Vile vile marafiki ambao wanataka kutuchangia wawe huru kutuchangia na tusitozwe kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia maeneo mengi kwa mfano vituo vya utafiti ambavyo ni vya Kiserikali pia vinatozwa kodi. Halmashauri zetu pia zinatozwa kodi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri angetanua wigo huo, nina uhakika kwamba hapo tungeweza kwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia tungeangalia kwa mfano, kwenye mitambo ya kuchimba maji, kutengeneza mabwawa na kadhalika, tungeondoa kodi ili iwe mingi nchini tuondokane na hii kero ya maji kabisa na hasa katika hii Sekta ya Kilimo katika umwagiliaji na uvunaji wa maji tuweze kwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye Sekta ya Madini, pia tunaishukuru Serikali imepiga marufuku kupeleka nje madini yetu. Tukija kwenye Sekta ya Vito, kama hatuna mashine za kutosha hapa nchini za kuchonga na kusanifu, wangeweka *incentives* kwamba waondoe kodi kwenye zile mashine za

kuchonga ili zije kwa wingi nchini kwa bei nafuu zaidi, kwa sababu kama kodi ya asilimia 18 wakiondoa, tayari kutakuwa na mabadiliko karibu asilimia 30 kwenye bei ili watu wengi waweze kutumia.

Mheshimiwa Spika, mbali na hiyo, Serikali bado haijawa na mkakati wa kusaidia viwanda vya ndani. Bado kabisa. Tunashukuru, kwa mfano, kwenye taulo za akina mama wamefuta kodi, lakini hii itakuja kusaidia zile zinazotoka nje ya nchi. Hawa wa ndani ya nchi hawataweza kudai *import tax* na bei kwa viwanda vya ndani itakuwa hatujavisaidia.

Mheshimiwa Spika, mbali na hiyo, hata kwenye viwanda vingine kwa mfano chakula cha mifugo, nashukuru kwamba tumeweza kuongeza bidhaa nyingine kwa mfano mashudu, lakini bado tungefikia mwisho kwamba zile zote ambazo zinazalisha chakula cha mifugo na masuala yale yote yangefutiwa kodi ili tuweze kuhakikisha kwamba viwanda vya ndani vinalindwa.

Mheshimiwa Spika, leo tuna viwanda vingi vinashindwa kushindana na viwanda ambavyo viko kwenye nchi za Afrika Mashariki. Bidhaa zetu ukipeleka nje, yaani uki-*export* hakuna kodi. Kwa hiyo, ukirudisha ndani inakuwa haina kodi nchi za jirani. Kwa hiyo, sisi tutakuwa tunaendelea kubaki kuwa soko badala ya kuwa wazalishaji na kuwa tunatuma huko nje.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine muhimu ni kwamba Serikali na Waheshimiwa Wabunge tungekaa na wataalam kuangalia zaidi kwenye Sekta ya Kilimo, Mifugo, Uvuvi na Utalii tuone kikwazo ni nini kwenye sekta hizo? Ili tuweze kuwekeza zaidi humo kwa asilimia 80 ya wananchi ambao wako huko. Tukiwawezesha kiuchumi tukajua vikwazo ni nini na kuwasaidia katika usindikaji wa mazao yote hayo, nina uhakikika, wananchi wakiwa na uchumi mzuri na *spending power,* Serikali pia itakuwa inakusanya kodi nyingi zaidi na tayari mapato yetu yataendelea kuongezeka.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tusiangalie kwenye sekta ya kikodi tu. Serikali ingewekeza kwenye maeneo pia ambapo moja kwa moja hawatapata kodi au mapato, lakini watakuwa wamekuza uchumi na kutokana na *indirect tax* yaani kodi ambazo hawakusanyi moja kwa moja, watapata mapato mengi.

Mheshimiwa Spika, niendelee kuomba jambo la mwisho. Binafsi nilikuwa bado naona katika Serikali hakuna *coordination,* yaani Wizara moja na nyingine bado haziongei vizuri. Idara na Idara haziongei vizuri. Leo tunapata matatizo kwa sababu kila mmoja anakurupuka.

Mheshimiwa Spika, niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge kwamba ni vizuri na Bunge sasa likakaa imara kwa sababu hii mamlaka tunavyoiachia Serikali kwamba kila Waziri akitaka kwenye kanuni akabadilishe ada, tozo na mambo mbalimbali, tuibane hiyo. Tunatakiwa turudishe kwetu, Bunge ndiyo liwe linapanga. Kwa sababu baada ya hapo tunakuta tuwe na *guided frame lines* kwamba kwenye kanuni awe na uwezo wa kubadilisha mambo fulani fulani tu, siyo kila siku akiamua anapandisha tozo na ada. Hii *blue print* itakuwa haina maana kama hatutaweza kuibana Serikali na kuhakikisha kwamba mambo yote yanaenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo ambalo ni muhimu sana, Serikali iunde timu ya kudumu ambayo itashirikiana na Bunge lako kwamba kila wakati tuwe tunapata mawasiliano kutoka kwa wadau, lakini tukae na Serikali tupate mifano halisi na hai ili kuangalia sekta zote, kwa sababu leo ukisema kwenye sekta fulani tuwaondolee msaada wa kitu kimoja tu inakuwa hujaisaidia hiyo sekta.

Mheshimiwa Spika, inatakiwa tuje na mabadiliko makubwa *(total reform)* kwenye Sera ya Kodi lakini pia mambo mbalimbali ambayo yanatozwa na *Regulatory Boards* na kadhalika. Tukifanya hivyo, tutaona uchumi wa Tanzania unakua na Sekta zote za Kilimo, Mifugo na Utalii zitaweza kukua vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bado naendelea kushauri kwamba yale ambayo Kamati imekuja nayo kwenye *schedule of amendments,* Serikali ifikirie kwa sababu tumeyachambua kwa muda mrefu na mengi ya hayo mawazo yanatokana na miaka miwili, mitatu, minne ambayo Serikali ilishaahidi kuyafanyia kazi na bado haijafanyia kazi.

**SPIKA:** Mheshimiwa, muda wako ulishakwisha kitambo.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, dakika kumi atafuatiwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali dakika kumi pia.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami kuchangia katika hoja hii ya Serikali ya Muswada wa Fedha ulio mbele yetu. Kwanza kabisa naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuunga mkono hoja, naomba nitoe ufafanuzi na namna gani tunafikiria tunaweza kuendesha kilimo chetu hapa nchini kwa usahihi na uhakika mzuri zaidi utakaozingatia maslahi mapana ya wakulima wa nchi hii.

Mheshimiwa Spika, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015 - 2020 inataja bayana kwamba mfumo wa ushirika ndiyo utakaotumika vizuri katika kuhakikisha kwamba kilimo kinastawi na wakulima wananufaika. Ndiyo maana utaona jitihada kubwa imewekwa kuhakikisha kwamba ushirika unafufuka na mambo ya ovyo ovyo yaliyokuwepo katika ushirika yanakoma.

Mheshimiwa Spika, ushirika unatarajiwa sasa ujengwe kwa namna mpya na katika hili, mabadiliko ya Sheria Na.6

ya Ushirika yaliyofanyika, yalikuwa yamelenga kuhakikisha kwamba takwa hili la Ilani ya Uchaguzi ya Chama Tawala linatekelezwa na sisi tumeanza kulitekeleza kwa vitendo.

Mheshimiwa Spika, tumefanya mabadiliko makubwa katika mfumo wa ununuzi na uuzaji wa mazao hapa nchini. Katika kufanya mabadiliko hayo, pia tunatarajia na tumekwishaanza kwamba hata uhudumiaji wa kilimo wa mwananchi mmoja mmoja katika kilimo utafanyika kwa kiasi kikubwa kupitia mfumo wa ushirika. Ndiyo maana leo tumeweka utaratibu wa kuuza kahawa na pamba kupitia ushirika. Pia tunahimiza wakulima wa chai nchini wauze kupitia ushirika.

Mheshimiwa Spika, pia tumbaku hapa nchini inalimwa na kuhudumiwa yote kupitia ushirika. Eneo moja pia ambalo sasa mkazo utaendelea kuwekwa ni kuhakikisha kwamba huduma kwa wakulima wa korosho, mauzo ya korosho na mambo mengine yote yanahusu hili zao pia na yenyewe yatapitia ushirika.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tunafikiria pia kuingiza mazao mengine yanayokuwa makubwa sana kama vile ufuta na mengineyo ili na yenyewe ianze kuhudumiwa kupitia ushirika.

Mheshimiwa Spika, ni katika mkakati huu, Soko la Mazao *(Commodity Exchange),* sasa hivi litaanza rasmi, maelekezo yamekwishatolewa ili hata uuzaji wa mazao mengine ambayo hayajwa na ushirika bado yaweze kuuzwa kupitia soko hilo na tutawashawishi wananchi wawe wanaweka kwa pamoja ili *volume* inayoingia katika *Commodity Exchange* iwe ni kubwa ku-*attract* wanunuzi waweze kununua mazao haya. Kwa hiyo, chai, tumbaku, korosho, pamba, alizeti na mazao mengine yote tuna-*advocate* kwamba yahudumiwe kupitia ushirika.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa tunavyozungumza mfumo huu wa ushirika na mfumo wa stakabadhi ghalani umeanza kufanya vizuri pia katika mazao mengine. Juzi tumeanzisha mfumo huu kwa zao la ufuta, wako waliosema wao hawajajiandaa lakini wengi waliosema wamejiandaa na wakaingia, tumeyaona mafanikio makubwa baada ya minada miwili mitatu ya mwanzo. Ufuta uliokuwa unauzwa kwa bei ya chini sana ya Sh.1,400 na Sh.1,500 kwa kilo moja. Minada miwili ya kwanza imeutoa kwenye Sh.2,710 mpaka Sh.2,840. Mnada wa tatu utakaofanyika Jumapili wiki hii, tunatarajia huenda ukaipeleka bei ya ufuta kwa kilo moja kufika kwenye Sh.3,000.

Mheshimiwa Spika, Dodoma hapa sehemu ya barafu pale, ufuta umefika Sh.2,700 na kwa sababu una-*respond* kwenye soko linaloendeshwa kwenye stakabadhi huko Mikoa ya Lindi na maeneo fulani ya Mkoa wa Pwani.

Mheshimiwa Spika, sasa namna gani tutahudumia mazao yote haya, mazao makuu yetu haya na yanayojitokeza kwa sababu tunaposema mazao makuu, labda naomba tueleweke vizuri Waheshimiwa Wabunge, siyo kwamba zao lingine hata likitokeza kukua au kupata *demand* kubwa na likazalishwa kwa wingi tutali-*exclude* kwenye utaratibu mzima wa Serikali. Mazao yale yalianza, lakini mengine hayazuiwi kuingia na hayazuiwi kuingia kutegemea na eneo la uzalishaji na kule yanakohitajika kuuzwa.

Mheshimiwa Spika, leo huwezi kuamini kwamba ufuta umepata *demand* kubwa na unazalishwa kwa wingi zaidi kuliko chai, tumbaku na kahawa. Kwa hivyo, kwa eneo la uzalishaji wa hili zao, hilo tayari ni zao la kipaumbele, huduma kwa mazao ya namna hii, itabidi tuendelee kusisitiza kwamba ni ushirika ndiyo itakuwa *vehicle* ya kuhudumia na kuuza mazao ya namna hii.

Mheshimiwa Spika, leo kwa mfano, kupitia Ushirika katika mikoa inayozalisha korosho *sulphur* ya maji karibu lita 320,000 zimekwishasambazwa kwa wakulima. Vinginevyo jambo hili lisingewezekana, kilichofanyika tu ni kwamba Bodi

imezungumza na Vyama vya Ushirika vya Msingi na Vyama Vikuu, wametoa mahitaji yao na mahitaji yao yale tumeingia katika *contract* na *supplies* na wale *supplier* wamepeleka, sasa huduma inakwenda kwa wakulima moja kwa moja bila ujanja katikati hapa. Kwa hivyo, tunatarajia katika pembejeo zingine tutafanya hivyo hivyo, kwamba huduma, kama ni *sulphur*, kama ni nini, tutapitishia kwenye ushirika kuwahudumia wakulima.

Mheshimiwa Spika, wakulima kupitia vyama vyao vya msingi vitatoa mahitaji yao, Bodi za Mazao haya zitazungumza na vyama, watakubaliana utaratibu wa kupata mitaji na kadhalika na Serikali ipo, pale ambako itakuwa inahitajika kupeleka fedha kutegemea na mahitaji yaliyoletwa na wakulima kupitia vyama vyao, Serikali itafanya namna hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo, niombe sana Waheshimiwa Wabunge, wasiwasi huu unaojengeka usitufanye tuondoke kwenye mkakati ambao utatuwezesha kuhudumia mazao yote kwa namna moja na kwa uhakika. Kwa sababu ni kupitia Ushirika ndiyo Serikali tunaweza kuwa na uhakika kwamba hili jambo kweli lina-*represent interest* za wananchi wote kwa upana wake na siyo watu wachache kunufaika katika mnyororo mzima wa thamani.

Mheshimiwa Spika, pia niombe kutumia nafasi hii kusema kwamba uhakiki wa miche ya korosho iliyozalishwa lengo letu ilikuwa kuzalisha mikorosho miche milioni kumi, uhakiki umefanyika, tumekwishafika Mikoa ya Kusini tumemaliza sasa tutaingia Morogoro, Pwani, Dodoma na Tabora, miche milioni nane na laki mbili imehakikiwa na waliozalisha kwa utaratibu usiokuwa na kona kona, fedha yao itatolewa na Serikali na wao watalipwa fedha yao.

Mheshimiwa Spika, fedha kwa ajili ya utafiti katika vyuo vyetu, kama nilivyosema juzi shilingi bilioni tatu zimekwishatolewa ili ikaendelee kuhudumia shughuli za utafiti katika zao letu. Jambo la msingi kubwa hapa ni kwamba

shughuli za utafiti, Bunge lako Tukufu lilipitisha Sheria ya kuanzisha Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania *(TARI)* na itakuwa kupitia sasa Taasisi hii, ndiyo taasisi zote za utafiti tunazo sita kwa sasa katika Kanda zetu Sita zitahudumiwa kupitia *umbrella organization* yao inayoitwa *TARI*.

Mheshimiwa Spika, tulikuwa hatujapata Mwenyekiti wa *TARI*, Mheshimiwa Rais amekwisha mteua Mwenyekiti wa *TARI*, Mtendaji Mkuu yupo, *establishment* imekwisharidhiwa tayari na Wizara ya Utumishi Ofisi ya Rais, kwa hivyo sasa tuna-*take off, TARI* watahudumiwa kupitia vyanzo vya Serikali, lakini Sheria waliyoipitisha inawaruhusu pia wao kuwa na mapato yao ya ndani yasiyotegemea Serikali.

Mheshimiwa Spika, tumekuwa tunasisitiza kwamba, hivi vyuo vitumie *capability* waliyonayo kuzalisha fedha, wasibaki kufanya utafiti ambao hauunganiki na uzalishaji na hiyo ni fursa kwa wao kuweza kutengeneza fedha na kupunguza utegemezi kutoka Serikalini.

Mheshimiwa Spika, kwa kifupi...

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa**.**

**WAZIRI WA KILIMO:** Muda umekwisha! Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na nakushuru sana.*(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, kama ulivyosema hawa wanaofuatilia habari ya miche wafike Kongwa na Mpwapwa, Kongwa na Mpwapwa peke yake ina miche zaidi ya laki nne ambayo ilikuwa *distributed* mwaka huu peke yake. Ndiyo Mheshimiwa Waziri wa Kilimo...

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, kidogo tu, kwamba mnada wa jana wa ufuta Kibiti, bei ya kilo moja imefika Sh.3,100. *(Makofi).*

**SPIKA:** Mambo hayo kwa Mheshimiwa Ungando huko! Huko Kibiti kwa bei hiyo, nafikiri watu wote watacheza singeli. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali tafadhali dakika kumi.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia muda kuwa mchangiaji wa pili kwenye sheria hii tunayoijadili.

Mheshimiwa Spika, nitagusia mambo mawili, matatu katika mchango wangu. Kwanza, itakuwa inahusu Mfuko wa Korosho, halafu nitazungumzia kidogo Tume ya Mipango, nitazungumzia Suala la Akaunti ya *TSA* na kama muda utaniruhusu, nitazungumza kidogo kulikuwa na suala linalohusu kutozwa kwa *VAT* kwa umeme unaouzwa Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, nikianza na suala la Mfuko wa Korosho, kulikuwa na tuhuma hapa kwamba Mwanasheria Mkuu wa Serikali, amelipotosha Bunge katika suala hili na katika masuala kadhaa. Ninalopenda kusema mbele yako, wazi kabisa kwamba *position* aliyoitoa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ndiyo sahihi kabisa kisheria. Jambo la kwanza lililozungumzwa katika eneo hilo la korosho ni kwamba, tozo ya *export levy*, ilianzishwa na wakulima.

Mheshimiwa Spika, hiyo siyo sahihi, tozo ya *export levy au levy* kwa ujumla haikuanzishwa na wakulima. *Levy* hiyo ilianzishwa na Sheria ya *Cashewnuts Board of* Tanzania ya mwaka 1984 na ni kifungu cha saba (7). Nisome tu kwa rejea kwa sababu mambo haya wakati mwingine inabidi msomeane ili watu waamini. Kifungu kinasema:

*"7(1) The Minister may, after consultation with the Minister for the time being responsible for Finance and with the Board, and by order published in the gazette, impose a levy on cashewnuts or any category, cashewnuts produced or processed in the United Republic.*

*(2) Levy imposed under sub-section (1) shall be computed and collected at such rate and in such manner as*

*may be prescribed by regulations made under this Act and shall form part of the financial resources of the Board."*

Mheshimiwa Spika, hizo *regulations* za mwaka 1996 zinasemaje, hizo *regulations* ambazo zinaitwa *cashewnuts marketing regulations* za mwaka 1996, Kifungu cha 21 kinasema;:

*There will be payment of export levy and quality standard to be observed.*

Kifungu kidogo katika hicho kifungu cha 21, kinasema:

*The exporter shall prior to making shipment of each export consignment observe quality standards are specified in relevant sales contract and pay export levy applicable.*

Mheshimiwa Spika, *export levy* haikuanzishwa na wakulima, ilianzishwa na Serikali.

**SPIKA:** Ehee wale wote mnajibiwa tulieni. *(Kicheko)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, jambo la pili, nini hasa uamuzi wa Mahakama ya Rufaa. Je, uamuzi wa Mahakama ya Rufaa ulikuwa na athari ya kusema *export levy* ni fedha za wakulima au ni fedha za Serikali. Namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu Ole Nasha, alitoa maelezo kidogo, wakati hoja hiyo ikitolewa.

Mheshimiwa Spika, itoshe kusema, Bodi ilikuwa inakusanya *export levy* na ile *percentage* inayokwenda kwenye Mfuko wa Korosho ilikuwa inatolewa na Bodi ilianzia mwaka 1996. Mwaka 1998 baada ya kutokea ubadhirifu, Serikali ilitoa maelekezo Bodi ya Korosho isipeleke zile fedha kwenye Mfuko wa Korosho.

Mheshimiwa Spika, baada ya uamuzi huo, Mfuko wa Korosho ukafungua kesi Mahakama Kuu, kama nilivyoeleza katika maelezo yangu ya awali, Mahakama Kuu kimsingi ilisema mambo matatu, Bodi ilikuwa inakusanya zile fedha

za kwa niaba ya Serikali, zile fedha ni za Serikali na Serikali ndiyo ina mamlaka ya kupanga matumizi ya fedha hizo. Mfuko wa Korosho haukuridhika ukakata rufaa Mahakama ya Rufaa. Mahakama ya Rufaa ilisema nini? Mwisho kabisa, sentensi ya mwisho, "*the appeal is lacking in merit, we accordingly dismiss the appeal with costs.*"

Mheshimiwa Spika, unapokuwa na kesi, Mahakama fulani ikaweka msimamo na Mahakama Kuu, niliweke hili wazi, kisheria Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufaa zinajulikana kama *Court of Record.* Ni Mahakama zinazoweza kuweka msimamo wa kisheria. Sasa Mahakama Kuu imetoa maamuzi wamekata rufaa kwenda Mahakama ya Rufaa, Mahakama ya Rufaa imetupitia mbali rufaa, maana yake nini? Uamuzi wa Mahakama Kuu unabaki.

Mheshimiwa Spika, katika hukumu hii ni kweli Mheshimiwa Cecil Mwambe nafikiri alikuwa anafanya *reference*, Mahakama ya Rufaa ilizungumza, zungumza mambo mengi, lakini kama alivyoeleza vizuri kabisa Mheshimiwa Ole Nasha, katika hukumu yeyote na hii tunaitoa katika misingi ya uangalizi wa sheria, tunapokuwa tunaiangalia hukumu tunaifanyia *analysis* ya namna gani.

Mheshimiwa Spika, kuna kitu kinaitwa *dictum* uamuzi wa mwisho, kuna kitu kinaitwa *orbiter dictum* ni maoni ya Jaji, wanayoyazungumza yote hayo yalikuwa ni maoni ya Jaji, lakini uamuzi wa mwisho ambao ni *dictum*, ni hii *appeal is lacking in merit, we accordingly dismiss it*, tena na gharama juu. Msimamo wa Mahakama Kuu ndiyo msimamo unaobaki mpaka hapo.

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu, kulikuwa na madai kwamba, wakulima wa korosho, waliingia mkataba na *TRA*, uliopelekea yale mabadiliko katika *Finance Act,* 2010 na ikaweka ile *formula* ya asilimia 65 kwa 35, huu ni upotoshaji. Hakuna mtu yeyote binafsi anaweza kwenda kukubaliana na *TRA,* namna ya kutoza kodi na mahali pa kuzipeleka. Kwa hiyo, tukomee hapo ni upotoshaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho kuna mapendekezo, tuiache *Finance Act* 2010 katika suala la korosho iendelee kubaki ilivyo. *Finance Act* ya 2010 ilifanya *ammendments* kwenye ile sheria *Cashewnuts Industry* ya 2009. Kama nilivyoeleza katika mchango wa awali hii Sheria ya *Finance Act* ya 2010 iliyorekebisha Sheria ya *Cashewnuts Industry* 2009, ilikuwa na matatizo ya kimsingi ya kisheria haifai kuiacha ilivyo.

Mheshimiwa Spika, tatizo la kwanza nilieleza ilitambua Mfuko ambao haujaanzishwa kwa mujibu wa sheria kama ilivyoelezwa katika Katiba Ibara ya 135(2), pia kama ilivyolezwa katika sheria mbalimbali. Kwa hiyo haiwezekani kuendelea na sheria inayoutambua Mfuko ambao haupo kisheria, lakini pia haujaanzishwa na amri ya Waziri kwa kadri au na minajili ya kifungu cha 12 cha Sheria ya Fedha za Umma, 2001 *(The Public Finance Act,* 2001). Kwa hiyo, hilo lilikuwa tatizo la kwanza kisheria.

Mheshimiwa Spika, tatizo la pili, lipo humo, kwa sababu hii *Finance Act, 2010* sasa inamtaja *TRA* ndiye mkusanyaji wa hizi *export levy*, lakini ukienda Kifungu cha 24(1) cha Sheria ya *TRA*, kinasema *TRA* akishakusanya hizi fedha anapeleka kwenye Mfuko Mkuu *(Consolidated Fund),* hawezi kupeleka sehemu nyingine, lakini hata hii Katiba, Ibara ya 135(2) iko wazi, makusanyo yote yanayofanywa na Serikali yanakwenda Mfuko Mkuu. Kwa hiyo, Sheria hii ilivunja Katiba, sheria hii ilivunja Sheria ya *TRA*, ilivunja Sheria ya *Finance Act*. Haiwezi ikaachwa.

Mheshimiwa Spika, Sasa nihame kutoka kwenye Korosho niende kwenye Tume ya Mipango.

**SPIKA:** Malizia Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, nilifikiri ni dakika tano za kwanza.

**SPIKA:** Malizia, muda umekwisha tayari, lakini malizia.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, basi kwa haraka haraka kabisa, kufuta Sheria hii ya Tume ya Mipango hakuna shida, kwa sababu cha msingi ni majukumu, majukumu yake yataahamishiwa katika Wizara ya Fedha na kutunga sheria nyingine mpya kama itahitajika siyo jambo zito wala kubwa, hili linaweza likafanyika kwa muda mfupi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la *TSA* kuvunja Katiba, hasa kile kifungu cha 143(2)(a) kwamba fedha zinazokusudiwa kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali, basi lazima ziwe zimeidhinishwa na Bunge na kwamba katika *TSA* kutaingia aina fulani ya fedha zinazoitwa *unspent funds.* Fedha hizo zilishaidhinishwa kwenye bajeti iliyotangulia ila imefika mwisho wa mwaka wa fedha, mwaka wa fedha una *limit* yake, haziwezi kutumika baada ya hapo, zinaingizwa zinahesabiwa kuwa ni *unspent funds* lakini zilikuwa zimeshaidhinishiwa matumizi yake.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kuna utaratibu ambapo Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, anatoa kibali cha kuzitumia zile fedha kwa makusudi yaliyokuwa yameidhinishwa na Bunge na anatoa kipindi maalum ambapo fedha hizo ziwe zimetumika.

Mheshimiwa Spika, nizungumze kidogo kwa ufupi kuhusu suala lililoibuka la kutoza *VAT* Umeme unaopelekwa Zanzibar. Mapendekezo yalikuwa ni kwamba tulete mabadiliko katika hii *Finance Bill*, ushauri wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ilikuwa ni kwamba, ingefaa mabadiliko haya yafanyike kupitia *Miscellaneous Amendments* kwa sababu moja kubwa, *Miscellaneous Ammendments* huwa zinapita kwenye Baraza la Mawaziri, zitapita kwenye Kamati ya Bunge, Kamati ya Baraza la Mawaziri kuhusu masuala ya Miswada na hapo tutaweza kuwa na Waziri wa Fedha, Waziri wa Nishati kwa sababu ni suala la Nishati hilo, lakini pia Waziri anayehusika na masuala ya Muungano kwa sababu pengine yako masuala ya mahusiano kati ya Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar. Kwa hiyo, ushauri

wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali isiingie katika *Finance Bill* hii, ishughulikiwe katika *Miscellaneous Amendments*,

Mheshimiwa Spika, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, tunajifunza kitu kimoja hapo, Mheshimiwa Cecil Mwambe alikuwa anamwambia Mwanasheria Mkuu wa Serikali mwongo, apelekwe kwenye Kamati ya Maadili, sasa imethibitika kwamba yeye ndiyo mwongo, sasa sijui na yeye tumpeleke kwenye Kamati ya Maadili au vipi? Ndio maana lugha za Bungeni hapa zinataka utumie lugha za kistaarabu zaidi, unapofikisha meseji yako, maana isiwe tu kwamba kwa fulani sawa, lakini kwako wewe ikirudi isiwe sawa. Katika mazingira ya kawaida ilitakiwa na wewe usonge mbele kule ushughulikiwe. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Mpango.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kutoa shukrani za dhati kabisa kwako binafsi kwa kuendesha vizuri majadiliano kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha ya mwaka 2018. Napenda kutambua michango ambayo imetolewa na Kamati ya Bajeti hususani Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia Mbunge wa Mtwara Vijijini, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti na Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia kwa kuzungumza au kwa maandishi hapa Bungeni. Nawashukuru wote kwa michango yenu.

Mheshimiwa Spika, jumla ya Waheshimiwa Wabunge 21 wamechangia katika kuboresha Muswada huu, ambapo Waheshimiwa Wabunge 15 wamechangia kwa kuzungumza na Waheshimiwa Wabunge sita wamechangia kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nifafanue baadhi ya hoja ambazo zimetolewa na Kamati ya Kudumu ya

Bunge ya Bajeti pamoja na Waheshimiwa Wabunge ambazo ningependa nizitolee ufafanuzi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bajeti ilitoa hoja ya kuongeza aya nyingine ambayo itaruhusu ushuru wa bidhaa kwenye vinywaji vikali yaani *spirits* vinavyotengenezwa hapa nchini kwa mchuzi wa zabibu unaotengenezwa hapa nchini kwa kiwango kisichopungua asilimia 75 kinachotoza kodi ya kiwango cha Sh.450 kwa lita.

Mheshimiwa Spika, najua na wewe unalima zabibu nami najifunza naomba nitoe maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, huko nyuma Serikali iliwahi kutoa msamaha wa ushuru wa bidhaa kwa kiwanda cha kutengeneza *valour* ambacho ni kiwanda tanzu cha *TBL*. Lengo la kusamehe kodi hiyo ni kutoa unafuu kwa ajili ya kiwanda hicho ili kiweze kununua mvinyo yaani mchuzi unaozalishwa na kampuni ya *CETAWICO* na hivyo kuwezesha wakulima wa zabibu kupata soko la uhakika wa zabibu.

Mheshimiwa Spika, msamaha huo ulitolewa kwa mujibu wa Sheria ya Ushuru wa Bidhaa kwa kipindi cha miaka mitano, mwaka 2002 mpaka mwaka 2007 kwa masharti maalum na ili kuweza kudhibiti matumizi ya msamaha huo kwa kuanzia hati ya msamaha *(GN)* ilitolewa kwa miaka miwili kwa sharti la kuongeza muda iwapo watakuwa wametekeleza makubaliano yaliyowekwa, yaani masharti ya msamaha huo. Palikuwepo na *performance indicators* ambazo zilikubaliwa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia maoni ya Wabunge juu ya kuweka mfumo wa kodi ya ushuru wa bidhaa ili kusaidia kiwanda cha *CETAWICO* na wakulima wa zabibu, Serikali inaangalia uwezekano wa kuweka utaratibu kama huo ambapo itaingia mkataba na viwanda vinavyotumia mchuzi huo na kutoa msamaha huo wa ushuru wa bidhaa kwa kipindi maalum. Serikali itaweka vigezo maalum ili kuhakikisha kuwa msamaha

huo unasaidia viwanda vinavyotengeneza mchuzi na kuendelea kuhamasisha kilimo cha zabibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, iwapo Serikali itapunguza ushuru wa bidhaa wa pombe kali inayotokana na mazao ya zabibu ambayo inaitwa *valour, HS code* 22.08 ambayo inazalishwa hapa nchini, Serikali itapoteza mapato ya kiasi cha shilingi bilioni 18 kwa mwaka, kwa kipindi hiki bado inatuwia vigumu kupata mahali pa kupata hizi mbadala shilingi bilioni 18. Kwa hiyo naomba utaratibu huu tukiuzingatia tutakuwa tumeweza kutekeleza kile ambacho wakulima wa zabibu wanahitaji.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bajeti pia ilishauri kwamba tuongeze ushuru wa bidhaa kwa Sh.50 katika juisi ambayo inaagizwa kutoka nje, *HS code* 20.09.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 124(2) cha Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura ya 147 kinaelekeza kuongeza viwango wa ushuru wa bidhaa kwa kiasi cha mfumuko wa bei au viashiria vingine vya uchumi jumla, hivyo ongezeko lililofanywa kwenye juisi ni kwa kuzingatia utaratibu huo.

Mheshimiwa Spika, tulishauriwa pia kwamba tuongeze ushuru wa bidhaa kwa Sh.500 kwa bidhaa zenye *HS code* 2204.10.00, *HS code* 2204.21.00 na *HS code* 2204.29.00. Kifungu cha 124(2) cha Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura hiyo ya 147 kinaelekeza kuongeza kiwango cha ushuru wa bidhaa kama nilivyokwishasema kwa kiwango cha mfumuko wa bei au viashiria vingine na hivyo ongezeko ambalo limefanywa kwenye bidhaa tajwa kutoka nchi za nje ni kwa kuzingatia utaratibu huo.

Mheshimiwa Spika, Mwanasheria Mkuu wa Serikali amezungumzia kwa kifupi kuhusu kufuta Sheria iliyoanzisha Tume ya Mipango nami naomba niongezee maelezo, hasa kwa kuzingatia kwamba nilikuwa Mkuu wa Tume ya Mipango takribani kwa miaka sita. Nilieleza hili wakati wa kuhitimisha bajeti tarehe 26, kwamba kwa kweli mapendekezo haya ni mabadiliko ya kimuundo na siyo

kufuta kazi muhimu za kupanga mipango ya Maendeleo ya Taifa kwa muda wa kati na mrefu.

Mheshimiwa Spika, pia nilieleza kwamba ukiangalia historia ya muundo wa Tume ya Mipango iko wazi kabisa tumekuwa tunahama. Kuna nyakati Mipango ilikuwa ni Tume, kuna wakati Mipango ikawa ni Wizara inayojitegemea, kuna wakati hata huko nyuma Mipango ilikuwa ni sehemu ya Wizara ya Fedha na Mipango.

Mheshimiwa Spika, nilieleza kwamba hata ukiangalia nchi jirani ya Uganda, nchi jirani ya Rwanda wao nao kazi ya kupanga, taasisi inayopanga iko ndani ya Wizara na inaitwa *Ministry of Finance and Economic Planning*. Lengo hili la kuunganisha taasisi hizi mbili nilieleza kwamba, ugawaji wa rasilimali inakuwa ni gumu kweli wakati hizi taasisi mbili zimetenganishwa, kwa hiyo ni sababu moja ya msingi sana. Sababu ya pili Serikali hii ilishaamua kwamba tujitahidi kadri inavyowezekana kupunguza gharama za Serikali. Hivyo, hiyo ni kati ya mambo yaliyozingatiwa.

Mheshimiwa Spika, kubwa kazi zote ambazo zinafanywa na Tume ya Mipango zimeendelea kufanyika. Watumishi wale baada ya kuwahamishia ndani ya Wizara ya Fedha bado wameendelea kuandaa Mpango wa Maendeleo wa mwaka, kwa kuzingatia Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano na Dira yetu ya Maendeleo ya Taifa 2025. Pia wameendelea kufanya *monitoring and evaluation* kwa kukagua miradi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, pia Wataalam hawa tayari wameshaandika mkakati wa kutekeleza Mpango wa Pili wa Maendeleo ya miaka mitano. Kwa hiyo, hili ndilo jambo la msingi kazi zake zimeendelea kama kawaida kabisa na zinapokuwa chini ya Wizara ya Fedha sasa inakuwa ni rahisi zaidi kuhakikisha kwamba mahitaji yake yanazingatiwa.

Mheshimiwa Spika, yapo maeneo ambayo pia bahati nzuri tulikubaliana na Kamati ya Bajeti labda haya niyaache kwanza kama muda utaruhusu nitayarejea. Kamati ya Bajeti

inapendekeza kupandisha tozo ya *petrol* na *diesel* kutoka Sh.313 kwa lita hadi Sh.363 kwa lita ambayo ni ongezeko la Sh.50 kwa lita na kiasi hiki cha fedha kinapendekezwa ili kiweze kupelekwa kwenye Mfuko wa Maji. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba tusikilizane tumsikilize Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, kupandisha tozo ya mafuta ya *petrol* na *diesel* kutafanya bidhaa hiyo kupanda bei na hatimaye kupandisha bidhaa nyingine nchi nzima. Serikali imelitafakari sana jambo hili, tumefanya uchambuzi wa kina, tumetazama mwenendo wa bei ya mafuta katika soko la dunia, ni dhahiri kabisa kwamba bei ya mafuta inapanda. Hata ukiangalia *projection* za mwaka ujao wa fedha bei ya mafuta inaendelea kupanda, hii itaathiri sana mfumuko wa bei katika Taifa letu na hivyo kuathiri gharama za maisha nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, siyo hivyo tu tulipofanya uchambuzi nilieleza hapa kwamba tulikuta kwamba bidhaa hizi za mafuta zina tozo nyingi sana na kuweka ongezeko hili maana yake ni kwamba tunaendelea kubebesha chanzo hiki kimoja mzigo mkubwa zaidi. Pia kazi kubwa ambayo Waheshimiwa Wabunge walishauri ni kwamba tupate chanzo cha uhakika cha kugharimia miradi ya maji.

Mheshimiwa Spika, hili tumelizingatia kwa maana kwamba kuanzia mwaka ujao wa fedha nimekwishatoa maelekezo kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha, bajeti ya miradi ya maji ambayo wamepitisha itakuwa kati ya fedha ambazo zinapewa kipaumbele na kuangaliwa kwa karibu kuhakikisha kwamba fedha walizozipitisha zinatolewa kwa kadri inavyowezekana.

Mheshimiwa Spika, naamini kabisa kwamba pamoja na hatua hizi za mapato wakitupitishia maana yake ni kwamba fedha iliyotengwa kwanza kwenye bajeti itatoka, vilevile Serikali imeendelea kufanya jitihada kuongeza vyanzo vingine. Nilieleza kwamba tayari tumeshapata

mkopo wa dola milioni 350 kutoka Benki ya Dunia, kati ya hizo dola milioni 60 tayari zimepatikana na zitaanza kupatikana mwezi ujaowa Julai, hata hizo nyingine nazo zinaweza kupatikana kwa haraka itategemea tu kiasi ambacho utayari wa miradi yenyewe lakini fedha ziko tayari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama hiyo haitoshi, tulishalitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba zile dola milioni 500 kwa ajili ya Miji 21 Tanzania Bara na Zanzibar hizi tayari tulishasaini makubaliano, nazo zitapatikana katika mwaka ujao wa fedha bila wasiwasi wowote. Vilevile tumefanya mazungumzo na Shirika la Maendeleo la Ufaransa hawa nao wako tayari kutupatia pesa kwa ajili ya miradi ya maji kuanzia mwaka ujao wa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo muhimu ambalo ningependa kusisitiza, Waheshimiwa Wabunge wanafahamu tumekuwa na matatizo makubwa sana kwa maana ya matumizi ya fedha hizi za miradi ya maji. Kwa hiyo, siyo vizuri tuendelee kupeleka hela bila kupitia upya na kujiridhisha kwamba utekelezaji wa miradi ya maji na fedha zile zitatumika ipasavyo, ndiyo maana Wakala wa kutekeleza Miradi ya Maji Vijijini unakwenda kuanzishwa, pia Wizara ya Maji inafanya marekebisho ili kuhakikisha kwamba fedha hizi zinatumika vizuri. Tukishaweka mfumo mzuri wa kuhakikisha kwamba fedha hizi zinasimamiwa vizuri kwa hakika kabisa Serikali haitasita kuongeza fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tulishauriwa pia kwamba tupunguze kodi ya mapato kwa makampuni yanayotengeneza bidhaa zifuatazo: Taulo za akina mama, vifaa vya kilimo, vifaa vya kuhifadhi mazao ya samaki na yenye mkataba na Serikali kutoka asilimia 30 hadi 20 kwa miaka mitano ya mwanzo.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeamua kutoa vivutio vya kikodi kwenye kampuni mpya zitakazoanzisha utengenezaji wa madawa ya binadamu na bidhaa za ngozi na lengo letu ni kuvutia wawekezaji wapya. Aidha, hatua inaakisi

malengo ya Serikali ya kuvutia wawekezaji kwenye viwanda vya madawa ili tupunguze mzigo wa kununua madawa ya binadamu nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, kivutio cha unafuu wa kodi kwa watengenezaji wa bidhaa za ngozi unalenga kuhamasisha uchakataji wa ngozi zinazozalishwa ndani ya nchi. Watengenezaji wa taulo za akinamama waliomba msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani kwenye *sanitary pads* ili kufanya bidhaa hiyo iwe bei nafuu. Ni kipaumbele cha Serikali kuvutia wawekezaji katika eneo hili kwa kuwapunguzia kodi ya mapato.

Mheshimiwa Spika, hivyo, katika tasnia vifaa vya kilimo na vifaa vya kuhifadhia mazao ya samaki vifaa vingi katika kundi hili hasa zile za kilimo zina msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani na lengo la Serikali ni kuvutia wawekezaji wapya, lakini Serikali haikusudii kupunguza kodi ya mapato katika tasnia hii ili kulinda mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bajeti ilishauri tufute Sehemu ya Nane ya Muswada na Serikali kupitia jedwali la marekebisho imefuta Sehemu ya Nane ya Muswada. Vilevile ilishauri tufute Ibara ya 30 ya Muswada na kupitia jedwali la marekebisho tumefanya hivyo. Tulishauriwa pia na Kamati ya Bajeti tufute Ibara ya 35 ya Muswada na tumefanya hivyo. Siyo hivyo tu, tulishauriwa kufuta sehemu ya Kumi na Moja ya Muswada na kupitia jedwali la marekebisho tumefanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na suala hapa limesemwa kwamba *Tresuary Single Account* itamfanya mtu mmoja tu kuchukua fedha zote. Hili siyo sahihi, fedha zinagawiwa kwa kila Fungu husika kupitia *exchequer* na siyo kwenye akaunti, hivyo haiwezekani kabisa kwamba mtu mmoja anaweza akachukua fedha zote kwa sababu tu zimepita kwenye *Treasury Single Account*. Fedha hizi zinapita kwa mwenye Fungu mwenyewe na huyo ndiye atakayekuwa analipa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja kuhusu kodi ya majengo na vizuri nikalitolea ufafanuzi, kwenye upande wa kodi ya majengo kifungu ambacho kimeondolewa kilikuwa kinarekebisha baadhi ya maeneo katika sheria ili iweze kutekelezwa vizuri, lakini ni vizuri ifahamike kwamba kipengele hicho kilichoondolewa hakiondoi ukusanyaji wa kodi ya majengo kutoka Mamlaka ya Mapato. Ukusanyaji wa kodi ya majengo utaendelea kukusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania na siyo Halmashauri kama Mheshimiwa Mbunge alivyosema.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na ushauri kwamba *slot machines* zitozwe shilingi elfu 60 badala ya laki moja na kwamba *winning tax* itozwe asilimia 18 badala ya asilimia 20. Mapendekezo mapya katika Muswada wa Fedha wa 2018 niliouwasilisha Bungeni yalizingatia maoni ya wadau na Waheshimiwa Wabunge ambayo yamelenga kuweka usawa na haki katika michezo inayoshabihiana katika sekta ndogo ya michezo ya kubahatisha. Hivyo, Serikali inapendekeza kuendelea na marekebisho mapya ya Muswada wa Sheria ya Fedha 2018 katika kipengele hiki cha Sheria ya Michezo ya Kubahatisha, Sura ya 41 kama nilivyowasilisha Bungeni.

**SPIKA:** Malizia sasa Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, naomba tena nisisitize kwamba Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2018 ni sehemu ya bajeti ya Serikali ya mwaka ujao wa fedha niliyoiwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu. Ni muhimu kwa sababu Muswada huu ndiyo unawezesha utekelezaji wa kisheria wa bajeti iliyopitishwa na Bunge tarehe 26 Juni, 2018.

Mheshimiwa Spika, ili Serikali iweze kutekeleza ahadi zake kwa wananchi ikiwemo kutatua matatizo na kero zinazowakabili wananchi ni vema Bunge lipitishe Muswada huu na Muswada huu ndiyo unaidhinisha kisheria kodi, tozo na hatua mbalimbali za kiutawala za kukusanya mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya nawaomba sana Waheshimiwa Wabunge waridhie Muswada huu ili upite na kuiwezesha Serikali iingie kazini kukusanya mapato kwa ajili ya kuwahudumia Watanzania na kutekeleza bajeti hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Hoja imetolewa na imeungwa mkono, tunaomba tukushukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa ufafanuzi wako. Nina hakika ulikuwa na maelezo mengi zaidi kama muda ungeruhusu lakini itoshe hapo tulipofika. Kwa kweli kwa uchambuzi uliopo kama kuna Muswada umechambuliwa, huu umechambuliwa kweli kweli! *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea Katibu.

**NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**MWENYEKITI:** Natumaini kila Mheshimiwa ana *amendments* zote za Mbunge mmoja mmoja, za Kamati na za Serikali. Kwa hiyo, naomba twende kwa umakini ili tuifanye kazi yetu vizuri, maana kama nilivyosema mwanzoni maeneo mengi kweli yanaguswa na naomba tusikilizane wale ambao wanaongea ongea kila wakati *at least* twende pamoja sasa katika hili, nawaombeni sana. Katibu.

**NDG. LAWRANCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:**

**Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2018**
***(The Finance Bill, 2018)***

Ibara ya 1
Ibara ya 2

Ibara ya 3

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 4

**MHE. HAWA A. GHASIA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:** Mheshimwa Mwenyekiti, Kamati ilikuwa inapendekeza katika Kifungu cha 4(i) ambapo kuna neno *voted* na *non voted funds* libadilishwe na badala yake iwe *voted funds and balance carried forwards.* Pia ili kuwa na *harmonization* basi katika maeneo yote ambayo maneno hayo yametumika yatumike *voted fund and balance carried forward. (Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ni jambo ambalo mlikuwa hamjakubaliana bado mpaka sasa?

**MHE. HAWA A. GHASIA – MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilisema itakuja na *definition* sasa hatujaona, sasa sijui bado wanachukua ya kwetu au wanayo ya kwao.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri ufafanuzi.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa minajili ya sehemu hii Serikali inasema *voted funds means receipts from budgeted revenues of the Governments which are deposited in and paid from the consolidated fund.* Halafu ile iliyokuwa *non voted* ni *unspent funds which means receipts of the Government from the various sources which are deposited in and paid from the deposit accounts ot her than the Consolidated Fund*.

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mara ya mwisho Mheshimiwa Waziri hii *non voted* alikuwa anasema ni *unspent,* sasa labda anipe tu ufafanuzi

kwamba hiyo *definition* anayoitoa iko sawa kwamba *non voted* ni sawa kwamba ni *unspent money* ili tuweke mambo vizuri.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachosema hapa ni kwamba zipo fedha ambazo zinakuwa tayari tulizipigia kura humu ndani na ndiyo maana inaitwa *voted.* Sasa zipo fedha ambazo tumezi-*vote* humu ndani, lakini inafika mwisho wa mwaka zinapitiliza mwisho wa mwaka wa fedha. Sheria ya Matumizi imeelekeza kabisa kwamba baada ya tarehe 30 Juni zile fedha zina-*collapse,* lakini fedha nyingi, kwa mfano upande wa maendeleo ni kwamba zina-*cross over* zinakwenda mwaka mwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ndiyo maana katika *nomenclature* ya zamani zilikuwa zinaitwa *non voted* siyo kwa maana kwamba hazikuridhiwa na Bunge hili kwa ajili ya matumizi, lakini kwa maana kwamba kwa ile sheria ambayo inaweka mpaka maana yake zinakuwa ni tofauti na zile ambazo ni *voted* kwa mwaka ule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, baada ya majadiliano na Kamati ya Bajeti ndiyo maana tunasisitiza kwamba *unspent funds means receipts of the Government from the various sources which are deposited in and paid from the deposit account other than the Consolidated Fund. (Makofi)*

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakubaliana na *definition* yake lakini pia naomba ili kuwa na *harmonization* akafanyie marekebisho kwenye Sheria ya Benki Kuu, vifungu vya 35, 36 na 37 ili kote tuwe tunatembea na *definition* inayofanana.

**MHE. ZITTO Z. R. KABWE:** *(Aliongea bila kutumia kipaza sauti)*

**MWENYEKITI:** Mwenye marekebisho yake karidhika na wewe hukuwa na marekebisho yoyote na angealika kwamba

sijaridika jambo hili lijadiliwe hapo ndiyo tungefungua, ndiyo utaratibu wetu. Sasa anapewa nani taarifa, siyo utaratibu Mheshimiwa Zitto, subiri tu kama una kipengele huko mbele utasema. Akisharidhika yule aliyeleta *amendment* hapa na ndiye mwenye *amendment* sasa tunafanyaje, tunafungua *debate,* haiwezekani.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 5
Ibara ya 6
Ibara ya 7

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 8

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kifungu hiki cha 14A(1) tulikuwa tunapendekeza kwamba kifutwe na badala yake maneno yafuatayo yawekwe kwamba:

*"There shall be a register to be kept by every licensing authority at its principal office which shall contain name of the business, particulars of the owner, type of business and such other business license information as may be prescribed in the regulations".*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nia na lengo ni kwamba badala ya kuiachia kama wao walivyoiweka kwenye Muswada kwamba ikafanyiwe tu moja kwa moja kwenye kanuni, tunataka sasa zile *prescribed forms* na *prescribed register* tuwe tumeiona kabla kwamba itakuwa inahitaji nini na nini badala ya wao kuja baadaye na kuiletea mabadiliko wanavyopenda huko kwenye *regulations.* Tunataka kwenye hizo *regulations* tuwe umeiona kabla na hizi *items* ambazo tumetaja hapa kwamba kama jina, *business license*

*information* na aina ya biashara yote hayo yawe yamewekwa wazi kabla kwenye kila eneo.

**MWENYEKITI:** Mbona siwaelewi hii Kamati, yaani suala linalohusu *regulations* ninyi muwe mmeona kwanza, ndiyo utaratibu?

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Tulichokuwa tunasema hapa badala tu ya kusema Waziri atatengeneza fomu bila kusema kwenye hiyo fomu kutakuwa na vitu gani na sasa hivi tunataka mazingira wezeshi kwa ajili ya biashara zetu. Kwa hiyo, tuliiuliza Serikali kwamba hiyo fomu mnataka iwe na nini ndiyo wakatuambia. Kwa hiyo, tukasema badala ya kusema ataenda kutengeza fomu, tuseme tu kutakuwa na fomu yenye kuonyesha mwenye jina la kampuni na kila kitu. Kwa hiyo, kionekane kwenye sheria badala ya kwenda kukaa kwenye Kanuni. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Fedha, ufafanuzi tafadhali.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ambazo zinatajwa kuhusu jina la biashara, taarifa za mmiliki, aina ya biashara kama inavyopendekezwa na Kamati tayari zipo kwenye fasili ya neno *business license information* lililotumika katika Muswada. Neno *business license information* ni neno pana zaidi linaloweza kujumuisha taarifa nyingi zaidi kulingana na mahitaji ya wakati husika. Uandishi wa kutaja neno moja moja changamoto yake ni kuwa kisichotajwa kinakuwa siyo sehemu ya taarifa zinazokusudiwa. Hivyo, tunapendekeza kuendelea na mapendekezo yaliyomo katika Muswada kuhusu kifungu hiki. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nadhani maelezo kama yana uzito vile, Kamati.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakubali maelezo ya Waziri, lakini tunaendelea kama tulivyosema

hata katika michango Wabunge wengi kwenye kanuni kwa sasa hivi ule mfumo naomba uusimamie, Kanuni kabla hazijapitishwa/hazijatangazwa zije Bungeni kwenye Kamati na Kamati yako ikiridhika kwa niaba ya Bunge ndiyo sasa iende itolewe kama *GN*, la sivyo tutapata shida. *(Makofi)*

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Naombeni Waheshimiwa tupeane ushirikiano kwa sababu mnagawiwa makaratasi ni ghali sana ku-*print* haya na kugawa halafu tunapohoji hapa wengine mmenyamaza tu.

Ibara ya 9
Ibara ya 10

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 11

**MWENYEKITI:** Kamati mna marekebisho? Rekodi zetu zinaonesha 12 ndiyo kuna mambo ya Kamati, yeye yupo 11.

Mheshimiwa Mwambe marekebisho ya Serikali hayaja-*capture* ulichokitaka? Haya nakupa nafasi.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hoja niliyoileta kwako nilikuwa naomba kifungu hiki kiondolewe, lakini ikifaa basi tuongeze ili kuweza kuboresha zaidi kwa sababu athari ambazo tumeziongea kwa hiki kipindi chote zinazotokea kwenye tasnia ya korosho, kwa hiyo naomba tu Mheshimiwa Waziri aridhie ombi langu la kuondoa hiki kifungu kwa sasa hivi.

**MWENYEKITI:** Kwa sababu hoja yako ni ile ile, hebu na Ibara ya 12 ume-*suggest* kwamba vyote viwili viondolewe. Kwenye maelezo yako hebu unganisha kabisa.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu siyo 12 ni 15.

**MWENYEKITI:** Ni 11 na 12

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba ziondolewe kama ambavyo zipo hapa, kwa sababu tunachotaka sisi hasa kitokee pale kwenye hii *Section 12* ya *Principle Act,* wao wanataka *total amount of export levy collected under subsection 1* ili kuwa *deposited* kwenye ile *Consolidated Account.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafikiri kama ambavyo tumekuwa tukisema kila mara kwamba badala ya kuwa *collected* na kuwa *deposited* kwenye *Consolidated,* mwisho wa siku hii hela kulikuwa na makubaliano ambayo yamefanyika kati ya wale wadau pamoja na wale waliokuwa wanakusanya kwamba *only 35 percent* ibakie Serikalini kwa maana ya matumizi ya huku na *Consolidated Account, the rest* 65 *percent* irudi kwa ajili ya kwenda kufanya kazi zile ambazo kimsingi zilikuwa zimeainishwa ikiwa ni pamoja na masuala ya utafiti, ununuzi wa mbegu, kulipia pembejeo za ruzuku na mengine mengi kadri ambavyo tumekuwa tukijadili kwa muda mrefu sasa hivi.

**MWENYEKITI:** Sasa umependekeza kufuta bila pendekezo lolote mbadala ndiyo ulivyotaka si ndiyo? Maana *amendment* yako ni kufuta na kunyamaza.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Napendekeza kibakie kama vile ambavyo ipo sasa hivi kwenye sheria iliyopita. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Hiyo ya ibakie kama ilivyo kwenye sheria mama hukuandika huku, wewe umesema ifutwe tu halafu ukanyamaza. Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza katika maelezo yangu, sheria ile ikibaki kama ilivyo inaleta shida kwenye Katiba. Ibara ya 135(1) inasema fedha zote za umma zinapokusanywa

zipelekwe katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Pia nilizungumza kile Kifungu cha 24(1) cha Sheria ya *TRA* kwa sababu ndiyo iliyopewa kazi ya kukusanya hiyo kodi, kinaitaka *TRA* inapokusanya kodi ile ipeleke kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali. Kwa hiyo, ukiiacha hivyo maana yake itaendelea kusema ipelekwe katika mfuko huo. Tatizo la tatu, Mfuko ule haupo kisheria, haujaanzishwa kwa sheria yoyote kama inavyoeleza Ibara ya 135(2) ya Katiba, lakini pia kama inavyoeleza Kifungu cha 12 cha Sheria ya Fedha za Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, umuhimu wa hizi pesa ulikuwa ni kwenye masuala ya *research,* masuala ya mafunzo, mambo ya masoko pamoja na kuendeleza viwanda ikiwezekana, na *any other requirement aimed at developing the Cashewnut Industry.* Sasa leo tunapotaka kuondoa kifungu kile na Serikali kuweka wanavyotaka wao kabla mambo haya hayajajadiliwa kati ya wadau pamoja na Serikali maana yake kutakuwa na sintofahamu hapa katikati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba tu tujadili jambo hili na tuone namna watu wanavyoweza kumsaidia. Naomba kutoa hoja.

**MWENYEKITI:** Sasa unataka kijadiliwe kitu gani Mheshimiwa Cecil? Ngoja kwanza, tuwe tunaelewana ili hata kama kuna mjadala basi watu wawe wanaelewa tujadiliane nini. Kwa sababu hoja yako ni kwamba hii *proposal* iliyopo hapa ifutwe ibakie iliyokuwepo, iliyokuwepo inasema hela zipelekwe kwenye Mfuko na wewe unaambiwa Mfuko ni *non-existent,* haupo! Sasa unataka tujadili kwamba hela iende mahali ambapo hakupo! Sasa huo mjadala kweli tukiruhusu si tunapoteza muda tu? *(Kicheko)*

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati unaziunda wewe kwa mujibu wa sheria na ni sehemu ya Bunge hili. Mapendekezo ya Kamati pia wanafikiria sawa

na hii ninayoisema, pamoja na kwamba hapa hujasoma. Kwa hiyo, mimi naunga mkono hoja hii ya Kamati ambayo haujaisoma kwa sababu wanataka wao pia tufanye hivi ninavyovisema mimi ndiyo maana wao pia wameleta *amendment.* Kwa hiyo, tunaomba hiyo iingizwe, Serikali ione namna bora ya kukaa na wadau ili... *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Hebu basi ngoja maana yake hoja yako imekuwa kidogo ndiyo hivyo, sasa tuwasikie Kamati kwenye 12 sasa, baadaye nitazihoji moja moja maana yake zinakwenda pamoja ndiyo maana na wewe ulizileta pamoja pia. Kamati ninyi 12.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati tunapendekeza kwenye ile ya 12 pawe na maboresho, iwe *amended* kwa kufuta hiyo nanihii na kwa kuiweka isome, *by adding a new...*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jitu Soni, katika hatua hii nanihi nanihi... *(Kicheko)*

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo nasoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *by adding a new clause 12A after the proposed clause 12 as follows:-*

*"12AThe Principal Act is amended in Clause 17A as follows:-*

*(a) deleting subsection (2) and substituting for it the following:-*

*(2) The total amount of export levy collected under subsection (1) shall be apportioned to the Consolidated Fund and be spent after consultations with the Minister responsible for Finance and the Minister responsible for Agriculture and the Stakeholders of the Cashewnut Industry.*

(3) *The money apportioned to the Board shall have due regards to the following requirements:-*

*(a) research necessary for the development of the cashewnut industry;*
*(b) training and capacity building;*
*(c) marketing information;*
*(d) industrial development aimed at cashewnut crops processing; and*
*(e) agricultural input.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa kupitia mfumo wa kawaida kwenda kwenye mfuko kwenda Wizara ya Kilimo ambayo itapeleka kwenye Bodi ya Korosho, Bodi ndiyo itafanya majukumu yote haya. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Naamini kabisa Waheshimiwa Wajumbe wala hawajaelewa, au mmeelewa wenzangu? *(Kicheko)*

**WABUNGE FULANI:** Tumeelewa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tafadhali.

**MHE. HAWA A. GHASIA – MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda niseme kwamba Serikali ilikuwa inapendekeza kukifuta kile kifungu (A), lakini kama Kamati tulichokuwa tunasema, kile kifungu kisifutwe kwa maana ya kwamba pesa zikusanywe isipokuwa tulitaka tuongeze kifungu kingine. Kwa kuwa Mfuko wa Kuendeleza Zao la Korosho haupo na majukumu yake yamehamishiwa Bodi ya Korosho, kwa hiyo pesa ambazo zilikuwa zinakwenda kwenye mfuko ambao haupo, zipelekwe Bodi ya Korosho kwa kupitia Wizara ya Kilimo ambapo pia itashirikisha na wadau wa korosho wakiwemo Vyama Vikuu vya Ushirika vya kuzalisha korosho. Kwa hiyo, tunafuta lakini tunaweka na mbadala. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, sasa tukubaliane kwanza ile 11 hakuna hoja pale Mheshimiwa Cecil Mwambe, ili nihoji hiyo tuhamie tu 12 sasa.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 12

**MWENYEKITI:** Sasa tumesikia habari ya Kamati, Mheshimiwa Katani kama una maoni tofauti kwenye eneo hilo hebu tukusikie.

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni yangu ni kufuta Kifungu kidogo chote cha (2) na kufanya marekebisho yanayosomeka kama ifuatavyo:

"*(2) The total amount of export levy collected under section (1) shall be distributed in such manner that:-*

*(a) 50 percent would be remitted to the Cashewnut Board of Tanzania; and*

*(b) 50 percent would be remitted to the Consolidated Fund.*

*(3) The Minister responsible for Agriculture shall be in consultation with stakeholders, make regulations prescribing a mechanism for distrubution and use of the levy collected in terms of sub-paragraph (a) amongst Cashewnut Stakeholders. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo yangu haya nimeona nia njema ya Serikali ya kutaka kukusanya fedha. Sasa kwenye *win-win situation* nikaona asilimia 50 iende kwenye Bodi ambacho ni chombo cha Serikali tofauti na ile ya mwanzo ambayo Mwanasheria Mkuu amejaribu kutuelekeza kwamba ule Mfuko kama ulivyofutwa na Waziri Mkuu. Sasa hizi fedha ziende kwenye Bodi ya Korosho ambako taratibu nyingine zinaweza kutumika kwa kushirikiana na Waziri mwenye dhamana ya Kilimo.

**MWENYEKITI:** Msingi wa hoja yako ni nini? Kwa nini zisiwe 60/40 au 30/70, unatushawishi nini?

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuona kwamba ile 35 inawezekana ilikuwa haitoshi Serikalini, nikaona *win-win situation* niliyoisema, basi na Serikali wao wapate asilimia 50 na Bodi wapate asilimia 50 ili mambo yaweze kwenda kwa nia njema na Serikali iweze kukusanya. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, ufafanuzi.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua sana shauku ya Waheshimiwa Wabunge kuona kwamba fedha mahsusi inakwenda kusaidia zao moja au lingine. Kwa kweli Serikali, kama nilivyozungumza hapa wakati nachangia hoja iliyokuwa mbele yako, nimesema kwamba mfumo tunaouanzisha sasa ni ule ambao utatuhakikishia mazao yote yanakuwa *funded* kupitia utaratibu unaofanana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu maalum *(Subvote)* limekwishaanzishwa tayari katika Wizara ya Kilimo ambayo itakuwa ina-*address* suala la korosho, ndiyo maana hata kwa utaratibu huu ambao Waziri wa Fedha ameusema, hizi shilingi nilizozisema bilioni 13, zimepata dirisha la kwenda kwenye Bodi ya Korosho. Kwa hivyo, hakuna sababu ya ku-*distort* mfumo wa jumla wa kilimo wa Kitaifa kwa kulenga Bodi moja ambayo bado inayo nafasi ya kupata *funding* kutoka Serikalini kwa utaratibu wa kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo niombe tu Mheshimiwa Katani na Kamati waelewe kwamba nia ya Serikali haiwezi ikawa kuua zao. Ili anufaike nani tunapofanya hivyo? Tunachotaka tusifike mahali na naomba hili Waheshimiwa Wajumbe tulione tu vizuri, keshokutwa watu wa tumbaku nao wanaweza wakaanzisha kwamba fedha fulani iende kwenye Bodi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hii ni bora kwenda na mfumo wa Serikali...

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tuwe tunasikilizana katika masuala ya hoja.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni bora twende na mfumo ambao haututengenezei mazingira ya kuwa na *double standard* katika kuhudumia wakulima wa nchi hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Kamati.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza *by implication,* Waziri anakubaliana na maoni ya Kamati. Naomba nimnukuu Waziri, amesema kwamba imeshafunguliwa *subvote* ambayo imepokea bilioni kama 13, kupitia *subvote* hiyo fedha hizo zimeenda kwenye Bodi. Proposal ya Kamati ukitazama hiyo *mandate* haina *legal framework,* Kamati imetengeneza *a legal framework* kufanya jambo hilo na Kamati ina-*propose, and this is in good faith,* kwamba fedha zitakusanywa na *TRA according to the law* na kutokana na Katiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha zitapelekwa kwenye *Consolidated Fund* vilevile, hicho kiwango ambacho kinatakiwa kwenda kwenye zao hili kitatokana na *consultation* kati ya Wizara ya Fedha ambaye ni msimamizi, Wizara ya Kilimo ambaye ni msimamizi na wadau. Kwa hiyo, nashauri kwamba tukubaliane Mfuko umeondoka haukuwa na *legal framework* ya kuwepo wala uhalali wa kuendesha zoezi hilo, lakini fedha hizi zinakwenda kuendesha zao, msimamizi atakuwa aliye-*collect* Wizara ya Fedha, msimamizi atakuwa Wizara ya Kilimo vilevile Bodi ndiyo *executor according to the law.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali hili ni jambo ambalo linatutengenezea, kwa hiyo naomba tu kama tutakubaliana hatuna sababu ya kujadili, lakini kama hatutaelewana naomba tulijadili kwa pamoja tuweze kufikia muafaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**MWENYEKITI:** Hoja yako haikuungwa mkono.

**WABUNGE FULANI:** Aah!

**MWENYEKITI:** Si mnaona? Tunaendelea na mjadala huu. Kwa nini Bodi ya Serikali iwe inakwenda eti kujadiliana na Serikali katika kugawa, hilo jambo liko wapi pengine ili hili liwe la pili?

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *with due respect,* zao la pamba lina utaratibu ufuatao:-

Kabla ya kukubaliana shilingi ngapi wakulima wakatwe, wadau hukutana na Serikali na mwaka huu kwenye zao hili la pamba kikao kiliongozwa cha upande wa Serikali na Waziri, Mheshimiwa Dkt. Tizeba na wakafikia muafaka kwamba bei ya pamba itakuwa Sh.1,200 na Sh.100 itakatwa kwa mkulima kwa ajili ya kwenda kuwasaidia wakulima pembejeo na vifaa vingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nikienda kwenye zao la tumbaku, *consulatation* inafanyika kwa utaratibu... *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilichouliza Mheshimiwa Hussein Bashe, Bodi za Mazao ziko nyingi ni Bodi gani? Kwa sababu kumbuka Bodi ya Serikali Mwenyekiti anateuliwa na Rais, Wajumbe wanateuliwa na Waziri, unanielewa? Sasa Bodi gani nyingine ambayo inapatikana katika utaratibu huo halafu inakwenda kukaa na Serikali tena kugawa mapato? Swali dogo tu, mkituambia labda ni Bodi fulani inafanya hivyo, basi tunaendelea.

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mazao yote yana Bodi zake na mazao yote yana mikutano ya wadau. Yanajadili pembejeo zinapatikana vipi, kwa gharama zipi, lakini yanakaa kila mwaka kupanga bei na wanapopanga bei na mambo mengine yote yanakuwepo. Sasa namuomba tu Waziri wa Fedha na *Attorney General...*

**MWENYEKITI:** Mwenyekiti, nilichouliza mimi ni bodi ipi? Sijauliza wadau wapi, lakini basi Mheshimiwa Waziri endelea.

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa *AG* hebu aone kwa mujibu wa Sheria ya *Cashewnut Industry.* Kwa sababu kwa maana ya Kamati hatujataja viwango na tumependekeza kwamba kwa sababu Wizara iko *center,* wanavyonunua hizo pembejeo kule chini Wizara zinakwendaje, zinagawanywaje? Ni lazima wataihitaji Bodi ya Korosho watake wasitake na Vyama Vikuu vya Ushirika. Wakati wa *marketing* wataiihitaji Bodi, hata kutoa korosho kusafirisha nje hazipiti *TRA* kama hazina kibali cha Bodi ya Korosho. Kwa hiyo, kwa maana ya Serikali na Bodi ukiacha Mwenyekiti na Wajumbe, *the rest* ni watumishi wa Serikali chini ya Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namwomba *AG* na Waziri wa Kilimo, nadhani wana uwezo wa kulimaliza hili kwa njia ambayo, kwa sababu mimi siyo Mwanasheria, mimi ni Mchumi na nina uzoefu wa zao hili, lakini Mwanasheria sasa atumie utaalamu wake wa kisheria kuliweka vizuri hili hapa ambapo tumependekeza.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Sasa maana yake umeshamuachia Mwanasheria, usimpinge tena baadaye.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tuanze na *principle* ya ukusanyaji wa fedha hizo. Sheria ya Korosho kama ilivyorekebishwa na Sheria ya Fedha 2010 inaikabidhi *TRA* kazi ya kukusanya fedha hizo. Naomba nisome sasa baada ya *TRA* kukusanya kinatokea nini:

*"All revenue collected by or payable to the authority under this Act, including now the export levy, shall be credited to the Exchequer Account on a weekly basis and be payable to the Consolidated Fund"*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo hakuna mwanya wa kuipeleka kwa Bodi inapokusanywa. Inakwenda kwenye *Consolidated Fund* na nimesema hata Katiba Ibara ya 135

(1) nayo inasema fedha hizo ziende *Consolidated Fund.* Hatuwezi tukatunga sheria sasa ya kusema zikifika *Consolidated Fund* lazima tena zigawanywe kwa *portion* hii na hii, hapana! Kwa sababu hiyo itaingia katika mipango ya Wizara ya Kilimo na zitafika huko chini kupitia mipango ya Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Watoa hoja, Kamati.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mimi nisome kama tulivyopendekeza kwa maandishi.

**MWENYEKITI:** Mbona mnaturudisha nyuma tena?

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, alivyosema Mheshimiwa *AG* yuko sahihi kabisa.

**MWENYEKITI:** Sasa kama yuko sahihi, nini tena?

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wala huko hatujakataa, ila kwenye *section* (2), kwenye ile *framework* ambayo tumependekeza iwepo, kwamba namna zile pesa zikishaletwa kwa kupitia Wizara ya Kilimo kuja kwenye Bodi itakavyoenda kufanya kazi huko chini. Ndiyo tumependekeza hiyo *total amount of export levy collected under section (1) shall be apportioned* kupitia...

**MWENYEKITI:** Si ndiyo amejibu hapa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwamba hatuwezi kwenda mbali kiasi hicho, hamkumsikiliza vizuri?

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumemsikiliza. Kwenye (b) yake tunasema kwenye upande wa Bodi, ikishaletwa kwenye Bodi, mpaka walete kwenye Bodi si jukumu lao, lakini ikishakuja kwenye bodi tunasema

*money apportioned to the board shall have due regards to the following requirements;* ndiyo tumetaja:-

*(a) research necessary for development of the cashewnut industry;*

*(b) training and capacity building;*

*(c) marketing information; and*

*(d) industrial development aimed at cashewnut crop processing and agricultural inputs required for the industry.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yaani kwa upande wa bodi sasa ndiyo tumeweka (b) yake. Ndiyo tulivyopendekeza.

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, mna-*assume* bodi itakuwa inapewa hela tu wanatumia wanavyotaka wao?

Mheshimiwa Zitto.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kila bodi ya mazao kwa sheria zote, Sheria ya Chai, Sheria ya Pamba, Sheria ya Kahawa, Sheria ya Tumbaku, inapewa *power* ya ku-*raise* mapato, sheria zote. Nashangaa sana kwa nini Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa mara nyingine tena ame-*mislead* Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *rule* iliyotangazwa mwaka 1996 ilitokana na Sheria ya zamani ya Korosho ambayo iliipa Bodi ya Korosho *power* ya kukusanya hiyo *export levy.* Pendekezo ambalo Kamati inatoa ni pendekezo ambalo linaturudisha kwenye *powers* za Bodi ya Korosho kama zilivyo bodi zingine zozote zile hapa nchini kwa ajili ya ku-*raise revenue. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nisisitize tena, ni muhimu sana tuheshimu Katiba yetu. Ibara ya 136(1) ya Katiba, inazungumzia fedha ambazo haziendi Mfuko wa Mkuu wa Serikali kwa ajili ya matumizi maalum, siyo kweli

kwamba kila fedha inayokusanywa na *TRA* inakwenda Mfuko Mkuu wa Serikali. Fedha ya *VETA* inayokusanywa na *TRA* haiendi Mfuko Mkuu wa Serikali inaenda kwenye *account* ya *VETA* Benki Kuu; *wharfage* inayokusanywa na *TRA* kwa ajili ya Mamlaka ya Mapato Tanzania inaenda kwenye *account* ya *TPA* Benki Kuu; fedha ambayo tunakusanya hapa ya *fuel levy* na tutakuja kujadili tena hapa baadaye, haipelekwi Mfuko Mkuu wa Serikali *(Consolidated Fund),* inapelekwa kwenye *account* ya Benki Kuu ya *TANROADS* au sasa hivi itakuwa *TARURA* na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sielewi ni kwanini, kwa maksudi kabisa tunaamua kuikanyaga Katiba. Katiba imetenganisha mifuko, Katiba imeweka Mfuko Mkuu ambao ndiyo hizi hela tunazopitisha hapa na Katiba imeweka mifuko mingine iliyoundwa. Hoja ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na hoja yako asubuhi, hii *Cashewnut Trust Fund* haipo kisheria, Bodi ya Korosho ipo kisheria, ndiyo mapendekezo ambayo Kamati inayatoa, haya mapendekezo ni *compromise, is a win-win situation, at the end of the day, the amount of money going to cashewnut will be determined* na Serikali yenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nadhani sijui sitaki kutumia lugha mbaya kwa sababu yako. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** *Actually* umepiga kelele wala hatujakuelewa unasema nini! Tumeona umekasirika tu sijui unataka useme maneno gani tena ya ajabu ajabu Shekhe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mbunge, ukipewa nafasi ya kujenga hoja, jenga hoja tu usipandishe jazba kwa sababu haisaidii. Hapa tunajaribu kujenga mifumo ambayo inafafana kwa nchi nzima. Hatutengenezi *special babies* hapa, ndiyo ule ubaguzi aliokuwa anausema rafiki yangu Mheshimiwa Mchengerwa asubuhi kwamba kuna ubaguzi na ubaguzi. Kwa hiyo, hatuwezi kukaa hapa kutengeneza ubaguzi, tunatengeneza mifumo ambayo kesho na keshokutwa *Administrator* yeyote unapofanya uamuzi uwe tayari na

kesho kufanya uamuzi kama ule ule katika mazingira yanayofafana na yale yale. Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, anachozungumza Mheshimiwa Kabwe Zitto Mifuko kama ya *VETA* na kadhalika inaitwa *Special Funds* na ziko *provided* vizuri Ibara ya 135(2) ndogo ya Katiba. Hizo *special funds* ni lazima ama ziwe zimeanzishwa kwa sheria maalumu ilitungwa na Bunge au kwa *order* ya Waziri wa Fedha kwa kufuata Kifungu cha 12 cha Sheria ya Fedha za Umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Kabwe Zitto *actually* ndiyo anaepotosha anaposema Bodi imeanzishwa kisheria lakini Bodi haijaanzishwa kama Mfuko Maalum kisheria. Bodi ni Bodi tu, Bodi siyo Mfuko Maalum kwa minajili ya ile Kifungu kidogo cha (2) cha Ibara 135 ya Katiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Unajua tatizo la Mheshimiwa Kabwe Zitto hajajua kama Mwanasheria Mkuu wa Serikali safari hii anaijua kazi yake. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Waziri Mkuu, tafadhali.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, nawasihi Waheshimiwa Wabunge kwanza tuamini kwamba maelezo ya Mwanasheria Mkuu ndiyo maelezo ambayo tunalenga tuhudumie mazao yetu yote kwa mfumo huo bila ya kuwa na *double standard*. Natambua sana kwamba kila zao linahitaji maendeleo zaidi, zao la korosho pia linahitaji maendeleo zaidi, Wabunge wameeleza vizuri katika kipindi chote na wamechangia vizuri na mawazo yao yamechukuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mwanasheria Mkuu amejaribu kufafanua utaratibu ambao utasaidia na Mheshimiwa Waziri wa Kilimo ameeleza namna ambavyo

sasa iko *committed* kuhakikisha kwamba mazao haya yanafanikiwa. Napenda sana niwashawishi na nieleze tu Waheshimiwa Wabunge kwamba tukubali kama ambavyo Mwanasheria ametuongoza ili sasa Serikali ichukue *commitment* ya kuhakikisha kwamba kila zao tunalipa nafasi ya kulihudumia kutokana na mahitaji halisi ya zao hilo na wale wote ambao tumewapa *commitment* ya kusimamia mazao haya tutawasimamia ili waweze kuwajibika kikamilifu, tutahakikisha kwamba kila zao linahudumiwa kuanzia kilimo chake, pembejeo zake, mpaka masoko yake, kama ambavyo tumeweza kufanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna mahali ambako tunaweza tukaacha zao likiharibika, Serikali ikaridhika wakulima wanahangaika bila kuwa na hatua thabiti ya kuhakikisha kwamba zao hilo linahudumiwa na wakulima wanapata huduma stahiki ili tuweze kupanua wigo wa mazao haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnajua wote kwamba Serikali katika awamu hii tumejizatiti zaidi kwenye viwanda na katika kudhatiti viwanda kilimo ndiyo hasa kitakachoweza kuendesha viwanda. Kwa hiyo dhamira yetu ni ya dhati na nawasihi sana tuendelee kumuunga mkono Mwanasheria Mkuu wa Serikali na maelezo ya Waziri wa Kilimo kama ambavyo pia Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti amekuwa akitaka pia Wizara iwajibike kwa mazao haya yote ili tuweze kupata mafanikio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 13

*(Ibara iliyotajwa hapo ilipitishwa na Kamati ya Bunge zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 14

**MWENYEKITI:** Ibara ya 14, Kamati.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Kifungu Na. 14 Kamati inapendekeza kwenye ile *fourth schedule* tu-*amend* kwenye *heading* 20.09 *imported fruits juices* kutoka shilingi 221.00 *per litre* kwenda shilingi 271.00 *per litre*. Hii itaongeza Sh.50 kwa kila lita ya juisi ambayo inatoka nje ya nchi ambapo sehemu kubwa ndiyo inayotumika kuagiza *concentrates* ambazo zinakuja kutengeneza juisi ambayo tunakunywa humu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia juisi hizi tukiziongeza bei ya Sh.50 itaongeza mapato ya Serikali kwa sehemu kubwa na huko nyuma pia tulishawahi kuitoa kuanzia Sh.8 kuja Sh.58 kuja Sh.128 pia kufikia mpaka Sh.221 na bado hizo juisi zinaagizwa kwa sehemu kubwa kutoka nje ya nchi na inafanya juisi zinazozalishwa ndani ya nchi ambazo zinazalishwa kutokana matunda ndani ya nchi zisishike kasi kabisa. Kwa hiyo tumependekeza tuongeze Sh.50 hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwenye jedwali hilo hilo tumependekeza pombe kali ambayo inatoka nje ya nchi *spirits* yenye HS. *code* ambazo tumeweka kwenye *schedule* pia zipande kwa Sh.500 kwa lita badala ya ile iliyopendekezwa na Serikali. Vilevile tunapendekeza kwenye HS. 2208 kwa *spirit* inayotengenezwa ndani ya nchi kutokana na zabibu au mchuzi wa zabibu ambao unazalishwa Dodoma peke yake iweze kushuka ichajiwe kwa Sh.450 kwa lita, ili kilimo cha zabibu kiweze kukua. Pia viwanda ambavyo vitatengeneza pombe kali kutokana zabibu viweze kushindana kwenye soko dhidi ya pombe kali inayotoka nje ya nchi na pombe zingine ambazo zinatengenezwa kutokana na aina nyingine, kwa mfano miwa kwa sababu ile inayotengenezwa na miwa kutokana na *molasses* ni *by-product* ndiyo inaenda kutengeneza hiyo pombe, lakini hii ya zabibu hakuna *by-product* ni moja kwa moja zao linaenda kusindikwa ili iweze kutoa mchuzi

na ili iweze kusindikwa kwa kutoa hiyo *spirit* yaani pombe kali ambayo inatengenezwa hapa Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo ili kulinda sekta nzima hii ya zabibu tunaomba Serikali itukubalie iwe Sh.450 na tayari hapo tumeshawaongezea Sh.500 kwa pombe zote kali inayotoka nje ya nchi ili kulinda viwanda vya ndani. Viwanda hivi tusiangalie tu faida ambayo inapatikana kutokana na mapato ya kiwanda kimoja, tuangalie faida itakayopatikana kwa ujumla kwenye sekta nzima hii ya mvinyo na leo hii ni tatizo ni kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo naomba Serikali itukubalie kwa mapato haya tumeshawaongezea sana kutoka huko.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa. Sasa rafiki zangu wa Kamati ya Bajeti haya mambo ninyi huko hamkuyajadili?

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeyajadili hatukuafikiana.

**MWENYEKITI:** Mbona mnatuletea tena mambo yenu ya huko, mnatuletea hapa?

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumejadili lakini hatukuafikiana na hii siyo mara ya kwanza naileta, huu ni mwaka wa nne naleta hili jedwali hapa na iko kwenye *Hansard* kila mwaka tunajitahidi na hata hii ya juzi tumetoa kuanzia Sh.8 mpaka kufikia Sh.221 na hakuna mahali tumeathirika. Kwa hiyo, lengo ni kuongeza mapato ya Serikali na hii ya ndani tupunguze ili tulinde viwanda vya ndani na wakulima wa ndani. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Kwa sababu ni vema tukaelewana *actually* Kamati zote, wala siyo hii Kamati ya Bajeti peke yake. *Amendments* za Kamati zinapaswa kuwa chache iwezekanavyo, unatuletea mambo mawili matatu, moja ya msingi kabisa, yale mengine si mnaendelea tu huko kubishana

na kufanya nini mnaendelea tu. Ninyi mnataka kwa mwaka mmoja m-*solve* yote, mnaendelea huko, ndiyo maana Kamati zinaendelea. Kamati hazimalizi muda wake kwa sababu yapo mambo ya kuendelea nayo kila kukicha.

Waheshimiwa Wabunge, sasa kama kila jambo ambalo hamjafikia muafaka mnalileta kwenye Kamati ya Bunge Zima *actually* mnaligeuza Bunge lote hili kuwa Kamati ya Bajeti, kitu ambacho siyo sawa. Wabunge hawa mnawaonea kabisa mambo kama haya, haya mnapaswa tu mwendelee tu kuwa mnajadiliana huko mpaka mtakapofika mahali pa kuelewana.

Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba tena Waheshimiwa Wabunge na Kamati ya Bajeti watukubalie tu mapendekezo ya Serikali. Kwa sababu kuna msingi, nikizungumzia ile kuongeza tozo kwenye ile juisi, msingi wake ni kwamba tuliamua tuvisaidie viwanda vya ndani ndiyo vilivyo vingi tulibakiza hatukupandisha *excise duty* vya nje tuliamua tuongeze *excise duty* lakini siyo *arbitrarily*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliongeza kwa mfumuko wa bei kwa kiwango cha asilimia tano, maana katika misingi ya kodi huwezi tu kuongeza bila kuwa na msingi ambao unazingatiwa, vinginevyo tutakuwa tunauvunja na huzuii viwanda vingine kulalamika kwa nini mimi unanipandishia kiasi hiki wakati wengine ume-*apply a uniform rate*. Hilo jambo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, wakati najaribu kuhitimisha hapa nimejitahidi kueleza jitihada ambazo tunataka tufanye kuhusiana na mchuzi unaotokana na zabibu zinazouzwa hapa nchini. Kitu cha msingi nilichosema ni kwamba ndani ya muda mfupi tunataka tukae tena na hiki kiwanda husika tuangalie ule utaratibu ambao tulitumia wakati ule wa kutoa *GN* ili

wasamehewe, *excise duty* lakini tukiwa tumewekeana makubaliano na hayo inabidi yazingatiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nazidi kuwasihi tena Kamati ya Bajeti, tukishawekeana vigezo na kampuni husika tutakwenda vizuri na bahati nzuri nami nimeshaanza kulima zabibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama huo ndiyo mpango wa Serikali, tunaipongeza Serikali na tunawakubalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

*(Ibara iliyotajwa hapo ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara 15

*(Ibara ziliyotajwa hapo zilipitishwa na Kamati ya Bunge zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara 16

*(Ibara iliyotajwa hapo ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara 17

**MWENYEKITI:** Kamati.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna-*withdraw* hiyo, marekebisho ya Serikali yaendelee.

*(Ibara iliyotajwa hapo ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 18
Ibara ya 19
Ibara ya 20
Ibara ya 21
Ibara ya 22

*(Ibara zilizotajwa hapo zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 23

*(Ibara iliyotajwa hapo ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 24

**MWENYEKITI:** Ibara ya 24 Kamati.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru kwa Serikali kwa kuleta *amendment* hii, nasi tulikuwa tunapendekeza kwa *amendment* ya Kamati kwamba tu-*delete paragraph* (a) na kuongeza *delete paragraph* (b) na *replace it with the following:-*

"(c) *a newly established entity, or any entity which has been in production for three years at the commencement of this Act, dealing in the manufacture of pharmaceutical for human or veterinary medicines, sanitary pads, agricultural input and implements or leather products or for preserving fishery products having a performance agreement with the Government of the United Republic of Tanzania shall be taxed at a reduced corporate rate of twenty percent for five consecutive years from the year of commencement of production.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo hapa Serikali ilileta viwanda tasnia mbili tu ya madawa *(pharmaceutical)* na ngozi. Sisi tumependekeza kwa sababu lengo ni kuhamasisha kilimo na kiwanda chochote pamoja na masuala ya uvuvi tulikuwa tunapendekeza, kwa sababu viwanda vikianzishwa

inachukua muda mpaka wapate faida kubwa. Kwa hiyo, hata kwa hivi viwanda vilivyopo ambavyo vinasuasua kama kwenye ngozi na hivi vingine ambavyo vilivyopo...

**T A A R I F A**

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hii Kamati ya Bajeti ni zaidi ya wiki mbili sasa wanarudi saa nane za usiku na wanakutana na watu wa Wizara ya Fedha. Sasa nashangaa badala ya watu binafsi au Wabunge binafsi kuleta mapendekezo ya kubadilisha wanaleta wao, sasa inakuwa faida yake ni nini hii Kamati ya Bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sioni faida yoyote ya Kamati ya Bajeti kusema kweli inatupotezea muda tu hapa. *(Kicheko)*

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Kessy akasome Kanuni.

**MWENYEKITI:** Si mnaona jamani Kamati ya Bajeti, ndiyo maana nikawaambia mngekuja na mambo mawili, matatu wala msingepata hiyo. Sasa inaelekea mmeshindwana na Serikali *almost everywhere,* sasa lazima kuna shida mahali, ndiyo Mheshimiwa malizia maelezo yako. *(Kicheko)*

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yote tunalenga kwa ajili ya viwanda vipya vinavyoanzishwa hapa nchini, kwa sera hii ya Serikali ya viwanda. Lengo hapa ni kutoa tu msamaha wa asilimia kumi kama walivyofanya kwenye madawa na ngozi na kuna viwanda ambavyo leo hii vinakaribia kuanza. Labda vimeanza kabla ya siku mbili kabla ya hiyo sheria kutungwa huoni kwamba itakuwa imemwacha nyuma na yule atakayeanza baada ya Julai Mosi atakuwa amenufaika, lengo ni kuchukua wale wote waingie kwenye mkumbo huo na hakuna mahali ambapo Serikali mapato yake yatateremka bali itaongeza nia ya Serikali kuhamasisha masuala ya viwanda.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa nani?

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Kuchauka.

**MWENYEKITI:** Haya Mheshimiwa Kuchauka.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe taarifa mwongeaji kwamba, kama ulivyosema kwamba kuna mashindano ya Kamati na Serikali lakini kwa mujibu wa Kanuni zetu, Kamati inafanya kazi kwa niaba ya Bunge zima. Kwa hiyo, mashindano haya ni mashindano ya Bunge na Serikali kwa maana ya kwamba Serikali haiheshimu maamuzi ya Bunge. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sidhani kama hilo ni kweli. Mambo mengi sana wamekubali na wamerekebisha. Sisi tulichokuwa tunasema maana wote tunajifunza, yaani kule kwenye Kamati mambo mengine moja moja wangegawana tu mtu mmoja mmoja akaleta hapa *amendment* kama yeye lakini yale ambayo wanasimama kama Kamati yanapaswa kuwa mawili, matatu. Kwa kawaida ukileta kweli *amendment* hizo chache na nzito Bunge litawaunga mkono, lakini mkileta mambo 20 mnakuwa *irrelevant* sasa. Maana yake sasa kila hatua ni ninyi, kila hatua ni ninyi inakuwa kidogo si nzuri.

Mheshimiwa Waziri ufafanuzi katika hayo yaliyosemwa.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mijadala yetu na kama wao wenyewe walivyokiri, tulijitahidi sana kuwa *flexible*, sana tu. Hizi *reforms* nadhani ni muhimu tukazipima kwa uzito wake. Kwa hiyo, tumeamua angalau tuanze na haya maeneo machache tuone *mileage* ambayo tunapata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaomba kwa sasa Bunge liridhie tubakie hapo halafu tunavyoendelea

mbele mwaka ujao wa fedha tuangalie kama tunaweza tukaongeza na maeneo mengine.

**MWENYEKITI:** Kamati?

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakubali.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, tunashukuru.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ib.ara ya 25

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 26
Ibara ya 27
Ibara ya 28

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilifutwa)*

Ibara ya 29

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Kamati.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakubaliana na marekebisho yote ya Serikali.

Ibara ya 30

**HOJA YA KUTENGUA KANUNI ZA BUNGE**

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, kwa kazi iliyopo nikisema *guillotine* hapa kila mtu atanimeza. Kwa hiyo,

tunaomba kama Waheshimiwa Wabunge wako tayari utuongezee muda hadi hapo tutakapomaliza kazi hii. Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 153 na Kanuni ya 26(6), naomba nitoe hoja ili Bunge lako liridhie kazi hii iendelee kufanyika na Bunge lije kuahirishwa pale ambapo tutakuwa tumeshakamilisha kazi ambayo ipo mezani kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Bunge liliridhia kuongeza muda mpaka litakapokamilisha shughuli zake)*

**MWENYEKITI:** Hoja imeungwa mkono na walioafiki wameshinda. Ipo siku nitasema wasioafiki wameshinda halafu itakuwa tabu hapa. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru sana, naomba basi wote tusiondoke ili tumalize jambo hili.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, kifungu cha 30 kinafutwa kwa mapendekezo ya Serikali na mapendekezo ya Kamati.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilifutwa)*

Ibara ya 31

**MWENYEKITI:** Kuna marekebisho ya Serikali, Kamati na Mheshimiwa Gekul, ni kweli una marekebisho hapa? Haya tuanze na Kamati.

**MHE. JITU V. SONI:** Tunakubali mapendekezo ya Serikali.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Gekul.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi langu ni moja katika Kifungu namba 31, kwenye 33A.-(1)(c), niongezee neno *"private". Inasomeka* hivi *"Government institution or private organisation use".* Mengine nakubaliana na marekebisho ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la ku-*insert* neno *"private"* ni kujumuisha shule na hospitali ambazo ni binafsi siyo lazima za kidini, ni za watu binafsi waweze kusamehewa pia hili ili angalau zile tozo ambazo wamekuwa wakililia muda mrefu zipungue na wazazi tuweze ku-*afford* au wananchi tuweze ku-*afford* huduma ambazo wanazitoa. Lengo ni jema naamini Waziri atapokea. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Ashatu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemsikia Mheshimiwa Gekul amelisemea sana lakini nimwombe tu akubaliane na mapendekezo ya Serikali kwa sababu shule na hospitali hizi binafsi anazosema na kumekuwa na malalamiko ya wananchi kwamba pamoja na kupunguziwa baadhi ya tozo ambazo Bunge lako limepitisha mwaka jana bado bei iko juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niombe tu kusema kwamba hao wanafanya biashara, wanatoa huduma sawa lakini ni huduma kwa misingi ya kibiashara. Kwa hiyo, nimuombe tu ibaki kama mapendekezo ya Serikali yalivyo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Gekul.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wanafanya biashara lakini kama tuliwasikiliza katika Bunge hili hao wadau hasa wa shule binafsi wamekuwa *very honesty* kwamba *fine,* mnataka watoto hawa wafaulu lakini pia wakati huo sisi tutoze *reasonable* ada wakati huo tuna tozo hizi wameziorodhesha, wanazifahamu ni nyingi. Mimi sioni tatizo, kama mkiwapunguzia hili na wote wako kwenye *industry* moja hiyo, Serikali mnapata shida gani? Kama kwenye *Central Government* mmetoa, kwenye *Local Government* mmetoa na kwenye *religious institutions* mmeondoa. Hawa watu ambao wamejitahidi na ni wawekezaji katika nchi yetu, mnashindwa kweli kutoa tozo hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali itafakari upya.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo ya Mheshimiwa Mbunge ni kuongeza neno *“private”* lakini katika *formulation* ya kifungu hiki limetumika neno, *“non-profit organizations”.* Hii ina-*cover* iwe *private*, iwe *public,* iwe nini, ni *non-profit organisations* ndiyo zimelengwa. Kwa hiyo, kama hiyo *private* iko kwenye *non-profit organisations* hakuna tatizo.

**MWENYEKITI:** Ahsante.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 32

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti...

**MWENYEKITI:** Nadhani hapo hakuna neno Mheshimiwa Gekul, hakuna tatizo.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 33

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 34

**MWENYEKITI:** Hapa kuna marekebisho ya Mheshimiwa Gekul, Serikali na Kamati pia. Kamati hamna hapo, ni Mheshimiwa Gekul peke yake.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya *TSA* kutokugusa *own source* maana yake sasa nimekubaliana na marekebisho ya Serikali.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 35

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 36

**MWENYEKITI:** Hapa kuna marekebisho ya Mheshimiwa Mollel, Mheshimiwa Gekul, Kamati na Serikali? Tunachukua muda kidogo kwa sababu Serikali ilileta marekebisho halafu tena wameyafuta yale marekebisho ndiyo maana tunaangalia hapa ili kuweka mambo vizuri. Labda Serikali mtuweke vizuri sasa hapa mlitaka nini, kwa sababu kuna *Schedule of Amendment* iliyokuja halafu na yenyewe mmeifuta tena. Mheshimiwa Jafo tafadhali, Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, tume-*submit* marekebisho ya Serikali ambayo yana-*amend* lile Jedwali la Marekebisho ya mwanzo katika kifungu hicho ambapo tumependekeza kwamba kui-*delete* na ibakie kama ile *original Bill* ilivyokuwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, inabakia kama *original Bill* ilivyo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA):** Ndiyo.

**MWENYEKITI:** Sawa. Sasa tunaanza na Mheshimiwa Komanya halafu Mheshimiwa Mollel.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naondoa *schedule* yangu kwa sababu Serikali imeshachukua mawazo yangu imeyafanyia marekebisho. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Amina Mollel.

**MHE. AMINA S. MOLLEL**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Samahani, kwanza naomba ufafanuzi vizuri kwa sababu bado hatujaelewa vizuri kuhusiana na hii sheria kwa sababu unasema kumeletwa mabadiliko na hayo mabadiliko bado hatujayaona tena, samahani kidogo kwa hilo.

**MWENYEKITI:** Wamefuta marekebisho yao imebakia kama ilivyo hiyo ulioyo nayo, imebakia kama ilivyo kwenye sheria.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama imebakia kama ilivyo kwenye Sheria ya 50 kwa 50 mimi naomba kwamba mabadiliko yangu ...

**MWENYEKITI:** Hivi ni hamsini kwa hamsini?

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu wanasema kwamba yamebaki jinsi yalivyo na mimi mapendekezo yangu ilikuwa kwamba, katika hiyo asilimia 50 kwa 50, kwanza liongezwe neno la *"Persons with disability"* kwa sababu ilikuwa inawazungumzia wanawake na vijana.

**MWENYEKITI:** Nafikiri Mheshimiwa Amina hebu kaa tu kidogo.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** *Yes.*

**MWENYEKITI:** Kwa sababu nilimsikia Waziri kama sikosei akiongelea habari ya 40, 40, 20 akawa kama vile amechukua mawazo yako, sikumbuki vizuri, wajaribu kutuweka sawa kidogo.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Ndiyo Mheshimiwa, kuna mchanganyiko hapa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati, tusaidie unasemaje?

**MHE. HAWA A. GHASIA - MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maelezo ya Mheshimiwa Jafo, ame-*withdraw* hiyo 40, 40, 20 ina maana arudi 50, 50 kama ilivyo kwenye sheria na sisi tunaunga mkono.

**MWENYEKITI:** Mnaunga mkono 50 kwa 50? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Waziri tusaidie, nilisikia ukitoa maelezo fulani.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa na *Bill* ambayo inazungumzia asilimia 50 kwa 50 yaani maana yake vijana asilimia 50 katika ule mgao wa *own source* na wanawake asilimia 50. Sasa katika *amendment* Jedwali la mwanzo ilikuwa ni kama asilimia 40, 40, 20 lakini kutokana na mgawanyiko wa mambo mbalimbali tuliyoyapata, kwa

mfano, kuna makundi mengine utakuta kundi la walemavu, kundi la wazee na juzi juzi hata Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii alikuja na hoja ya kwamba watu walioathirika na *HIV,* kwa hiyo, hili jambo lake ni pana sana. Ndiyo tukaona ni vyema tubakie katika ule utaratibu wa 50 kwa 50 lakini kwa Waraka tuliotoa ni kwamba katika mgawanyo huu watu wote ambao wana mahitaji maalum watakuwa *considered* katika makundi hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Amina halafu Mheshimiwa Gekul.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakataa mapendekezo ya Serikali. Tumekuwa tukijichanganya tunapozungumzia watu wenye ulemavu, naomba ninukuu Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Watu wenye Ulemavu unatafsiri nini au *definition* yake juu ya watu wenye ulemevu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Mkataba wa Watu wenye Ulemavu ambao ni wa Umoja wa Mataifa wa mwaka 2006 na Serikali ya Tanzania kwa sababu imeridhia mkataba huo na kutunga Sheria Na.9 ya mwaka 2010, nanukuu kama huo mkataba unavyosema, unasema kwamba:-

*“Persons with disabilities include those who have long-term physical, mental, intellectual or sensory impairments which in interaction with various barriers may hinder their full and effective participation in society on an equal basis with others”.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni kwa mujibu wa Sheria ya Umoja wa Mataifa inayozungumzia haki za watu wenye ulemavu. Kwa hiyo...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mollel, muda hauko upande wako jaribu kufanya *short*.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima iwe 40 kwa 40 na 20 kwa watu wenye ulemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana wakati tunapitisha bajeti hapa, Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana wakati huo akiwa Mheshimiwa Simbachawene alizungumza dhahiri na kwa sababu ya mapendekezo ya Waheshimiwa Wabunge kwa hiyo akaichukua moja kwa moja na kuzitaka Halmashauri zetu zitoe asilimia mbili kwa watu wenye ulemavu. Baada ya hapo TAMISEMI ilituma Waraka katika Halmashauri zetu na tayari hizi Halmashauri zilikwishaanza kugawa hizo asilimia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sikubaliani na mapendekezo ya Serikali, naomba kutoa hoja Waheshimiwa Wabunge waniunge mkono ili hii asilimia mbili iende kwa ajili ya watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa hoja, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nimewaona Waheshimiwa. Mheshimiwa Gekul, maana ni eneo hilo hilo si ndiyo?

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** *Yeah*

**MWENYEKITI:** Ndiyo, ahsante.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba nichangie kwa namna hii. Maana yake sasa tumerudi kwenye *Bill* hii ya Mheshimiwa Waziri kwamba hata ile riba imefutwa ambayo walikuwa wameridhia ya asilimia mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mantiki hiyo, naomba nipendekeze. Napendekeza hizi asilimia kwanza ziwe 3, 3, 2, 2 kwa sababu zifuatazo. Asilimia tatu iwe ni vijana, asilimia tatu iwe ni akinamama, asilimia mbili iwe ni walemavu na asilimia nyingine mbili iwe ni wazee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu zifuatazo. Kwanza suala la asilimia mbili la walemavu lilishaletwa kwa mwongozo kwenye Halmashauri zetu na ombi ambalo limekuwa likizungumzwa...

**TAARIFA**

**MHE. AMINA S. MOLLEL**: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Gekul pokea taarifa.

**MHE. AMINA S. MOLLEL**: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tusiingize mambo ambayo hayapo katika mkataba ambao Tanzania imeridhia mkataba huo unaoelezea watu wenye ulemavu. Naomba katika hili tumuogope Mungu, tulishakubali asilimia nne kwa wanawake, asilimia nne kwa vijana na asilimia mbili kwa watu wenye ulemevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi leo hii wazee tunawawekaje katika hii biashara?

**MWENYEKITI:** Kuwa na uvumilivu Mheshimiwa Amina Mollel. Mheshimiwa Gekul.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Hamna, inaumiza.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Gekul, wakisema wanawake maana yake na wanawake wazee wamo.

**WABUNGE FULANI:** *Yes*.

**MWENYEKITI:** Yaani iko hivyo. Hakuna mahali imesema wanawake vijana.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri nikasikilizwa kwa sababu nina *amendment* yangu mezani, naomba nisikilizwe.

**MWENYEKITI:** Lakini *amendment* yako siyo suala la ...

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nipe nafasi niseme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo hivi...

**MWENYEKITI:** Maana hili mtalikoroga mwisho wake watu watachoka. Hebu wewe hoja yako iwe kwa hao wazee peke yake maana ndiyo *difference*. *(Kicheko)*

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu iko hivi, suala la wazee wa jinsi ya (*ME*) hawako *covered* popote, wa jinsi ya (*KE*) wako *covered* kwenye...

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila utaratibu)*

**MHE.PAULINE P. GEKUL** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalize, naomba tu nimalize *with due respect*.

**MWENYEKITI:** Hebu taarifa ziacheni, twende na muda.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** *Yes*.

**MWENYEKITI:** Haya twende.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, iko hivi wazee wetu wa jinsi ya kiume hawako *covered* kwenye kifungu hiki kwa sababu akinamama wazee wako *covered* kwenye asilimia ya akinamama. Ndiyo maana nasema Mheshimiwa Waziri Jafo alituambia subirini tutaingiza kwenye sheria wakati wa bajeti na ndiyo hii imekuja. Tumeleta *amendment* hii kwa sababu vijana wanapata, akinamama wanapata na walemavu tulishaanza kutoa. Halmashauri ya Mji wa Babati inafanya vizuri kwenye Mkoa wa Manyara, tunasimamia hiki kifungu kila siku unafahamu hiki kifungu kinatolewaje, vijana wanapata, akinamama wanapata, walemavu tumetoa juzi sisi milioni 100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachopendekeza hiki kifungu ki-*cover* wazee ila iwe *revolving,* iwe na akaunti yake peke yake. Wakati huo huo, hizi fedha zikitolewa kwa wakati na wazee wakipata kelele zitaisha, kwa hiyo, naomba ikubaliwe.

**MWENYEKITI:** Yaani tukifika mahali hapa Mheshimiwa Gekul ni lazima mtu uwe *specific.* Maana hapa unafungua mambo mengi iwe na akaunti *specific,* watu walishatoka kwenye hizo akaunti *specific,* siku hizi hata kama ni Halmashauri wana akaunti kadhaa chache na ni hizo hizo. Kwa hiyo, unafungua *a lot of* windows, wewe ungesimamia neno lako hasa ni nini? Nafikiri neno lako ni wazee na kama neno hilo ni wazee, ujumbe umeshafika tuachie wengine nao wajadili.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nihitimishe kwamba, neno langu ni iwe na *ratio* ya 3:3:2:2 kwa maana ya wanawake, vijana, walemavu na wazee na Bunge liridhie.

**T A A R I F A**

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Martha Umbula, nilikuona ulisimama.

**MHE. MARTHA J. UMBULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nilikuwa nataka kuwapa taarifa mwenzangu kwamba, nadhani hizi fedha hazitolewi kama zawadi. Fedha hizi zinatolewa kama mikopo na vilevile inaweza kuwa ni ya hiyari anayepewa apokee au asipokee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nashauri kwamba, nadhani wazee, watu wenye ulemavu, vijana, wanawake ni sehemu ya jamii nzima ya Watanzania. Kwa hivyo, wale wote watakaopokea mikopo hiyo hawatabaguliwa katika misingi ya *disability*, wala misingi ya kuwa ni mzee bali ni katika misingi ya *ability* ya kufanya biashara na kurejesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kueleza hivyo.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** *After all* ninyi wenyewe ndio Madiwani.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, inawabagua.

**MWENYEKITI:** Mnaoenda kukaa kwenye vikao vya kuamua nani apewe na hela hii ni mkopo. Hao wazee si wake zao watakopa, sasa kuna shida gani si watakuwa wamepata? Zaidi mnaoamua ni ninyi wenyewe Madiwani. Sasa mkitaka kazi hiyo iwe ya Bunge *are you being fair* wakati hii kazi ni ya kwenu ninyi? Hapa ni asilimia tu inayogomba.

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Silinde kwa kifupi.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Wazo la awali la Kamati lilikuwa ni *ratio ya* 4:4:2 ambapo Wizara ya Fedha ilipokuja kwenye Kamati ya Bajeti ilikubali na *amendment* wakaleta ndani ya Bunge. Kwa nini tulikuwa tunataka wanawake asilimia 40, vijana asilimia 40 na walemavu asilimia 20? Sababu ilikuwa ni moja tu kwamba kundi la walemavu ni maalum, lakini la pili kwenye walemavu kuna wazee wa kiume namaanisha ambao wanakuwa hawaingii kwenye *category* ya vijana au wanawake na ni walemavu lakini hawana uwezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tulipoongea hii hoja Serikali ikawa imekubali. Cha ajabu sasa Serikali upande wa Wizara ya Fedha iliona mantiki, Serikali upande wa TAMISEMI haikuona mantiki, yaani ndani ya Serikali moja haikuona umuhimu wa kuwa na walemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana kama mngekubali kusikiliza maoni ya...

**MWENYEKITI:** Nashukuru sana Mheshimiwa David. Serikali mlishakubali na mkaleta na *amendment* ya 40,40,20. Swali langu kwao, kwa nini wanaifuta tena hiyo *amendment*? Mnatusababishia tu mjadala ambao hauna sababu. Mbona hiyo 40,40,20 haina ugomvi yaani kuna nini? *(Makofi)*

Jamani hatuli muda bure tu maana *amendment* zote mbili tunazo hapa ya 40,40,20 na ya 50,50, kwa hiyo hapa ni hesabu tu ndiyo inayogomba, basi. Tukiwachukua na walemavu tukawaonyesha kabisa, inaonesha ile *compassion* na kutambua jambo hili, mbona haina shida, mimi sioni tatizo. (*Makofi*)

Haya Mheshimiwa Jafo, hebu tuambie tatizo liko wapi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niseme sisi TAMISEMI naomba niwaambie ukweli, Mheshimiwa Amina Mollel na Wabunge wengine wanafahamu, katika Wizara ambayo kwa kiwango kikubwa chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, sisi TAMISEMI tumekuwa tukitoa kipaumbele zaidi kwa maelekezo ya Waziri Mkuu kwa suala zima la kuwahudumia walemavu. Mheshimiwa Mollel anafahamu hata juzi juzi katika Mikutano yote ya Walemavu mpaka kule Simiyu ni sisi tuliokaa kujadili kwa kina ni kwa jinsi gani tunaweza kuwasaidia walemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumze wazi, ndiyo maana hata katika maelekezo hivi sasa, Mheshimiwa Gekul pale ni shahidi, Halmashauri zote hivi sasa hata ule mgao makundi ya watu wenye ulemavu ni *inclusive*. Tuelewe makundi haya ya vijana na akinamama walemavu nao wapo ndani yake kwa maelekezo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika *analysis* tuliyofanya sasa hivi walemavu hao idadi yake, kwa mfano, kuna

Halmashauri nyingine walemavu ni wachache kuliko watu ambao siyo walemavu. Hilo ni eneo la moja na Halmashauri zingine walemavu ni wengi.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila utaratibu)*

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa Jafo, nikushauri tu Mheshimiwa Waziri, unapoingia kujadili mambo haya yanayohusu makundi maalum yaani ni mambo ambayo ni *very delicate*. Ukijadili mambo yanayohusu wanawake na walemavu, makundi kama hayo ni *very delicate,* ndiyo maana nilikuwa nawaepushia shari kwa kusema mbona 40,40,20 haina ugomvi, haina shida? Mturahisishie tu, msiwafanye akina Mheshimiwa Amina Mollel wakatoka hapa, unamwona amesimama masaa yote haya, unataka walie humu ndani jamani? Mheshimiwa Stella jamani hebu tusiingie huko.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kidogo tu, kwa nia njema.

**MWENYEKITI:** Haya, haya, haya.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unafahamu kabisa mimi ninao watoto wenye ulemavu, kwa hiyo, anapozunguzwa mtu mwenye ulemavu unafahamu inanigusa vipi, hata Mheshimiwa Amina Mollel anafahamu. Nadhani lengo limekaa katika sura hii, kwamba katika Halmashauri zetu mgawanyo wa fedha zinazoweza kupatikana zinaweza zikawa ni nyingi. Kama utakuwa umesha-*specify* na wakati tunafahamu fika kundi hilo ni wachache, kwa hiyo, ina maana fedha zikae mwaka mzima, haziwezi kuwasaidia wengine wakati zingeweza kusaidia wengine?

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo ndilo mimi nadhani suala la msingi vinginevyo napenda mtu mwenye ulemavu apewe *priority* katika kupewa fedha hizo.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kusema kwamba tunakuwa na fungu lao pengine, tunaweza kuona ni hela ndogo lakini ni hela nyingi hiyo inakaa tu mwaka mzima. Huo ndiyo mtazamo wangu.

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila utaratibu)*

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nafasi dakika moja tu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Komanya, naona liligeuka hili, sijui unasemaje? Mwanzo nafikiri ulielewa ile 40,40,20 au ilikuwaje?

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niliamini 40,40 ambayo Mheshimiwa Waziri wa Fedha aliwasilisha katika ukurasa wa nane. Kama Serikali inasema kwamba walemavu watapewa vipaumbele bila jambo hili kuingizwa katika sheria tukumbuke kwamba kuna walemavu wanaume ambao hawaangukii kwenye *group* la umri wa vijana. Je, wale watasaidiwaje wakati hawako kisheria? Mimi nashauri twende na 4:4:2.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nafasi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Upendo Peneza nimekuona.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ni Mheshimiwa Upendo.

**MHE. UPENDO F. PENEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi hii. Niseme tu kwamba hata pendekezo alilokuwa amelileta Mheshimiwa Amina lilikuwa ni kwa ajili ya kuongeza neno *disability* kwa maana nzima ya huo mgawanyo. Hata hivyo, Serikali kwa maana ya kushirikiana na Kamati walileta pendekezo ambalo ni nzuri zaidi ambayo ni hiyo 40,40,20.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kwamba, kwa sababu bado hatujamaliza tunaweza tuka-*retain* ile lakini tuangalie kwenye kipengele cha (3), Serikali ilivyokuwa inasoma bajeti ilisema mikopo hii itakuwa haina *interest whatever* lakini ukiangalia kwenye marekebisho pia wameandika *loan issued under this section shall be charged two percent interest.* Kwa hiyo, kama tunakubali marekebisho haya ya Serikali tukubali kwa maana ya kile kipengele cha (2)(a),(b) lakini kipengele cha (3) ambacho kinasema *two percent* na tulishawambia wananchi itakuwa haina *interest* nadhani tutakuwa waongo.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nafasi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, jamani mtuvushe, hili jambo mbona siyo kubwa hivyo.

**MHE. KABWE Z.R. ZITTO:** Tupige kura.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona *concerns* za Waheshimiwa Wabunge na hasa kwa kuzingatia kwamba tunapozungumzia kundi hili la watu wenye ulemavu tunazungumzia kundi ambalo ni *very sensitive.*

**MBUNGE FULANI:** Maalum.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU):** Ndiyo maana yake hiyo, liko *sensitive* lakini ni kundi maalum. Hata hivyo, naomba Waheshimiwa Wabunge waone, nakubaliana na mwenendo wa hoja ya Mheshimiwa Amina lakini ili kuweka msingi ambao utasaidia utekelezaji wa sheria hii tunayoipitisha kwa sababu nitakazosema na kwa kuwa tuna kifungu cha (4) ambacho kinajieleza hapo wazi, naamini kwamba kitatusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha (4) kinasema:-

*"The Minister may, by regulations, prescribe the procedure for the management and distribution of such loans to registered groups of woman and youth".*

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda tunaweza kuongeza na hao wenye ulemavu kama anavyoisema Mheshimiwa Amina wote wakawa *inclusive.* Hiyo itatusaidia kwenye kifungu hiki ili kuondoa hiyo hofu inayojitokea. Hofu yenyewe ni moja tu, wenye ulemavu watapewa *priority* lakini Waziri itamsaidia kutengeneza mfumo pale ambapo ataona kwamba labda makundi ya wenye ulemavu hayako mengi, ataweza kutumia hizo *funds* pia kusaidia makundi ya watu wengine. Bila kufanya hivyo unaweza ukajikuta unakuwa na *funds* nyingi na makundi ni machache.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunapokubaliana na hii ya Mheshimiwa Amina lakini tuki-*insist* kwenye kifungu kile cha (4) tutapata *soft exit* nzuri tu. Wenye ulemavu watakuwa *considered* vilevile yale makundi mengine yatakuwa yamepata *priority* katika mazingira ambayo yanajitokeza.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA.** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nadhani hatutakuwa na shida kabisa na tutakuwa tumekwenda vizuri.

**MWENYEKITI:** Kwenye asilimia wewe unasemaje, Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mgao hata kama utabaki vile lakini kile kifungu cha (4) ni lazima tukipe nguvu ya kutengeneza mfumo mzuri.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapana.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo mzuri wa kusimamia hilo jambo lote.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mpina.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nafasi.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa nafasi. Hiki kinachozungumzwa, nataka kutoa *analysis* za kihasibu tu na hasa ndicho ambacho viongozi wengi hapa wamejaribu kukizungumza. Tukishaweka kwenye sheria kwamba ni 20%, ukienda kihasibu sasa Halmashauri za kawaida zinazokusanya mapato *own source* zinaenda mpaka kwenye shilingi bilioni tatu ambapo 10% yake ni shilingi milioni 300. Sasa shilingi milioni 300, kama umeshaweka kwenye sheria moja kwa moja kwamba una asilimia 20 ...

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, inaweza ikawa ndogo au kubwa sana. Halafu kwenye mgao ikitokea ile fedha katika eneo husika walemavu ni wachache na mahitaji ya fedha dhidi ya miradi yao ikawa midogo...

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA.** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Maana yake ile fedha haiwezi kutumika kwenye kundi la vijana wala akinamama kwa sasabu tayari umeshaiweka huku kwenye kundi la walemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tafsiri nzuri ni ile aliyoisema Waziri kwamba, tukishaweka kwamba makundi ya walemavu yatazingatiwa, kwa maana hiyo ni kwamba miradi ya walemavu itapewa kipaumbele katika mgao ule wa 50,50, ile ndiyo itakuwa *proper.*

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Kwa sababu *revenue* hizi, Halmashauri zingine zinapata mpaka shilingi bilioni 10. Kwa hiyo, fedha hizi itakuwa hazina mahali pa kuzipeleka ikitokea eneo hilo lina walemavu wachache.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nihitimishe hoja, ni-*compromise*.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Hebu msiwashe *microphone* bila kuwa nimewatambua, hiyo ni kuleta fujo tu. *(Makofi)*

Sikutarajia sana kwamba jambo hili litatuchukua muda kwa sababu hata uchukue Halmashauri hizo mbili, tatu zenye kufikisha shilingi bilioni tatu kwenye *own source* ambazo ni chache kweli, ukapata hiyo shilingi milioni 300, shilingi milioni 300 ni kitu gani katika mikopo? Hata mtu mmoja ukipewa shilingi milioni 300, *what is 300 million*? Sasa wanagawiwa Wilaya nzima, wanawake, vijana, walemavu, shilingi milioni 300, mbona ni hela ndogo sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Zitto, tutoe hapo bwana ulisimama.

**MHE. KABWE Z.R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, twende na *provision* ambayo Mheshimiwa Amina ameitoa. Mbele ya ile *provision* tutasema *provided that, the Minister will provide regulations* kwenye mazingira ambayo watu wenye ulemavu watakuwa ni wachache *or something like that.* Kile kifungu ambacho kinataja mgao kama anavyopendekeza Mheshimiwa Amina kiwepo halafu Mwanasheria Mkuu wa Serikali atutengenezee utaratibu wa Kanuni ili hizo hofu ambazo Serikali inazo zitaweza kuwa *provided for. (Makofi)*

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Amina sijakuruhusu bwana, kwa kweli lazima tufanye maamuzi, inabidi tupige kura.

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nina wazo.

**MWENYEKITI:** Sasa tuna *school of thought* mbili. Tuna wanaosema 50 kwa 50 ambalo ni pendekezo la Serikali na tuna wanaosema 40,40,20 pendekezo la Mheshimiwa Amina Mollel.

**MBUNGE FULANI:** Na Kamati pia.

**MWENYEKITI:** Sijui tunahoji vipi sasa. *(Kicheko)*

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi, niungane na Mheshimiwa Amina Mollel.

**MWENYEKITI:** Sasa niwahoji kuhusu pendekezo la Serikali la 50 kwa 50, wanaoafiki wasimame.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walisimama)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, naomba mkae.

Sasa wale wanaokubaliana na pendekezo la Mheshimiwa Amina Mollel la 40,40,20, wasimamie.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walisimama)*

**WABUNGE FULANI:** *(Makofi/Vigelegele)*

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, 40,40,20 imeshinda.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

Ibara ya 37

**MWENYEKITI:** Kifungu hiki kina Marekebisho ya Kamati, haya Kamati.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakubaliana na Serikali.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 38
Ibara ya 39
Ibara ya 40
Ibara ya 41
Ibara ya 42
Ibara ya 43
Ibara ya 44
Ibara ya 45
Ibara ya 46
Ibara ya 47

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilifutwa)*

Ibara ya 48
Ibara ya 49

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 50
Ibara ya 51
Ibara ya 52
Ibara ya 53

**MWENYEKITI:** Kamati.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakubaliana na mapendekezo ya Serikali.

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 54
Ibara ya 55

Ibara ya 56

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwambe bado una neno hapo 54. Wewe unafuta vifungu vyote vitatu, 54, 55 na 56.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ku-*withdraw* kwa sababu Serikali imefanya mabadiliko.

**MWENYEKITI:** Katibu, hebu sasa soma kimoja kimoja.

Ibara ya 54

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 55

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 56

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 57
Ibara ya 58

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa Mwambe, unavifuta vifungu hivi.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa MWenyekiti, ndiyo na vyenyewe nimevindoa pia.

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 59

**MWENYEKITI:** Kamati.

**MHE. HAWA A. GHASIA – MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakubaliana na marekebisho ya Serikali kwa sababu wamerudi pale ambapo sisi mwanzo tulipendekeza. Tulitaka iwe mwanzo Desemba lakini baada ya mashauriano wao wakasema Septemba na tukawakubalia, lakini tunashukuru wamerudi ileile miezi sita ambayo sisi tulipendekeza. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zitto na wewe asubuhi ulikuwa unasema hayo hayo, haya bwana.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 60

**MWENYEKITI:** Kamati.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi pendekezo letu ni ku-*reinstate* kifungu cha 60 kama kilivyokuwa kwenye *original Bill* ilivyokuwa imeletwa ambacho kilikuwa kinasema: *"The principal Act is amended in section 12 by adding immediately after subsection (1) the following proviso:*

*Provided that, this subsection shall not apply to amounts allocated to the fund from the Consolidated Fund and any other funds or moneys referred to under Article 135(2) of the Constitution".*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tunaomba hiki kiwe *reinstated* kwa ajili ya ku-*protect* zile *funds* na tuki-*refer* tumerekebisha Sheria ya BoT kwenye *voted* na *non-voted* ili kuweza ku-*maintain Constitutional demands*.

**MWENYEKITI:** Sijakuelewa Mheshimiwa Bashe kwa sababu Serikali hapa kwenye 60 haina *amendment* yoyote, iko kama unavyosema.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Ilifuta.

**MWENYEKITI:** Walifuta?

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** *Yes*.

**MWENYEKITI:** Kuna *amendment* ya kufuta?

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo.

**MWENYEKITI:** Hakuna.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, basi kama wameleta mpya *it is okay* lakini tuliyokuwa tumepokea jana usiku walikuwa wamefuta.

**MWENYEKITI:** Mezani kwangu hapa hakuna.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Kwa hiyo, *this is maintained,* basi ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 61
Ibara ya 62
Ibara ya 63
Ibara ya 64
Ibara ya 65
Ibara ya 66
Ibara ya 67
Ibara ya 68
Ibara ya 69

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 70
Ibara ya 71

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 72
Ibara ya 73
Ibara ya 74
Ibara ya 75
Ibara ya 76
Ibara ya 77
Ibara ya 78
Ibara ya 79

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara Mpya ya 80

**MWENYEKITI:** Kamati.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hii ya 80, *the Principal Act is amended in section* 48 *by adding a new subsection* (2) *as follows-*

"48.-(2) *Notwithstanding the provisions of subsection (1) of this section, where water, gas, oil, electricity or thermal energy is supplied through pipeline, cable or other continuous distribution network from a place in Mainland Tanzania and delivered to a place in Tanzania Zanzibar shall be treated as a supply made in Zanzibar*.

**MWENYEKITI:** Tulikuwa tumejichanganya Mheshimiwa Waziri yaani kabla ya 80 yenu, wao wanaingiza *new clause* ya 80, sijui kama mmeona. Nafikiri ndio hivyo Kamati?

**MHE. HAWA A. GHASIA – MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI:** Ndiyo.

**MWENYEKITI:** Nimeeleza vizuri kwamba hii ni *new clause* mnapendekeza kabla ya hiki kifungu cha 80 tulichonacho?

**MHE. HAWA A. GHASIA – MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI:** Ndiyo.

**MWENYEKITI:** Kama Mheshimiwa huna nakala tukupatie hii ya Mezani. Hebu rudia tena *justification* ya kuongeza *clause* hiyo. Kule nyuma kabisa, Mheshimiwa King.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Tumeweka hii kwa sababu umeme ambao unakwenda Zanzibar unachajiwa *VAT,* asilimia 18 hapa *origin* na ukifika kule kwa mtumiaji anachajiwa tena *VAT* asilimia 18, kwa hiyo mtumiaji anakuwa analipa amelipa *VAT* asilimia 36. Kuwepo kwa kifungu hiki kipya na kingine kilichokuwa *proposal* ambacho kitachofuata kitasababisha kulipa *VAT* asilimia 18 katika *destination* kama wananchi wangine wote wa Tanzania wanavyolipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilieleza katika maelezo yangu ya kuhitimisha hoja kwamba ushauri wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ni kwamba marekebisho haya yaje kupitia *Miscellaneous Amendment* na siyo kupitia *Finance Act* na nilieleza sababu. Kwa sababu yako mabadilko katika Sheria ya *VAT* yaliyofanyika mwaka 2016 na katika mabadilko hayo ndiyo inaonekana kwamba sasa huduma za umeme kwenda Zanzibar zinatozwa *VAT*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwanasheria Mkuu wa Serikali anashauri ipitie kwenye *Miscellaneous Amendment* kama nilivyosema kwa sababu hiyo itaipa nafasi kwanza Baraza la Mawaziri na Kamati ya Baraza kujadili ambapo wataketi Waziri wa Fedha, Waziri wa Nishati na pia

atakuwepo Waziri anayehusika na masuala ya Muungano kwa sababu humu ndani ya hili suala yamejificha masuala ya mahusiano ya Muungano. Tukitumia sheria hii kuyabadilisha haya yote hatutapata nafasi ya kuweza kuyafanyia kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa AG kama anachosema Mheshimiwa Ali King ni kweli kwamba wenzetu wanalipa kodi asilimia 36, kweli? *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni sahihi.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *point of information*.

**MWENYEKITI:** Ndio Mheshimiwa Bashe.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini sisi kama Kamati tumelichukua jambo hili, *as we speak* sasa hivi Shirika letu la Umeme (*TANESCO)* na Shirika la *ZECO* la Zanzibar, kuna *dispute* ya shilingi bilioni 36 iliyosababishwa na *increase* ya 18 *percent. ZECO* wanasema hivi sisi tunapochukua umeme kutoka *TANESCO* tunachajiwa asilimia 18 na *Value Added Tax* ni kodi inayoenda kuchajiwa kwa mlaji, *ZECO* sio mlaji. Kwa hiyo *ZECO* sasa ile asilimia 18 naye anai-*pass* kwa mwananchi na ana-*add another* 18 *percent.* Kwa hiyo, umeme anaoenda kutumia mlaji wa mwisho Zanzibar unakuwa *expensive. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliwashauri Serikali kwamba hili jambo siyo la kimuungano hatuwezi kuweka kwenye *list* ya kero za Muungano, ni jambo la *principle* za kibiashara. Tukawaambia haileti taswira nzuri *TANESCO* anafunga hesabu zake za mwisho wa mwaka anataja anamdai *ZECO figure* ambayo *at the end of the day* hawezi kuikusanya. Kwa hiyo, tukawashauri tuliondoe jambo hili ili kupunguza migogoro isiyokuwa na msingi na upande wetu wa pili wa Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya kwamba iletwe kwenye *Miscellaneous,* hili ni suala la *finance,* kwa nini haliwezi kuingia hapa? Kwa hiyo, Serikali ichukue busara ya jambo hili. *(Makofi)*

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbogo, hakuna cha taarifa kama unataka kusema wewe sema tu, nakupa nafasi, sasa taarifa utakuwa unampa nani?

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye *VAT* kuna kodi ya kwenye manunuzi na kodi ya kwenye mauzo. Endapo kama *ZECO* atakuwa ni *agent* wa *TRA* kwamba yuko *VAT registered* maana yake ni kwamba ile *VAT* anayoilipa wakati ananunua umeme anatakiwa aidai kama *import tax* na akija upande wa pili wakati anauza umeme kwa wateja ndiyo anachaji *VAT* kwenye mauzo kama *output tax.* Kwa hiyo, kunakuwa hakuna *double taxation* sana sana itatokea kama analipa nyingi huku upande wa *TANESCO* kama *import tax* ndipo siku zote atakuwa anaidai *TRA,* anakuwa na *negative* badala ya kupeleka kama *payable. (Makofi)*

**MWENYEKITI:** Rudia tena Mheshimiwa Mbogo, kwa kifupi sana, tumekusikia lakini hebu irudie tena hiyo.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano huko hivi kama *ZECO* amenunua umeme wa shilingi bilioni 10 na akachajiwa *VAT* 18 *percent,* kwa hiyo ata-*post* gharama yake ya shilingi bilioni 10 na *VAT* ya shilingi bilioni 1.8. Baada ya hapo akiuza labda ameuza kwa shilingi billioni 20 atakusanya *VAT* toka kwa wateja.

**MWENYEKITI:** Anapokuwa anauza kule anauzaje sasa?

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, anachukua bila *VAT* kwa sababu yeye anaidai *TRA.*

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila utaratibu)*

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Tulia.

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ikiwa *ZECO* yuko *VAT registered* anatakiwa aidai kama *import tax,* hatakiwi kuipelekwa kwa wateja.

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama *ZECO* yuko *VAT registered* hakuna *double taxation*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbogo hebu subiri kidogo, Mheshimiwa Waziri wa Nishati nimekuona umesimama.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niwashukuru Waheshimiwa Wajumbe kuchangia katika hoja hii muhimu. Nawashukuru sana pia Wajumbe na Wabunge kutoka Zanzibar katika suala hili kwani wamekuwa wavumilivu sana na wafuatiliaji wazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Zanzibar inanunua umeme kutoka Bara, Unguja tunawauzia megawati 60 na Pemba megawati 20 kama wanunuzi wa bei ya jumla. Kwa hiyo, wanaponunua umeme kwa bei ya *bulk* kwenda kupeleka Zanzibar kupitia Shirika la *ZECO* na nao wana utaratibu wao wa kusambaza umeme kule Zanzibar, hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, wanaponunua umeme, kutokana na tafsiri ya Sheria ya *VAT* ya mwaka 2016, *goods and services* kutoka Bara ziliondolewa *VAT.* Umeme kutoka Bara kwenda Zanzibar nao unatafsirika kama *goods and services*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja hapa ya msingi ni kwamba kama umeme nao ni *goods and services* kwa nini unatozwa *VAT* unapokwenda Zanzibar? Ndiyo hoja ya msingi. Kwa hiyo, hoja hapa ni suala la tafsiri. *TANESCO* au Bara tunasema kwamba, kwa sababu sheria haikusema umeme kama *goods and services* sisi tunasema umeme kwa Bara siyo sehemu ya *goods and services* unapokwenda Zanzibar, hiyo ni tafsiri ya kwanza. Tafsiri ya pili Zanzibar wanasema, *which is also true* kwamba, kama umeme nao ni *services* au *goods* haukutakiwa kutozwa *VAT.* Kwa hiyo, hapa kinachogomba tafsiri sahihi ni ipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sisi kama Serikali hatua ya kwanza tumemwomba Mwanasheria Mkuu wa Serikali atupatie tafsiri sahihi halafu Kamati tutashirikiana na Mwanasheria Mkuu wa Serikali kulitolea maelekezo au ushauri wa Kiserikali, hilo la kwanza. Naungana pia na Mwanasheria Mkuu wa Serikali kusema waendelee kulifanyia kazi zaidi kwa sababu kuna suala la tafsiri na suala la *consultation. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningesema kama Serikali tunatambua hili suala ni muhimu kweli kweli kwa watu wa Zanzibar, tena sana na hasa Mheshimiwa Saada alivyolifanyia kazi. Labda ushauri wetu sisi Serikali tulifanyie kazi kwa haraka ili liweze kupata mustakabali wa masuala ya Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, napenda kutoa masahihisho kidogo kwa Mheshimiwa Bashe, deni linalodaiwa kuhusu *VAT* ni shilingi bilioni 16.2 siyo shilingi bilioni 36, shilingi bilioni 36 ni deni lingine la *KVA* siyo la *VAT*. La tatu, niwapongeze Zanzibar kwa malipo ya madeni mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka tu kutoa ufafanunuzi kuhusu hilo, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chenge, nilikuona.

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana. Tuko katika hatua muhimu sana ya

kutunga sheria na mbele yako kuna hii *Schedule of Amendment* ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi kwa mujibu wa Sheria ya Ongezeko la Thamani, *supply* ya umeme ambayo ni huduma, Sheria ya *VAT* inatoa *zero rating* kwa bidhaa ambayo inaenda upande wa pili wa Muungano. Hata hivyo, kwa huduma, sheria ilivyokaa sasa hivi haitoi mwanya huo na sheria ya *VAT* siyo ya Muungano, kwa hiyo, ndiyo tatizo linaanzia hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili limekuwa la siku nyingi sana. Mimi nasema kwa upande wa Serikali unapopata *a good opportunity* kama ilivyo sasa hivi ya kulinyoosha suala hili, nadhani tungeliona katika faida ya Muungano wetu. Ndiyo maana mimi naliona kwa *spirit* hiyo ya kutozalisha kero nyingine ambayo haipaswi kuwa kero. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Saada Mkuya, nilikuona ulisimama.

**MHE. SAADA MKUYA SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Nami naunga mkono mapendekezo ya Kamati kutokana na *spirit* ile ile ambayo Mheshimiwa Chenge ameielezea. Hili jambo ni la siku nyingi sana toka mabadiliko ya Sheria ya *VAT* ya mwaka 2014. Hivi tunavyozungumza kila mwez bili ya umeme ambayo inakwenda Zanzibar kupitia *ZECO* inatozwa na *VAT.* Naye kwa sababu kuna gharama ambazo anazi-*incur during the way* kwa ajili ya kwenda kuu-*transform* umeme kwa *end user* na *principle* ya *VAT end user* ndiye ambaye analipa inabidi lazima atoe *VAT.* Kwa maana hiyo, Mheshimiwa Bashe nadhani alisema wanatozwa asilimia 36.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilimwomba sana Mheshimiwa Waziri wa Nishati, Mwanasheria Mkuu na Waziri wa Fedha, walitazame katika *context* hiyo. Hayo

majadiliano, mimi naona katika *plate* yetu ya majadiliano kuna *plate* imejaa na inamwagika. Hili ni moja katika kuwapunguzia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba hili likubalike kama vile Kamati wanavyopendekeza ili kuwe na *a very good and strong spirit* kwa ajili ya Muungano kwa sababu hili jambo linatozwa kabisa kinyume na utaratibu. Tunaiomba sana Serikali, hili siyo jambo la *Miscellaneous,* hili ni jambo la kwenye *Finance Bill. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wa Nishati ameeleza vizuri sana lakini katika maelezo yake akasema kuna *elements* za *consultation.* Hata Mheshimiwa Chenge alipokuwa anachangia, ameeleza pia kuna shida za kisheria hapa katika sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana kutoka mwanzo nilipendekeza kwamba itakuwa siyo sahihi kulitatua tatizo hili kwa kupitia *Finance Act.* Jambo hili linataka *process* ambayo itakuwa *more consultative,* iwahusishe wadau wengine wengi wanaohusika hapa ndiyo tunaweza tukapata muafaka. Hata hivyo, Waziri wa Nishati ameshaeleza kwamba hatua zilikwishaanza na sisi tutalichukua kwa *speed* inayotakiwa lakini hapa tukililazimisha kupitia kwenye *Finance Act...*

**MHE. MATTAR ALI SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Tutaibua tena matatizo mengine huko baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MHE. MATTAR ALI SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**T A A R I F A**

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa, nami nataka kutoa taarifa.

**MWENYEKITI:** Haya, Mheshimiwa Keissy, halafu Mwenyekiti wa Kamati.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tukitaka kutoa ubishi kabisa hapa, kwanza tujue *TANESCO* inawauzia umeme Zanzibar kwa bei gani? Maana hata sisi huku tunalipa *VAT.* Mimi Namanyele nikinunua umeme kuna *VAT.* Tujue inawauzia umeme Zanzibar kwa bei gani, ndiyo tujue!

**MHE. MATTAR ALI SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni juu ya Serikali ya Zanzibar kutoa *VAT* kule kwao lakini kutoa *VAT* huku haiwezekani maana na sisi huku tunalipa *VAT.* Mimi nikinunua umeme Namanyele, *unit* moja nanunua Sh.357. Zanzibar wanalipishwa *VAT* mara mbili *(double payment)* siyo mara mbili, tujue wanauziwa umeme wa jumla kwa bei gani, tujue kwanza, *unit* moja wanauziwa bei gani, ndiyo tujue!

**MHE. MATTAR ALI SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Naomba tusaidiane ili tuweze kuvuka vizuri. Mwenyekiti utafuatia baada ya Mheshimiwa Saed Kubenea.

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na mimi kunipa nafasi ya kuchangia kidogo. Nataka nifafanue, kwanza *ZECO* siyo Wakala wa *TANESCO, ZECO* ni Shirika la Umma la Zanzibar. Umeme

unaozungumziwa hapa hauzungumziwi umeme huu wa mtu mmoja mmoja, unazungumziwa umeme wa viwandani ambao ndiyo umeme Waziri anaozungumzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa umeme huo unapokwenda Zanzibar, *ZECO* inalazimika kuuza umeme kwenye makampuni makubwa kama hoteli za kitalii kwa bei ya juu. Kwa maana ya kwamba umeme unaouzwa viwandani Bara na *TANESCO* ndiyo bei hiyo hiyo wanayouziwa *ZECO* Zanzibar. Hiyo ndiyo hoja na umeme huo unatozwa kodi ya *VAT.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya msingi ni kwamba bei ya umeme inayopelekwa Zanzibar, kwanza ule mfumo wenyewe wa usafirishaji wa umeme Zanzibar imechangia, ni mfumo wa Muungano siyo mfumo wa *TANESCO* peke yake. Hili ni jambo ambalo linashirikisha nchi mbili zilizoungana katika Jamhuri ya Muungano.

**MHE. MATTAR ALI SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kuitoza Zanzibar *VAT* siyo sahihi hata kidogo. Ndiyo maana Waziri mwenyewe anakiri na Mheshimiwa Chenge ameeleza hapa kwamba hilo jambo la umeme siyo suala la Muungano.

**MHE. MATTAR ALI SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimsawazishe kidogo tu, taarifa hapa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mattar kwa nini hamuwi wavumilivu kumsikiliza mtu? Mimi nitawapa nafasi tu, *as long as* mko tayari kuendelea kubaki hapa wala haina shida.

**MHE. MATTAR ALI SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kitu kidogo nilikuwa nataka kukitengeneza cha Mheshimiwa Kubenea.

**MWENYEKITI:** Haya Mheshimiwa Mattar.

**MHE. MATTAR ALI SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpe taarifa Mheshimiwa kuwa mfumo uliotoa umeme kutoka Tanzania Bara kwenda Zanzibar ni mfumo ambao Serikali ya Mapinduzi imegharamia asilimia 100. Ni wa kwetu wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimpe taarifa ili aweze kuendelea vizuri na mchango wake.

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, naomba nimalizie tu dakika moja. Kwanza nimeipokea taarifa hiyo na naifahamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la msingi ni kwamba jambo hili limekuwa sehemu ya kero ya Muungano. Ni vizuri sana kama tunautakia mema Muungano huu tuondokane na jambo hili. Wabunge wa Zanzibar wameongea kwa hisia kali sana juu ya jambo hili. Wananchi wa Zanzibar wanaumia, leo hoteli za kitalii za Zanzibar hazitumii umeme wa *TANESCO* kwa kiwango kikubwa, wanalazimika kuwasha ma-*generator* kutokana na umeme wa *TANESCO* unaouzwa Zanzibar kuwa ghali. Umeme huu Bara wanapouza kwenye nchi nyingine wanauza bei rahisi zaidi kuliko wanavyouza Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ni hilo tu, nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mwenyekiti wa Kamati.

**MHE. HAWA A. GHASIA - MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niweke jambo moja sawa kama alivyokuwa anazungumza Mheshimiwa Mbogo na hata Mheshimiwa Keissy kwamba hata sisi huku Bara tunalipa *VAT.* Nataka nitoe ufafanuzi kwamba tozo ya *VAT* ni ya mlaji na pia *VAT* siyo kodi ya Muungano. Ina maana kama *ZECO* ingekuwa Tanzania Bara akinunua *TANESCO* kama yuko *VAT registered* halafu akaenda kuuza kwa wananchi, akawatoza *VAT,* ile aliyonunulia *TANESCO*

angerudishiwa na *TRA* kama ambavyo inavyofanyika huku. Sasa kwa sababu *VAT* siyo ya Muungano, *ZECO* akinunua umeme huku anailipa *TANESCO* ile *VAT* asilimia 18 inaenda *TRA* mali ya Tanzania Bara na akiuza kule kwa asilimia 18 kwa wananchi inaenda *ZRB. (Makofi)*

**MHE. SAADA MKUYA SALUM:** *Yes.*

**MHE. HAWA A. GHASIA - MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mtaji wake ule unasinyaa kila siku, inachukuliwa huku *VAT* ya Bara inabaki Bara na kule inaenda Serikalini. Kama ingekuwa sisi huku tunavyonunua ni tofauti kama ingekuwa ni ya Muungano. Ndiyo maana wanapendekeza huku akinunua asinunue na *VAT* kwa sababu hii *VAT* ni ya huku apewe kwa bei isiyokuwa na *VAT* kama zinavyopelekwa bidhaa nyingine. Bidhaa zote zinazozalishwa huku kupelekwa Zanzibar hawauziwi na *VAT* kwa sababu kule zitakapouzwa zitatozwa *VAT.* Hata kama bidhaa imezalishwa Tanzania Bara ikifika Zanzibar inakuwa *considered* kama vile imezalishwa Zanzibar na *VAT* inatozwa Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niwaombe Serikali kwa nia nzuri tu kutoa *definition* na sidhani kama ni suala gumu sana. Pia hili ni suala la *Finance,* mambo mengi tumeyapitishia kwenye *Finance.* Ukitoa tu *definition* kwamba umeme na wenyewe ni *service* ambapo kweli wote tunakubaliana ni *service,* inakuwa *automatically* umeshaifuta hiyo *VAT* asilimia 18 kwa umeme unaoenda Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. SAADA MKUYA SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa tuweke sawa hili.

**MWENYEKITI:** Nimekuona Mheshimiwa.

**MHE. KHADIJA NASSIR ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuniona. Mchango wangu nita-*base* sana kwenye maoni ambayo ametoa Mheshimiwa *AG.* Katika

suala la umeme kuna hoja zaidi ya tatu lakini kwa vile kuna maongezi ambayo yanaendelea ndiyo maana kwa sasa hivi tumeleta hili suala la kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwambie tu Mheshimiwa *AG,* waliom-*feed,* wamem-*feed* vibaya. Suala ambalo liko kwenye maongezi ambalo anasema kwamba kuna *consultation* inaendelea ni suala la bei. Suala la msamaha wa kodi au *double taxation* halipo kwenye maongezi kwa sababu tumeshapita kwenye hatua ya maongezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Saada Mkuya.

**MHE. SAADA SALUM MKUYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwenye *VAT Act* ya mwaka 2014 masuala ya maji, gesi, *thermal energy* na *electricity* yanakuwa *defined* kama *essential serives,* kwa hiyo, *definitely* ile ni *services.* Hata hivyo, kifungu kile cha 48 kilivyokaa kinai-*defend* Tanzania Bara wakati inaponunua umeme kutoka nje na *VAT* inalipwa Tanzania Bara, hailipwi huko ambapo umeme unanunuliwa *especially* zile sehemu za *borders* ambapo tunanunua *from* Uganda na Zambia. *The same principle* kwamba *ZECO* na yeye anachukua umeme hapa anapeleka Zanzibar huko Zanzibar ndiyo kwenye watumiaji na *VAT* ni kodi ya *final consumer, ZECO* yeye sio mfanyabiashara.

**MWENYEKITI:** Nafikiri umeeleweka Mheshimiwa. Umeeleweka kabisa ila sasa ndiyo tuko njiapanda hapa. Kwa kweli yapo mambo Mheshimiwa Waziri wa Nishati sijui kwa sababu tulitawaliwa na Waingereza, tunapenda sana majadiliano, tunapenda sana. Wewe huyo huyo unanunua umeme toka Zambia hulipi *VAT* ya Zambia, wewe huyo huyo unanunua umeme kutoka Uganda hulipi *VAT* ya Uganda, ndugu yangu huyu Mzanzibari huyu, tuzungumze, tuzungumze. *(Makofi/Kicheko)*

Si imeandikwa, wapende wengine kama unavyojipenda mwenyewe.

**MBUNGE FULANI:** *(Hakutumia kipaza sauti).*

**MWENYEKITI:** Naam.

**MBUNGE FULANI:** *(Hakutumia kipaza sauti).*

**MWENYEKITI:** Hapana, haitakuwa hivyo, siyo vizuri. Linanipa tabu tu lakini kwa kweli kama Zanzibar wanalalamika yako baadhi ya mambo *we are being very unfair!* Kabisa, kabisa kama hili, mimi sikulijua, mimi nasikia tu maoni, ndiyo nasikia kwa mara ya kwanza, w*hy this now?* Kwa nini iwe hivyo? Yaani ndugu zetu hawa wanalipa asilimia 36? *(Makofi)*

Ndiyo maana ukienda Zanzibar hoteli ghali, tuna Ofisi kule Zanzibar, tungeweza kuwa tunapeleka baadhi ya Kamati zinakutana Zanzibar hatufanyi hivyo hata siku moja kwa sababu yaani hii posho ya hapa ukiipeleka Zanzibar inayeyuka. Maisha ni ghali sana Zanzibar. Hoteli yaani chumba kimebana hivi bei ni mbaya. Labda huenda na mambo ya umeme yanachangia kwenye kuwa hivyo. *(Makofi)*

Sasa hapa nahitaji kwa kweli ushauri, sijui tunatokaje hapa.

**MBUNGE FULANI:** Tupige kura.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri.

**MWENYEKITI:** Kutoka kwenye Kamati?

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Ndiyo.

**MWENYEKITI:** Sasa toa ushauri ili tuweze kuvuka maana karibu tunamaliza.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Serikali wanatafakari kutumia busara na Mheshimiwa Waziri wa Nishati ali-*clarify* lile deni la shilingi bilioni 16 siyo 32,

ili muone tatizo lililoko Zanzibar, bei yao *per kilowatts* imepanda kutoka Sh.8,100 na zaidi mpaka Sh.16,000.

**MHE. SAADA MKUYA SALUM:** *Yes.*

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *on top of that,* tunawawekea asilimia 18 *VAT* na *price* hii wanayochajiwa wao *is expensive* kwenye *region* hata uki-*compare. (Makofi)*

**MHE. SAADA MKUYA SALUM:** Kabisa.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo na sisi kwenye Kamati tuli-*plea* na hii ndiyo maana unashangaa tunakesha halafu bado kuna mambo tunakuja huku. *This is a scenario* kwamba mna-*plea* kuwaomba na mpaka kuna wakati tunasema, jamani tusaidieni hasa sisi Chama tunachotawala kupunguza kelele na matatizo kwa watu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Nishati.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi lakini namshukuru pia Mheshimiwa Bashe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako mambo mawili hapa. Liko jambo la kisheria ambalo napenda tu kusema kidogo. Nadhani kinacholeta shida nilieleza hapo mwanzoni kwamba ni suala la tafsiri na tunaotunga sheria ni sisi. Mimi ningeshauri kwamba kwa sababu kinachoongelewa hapa na wala kimsingi hakina mgogoro ni suala tu la kunyoosha vizuri tafsiri na utekelezaji ukafanyika.

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila utaratibu)*

**WAZIRI WA NISHATI:** Kwa hiyo, kwa sababu...

**MHE. MATTAR ALI SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mweyekiti, kwa sababu Mwanasheria Mkuu wa Serikali yuko hapa na kwa sababu na taratibu za uwekaji wa sheria ziko vizuri, mimi jambo la msingi ningeshauri kwamba sisi Serikali tulifanyie kazi haraka jambo hili kupitia utaratibu wa kawaida liende.

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila utaratibu)*

**WABUNGE FULANI:** Aaaa.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini suala la pili ambalo napenda kuliongelea ambalo Mheshimiwa Bashe amezungumza ni hili suala la Sh.16,000 na Sh.8,000, ni mambo mawili tofuati.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Tumalize kwanza hili.

**WAZIRI WA NISHATI:** Hili la kwanza ni *KVA* tusiyachanganye yatatuletea shida. Nashauri tulimalize jambo hili halafu twende na ajenda nyingine.

**MHE. MATTAR ALI SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Jamani, inatosha, mmeshachangia. Sidhani kama mnaosimama mna jipya sana labda Profesa hajaongea.

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mimi ni *member* wa Kamati ya Bajeti na Mwenyekiti wetu ameshatoa msimamo wetu pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nisaidie tafsiri. Tafsiri wala siyo suala la kisheria hapa, ni suala la kiuchumi kwa sababu *either you have a good or you have a service, there is nothing in between.* Hilo naomba nalo lieleweke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama sheria inasema kama alivyosema Mheshimiwa Waziri kwamba *goods and services to Zanzibar are exempted from taxation,* kwa hiyo, hapa tunafanya nini? Yaani ni moja kwa moja

kwamba *the issue is settled* kwa sababu *electricity itself, however way you take it, it is actually a good* kwa sababu ni bidhaa ambayo inazalishwa *(produced),* inakuwa *transmitted* na inakuwa *distributed. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, anachofanya *TANESCO* ana-*produce* na ku-*transmit a good to* Zanzibar. Sasa kama sheria inasema *goods* ziko *exempted, automatically* umeme uko *exempted. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *I beg to submit. (Makofi)*

**MWENYEKITI:** Umetupa *point* muhimu kweli kwamba kama *goods and services are exempted,* sasa wewe unahangaika na *definition,* tafuta ya tatu sasa maana *goods and services are exempted unless* huu umeme tunatafuta tena ni kitu gani kingine *out of goods and services,* sijui. *(Makofi)*

Sasa kiutaratibu wa Kibunge ni kwamba *amendment* imeletwa, tumeipokea, kwa kadri ya Kanuni zetu ni *amendment* na Serikali natumaini mliipata hiyo *amendment on time*. Maana iko mezani kwangu hapa na waliotoa ni Kamati, sasa ninyi ndiyo wa kutuambia kama watoa hoja mnasemaje, mna-*withdraw,* mnataka sasa ipigwe kura, ninyi watoa hoja.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba tuifanyie maamuzi na kwa sababu tatizo lenyewe lilitokana na kuanzisha *VAT Act* mpya 2014, tupige kura tubadilishe sheria hapa *VAT* iondolewe. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ushauri wa AG kabla hatujapiga kura.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mambo mawili. Kama alivyomaliza kuzungumza Mheshimiwa Jitu, haya matatizo yametokana na mabadiliko ya sheria mwaka 2016. Mabadiliko haya yalikuja Bungeni hapa, Wabunge wote kutoka pande zote mbili za Muungano walikuwepo. Hii ndiyo *complication* ya kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha pili *VAT*, kama alivyoeleza vizuri sana...

**MWENYEKITI:** Kitu gani *in particularly* kilibadilika hiyo 2016?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ilikuwa inaelezea ile *VAT* ita-*apply* namna gani. Ikasema kama huduma hizi za umeme zinatolewa *Tanzania Mainland* ile *VAT* itachajiwa kwa mtumiaji aliyeko *Tanzania Mainland*. Pia kama huduma itatolewa nje ya Jamhuri wa Muungano wa Tanzania ile *VAT* itachajiwa kama vile huduma imetolewa *Tanzania Mainland,* hapo ndiyo kwenye shida.

**MWENYEKITI:** Sasa Zanzibar ni *part* ya wapi?

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila utaratibu)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Jambo la pili, kama alivyosema Mheshimiwa Chenge.

**MWENYEKITI:** Hapo hapo, Zanzibar sio nje ya Tanzania.

**MHE. MATTAR ALI SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba umwambie atusaidie Zanzibar siyo Tanzania.

**MWENYEKITI:** Jamani tusipoenda kwa hatua itakuwa ni klabu ya pombe. Tumpe nafasi Mwanasheria Mkuu, kwa maneno aliyoyasema ikitolewa nje ya Jamhuri ya Muungano, sasa Zanzibar si bado ni ndani ya Jamhuri ya Muungano, lilikuwa hilo tu, endelea Mheshimiwa.

**MHE. SAADA MKUYA SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa, naomba ni-*clarify* kuna sheria iko hapo.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumza sheria inavyosomeka, sheria ilipita Bungeni na ndivyo inavyosomeka.

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila utaratibu)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna ile changamoto Zanzibar hapa iko wapi?

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila utaratibu)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana Waziri, Mheshimiwa Kalemani akasema kuna suala pia la tafsiri hapa. La pili *VAT* siyo masuala ya Muungano.

**MHE. HAWA A. GHASIA - MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI:** Mheshimiwa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Ndiyo Mheshimiwa.

**MHE. HAWA A. GHASIA - MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, dakika moja tu, tangu umekaa hapo kwenye Kiti tunafanya *amendment* za sheria.

**MHE. SAADA MKUYA SALUM:** Ajabu.

**MHE. HAWA A. GHASIA - MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI:** Tumeanza na Sheria ya Benki Kuu, Sheria ya Leseni za Biashara, Sheria ya *Excise Duty,* Sheria ya Korosho, Sheria ya Michezo ya Kubahatisha, tumerekebisha sheria zaidi ya 19. Hapa tulipo tunarekebisha sheria ni pamoja na hii, tumefikia kifungu cha *VAT* na hiyo iingie. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Kwa haki ya Mungu katika hili, we are *bullying* Zanzibar. *(Makofi)*

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mwisho wa kuonewa ni leo.

**MWENYEKITI:** Kabisa, kabisa. Yaani duniani hapa tutakufa siku moja.

**MHE. SAADA MKUYA SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tuonee huruma.

**MWENYEKITI:** Hata kama tuko Serikalini au tuko wapi, jambo ambalo si la haki si la haki tu.

**MHE. SAADA MKUYA SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tuonee huruma.

**MWENYEKITI:** Sisi tunaosali kila Jumapili napata tabu yaani napata tabu au wanaosali Ijumaa. Kweli mimi Kongwa mnanipa hivi, Mbunge mwenzangu hapa akalipe mara mbili Tanzania hii hii. Au Zanzibar matajiri sana? Kidogo inatupa shida lakini sasa...

**WABUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoji.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa mimi niwaombe kama Mwenyekiti tuwaache wakajadiliane wanaopenda kujadiliana.

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila utaratibu)*

**MBUNGE FULANI:** Hapana Mheshimiwa.

**MWENYEKITI:** Maana liko wazi kabisa lakini tuwaache wakajadiliane. *(Kicheko)*

**MHE. BAHATI ALI ABEID:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa, mimi sijaongea.

**MHE. KABWE Z.R. ZITTO:** Kuhusu utaratibu.

**MWENYEKITI:** Tulieni wote, Mheshimiwa Bahati hujaongea siku nyingi, Mheshimiwa Bahati Ali Abeid.

**MHE. BAHATI ALI ABEID:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili lilipofikia sasa si la kupiga kura, Serikali ituachie Zanzibar ikijua kwamba *ZECO* wanayoichaji *VAT* kule inaenda kuhudumia mpaka Idara za Muungano. Kwa nini mnatunyanyasa sasa tena? Tuachieni Serikali, mtuachie, umefika wakati sasa mtuachie. *(Makofi)*

**MHE. KABWE Z.R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu utaratibu.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ushauri.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, *I have to admit* hili suala gumu sana.

**MBUNGE FULANI:** Wala siyo gumu.

**MWENYEKITI:** Hebu tuliache kwanza tumalizie vifungu vingine tutarudi hapo.

**WABUNGE FULANI:** Aaaaaaa.

**MWENYEKITI:** Katibu tuendelee na vifungu vingine tutarudi hapo.

Ibara ya 80

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 81

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake*

Ibara ya 82

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilifutwa)*

Ibara ya 83

**MWENYEKITI:** Kamati inashauri kifungu cha 83 kifutwe. Serikali mnasemaje? Wakifafanue kidogo? Haya Kamati kwa nini mnasema 83 ifutwe?

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa pia tuna *amendment* kwenye 81.

**MWENYEKITI:** Hiyo tulishapita, kifungu cha 83?

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna *withdraw* tuendelee.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 84

**MWENYEKITI:** Kamati kifungu cha 84.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kifungu hiki cha 84, mbali na ile iliyopendekezwa na Serikali ya mashudu ya pamba na alizeti tunapendekeza pia iongezwe pumba kwa ajili ya utengenezaji wa chakula cha mifugo na kwenye *amendment* tumeiweka hapo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Serikali hayo maneno ya pumba mnasemaje? Maana sasa sijui pumba ya nini?

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iliridhia. *(Makofi)*

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

**MWENYEKITI:** Haya tumemaliza sasa tunarudi kwenye kiporo.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bado kuna mengine huku mbele kwenye orodha. Tunashukuru kama Serikali imeridhia hizi *amendment* ambazo Kamati tumeleta ikiwa ni pamoja na marekebisho haya, ahsante sana Mheshimiwa Waziri.

**MWENYEKITI:** Kwenye nini?

**MHE. JITU V. SONI:** Kwenye *amendment*.

**MWENYEKITI:** Usifanye kitu katika *blanket*, kwenye kitu gani, kwa sababu mwisho wetu hapa si kifungu cha 84, kuna maneno tena?

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kifungu cha 84 kuna orodha nzima tuliweka *Schedule of Amendment,* kwa hiyo, kama wamekubaliana nayo, tunawashukuru sana.

**MWENYEKITI:** Orodha nzima orodha gani msije mkaingiza vitu ambavyo havipo.

**MHE. JITU V. SONI:** Ipo hapo.

**MWENYEKITI:** Wewe si umesimama ukasema pumba tu ndiyo imeongezeka?

**MHE. JITU V. SONI:** Ndiyo na vitu vingine ambavyo vipo hapa kwenye kifungu cha 84.

**MWENYEKITI:** Mbona huvielezei ni vitu gani?

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, Serikali ilileta mapendekezo ya *packaging material* kwa ajili ya *pharmaceutical,* sisi tumeongeza pia *packaging material* ya maziwa pamoja na mbegu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia upande wa maji tumeongeza *solar water pumps, water pumps* yenye mita, siku za nyuma ilishasamehewa lakini siku hizi *pump* za kisasa zinakuja na mita. Ikija pale *TRA* kwenye utaratibu wake unasema *pump* yenye mita itatozwa kodi ambayo haina mita haitozwi kodi. Sasa zile ambazo...

**MWENYEKITI:** Yaani hayo yote mliyazungumza huko na hamkuwa mmekubaliana?

**MHE. JITU V. SONI:** Ndiyo na tulishawapa kuanzia jana na *Schedule of Amendment* tulishaileta.

**MHE. HAWA A. GHASIA - MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI:** Wamekubali.

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, yame-*crop up* jana tu?

**MHE. HAWA A. GHASIA - MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI:** Amekubali.

**MHE. JITU V. SONI:** Siyo jana, haya ni majadiliano ya muda mrefu na yote haya walikuwa nayo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Fedha, mnatupa kazi kweli.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Hapana, Serikali ilichoridhia ni mashudu.

**WABUNGE FULANI:** Mmh.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Hayo mengine tuangalie huko mbele.

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Kamati, naomba mkubaliane katika hilo.

**MHE. HAWA A. GHASIA – MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI:** Sawa.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mashudu inaingia hayo mengine mtaendelea na mijadala. Ni mapendekezo mazuri hata baadhi yake nimeyaona lakini mwendelee kujadiliana. Sasa tunarudi kwenye kiporo.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani. Huko nyuma pia kuna kipengele ambacho uliruka ambacho kilikuwa ni *Schedule of Amendment*.

**MWENYEKITI:** Tulishaamua, tulishashamaliza huko, huturudishi tena Mheshimiwa.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, ni ile shilingi hamsini ya maji.

**MWENYEKITI:** Huku nyuma wapi.

**MHE. HAWA A. GHASIA - MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI:** Ni pendekezo la kuongeza shilingi hamsini.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa mlishaturuhusu tuvuke, hebu acha tuvuke. Mtaendelea Kamati ya Bajeti na Wizara, bado ni wenzenu tuendelee kuliongea hilo.

Mheshimiwa Waziri wa Nchi ulisimama, tusaidie kutoka kwenye Kifungu kipya cha 80.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili kadri ulivyoliona, ni jambo ambalo limegusa mioyo ya Wabunge wenzetu kutoka Zanzibar.

**MWENYEKITI:** Hata Bara pia.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo naendelea huko, lakini limegusa pia mioyo ya Wabunge kutoka Bara kwa maana halisi uliyoisema ya huo uwiano wa utozaji wa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ukitazama mfumo mzuri wa kufikia maafikiano ambayo yanaweza kuwa ni maafikiano ya amani na yenye mwelekeo sahihi na hasa linapotokea jambo la namna hii na wakati mwingine likiwa na mtizamo wa upande wa pili wa Muungano kama vile unanyimwa haki kwa namna moja ama nyingine, ni suala ambalo kwa heshima sana, sana ya kikao chako cha leo, Serikali tunaomba utupe nafasi haraka sana tukakutane na wenzetu wa upande wa pili.

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila utaratibu)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU):** Kwa sababu kwa upande mwingine...

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tumsikilize *Chief Whip*, fupisha tu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mwingine itabidi twende tukashughulike hata kama masuala ya kodi si masuala ambayo yanahitaji kuingizwa na tafsiri za Kimuungano lakini zipo sheria ambazo zitatakiwa zikafanyiwe kazi ili kuliweka hili jambo kuwa na *harmony*.

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila utaratibu)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Serikali tutoe hapa na tunatoa *commitment,* tutakapokutana kwenye Mkutano unaokuja...

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila utaratibu)*

**WABUNGE FULANI:** Aaaaaa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU):** Jambo hili tuwe tumelimaliza kabisa na liwe limepata sura nzuri na tuwe tumeondoa hilo wingu ambalo linaonekana kabisa kama upande wa pili wa wenzetu unanyanyasika ama kuonewa.

**MBUNGE FULANI:** Hapana.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hatua iliyofikiwa, tunahitaji *consultation* ya kutosha ndani ya Serikali ili kufikia muafaka wa hili. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Hapana, naomba Waheshimiwa mkae, tutoke hapa.

**WABUNGE FULANI:** Kuna hoja.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Mawaziri, hivi Zanzibar waje kujadiliana nini kuhusu hili? Hili ni jambo ambalo mnataka toeni, hamtaki msitoe. *(Makofi/Vigelegele)*

Maana mimi nakwambia kama jirani yako unaniumiza na wewe mwenyewe unaona kabisa ni dhambi hii unafanya, unataka tujadiliane, mnajadiliana nini? Hili ni jambo la ninyi wenyewe tu kukaa na kuliona, kwamba bwana katika hili kwa kweli, yaani kabisa Zanzibar wasafiri waje, sasa mnajadiliana nini? Haya mmekaa, mnawakatalia kwa mfano haya sisi tumekataa? Hili liko wazi kiasi hiki? *(Makofi)*

Viko vitu vya kujadili na vitu vingine ukishaambiwa bwana wewe hapa ulipokaa kwenye kitanda hiki unanibana mwenzio unasogea tu pembeni. Unambana mwenzio anakwambia halafu unamwambia tujadili bwana, mwenzio anazidi kuumia huku. *(Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Sasa nitawahoji kuhusu pendekezo la kuwapa muda Serikali.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**MWENYEKITI:** Waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Aaaa.

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo tumeshinda.

**MWENYEKITI:** Katibu toa taarifa.

**NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imekamilisha kazi yake.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, msife moyo, siamini kama mwakani tutakutana na hali kama hii lakini kwa kweli linasikitisha. Bunge linarudia.

*(Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba tukae, Mheshimiwa Waziri taarifa.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imepitia Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2018 *(The Finance Act,* 2018) kifungu kwa kifungu na kuukubali pamoja na marekebisho yake.

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila utaratibu)*

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba taarifa hiyo sasa ikubaliwe rasmi.

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila utaratibu)*

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Hoja imetolewa na imeungwa mkono, tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Haya,

wajibu wangu ni kuwahoji sasa kuhusu hoja iliyo mbele yetu. Nafikiri walioafiki wameshinda. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**WABUNGE FULANI:** Aaaaa.

**SPIKA:** Tuendelee, Katibu.

**NDG. LAWRENCE MAKIGI - KATIBU MEZANI:**

Muswada wa Sheria kwa ajili ya kutunga itakayotoza au kubadilisha baadhi ya kodi, ushuru, tozo na ada mbalimbali, kufanya marekebisho kwenye sheria mbalimbali zinazohusu ukusanyaji na usimamizi wa mapato ya umma [*A Bill for an Act to impose and alter certain taxes, duties, levies, fees and to amend certain written laws relating to collection and management of public revenues.*

*(Kusoma Mara ya Tatu)*

*(Muswada wa Sheria wa Serikali Ulipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Naomba niwapongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha, *AG*, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha, Wataalam wote mlioko huko mkiongozwa na Katibu Mkuu. Mheshimiwa Waziri Mkuu kipekee kabisa tunawashukuru sana Serikali kwa Muswada huu.

Pia tuwashukuru sana Kamati ya Bajeti mmefanya kazi *overtime*. Jana tu peke yake Kamati ya Bajeti wamemaliza shughuli zao saa nane usiku na juzi *almost* ilikuwa hivyohivyo, wamefanya kazi kwa *commitment* kubwa sana. Tunajivunia Kamati yetu ya Bajeti, hizi *challenge* tulizowapa ndogondogo zisiwavunje moyo hata kidogo, ni sehemu ya kazi tu lakini mmefanya kazi nzuri sana. Naomba Waheshimiwa Wabunge tuwapigie makofi Kamati ya Bajeti. *(Makofi)*

Vilevile tukushukuru Mheshimiwa Waziri umetuvumilia kwelikweli kupitia katika michakato yetu, umeona Bunge lilivyo na mambo kwa kweli yameenda vizuri.

Kwa kumalizia hilihili ambalo tumemaliza nalo, ninyi wenyewe mmeona *mood* ya Wabunge, Wanasheria yako mambo muwe mnaturahisishia, kabisa. Kwa sababu kama kitu ni *unfair* ni *unfair* tu, kinaonekana wazi kabisa. Sasa ukisema tujadiliane *unfair* inakuwa kidogo, lakini kwa kuwa kuna majadiliano basi mkajadiliane huko, tunatumaini jambo hili halitachukua muda mrefu, hata miezi mitatu, minne si vizuri likachukua muda. Ni vizuri ikafika mahali katika Muungano wetu tuwe watu wenye furaha, nchi moja, tunafanya mambo yetu vizuri. Kama tulivyoachiwa na Mwalimu nchi moja na kadhalika isionekane kama kuna vitu kama hivi vinawafanya baadhi ya wenzetu wanakuwa wanyonge sana.

Waheshimiwa Wabunge, nafikiri tulimsikia Mheshimiwa Bahati, Mheshimiwa Bahati ni mtu mpole sana lakini mmemsikia leo aliposimama anavyosema, ule ni ujumbe mzito sana. Tuuimarishe Muungano wetu, tuishi kama ndugu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya hayo, niwashukuru mno mmevumilia, mmekaa mpaka muda huu, kwa kweli nawashukuru mno. *(Makofi)*

Kwa hatua hii, niahirishe Shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi na baada ya kipindi cha maswali kesho, tutakuwa na Tamko la Serikali kama bado lipo la Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe na baada ya hapo Mheshimiwa Waziri Mkuu atakuwa anatufungia Bunge letu.

*(Saa 3.24 Usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Ijumaa, Tarehe 29 Juni, 2018, Saa Tatu Asubuhi)*